# MOTIFU YA SANAA ZA MAONYESHO YA JADI KATIKA TAMTHILIA YA KISWAHILI: MFANO WA *MASHETANI, PUNGWA, NGOMA YA NG'WANAMALUNDI* NA *MASHETANI WAMERUDI*

**NA**

**EZRA NYAKUNDI MOSE**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA, KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA KIJAMII ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA MOI**

**2021**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya utahini.

__________________________ ____________________

Sahihi Tarehe

**EZRA NYAKUNDI MOSE**

**SASS/DPHIL/16/2008**

Tasnifu hii imetolewa kwa ajili ya utahini kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu Cha Moi:

Sahihi Tarehe

**DKT. SAMUEL MOSETI OBUCHI**

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA MOI

Sahihi Tarehe

**DKT. MARK MOSOL KANDAGOR**

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA MOI

# TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa marehemu Babangu Josiah Mayaba Ragira na marehemu Babu yangu Mzee Samson Ragira Mayaba kwa mausia na wema wao kwangu walipokuwa hai (Mungu awalaze mahali pema peponi, wapumzike kwa amani). Naitabaruku kazi hii vilevile kwa mama yangu mpendwa Mary Kemunto Mayaba, wanangu Frankline Omwenga, Rosemary Kemunto, Sasha Mokeira, Shantel Nyabonyi na Josiah-Louis Okemwa bila kumsahau mke wangu mpendwa Sophia Bochere Okemwa ambao subira, maombi na heri zao njema ziliniwezesha kufikia hatua hii.

## SHUKRANI

Shukrani zangu kwanza ni kwa Mwenyezi Mungu ambaye bila baraka na ulinzi wake singeweza kuifanikisha safari hii ya kiusomi. Naungama kuwa imekuwa muda mrefu na mara nyingi nilihemewa kutekeleza majukumu fulani katika kazi hii kiasi kwamba aghalabu nilijipata nimekwama. Kwa wema wake Maulana nami pia nimefikia ufanisi huu wa kiusomi. Mungu ni Mkubwa!

Pili, nakishukuru Chuo Kikuu cha Moi kwa kunipa nafasi ya kusomea shahada ya uzamifu katika Kiswahili ili kujiendeleza kimasomo. Aidha, nawashukuru wasimamizi wangu wa Chuo, Dkt. Samuel Obuchi Moseti na Dkt. Mark Mosol Kandagor kwa kunihimiza kuendelea kujizatiti katika utafiti huu wakati nilipokuwa nimehemewa na kwa kujitoa mhanga katika kunipa maelekezo na ushauri wa busara ulionifaa katika kukusanya data na kuiandika tasnifu hii. Najivunia wasimamizi wangu kwa kuisoma kazi yangu bila kuchelewa na kwa ushauri wao wa kitaalamu. Nawashukuru pia wahadhiri wangu, akina marehemu Prof. Naom Luchela Shitemi (Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi), Prof. Nathan Oyori Ogechi, Prof. Father Joseph, K. Kahiga, Prof. Issa Mwamzandi na wahadhiri wengine ambao sijawataja kwa majina hasa walionifaa mimi na wanafunzi wenzangu katika usomi wetu na katika kutujenga kitaaluma.

Kwa wazamifu wenzangu ambao pamoja tuling’ang’ania titi la usomi na taaluma hii katika Chuo Kikuu cha Moi: Eucabeth Ong’au, Harriet Ipala, Charles Kotuni Wasike, Misikhu na Nilson Opande nawashukuru kwa kuhimizana na kupongezana kila tulipoonyesha uchovu kwa kupunguza mwendo katika kuhitimisha tafiti zetu. Marafiki na wenzangu kazini Dkt. Erick Ogwora, Dkt. George Anyona, Dkt. Christopher Okemwa, Dkt. Mecha, Dkt. George Nyandoro, Dkt. Margret Barasa, Dkt

Charles Nyandoro na wengine nawashukuru kwa mijadala yetu ya pamoja iliyonichachawisha na kunitia hamasa ya kutaka kufikia upeo huu wa juu.

Siwezi kuwasahau Wilfred Magato, Mhariri Philip Ochoi na mpiga chapa Paul Meltus walioisoma kazi hii kwa mchango wao adimu. Kwa wenzangu wengine walio katika safari hii ya usomi nawahimiza kujikaza ili kukamilisha jukumu hili zito. Kwa kweli wakati mwingine jukumu hili huwa zito kiasi kwamba usipojizatiti kuendelea mbele, unaweza kuzidiwa na ukawa unajikokota na ukachukua muda mrefu au hata ukateleza na ukakoma kabisa kwendelea na utafiti na uandishi wa tasnifu yako.

Kwa wote ambao sikuweza kuwataja kwa majina kwa ajili ya msaada walionipa wakati wa utafiti na uandishi wa tasnifu yangu, isionekane kama ni mtovu wa shukrani. Nahongera kwa misaada ya kila nui mliyonipatia. Asanteni sana kwa kila aliyechangia katika kufanikiwa kwa kazi hii. Mungu anayeneemesha baraka ndogo ndogo na baraka kubwa kubwa awabariki nyote kwa wema na ukarimu wenu.

# IKISIRI

Tasnifu hii ni zao la uchunguzi kuhusu matumizi ya Sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu ambayo yalijumuisha kupambanua tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika kama mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili, kuchanganua taswira zilizojengwa na kuibushwa na tanzu za jadi za sanaa za maonyesho zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na tatu, kusawiri umuhimu wa sanaa za maonyesho na maendeleo yake katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika miongo mitano ya utunzi. Utafiti uliongozwa na nadharia za Uhistoria Mpya iliyoasisiwa na Greenblatt na nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na Julia Kristeva. Nadharia ya Uhistoria Mpya ilituwezesha kubainisha kihistoria tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na mbinu mbalimbali za matumizi ya tanzu hizo katika mapito ya kipindi cha karibu miongo mitano. Nadharia ya Mwingilianomatini ilituwezesha kuainisha tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilivyotumiwa kwa mrudio katika kubuni tamthilia mpya ya Kiswahili. Aidha, nadharia ya Mwingilianomatini ilituwezesha kudhihirisha uhuru wa watunzi katika matumizi yao ya vipengele vya ujadi katika utunzi wa kazi zao ili kufanikisha ujumi, fani na maudhui katika utanzi wa tamthilia ya Kiswahili. Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo au kithamano. Sampuli ya utafiti huu ilihusisha tamthilia nne; *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* ambazo ziliteuliwa kimakusudi na ambazo katika usomaji wa awali zilidhihirisha matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika kama mbinu ya utunzi na kiungo cha ujenzi wa tamthilia mpya ya Kiswahili. Tamthilia zote ziliandikwa na waandishi Watanzania katika mapito ya kipindi cha karibu miaka hamsini. Ukusanyaji wa data ulihusisha usomaji wa ndani na nje ya maktaba ambapo kazi mbalimbali zilizokuwa na umuhimu na mchango kwa utafiti huu zilisomwa na kuainishwa ili kubainisha tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilizohusishwa katika utunzi wa tamthilia zetu teule. Uchanganuzi na uwasilishaji wa data yetu ulifanywa kwa njia ya maelezo ya kina yaliyohusisha udondoshaji na ufafanuzi wa dondoo za tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi tulizokusanya kutoka kwa tamthilia teule za utafiti huu kwa ajili ya kuchanganua mbinu za matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa watunzi wa tamthilia ya Kiswahili wametumia mbinu za masimulizi ya kingano, ushairi simulizi, nyimbo, ngoma, majigambo, uzungumzi wa hotuba, soga, malumbano ya utani, semi za kijazanda, methali miongoni mwa tanzu nyingine za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika kwa njia inayojirudiarudia katika kujenga na kuimarisha umbo la tamthilia ya Kiswahili na kuendeleza dhamira zao. Aidha, ilidhihirika kwamba matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi katika uumbaji wa tamthilia mpya ya Kiswahili yamechangia katika kupanua mbinu za utunzi na kujenga umbo la kipekee la tamthilia ya Kiswahili mbali na kuendeleza ujumi wa tamthilia. Tanzu za jadi za sanaa za maonyesho zilizotumiwa kubuni tamthilia ziliweza kupanua maana na dhamira za watunzi kwa kuzua taswira zilizohitaji kutafsiliwa ili kueleweka. Matumizi ya tanzu hizo katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili vilevile yaliweza kufanikisha utunzaji na uhifadhi wa utamaduni wa Kiafrika. Ili kuweza kuzitumia tanzu za jadi za sanaa za maonyesho ambazo pia ni mbinu za Fasihi Simulizi katika utunzi wa tamthilia ambayo ni utanzu wa Fasihi Andishi, watunzi waliweza kuzifaragua tanzu hizo kuziwezesha kuchukuana na kuafiki muundo wa tamthilia andishi ya ki-Aristotle.

# ABSTRACT

This thesis is the result of an investigation into the use of devices of African perfomance drama and cultural heritage in the constructon of the Kiswahili play. The research was based on three objectives. First, the identification and analysis of the use of different forms of traditional African perfomance drama items. Secondly, the research sought to establish themes developed by the African performance drama items used in constructing the selected Kiswahili plays. Thirdly, the research sought to establish the generational changes and developments that may have manifested in the Kiswahili play in the almost fifty years of its existence. In the investigation, the researcher analyzed four Kiswahili plays which were sampled purposively for the use of African performance drama as an archtype used in designing and constructing the modern Kiswahili play. The reseacher used purposive sampling technique in selecting four Kiswahili play texts published between 1971 and 2016 (almost fifty years), which through pre-reading depicted the use of drama items, themes, characterization, styles and methods only found in the various traditional African performance drama. The play-books analysed were *Mashetani*, *Pungwa*, *Ngoma ya Ng'wanamalundi* and *Mashetani Wamerudi*. The research took a descriptive format. Data collection was done through intensive reading where different texts and literature related to the research topic were read and analyzed to identify and establish different forms of African performance drama devices used in constructing the Kiswahili play. Data was analysed and presented descriptively based on the three objectives of this reseach. The analysis was guided by two theories namely; New Historicism by Greenblatt and the theory of Inter-textuality by Julia Kristeva that enabled the researcher to identify the different African performance drama items, their style and methods adopted by Kiswahili playwrights in constructing a typical modern Kiswahili play. The inter-textuality theory enabled the researcher to comparatively identify texts and the history of the themes adopted from African performance drama by the playwrights in a span of almost fifty years of the construction of a typical modern Kiswahili play. The inter-textuality theory also enabled the researcher establish the freedom of the Kiswahili play author in making reference to African performance drama items in their plays and in analyzing their style, methods and themes like the use of story telling techniques, dancing and singing skills, reciting of oral poems, oratory, characters, and themes adopted from African performance drama to reconstruct and realize a new and typical modern Kiswahili play. The research findings revealed that Kiswahili playwrights had defied the adoption of the Aristotolian style play and adopted inter-textually the use of many different items, styles, forms and themes borrowed from traditional African performance drama to construct a hybrid typical form of the Kiswahili play. It also emerged that the adoption of the use of items of traditional African drama in the construction of the typical hybrid Kiswahili play contributed to the opening up of new styles of creating a Kiswahili play, that have enhanced the aesthetics of the play and that have brought out the themes of the author. It was concluded that traditional African drama has been used creatively in the construction of the Kiswahili play and that its use in the Kiswahili play has also contributed to the preservation and maintainance of the African culture.

# YALIYOMO

IKIRARI ..... ii
TABARUKU ..... iii
SHUKRANI ..... iv
IKISIRI ..... vi
ABSTRACT ..... vii
YALIYOMO ..... viii
ORODHA YA MAJEDWALI ..... xiv
UFAFANUZI WA ISTILAHI ..... xv
AKRONIMU NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA ..... xvii
**SURA YA KWANZA ..... 1**
**MISINGI YA UTAFITI ..... 1**
1.0 Utangulizi ..... 1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti ..... 1
1.2 Suala la Utafiti ..... 4
1.3 Malengo ya Utafiti ..... 7
1.4 Nadharia Tete ..... 8
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ..... 8
1.6 Umuhimu wa Utafiti ..... 11
1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti ..... 12
1.8 Hitimisho ..... 13
**SURA YA PILI ..... 15**
**MAPITIO YA MAANDISHI KUHUSU MADA NA KIUNZI CHA KINADHARIA ..... 15**
2.0 Utangulizi ..... 15
2.1 Sanaa za Maonyesho ya Jadi na Tamaduni za Kiafrika ..... 15
2.2 Mwingilianotanzu ..... 22
2.3 Misingi ya Kinadharia ..... 24
2.3.1 Nadharia ya Uhistoria Mpya ..... 24
2.3.2 Mwingilianomatini ..... 26
2.4 Pengo la Maarifa ..... 31
2.5 Hitimisho ..... 31

**SURA YA TATU** ........................................................................................ **33**
**MBINU ZA UTAFITI** ................................................................................ **33**
3.0 Utangulizi ............................................................................................ 33
3.1 Muundo wa Utafiti ................................................................................ 33
3.2 Eneo la Kufanyia Utafiti ........................................................................ 34
3.3 Sampuli na Usampulishaji ..................................................................... 36
3.4 Mbinu za Ukusanyaji Data ..................................................................... 38
3.5 Uchanganuzi wa Data ............................................................................ 39
3.6 Uwasilishaji wa Data .............................................................................. 40
3.7 Hitimisho ............................................................................................... 41
**SURA YA NNE** ......................................................................................... **42**
**SANAA ZA MAONYESHO YA JADI NA TAMTHILIA YA KISWAHILI** ...... **42**
4.0 Utangulizi ............................................................................................ 42
4.1 Tamthilia ya Kiswahili na Sanaa za Maonyesho ...................................... 42
4.2 Matumizi ya Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Utunzi wa Tamthilia ya Kiswahili ........ 45
4.3 Uwasilishaji wa Sanaa za Maonyesho ya Jadi ya Kiafrika ......................... 51
4.4 Mwingilianomatini wa Sanaa za Maonyesho na Tamthilia ya Kiswahili ............. 58
4.5 Uainishaji wa Tanzu za Sanaa za Maonyesho ya Jadi .................................. 60
4.6 Sanaa za Maonyesho katika Utunzi wa Tamthilia Kimwingilianomatini ............ 67
4.6.1 Utambaji na Usimuliaji wa Kingano ................................................... 67
4.6.2 Wimbo, Ngoma na Uimbaji ................................................................. 68
4.6.3 Taswira ............................................................................................ 69
4.6.4 Mwingilianotanzu katika Sanaa za Maonyesho ya Jadi ........................... 70
4.6.5 Imani katika Pepo na Mizimu ya Jadi .................................................. 72
4.6.6 Tambiko ........................................................................................... 73
4.6.7 Kilinge ............................................................................................. 74
4.7 Hitimisho ............................................................................................... 75
**SURA YA TANO** ........................................................................................ **76**
**SANAA ZA MAONYESHO KATIKA TAMTHILIA YA KISWAHILI** ............ **76**
5.0 Utangulizi ............................................................................................ 76
5.1 Sanaa za Maonyesho katika Tamthilia ya *Mashetani* – Ebrahim Hussein ............ 76
5.1.1 Majigambo ........................................................................................ 79
5.1.2 Maigizo na Miujiza ya Shetani ........................................................... 81

5.1.3 Fumbo la Shetani ....................................................................................86
5.1.4 Masimulizi ..........................................................................................................88
5.1.5 Nyimbo na Ngoma..............................................................................................93
5.1.6 Tamthilia kama Utanzu wa Ushairi ...................................................................96
5.1.7 Malumbano ya Utani na Mchongoano...............................................................98
5.2 Sanaa za Maonyesho katika Tamthilia ya *Pungwa* - Said A. Mohamed (2016) .100
5.2.1 Tanzu za Jadi za Sanaa za Maonyesho katika Tamthilia ya *Pungwa* ...........102
5.2.2 Ufunguzi na Mbinu ya Usimulizi ...................................................................103
5.2.3 Ngomezi ...........................................................................................................106
5.2.4 Matumizi ya Wimbo .........................................................................................108
5.2.5 Majigambo .........................................................................................................111
5.2.6 Jadi ya Tamaduni za *Pungwa* .........................................................................115
5.3 Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* – Emmanuel Mbogo (1999) ..........................................................................................123
5.3.1 Nyimbo na Ngoma katika Tamthilia ya Ngoma ya *Ng'wanamalundi* .........126
5.3.1.1 Ngoma ya Nyamiti...........................................................................................127
5.3.1.2 Ngoma ya Sindimba .......................................................................................130
5.3.1.3 Ngoma ya Chidama .........................................................................................134
5.3.2 Mazungumzo katika Tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ..................140
5.3.2.1 Mbinu ya Hotuba .............................................................................................141
5.3.2.2 Mbinu ya Ulumbi.............................................................................................143
5.3.2.3 Mbinu ya Malumbano ya Utani.......................................................................146
5.3.2.4 Mbinu ya Soga.................................................................................................148
5.3.3 Mbinu ya Majigambo ya Chidama na Ng'wanamalundi..............................151
5.4 Sanaa za Maonyesho katika *Mashetani Wamerudi* - Said A. Mohamed (2016) .157
5.4.1 Wimbo katika Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* .......................................159
5.4.2 Usanii wa Fanani katika Sanaa za Maonyesho .............................................163
5.4.3 Usimulizi wa Kingomezi ..................................................................................166
5.4.4 Semi kama Mbinu ya Sanaa za Maonyesho ...................................................168
5.4.4.1 Mafumbo .........................................................................................................168
5.4.4.2 Lugha ya Kimafumbo na Tamathali za Semi katika *Mashetani Wamerudi* .....................................................................................................................172
5.4.4.3 Utanzu wa Jazanda ..........................................................................................172

5.5 Muhtasari wa Matumizi ya Tanzu za Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Utunzi wa Tamthilia Teule za Kiswahili ........................................................177
5.6 Hitimisho........................................................................................................181
**SURA YA SITA..............................................................................................183**
**TASWIRA YA TANZU ZA SANAA ZA MAONYESHO YA JADI ZILIZOTUMIWA KUTUNGA TAMTHILIA YA KISWAHILI .......................183**
6.0 Utangulizi.......................................................................................................183
6.1 Taswira ya Sanaa za Maonyesho katika Tamthilia ya Mashetani - Ebrahim Hussein...........................................................................................................184
6.1.1 Taswira ya Ukoloni Mamboleo katika Mchezo wa *Shetani na Binadamu*....184
6.1.2 Taswira ya Ukandamizaji na Utandawazi katika Jazanda ya Hadithi ya Chewa ..........................................................................................................189
6.1.3 Taswira ya Unafiki, Ubadhirifu na Unyanyasaji katika Ngoma na Nyimbo .192
6.1.4 Taswira ya Utabaka katika Jazanda za Ugonjwa wa Kitaru na Kumea Manyoya ..........................................................................................................200
6.1.5 Taswira ya Suluhisho la Matatizo ya Nchi za Afrika katika Motifu ya Safari ..........................................................................................................206
6.2 Taswira ya Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Tamthilia ya *Pungwa* – Said A. Mohamed ..........................................................................................................209
6.2.1 Taswira ya Ukoloni Mamboleo katika Majigambo ya Sauti ya Mzuka ........209
6.2.2 Taswira ya Utabaka, Unafiki na Uongozi Mbaya katika Ndoto za Bwana ...216
6.3 Taswira ya Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* – Emmanuel Mbogo.............................................................219
6.3.1 Taswira ya Ukandamizaji na Ukoloni Mamboleo katika Masimulizi ya Kingano ..........................................................................................................219
6.3.2 Taswira ya Unyanyasaji katika Ngoma ya Chidama ....................................222
6.3.3 Taswira ya Ukombozi katika Ngoma ya Shujaa Ng'wanamalundi ...............227
6.3.4 Taswira ya Utabaka katika Majigambo ya Ngoma ya Ng'wanamalundi ......230
6.4 Taswira ya Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* - Said A. Mohamed.........................................................................233
6.4.1 Taswira ya Ukoloni Mamboleo katika Jazanda Mbalimbali ........................234
6.4.2 Taswira ya Utandawazi katika Jazanda ya "Remote Control" katika *Mashetani Wamerudi* ..........................................................................................239

6.4.3 Taswira ya Vizingiti vya Ukombozi katika Mhusika "Prof." wa Kimajazi katika Mashetani *Wamerudi* ....243
6.5 Muhtasari wa Taswira katika Tamthilia Teule za Kiswahili ....245
6.6 Hitimisho....248
**SURA YA SABA ....250**
**MABADILIKO NA UMUHIMU WA MATUMIZI YA SANAA ZA MAONYESHO YA JADI KATIKA UTUNZI WA TAMTHILIA ....250**
7.0 Utangulizi....250
7.1 Mabadiliko na Umuhimu wa Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Utunzi wa Tamthilia ya Kiswahili....250
7.2 Usimulizi Katika Tamthilia ya Kiswahili ....256
7.3 Mitindo, Dhamira na Lugha ya Utunzi ....258
7.4 Matumizi ya Mwangaza Jukwaani na Mabadiliko ya Maonyesho ....260
7.5 Ufaraguzi wa Tanzu za Sanaa za Maonyesho katika Utunzi wa Tamthilia ya Kiswahili ....264
7.6 Tamasha za Muziki na Drama katika Shule na Vyuo ....267
7.7 Mwingilianomatini kati ya Tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* ...269
7.8 Tanzu za Jadi za Sanaa za Maonyesho kuwa Mianzo ya Tamthilia ....274
7.9 Muhtasari wa Maendeleo na Manufaa ya Sanaa za Maonyesho ya Jadi na Utamaduni wa Kiafrika....277
7.10 Hitimisho....278
**SURA YA NANE....280**
**MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ....280**
8.0 Utangulizi....280
8.1 Muhtasari wa Utafiti ....280
8.2 Matokeo ya Utafiti ....284
8.2.1 Tanzu za Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Tamthilia Teule....284
8.2.2 Taswira ya Tanzu za Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Tamthilia Teule ..290
8.2.3 Maendeleo na Umuhimu wa Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Utunzi wa Tamthilia ya Kiswahili ....295
8.3 Mchango wa Utafiti ....298
8.4 Hitimisho....298
8.5 Mapendekezo ya Utafiti....300
MAREJELEO ....301

VIAMBATISHO....................................................................................................307
Kiambatisho 1: *Mashetani*....................................................................................307
Kiambatisho 2: *Pungwa*........................................................................................310
Kiambatisho 3: *Ngoma ya Ng'wanamalundi*..........................................................314
Kiambatisho 4: *Mashetani Wamerudi*....................................................................316
Kiambatisho 5: Matokeo ya 'Plagiarism'................................................................320

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 5.1: Tanzu za Sanaa za Maonyesho katika Tamthilia ya *Mashetani*..............78
Jedwali 5.2: Muhtasari waTanzu za Sanaa za maonyesho katika Tamthilia ya *Pungwa* ...........................................................................................................103
Jedwali 5.3: Tanzu za Sanaa za maonyesho katika Tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ....................................................................................126
Jedwali 5.4.1 Nyimbo/Mashairi katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*...............162

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

**Jadi** : Sherehe za kitamaduni za jamii mbalimbali za Kiafrika kama ngoma, nyimbo, unyago, jando, arusi, matanga, pamoja na imani za jamii hizo ambazo zinaweza kujumuisha imani za kiungu, Mashetani, kiuchawi, pungwa, matambiko, makafara, miujiza na zingine ambazo zilitekelezwa kwa kupiga na kucheza ngoma, kughani mashairi na majigambo miongoni mwa shughuli zingine.

**Kikale** : Taswira kongwe inayojitokeza mara kwa mara katika kazi ya fasihi. Kikale huwasilisha dhana fulani kongwe inayopatikana katika jamii inayozungumziwa. Huweza kurejelea mhusika, motifu, ishara au taashira ambayo imekuwapo tangu zamani na inayojitokeza mara nyingi katika fasihi (Frye 1957, Plaks 1976 na Wafula, R 1999).

**Matambiko:** Hii ni aina ya dawa ya Kiafrika itolewayo kwa mtu aliyepandwa na pepo kwa ajili ya kurudisha maelewano baina ya watu. Pepo au mizimu huhitaji aina ya sadaka ili kuituliza na kuiliwaza kufuatana na mila na desturi za jamii mahususi.

**Motifu**: Mada, rangi au mbinu fulani ya utunzi inayojirudiarudia katika kazi yoyote ya sanaa.

**Mwingilianomatini:** Ni nadharia ambayo hutumiwa kuhakiki kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi nyingine ya kifasihi. Huchukulia kuwa kazi moja ya fasihi huwa na uhusiano na kazi nyingine au zingine zilizoandikwa awali kwa namna fulani.

**Ngoma:** Hurejelea nyimbo na dansi zenye misakato ya kiasili inayochezwa kuambatana na midundo ya ala za muziki ya ngoma. Pia ni mchezo wa kufuatia unaoandamana na ala ya muziki. Ngoma vilevile ni ala ya muziki iliyotengenezwa kwa kuwamba ngozi katika mzinga.

**Pungwa:** Hii ni njia ya utamaduni asili wa jadi ya Kiafrika inayotumiwa na waganga wa Kiafrika katika kuwatoa watu Mashetani au pepo waliowakumba na ambao husemekana kuwa hukaa vichwani mwa watu hao (Mohamed S. A 1988).

**Sanaa za maonyesho** : Hujumuisha sherehe za kijadi za ngoma, majigambo, miviga, jando na unyago, matambiko, utambaji hadithi na tanzu nyingine ambazo huwasilishwa ana kwa ana kwa hadhira kwa kucheza ngoma, kuimba, kucheza muziki, kutongoa na kughani mashairi simulizi, miondoko ya mwili na ishara za nyuso.

**Tamthilia:** Hurejelea michezo ya kuigiza ambapo ufananishaji hujitokeza kwa njia ya mwigizaji kujifananisha na mhusika katika mchezo. Aidha, ni utungo ulioandikwa au haukuandikwa ambao huliwasilisha wazo kwa kuigiza mbele ya hadhira.

**Taswira:** Mbinu ya utunzi inayotumiwa na waandishi kwa kutumia ishara katika kazi ya fasihi kuwakilisha wazo fulani linalowasilishwa kwa hadhira.

**Uhistoria Mpya:** Nadharia iliyoasisiwa na Stephen Greenblatt katika miaka ya 1940 inayotambua muktadha wa historia katika usomaji na uhakiki wa kazi ya fasihi.

**Utandawazi:** Huhusisha ueneaji na kusambaa kwa biashara, uchumi, mawasiliano, utamaduni miongoni mwa jamii mbalimbali za ulimwengu ukisaidiwa na maendeleo makubwa ya kiteknolojia ambayo yamefupisha muda wa mawasiliano kwa kuondoa vikwazo vya masafa na wakati na kuufanya ulimwengu kijiji kidogo.

## AKRONIMU NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA

| | |
|---|---|
| TUKI | : Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| TATAKI | : Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| Juz. | : Juzuu |
| k.h.j. | : Kama hapo juu |
| kr | : Kurasa |
| Uk | : Ukurasa |

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Katika utafiti huu tumeshughulikia motifu ya sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia teule za Kiswahili. Nia kuu ya utafiti huu ni kuchunguza namna tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika zilivyotumiwa kisanaa katika kuumba tamthilia ya Kiswahili, taswira zinazojengwa na matumizi ya tanzu hizo na maendeleo ya matumizi ya sanaa za maonyesho katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili kufikia sasa. Sura hii ya kwanza inatanguliza maelezo kuhusu usuli wa suala la utafiti huu, suala la utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti na hitimisho. Misingi ya utafiti huu imejadiliwa chini ya usuli wa suala la utafiti.

## 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Utunzi wa tamthilia umekua na kubadilika jinsi wakati unavyoenda ukibadilika kwa kupitia hatua mbalimbali. Mabadiliko haya yanadhihirika katika mitindo ya uandishi, fani, dhamira, maudhui na uumbaji wa wahusika katika mapito ya nyakati. Kazi za sanaa vilevile, huchota matukio mbalimbali ya kitamaduni na kihistoria kutoka kwa jamii na kuyafanya malighafi adimu ya kutungia kazi za sanaa kupitia kwa mbinu ya uchotaji wa tanzu mbalimbali ili kuunda utanzu mwingine wa kisanaa. Utunzi wa tamthilia ya Kiswahili vilevile umekuwa na athari ya uchotaji wa fani na maudhui kutoka kwa sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya Kiafrika yanayodhihirishwa waziwazi katika tamaduni na historia ya jamii za Kiafrika. Muhando na Balisidyia (1976) wanaunga mkono madai haya kwa kueleza kuwa tamthilia ya Kiswahili imezaliwa kutoka kwenye sanaa za maonyesho ya jadi na ambazo hazikuwa zimejitenga na hali halisi ya utamaduni na historia ya Mwafrika.

Uchotaji na matumizi ya sanaa za maonyesho ya Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili umeibua tamthilia mpya ambayo kwa mujibu wa Wamitila (2003) ni tamthilia iliyochota vipengele vya Fasihi Simulizi ya Kiswahili na kuviweka katika Fasihi Andishi ya Kiswahili, kwa lengo la kuleta vionjo vipya katika fasihi ya Kiafrika. Tamthilia mpya pia huitwa tamthilia ya majaribio inayotumia mbinu za kiubunifu ili kutunga tamthilia iliyoasi kaida za kijadi za uandishi. Uchotaji na matumizi ya sanaa za maonyesho ya asili ya Kiafrika kama mbinu ya sanaa na uhakiki hukusudia kufufua fasihi asili ya Kiswahili kwa kutumia mbinu na vipengele vya sanaa za maonyesho ya Kiafrika na Fasihi Simulizi kwa jumla katika utunzi wa tanzu za fasihi andishi za riwaya, hadithi fupi, novela, ushairi na tamthilia.

Majaribio ya kuchota na kutumia sanaa za maonyesho katika fasihi ya Kiswahili yamekuwa yakifanywa tangu mwanzo wa utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na waandishi maarufu wa tamthilia kama, Ebrahim Hussein na Penina Muhando. Ebrahim Hussein alitumia mbinu hii katika tamthilia yake ya *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* na Penina Muhando katika tamthilia yake ya *Lina Ubani*.

Mlama (1983) anaeleza kwamba, sanaa za maonyesho ni taaluma ya kisanaa ambayo huwakilishwa na fanani kwa hadhira wakiwa mkabala ana kwa ana. Kila jamii huwa na aina yake ya sanaa za maonyesho. Kwa sababu ya kuwa na makundi na makabila mengi katika jamii, huwa kuna aina nyingi za sanaa za maonyesho ya jadi hivi kwamba kuna mitindo mingi ya ngoma, matambiko, masimulizi ya hadithi, majigambo na tanzu nyingine. Baadhi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zimebadilika kimaumbo na kimuundo ilhali zingine zimepotea au zimefishwa kabisa na mabadiliko ya kiwakati yaliyoletwa na mabadiliko ya mifumo ya kijamii na tawala mbalimbali na mitindo mipya ya maisha ya Magharibi. Wakati wa ukoloni, kwa mfano, ulikomesha na kupiga vita sanaa za maonyesho za Kiafrika kwa kutumia dini

na elimu. Hivyo, nyingi ya sanaa za maonyesho hasa zile zilizohusiana na dini za jadi zilipotea wakati wa ukoloni zilipopigwa marufuku na tawala za kikoloni kwa kisababu cha kwenda kinyume na mafundisho ya Kikristo. Hata hivyo kwa sababu binadamu yeyote hukataa kutupilia mbali utamaduni wake, baadhi ya sanaa za maonyesho zimehimili na zimeweza kuchotwa na kutumiwa na waandishi katika utunzi wao wa tamthilia ya sasa. Senkoro (1987) na Mulokozi (1983) wanasisitiza kuwa watunzi wa tamthilia na riwaya huchota matukio mbalimbali ya kitamaduni na kihistoria katika jamii za Kiafrika na kuyatumia kama malighafi adimu ya kutungia kazi zao za sanaa.

Matukio hayo ya kitamaduni na kihistoria ambayo kisanaa yalijitokeza kama ngoma, majigambo, utambaji hadithi, miviga ya jando na unyago miongoni mwa mengine yamechotwa na waandishi wengi wa kazi za fasihi ambao wameyatumia kama malighafi katika utunzi wao wa tamthilia, riwaya, novela na hadithi fupi zao. Mtindo huu wa utunzi wa tamthilia mpya kwa mbinu ya uchotaji wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi umewezesha hali ya kukabiliana na mabadiliko yanayozikumba jamii nyingi za kisasa za Kiafrika.

Tamthilia ndio utanzu mchanga zaidi kuliko tanzu nyingine za Fasihi Andishi katika Kiswahili. Hata hivyo, asili ya tamthilia ndiyo ya kale zaidi kwa upande wa sanaa tendaji. Asili hii inachimbuka katika Fasihi Simulizi hasa katika utambaji wa ngano na hadithi, ngoma za kienyeji, jando, makafara, matambiko, mazishi na maigizo ya aina mbalimbali ambazo zote ni tanzu za sanaa za maonyesho zinazotokana na utamaduni wa Kiafrika. Maigizo haya ya kijadi yalishirikisha moja kwa moja msimulizi na hadhira yake katika utendaji na uigizaji kama katika mashairi ya majibizano, ngoma za watoto na watu wazima, michezo ya sarakasi miongoni mwa masimulizi mengine ambayo yalihusu matukio ya kila siku.

Rekodi za kihistoria zinaonyesha kwamba utawala wa kikoloni ulitumia dini ya Kikristo na mbinu zingine kupinga maendeleo ya sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika. Nyimbo za tohara, unyago, ndoa za kienyeji, matambiko, makafara na tamaduni nyingine zilizokuwa na sanaa za maonyesho zilipigwa marufuku. Aidha, Serikali ya kikoloni ilileta mfumo wa elimu wa kuwatenga wazazi na vijana wao ili kukwamiza tamaduni za Kiafrika na sanaa hizo za maonyesho ya jadi. Kwa kufanya hivi, waliharibu na kuvunja asasi ya mila na tamaduni za Kiafrika kama jando, unyago, matambiko na tanzu nyingine za fasihi asilia ambapo maonyesho mengi ya sanaa za maonyesho na utambaji yalifanywa. Mkondo huu wa matukio wa wakati wa ukoloni uliathiri tamthilia ya Kiswahili ambayo ilianza wakati huo na kuchukua maudhui na mtindo mpya.

**1.2 Suala la Utafiti**

Sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika zinaelekea kuwa sehemu muhimu ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu fani na maudhui katika tamthilia za Kiswahili. Aidha, kuna tafiti zinazozilinganisha fani na maudhui ya tamthilia mbalimbali zilizoandikwa katika nyakati mbalimbali. Hata hivyo, hakuna utafiti uliofanywa kuhusu matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika kama mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili kwa mtazamo wa kihistoria na Kimwingilianomatini kwa njia ya utathimini na ulinganisho wa kazi za fasihi za watunzi zaidi ya wawili katika mapito ya wakati.

Dhamira ya mwandishi wa kazi ya fasihi hutokana na mazingira yake ambayo humpa msukumo wa kutunga tamthilia au kazi yoyote ile ya fasihi ili aweze kueleza falsafa na hisia zake. Hivyo kazi ya fasihi ni tokeo la mwingiliano kati ya msanii na mazingira yake. Kazi ya sanaa inayotokana na msanii huwa ni matokeo ya tafsiri ya mazingira au mandhari yake kisanaa. Aidha, dhamira za mwandishi huathiri mtindo

wa uandishi wake. Mathalani mtindo anaoutumia msanii ni kijenzi cha kuibusha maudhui na dhamira anazonuia kuzijenga. Utafiti huu umeshughulikia uchunguzi wa mbinu za matumizi ya tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika kimuundo, kimtindo na kimaudhui kupitia taswira zinazojengwa na matumizi ya aina hiyo kwa ajili ya kuunda umbo zima na ujumi wa tamthilia mpya za Kiswahili. Vipengele vya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika hutumiwa sambamba na vipengele vyengine vya tamthilia ya ki-Aristotle kujenga na kuimarisha umbo kamili la tamthilia ya Kiswahili.

Kazi hii ambayo ni utafiti linganishi wa tamthilia teule za Kiswahili za Ebrahim Hussein, Said A. Mohamed na Emmanuel Mbogo ni tahakiki ya mbinu walizozitumia watunzi hawa kuchota na kutumia tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia zao. Utafiti huu vilevile ulinuia kudhihirisha taswira zinazojengwa kupitia kwa matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika katika kuimarisha umbo zima la tamthilia zetu teule. Sanaa za maonyesho ya Kiafrika huchukua nafasi adimu katika utamaduni wa Mwafrika. Ni nadra sana kwa wasanii kutumia sehemu hii ya utamaduni wa Kiafrika iliyosahaulika kwa ubunifu katika uumbaji wa kazi za sanaa za lugha ya Kiswahili katika kujenga na kuimarisha dhamira na maudhui yao. Kama Noordin (2006) anavyoeleza, ili kuwezesha maendeleo ya utamaduni wa Mwafrika ni muhimu kufufua johari hii ya jadi iliyofukiwa na kuhifadhi kwa ajili ya vizazi vipya. Nia ya utafiti huu vilevile ilikuwa kudhihirisha mbinu tofauti na kufanana kwa matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika kwa njia ya mwingiliano matini katika tungo za watunzi wa tamthilia Ebrahim Hussein, Said A. Mohamed na Emmanuel Mbogo, na katika vipindi vya ubunifu vya karibu ya miaka hamsini.

Utafiti huu ni tahakiki ya jinsi motifu ya sanaa za maonyesho ya jadi imechotwa na wasanii na kutumiwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ili kufanikisha dhamira za waandishi. Utafiti ulilenga kujibu swali, ni kwa jinsi gani sanaa za maonyesho ya Kiafrika zinajitokeza katika tamthilia ya Kiswahili kimuundo, kimtindo na kidhamira? Aidha, utafiti ulikusudia kujibu swali kuhusu ni vipi mbinu ya matumizi ya sanaa za maonyesho ya Kiafrika ya jadi ilivyotumika kushadidia ujenzi na uimarishaji wa fani na maudhui katika tamthilia ya Kiswahili.

Utafiti huu, vilevile, ulilenga kufafanua maendeleo na mabadiliko yoyote ya ubunifu na mtindo wa wasanii wa tamthilia ya Kiswahili kisanaa katika mapito wa wakati. Utafiti huu ulilinganisha tamthilia nne za Ebrahim Hussein, Said A. Mohamed na Emmanuel Mbogo zilizotungwa katika vipindi tofautitofauti ambavyo vinapishana kwa karibu miaka hamsini (1971 -2016) ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

Uchunguzi huu vilevile ulinakidi taswira mbalimbali zinazojengwa kupitia kwa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika zilizochotwa na kutumiwa kama motifu ya utunzi na uumbaji wa muundo na mtindo wa tamthilia ya Kiswahili. Kwa kufanya hivi, uhakiki huu pia ulikusudia kuchangia maarifa katika fani ya fasihi ya Kiswahili na fasihi kwa jumla. Utafiti wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika utachangia katika uhifadhi, uendelezaji na udumishaji wa utamaduni wa Kiafrika.

Tamthilia zilizochaguliwa kwa utafiti huu zimedhihirisha matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika kwa njia inayojirudiarudia kama motifu na mbinu ya kuwasilisha ujumbe katika Fasihi Andishi ya Kiswahili. Uhakiki wa tamthilia hizi ulichangia katika ufafanuzi na uelewaji wa sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika kwa jumla na zilivyotumiwa kama mbinu ya utunzi na mbinu ya

kuimarisha ujumi, muundo na dhamira za wasanii. Kutekeleza maazimio hayo, utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i. Watunzi wa tamthilia za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi,* na *Mashetani Wamerudi* wamechota na kutumia tanzu zipi za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia zao?

ii. Matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili yanaibua taswira na maana zipi kwa wasomaji wa tamthilia ya Kiswahili?

iii. Kuna maendeleo gani yaliyofikiwa kupitia kwa matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika mapito ya wakati?

**1.3 Malengo ya Utafiti**

Lengo muhimu la utafiti huu ni kutathmini mbinu za matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Ili kufikia maazimio yetu, utafiti huu ulizingatia malengo mahususi yafuatayo:

1. Kupambanua tanzu na namna sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika zilivyotumiwa na wasanii kama mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika kuimarisha ujumi na umbo la kazi zao.
2. Kuchanganua taswira na maana inayoibuliwa na tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.
3. Kufafanua maendeleo na nafasi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika mapito ya wakati.

## 1.4 Nadharia Tete

1. Sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika zimetumika Kimwingilianomatini kama mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.
2. Matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili huibua taswira na maana mahususi katika kazi zetu teule za fasihi.
3. Matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika ni motifu muhimu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili inayojirudiarudia na ambayo haibadiliki katika fasihi ya Kiswahili kama sehemu ya utamaduni wa Kiafrika.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Uchotaji na matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na tanzu nyingine za Fasihi Andishi za kisasa yamezua mijadala miongoni mwa wataalamu wengi. Utendaji na uwasilishaji wa sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika ulisababisha mgogoro mkubwa kiasi kwamba zilipigwa marufuku na wakoloni wakati wa ukoloni walioziona kama nyenzo ya kuendeleza uchawi pamoja na kuwa hali ya ushenzi iliyopinga maendeleo ya dini ya Kikristo wakati huo (Muhando, 1983 na Mlama, 1983). Uchunguzi wa ndani kuhusu uchotaji wa malighafi hii na matumizi ya sanaa za maonyesho ya kale katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili utachangia katika uelewaji na uendelezaji wa utamaduni wa Mwafrika na kuondoa kasumba hasi ya kikoloni ya kuuona utamaduni wa Mwafrika kuwa utamaduni wa kichawi na hali ya ushenzi. Utafiti huu utachunguza mchango wa tanzu za jadi za sanaa za maonyesho ya asili ya Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

Wamitila (k.h.j.) anafafanua kuwa matumizi ya matukio ya kitamaduni na tanzu za sanaa za maonyesho za jadi kama malighafi ya utunzi hayatokei tu katika muundo wa tamthilia bila kupangwa kimakusudi katika kiwango cha utunzi kwa nia mahususi ya kutaka kuendeleza suala fulani muhimu. Kwa misingi hii, utafiti huu ulikusudia kuchunguza nia ya watunzi wa tamthilia ya Kiswahili kuamua kutumia sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika kama malighafi na nyenzo ya kuwawezesha kutunga tamthilia zao na namna kunga hiyo inavyotumiwa katika kujenga umbo, taswira za kimaana na kuendeleza ujumi na maudhui katika tamthilia ya Kiswahili. Kupitia kwa uchunguzi huu, tulinuia vilevile kuongezea maarifa katika uhakiki na mbinu za utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na uelewaji na uendelezaji wa utamaduni wa Kiafrika.

Tangu kujinyakulia uhuru wa bendera kutoka kwa wakoloni, nchi za Afrika zimekuwa zikitafuta na kung'ang'ania kujinyakulia "uhuru wa utamaduni" wao (Senghor; 1996). Utafiti huu ulikusudia kutathmini mchango na msimamo wa watunzi wa tamthilia ya Kiswahili kupitia kwa matumizi yao ya tanzu asilia za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Mwafrika katika utunzi wa tamthilia zao ili kufikia uhuru wao wa kitamaduni.

Mulokozi (1983), P'Bitek (1973), Ngugi wa Thiong'o (1986) miongoni mwa wataalamu wengine wamehimiza na kutoa wito wa uchunguzi zaidi kufanywa kuhusu uhusiano uliopo baina ya Fasihi Simulizi ya Kiafrika hasa sanaa za maonyesho ya jadi na Fasihi Andishi hususan tamthilia na namna ukiukaji unavyofanywa kutoka kwa sanaa za maonyesho ya jadi na Fasihi Simulizi kwa jumla kwenda kwa Fasihi Andishi. Utafiti huu ni mwitikio wa wito wa Mulokozi kwa wataalamu wengine wa fasihi na lugha ya Kiswahili kuchunguza namna watunzi wa tamthilia ya Kiswahili

walivyochota maarifa kutoka utamaduni wa Kiafrika uliohifadhiwa katika tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho ya jadi.

Utafiti huu, vilevile, umechangia katika kupanua taaluma ya usomi kwa kuendeleza usomaji, uhakiki kwa misingi ya kinadharia, utunzi wa kisanifu na utamaduni wa Kiafrika na kuendeleza Fasihi Andishi kwa jumla. Kutokana na matokeo ya utafiti wetu ni matumaini yetu kuwa wasomaji wengine watachangamkia usomaji wa tamthilia zilizoandikwa kwa misingi ya tamaduni za Kiafrika zinazoendelezwa kupitia kwa sanaa za maonyesho. Aidha, utafiti huu unawatia changamoto wasomi wengine kufanya utafiti katika vipengele vya matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ambazo bado hazijashughulikiwa ili kukuza lugha ya Kiswahili na kuendeleza Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi kwa pamoja.

Sababu nyingine iliyohamasisha utafiti huu na uchaguzi wa mada hii, ni kuchangia katika uelewaji wa mbinu za matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili kama motifu inayojirudiarudia na mbinu ya kisanaa iliyotumiwa na watunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika kuumba na kukamilisha muundo wa tamthilia ya Kiswahili ili kuwasilisha dhamira na maudhui ya mwandishi.

Utafiti huu ulifaulu kudhihirisha taswira iliyojengwa na mtunzi katika tamthilia teule za Kiswahili kupitia kwa matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia hizo. Aidha, uchunguzi huu ulinuia na ulifanikiwa kudhihirisha kwamba sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika ni motifu ambayo inajirudiarudia Kimwingilianomatini na imetumika kimakusudi kama mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

**1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu ni mchango mkubwa kwa taaluma ya Fasihi Simulizi, fasihi linganishi na fasihi kwa jumla mbali na kuchangia katika kuendeleza na kudumisha utamaduni wa Kiafrika. Matokeo ya utafiti huu yatachangia katika uelewaji wa mbinu ya matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na uendelezaji na udumishaji wa utamaduni wa jadi wa Mwafrika.

Mbali na kupanua wigo wa marejeleo ya taaluma ya Fasihi Simulizi, kuingiza uhuru katika taaluma ya Fasihi Simulizi kwa kuifanyia utafiti, kujifunza utamaduni wa umma, kuelewa misimamo, itikadi na mahitaji ya utamaduni wa Kiafrika, utafiti huu vilevile utachangia kitaaluma katika kutoa tahakiki za kazi za sanaa mbalimbali. Hakuna jambo lolote litendekalo katika sayari yetu ambalo linajitenga kabisa na Fasihi Simulizi ambalo halijaguswa au halitaguswa na utanzu wa Fasihi Simulizi hasa sanaa za maonyesho ya jadi kutokana na utamaduni wa Kiafrika. Utafiti huu kwa jumla utawanufaisha wasomaji na wahakiki wa tamthilia ya Kiswahili katika kuelewa zaidi kuhusu mbinu ya kuchota na kutumia sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya Kiafrika katika kutunga na kuimarisha umbo na dhamira za watunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

Kupitia kwa matumizi ya nadharia ya Uhistoria Mpya na Mwingilianomatini katika uhakiki na uchunguzi wa mbinu ya matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili, matokeo ya utafiti huu vilevile yatachangia katika uelewaji wa mabadiliko na upekee wa muundo na mtindo wa watunzi Said A. Mohamed, Emmanuel Mbogo na Ebrahim Hussein katika kuibuka na fani na dhamira mahususi katika vipindi mbalimbali vya utunzi. Kwa kufanya hivi, utafiti huu umechangia katika uelewaji wa nyenzo na mbinu murua za kisanii zitakazowafaa

wasanii na wahakiki wa kazi za sanaa hasa katika kuchota na kutumia sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

**1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Kuna tamthilia nyingi ambazo zinadhihirisha matumizi ya masimulizi ya kingano, nyimbo, ngoma, majigambo, mafumbo, ushairi simulizi, semi na tanzu nyingine za jadi za sanaa za maonyesho pamoja na tamaduni za Kiafrika za pepo na Mashetani, pungwa, uganga, uchawi na miujiza katika utunzi wao. Hata hivyo, tamthilia ambazo zimechunguzwa zimechaguliwa kimakusudi ili kuwakilisha kazi nyingine za tamthilia ya Kiswahili. Vitabu vya tamthilia vilivyoteuliwa ni vile ambavyo vimeandikwa na waandishi Said A. Mohamed, Emmanuel Mbogo na Ebrahim Hussein ambavyo ni pamoja na vifuatavyo:

i) *Mashetani* (1971) kilichoandikwa na Ebrahim hussein

i) *Pungwa* (1988) kilichoandikwa na Said A. Mohamed

ii) *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1998) kilichoandikwa na Emmanuel Mbogo

iii) *Mashetani Wamerudi* (2016) kilichoandikwa na Said A. Mohamed

Kazi nyingine zozote ambazo zilikuwa na umuhimu kwa utafiti huu zilirejelewa kila ilipobidi. Aidha, tahakiki na majarida mengine ambayo yalikuwa na kazi ambazo zinahusiana na uchunguzi huu zilisomwa na kurejelewa katika kushadidia yale yaliyopatikana.

Tamthilia zilizoteuliwa zimechaguliwa kimakusudi kutumiwa katika utafiti huu kwa sababu kulingana na mapitio ya awali tuliyoyafanya ilithibitika kwamba ni miongoni mwa zile zinazodhihirisha matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Usawiri wao wa

sanaa za maonyesho ya jadi ulituwezesha kudhihirisha na kupambanua tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na kuchanganua taswira zilizozuliwa kupitia kwa matumizi ya aina hiyo. Matokeo ya uchunguzi huu yalidhihirisha kwamba tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika zinaweza kutumiwa kisanaa katika utunzi wa kazi za Fasihi Andishi ya Kiswahili kama nyenzo na mbinu ya utunzi katika kujenga na kuimarisha muundo na ujumi wa tamthilia ya Kiswahili mbali na kuendeleza dhamira za mtunzi.

Utafiti huu ulijifunga katika kuchunguza mbinu za matumizi ya tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika kimuundo, kimtindo na kimaudhui kwa ajili ya kubuni tamthilia mpya ya Kiswahili.  Watafiti walichunguza tanzu za jadi za sanaa za maonyesho za ngoma, nyimbo, majigambo, usimulizi wa kingano, mashairi simulizi, semi na tamaduni za Kiafrika za pungwa, uchawi, uganga na miujiza zilivyotumiwa sambamba na vipengele vyengine vya tamthilia ya ki-Aristotle ili kujenga na kuimarisha umbo zima la tamthilia mpya ya Kiswahili.

**1.8 Hitimisho**

Katika sura hii ya kwanza, tliueleza kuhusu suala la utafiti matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ambapo ilidhihirika kwamba kuna pengo linalofaa kuchunguzwa kuhusu nafasi ya tanzu hizo katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Utafiti huu ulikusudia kuonyesha kwamba tamthilia ya Kiswahili na Fasihi Andishi kwa jumla imechota vipengele vya sanaa za maonyesho ya jadi vya asili ya tamaduni za Kiafrika ambavyo ni sehemu ya Fasihi Simulizi na kuvitumia katika utunzi wa tamthilia andishi ya kisasa ya Kiswahili.

Sura hii, vilevile, imeshughulikia kwa undani, masuala ambayo yameuwekea utafiti huu misingi ya kisayansi. Watafiti waliyaeleza malengo matatu ya utafiti huu ambayo ni kupambanua namna tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika zilivyotumiwa na wasanii kama mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika kuimarisha ujumi na umbo la kazi zao. Pili, kuchanganua taswira na maana zinazoibuliwa na tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Tatu, kufafanua maendeleo na umuhimu wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika uliosahaulika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Masuala ya suala la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti pamoja na upeo wa utafiti huu pia yalishughulikiwa katika sura hii ya kwanza.

Sura inayofuata imefanya mapitio kuhusu yaliyoandikwa kuihusu mada ya uchunguzi pamoja na misingi ya nadharia zinazoongoza uchunguzi huu. Mapitio ya maandishi yalifanywa kupitia kwa mbinu ya uhakiki na yalituwezesha kubainisha pengo la maarifa na suala la utafiti huu. Nadharia ambazo zimejadiliwa ni zile za Uhistoria Mpya au Uyakinifu wa Kitamaduni iliyoasisiwa na mtaalamu wa kimarekani kwa jina Stephene Greenblatt. Nadharia nyingine ni ile ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na mtaalamu Julia Kristeva. Mihimili ya nadharia zote mbili imewekwa wazi na imeonyeshwa jinsi ilivyohusishwa na kuongoza utafiti wenyewe.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI KUHUSU MADA NA KIUNZI CHA KINADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza, tulishughulikia usuli wa suala la utafiti la sanaa za maonyesho ya jadi ambapo ilidhihirika kwamba kuna pengo lililofaa kutafitiwa kuhusu matumizi ya tanzu hizo katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Malengo matatu ya utafiti huu yaliibuka. Ilikisiwa kwamba sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika zimetumika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili kama mbinu ya utunzi na nyenzo ya kuzua taswira za kimaana. Aidha, kufafanua mbinu na taswira za matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika na taswira zinazojengwa na tanzu hizo ziliibuka kama sababu za kuchagua mada ya utafiti. Katika upeo wa utafiti huu, tamthilia nne za Kiswahili ambazo ni *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* ziliteuliwa katika utafiti huu. Katika sura hii ya pili tumefanya mapitio ya maandishi ya watafiti mbalimbali hasa waliyoyaandika kwa ujumla kuhusiana na suala letu la utafiti la matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika. Vilevile, tumefafanua nadharia za Uhistoria Mpya na Mwingilianomatini zilizoteuliwa kuongoza utafiti huu pamoja na kuoanisha malengo yetu matatu ya utafiti kimsingi na mihimili ya nadharia hizo.

## 2.1 Sanaa za Maonyesho ya Jadi na Tamaduni za Kiafrika

Sanaa za maonyesho ya Kiafrika ya jadi zimefanyiwa utafiti na wataalamu wengi kufikia sasa. Nyingi ya tafiti za mwanzo ziliongozwa na mtazamo wa ki-Aristotle ambao unasisitiza mipaka mahususi katika uainishaji wa tanzu za sanaa za maonyesho. Utafiti wa mwanzo wa kina katika miaka ya awali ya sabini uliochunguza sanaa za maonyesho ya Kiafrika na Fasihi Simulizi kwa jumla, uliongozwa na

mtaalamu Finnegan (1970) na mtaalamu wa Afrika Magharibi Okpewho (1985). Wote waliongozwa na mtazamo huo wa ki-Aristotle katika uchunguzi wao. Tafiti zaidi kuhusu sanaa za maonyesho na Fasihi Simulizi zimeongezeka baadaye katika miaka ya themanini, tisini na hivi sasa katika karne ya ishirini na moja.

Sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika kwa ujumla ni mada pana mno kuishughulikia kikamilifu. Wahakiki, wasanii na wataalamu mbalimbali wa fasihi tangu miaka ya sabini wameishughulikia kwa jinsi zinazotofautiana. Kutokana na mapitio ya fasihi za vipindi mbalimbali, ni dhahiri kwamba tangu enzi za Socrates na Plato wa Ugiriki sanaa za maonyesho zimetumika katika utunzi wa kazi za sanaa ili kujenga dhamira, maudhui, wahusika na mbinu za utunzi. Wasanii wa sasa wa Kiafrika vilevile wanaendeleza matumizi ya mbinu hii katika utunzi wa kazi zao. Matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho za jadi za asili ya Kiafrika katika utunzi wa kazi za Fasihi Andishi huumba maana mbalimbali ambazo zinaweza kufasiliwa kwa nji mbalimbali kwa wakati mmoja.

Wa Thiong'o (1972, 1981b) anaeleza kuwa yeye hurejelea sanaa za maonyesho na utamaduni wa Mwafrika katika riwaya zake ili kumwezesha kuhifadhi utamaduni na sifa za riwaya ya Kiafrika katika kazi zake. Aidha, Wa Thiong'o (1981a) anatambua kuwa Fasihi Andishi ya Kiafrika huchimbuka kutokana na tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiafrika zinazotetea utamaduni wa Mwafrika. Mbinu ya utunzi ya Ngugi wa Thiong'o ni nyenzo mwafaka ya Waafrika kuurejesha uhuru na utamaduni wa Mwafrika uliodunishwa na kubezwa na wakoloni kuwa wa kishenzi. Utafiti huu vilevile ulichunguza dhima na mbinu za matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho katika kutunga tamthilia ya Kiswahili katika kurejesha na kuupa hadhi utamaduni wa Kiafrika.

Obiechina (1975), akieleza kuhusu uhusiano kati ya sanaa za maonyesho ya Kiafrika na Fasihi Andishi, anahimiza watunzi na wahakiki kujitumbukiza katika taaluma hii iliyopuuzwa. Mtaalamu huyu anaona kuwa mbinu ya uchotaji wa tanzu za sanaa za maonyesho katika utunzi wa tamthilia andishi unafaidi na kurutubisha Fasihi Andishi katika kuleta vionjo vya kiasili na kuimarisha fani na maudhui ya kazi hizo. Obiechina (k.h.j.) vilevile alitambua kuwa waandishi wengi wa Afrika Magharibi pamoja  na Chinua Achebe, Wole Soyinka, Tatuola na Clark miongoni mwa wengine wamechota na kutumia ishara za sanaa za maonyesho ya kale ya Kiafrika na kuzitumia katika ujenzi wa fani na maudhui katika kazi zao za sanaa. Majina ya kimajazi ya wahusika katika kazi nyingi za Afrika Magharibi vilevile yana maana zinazoibushwa na tanzu za sanaa za maonyesho. Utafiti huu vilevile ulichunguza uchotaji na matumizi ya kimajazi ya majina ya wahusika katika mbinu ya Kimwingilianomatini na utunzi wa utanzu wa tamthilia andishi ya kisasa.

Hadithi za makafara ya Binadamu, vilevile, zimepewa nafasi kubwa katika Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi ya Kiafrika. Head (1977) kwa mfano, anasimulia tamaduni katili katika kisa chake “Looking for the Rain God” ambapo watoto wasichana Neo na Boseyong wanauliwa katika ibada za kimatambiko ya kijamii ya jadi ya kuituliza miungu ya mvua ili kukomesha kiangazi na kuleta mvua. Watoto hawa wanaonyeshwa kuwa wenye uvumilivu, ucheshi, ubunifu kwa jinsi wanavyowaiga wazazi wao kwa kuwaundia mifano ya vibonzo, na wasio wasumbufu kwa wazazi hasa katika wakati huo mgumu wa njaa na kiangazi. Licha ya kutoelewa chochote kuhusu miungu, chanzo na kisababishi cha matatizo ya jamii yao, jamii kupitia kwa mhusika mkuu Mokgobja anayeshikilia tamaduni za makafara ya watu, inawatoa watoto hao kuuawa ili kuwafanya matambiko ya kutuliza kero la miungu wa mvua kuzuia mvua isinyeshe. Watoto hawa wanafanyika kuwa wahusika wa matoleo ya

kimatambiko ambayo wakati wa kuyafanya yaliambatana na utendaji wa maonyesho yenye usanii mkubwa. Kiai na Munungi (1998) katika kufafanua hadithi hii wanatueleza kwamba utulivu wa kitoto wa watoto hao unazua huruma kwetu na kutufanya tuwapende wakati wanapofanywa viumbe dhaifu vya kunyongwa kwa ajili ya matambiko. Utafiti huu vilevile ulichunguza dhima na mbinu ya matumizi ya maonyesho ya sanaa za matambiko ya aina hii katika kujenga tamthilia ya Kiswahili.

Seitei (1980) amechunguza na kuandika kuhusu umuhimu wa utanzu wa ngano za kijadi. Katika kazi yake, *See so that we may see: Performance and interpretation of traditional tales from Tanzani*a, Seitei vilevile ameangazia namna ya usimulizi, utendaji na uelewaji wa ngano za kijadi za asili ya Tanzania bara kupitia kwa uhakiki na tafsiri inayofaa. Utafiti wake unachunguza utanzu wa jadi wa ngano wa Fasihi Simulizi tofauti na utafiti wetu ambao unachunguza tanzu za Sanaa za maonyesho ya jadi kwa jumla ambazo zimetumika kimakusudi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Utafiti wetu vilevile utachunguza maonyesho yaliyochotwa kutoka kwa utanzu wa ngano kwa ajili ya matumizi yake katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika mapito ya wakati kihistoria.

Wole Soyinka katika tamthilia zake za *The strong breed* (1973) na *Death and the King's Horsemen* anaandikia kuhusu makafara ya Binadamu ambao wanafanywa kuwa matoleo ya sadaka kwa miungu wa jamii kwa ajili ya kuzuia maafa na kuufanya ulimwengu kutokuwa na dhoruba na vimbwanga bali kuweka utaratibu na kuleta baraka kwa wanajamii. Elesin Oba katika *Death and the King's Horsemen* anaonyeshwa kama mhusika ambaye kizazi chake kimeteuliwa na miungu ili kufanywa sadaka kwa miungu. Katika jamii hii ya Yoruba, baba yake Oba alitolewa kama kafara kwa ajili ya jamii yake kwa kufanywa tambiko kwa miungu, Elesin Oba naye atatolewa kafara kwa miungu na kabla ya matambiko hayo atapewa wanawali

mabikira ambao atajamiiana na kuzaa nao. Mtoto mvulana wa kwanza atakayezaliwa na Elesin Oba kwa mabikira hawa, pia atatolewa kama kafara katika matambiko ya kuwatuliza miungu na utaratibu huo utaendelea hivyo katika vizazi vya baadaye. Mhakiki Eldred Durosini anaeleza ya kwamba ni wajibu na mwitikio wa damu inayotiririka katika mishipa ya ukoo wao kuchukua jukumu kubwa la kuzuia maafa ambayo yangeipiga jamii yao ya Wayoruba. Kazi hizi za Wole Soyinka zinaakisi tanzia ya wafalme wa kabila la Yoruba katika nchi ya Nageria na matambiko yanayoandama na matanga ya wafalme hao wakati wa kabla uhuru. Tofauti na tamthilia hizo za kitanzia, uchunguzi wetu uliangazia matumizi ya tanzu za sanaa ya maonyesho zinazoambatana na matambiko hayo katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na jinsi tanzu hizi zinavyoingiliana na kuathiriana katika mfumo wa Mwingilianomatini.

Alembi (2002) amechunguza taswira na athari za mitazamo ya kijamii na kitamaduni kuhusu asili na maana ya kifo miongoni mwa jamii yake ya Wanyore kupitia kwa utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi wa nyimbo za kuomboleza (maghani ya maziko) wakati wa matanga. Uchunguzi wake uliegemezwa katika nadharia ya ushairi wa kiethinografia (ethinopoetics) iliyoasisiwa na mtaalamu Anttonen (1994) ambayo hulenga mtindo wa ujumi na ushairi katika utanzu wa usemi wa sanaa za maonyesho ya jadi. Uchunguzi wake uliwekwa katika misingi ya pragmatiki, halia, isimujamii, ethinografia ya uzungumzi na sanaa ya utendaji katika Fasihi Simulizi ya Kimarekani. Tofauti na utafiti wake unaochunguza nyimbo za kuomboleza pekee, utafiti wetu ulichunguza mbinu walizozitumia watunzi katika uchotaji wao wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Utafiti huu hatahivyo ulichunguza taswira zilizoibuliwa kupitia kwa matumizi ya utanzu huu wa maghani

ya kuomboleza katika utunzi wa kazi za sanaa za sasa na athari ya matumizi ya mbinu ya Mwingilianomatini katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

Ndege (2003) naye ametafiti kuhusu utanzu wa ngano miongoni mwa jamii ya Wameru. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kwamba ngano za Wameru huwa na muundo maalumu wa sanaa za maonyesho ambao huzifanya kuwa na uamilifu maalumu kwa jamii hiyo. Utafiti huu umechunguza namna ngano kama utanzu wa jadi wa sanaa za maonyesho ya Kiafrika ulivyotumiwa kisanaa na watunzi katika kukamilisha umbo la tamthilia ya sasa ya Kiswahili. Tofauti na utafiti wa Ndege uliochunguza uamilifu wa ngano za kabila la Wameru katika tamthilia kwa jamii hiyo ya Wameru, utafiti wetu ulichunguza nafasi ya masimulizi ya kingano na tanzu mbalimbali za ngano za kijadi kama utanzu wa sanaa za maonyesho katika kujenga na kuimarisha umbo na taswira katika tamthilia ya Kiswahili.

Chacha (1997) ametafiti kuhusu majigambo ya kabila la Wakuria na kupambanua kuwa majigambo hutumiwa na Wakuria katika miktadha mbalimbali kwa lengo la kujisimulia na kutangaza sifa za mhusika mwenyewe mbele ya hadhira. Mtafiti huyu alitumia nadharia ya Semiotiki ambayo ilimwezesha kung’amua maana ya ishara na maumbo ya lugha yaliyotumiwa na fanani katika kujisifu. Utambuzi wa maana katika majigambo ya Wakuria uliwezeshwa na miktadha maalumu ya utamaduni wa Wakuria. Utafiti wa Chacha ambao ni wa misingi ya kiisimu uliwezesha utafiti huu kuelewa umuhimu na matumizi ya utanzu wa majigambo kama utanzu wa sanaa za maonyesho na mbinu ya Mwingilianomatini katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

Matti (1993) naye alichunguza sherehe ya tohara miongoni mwa jamii ya Watharaka. Tohara ni mfano wa sherehe za kitamaduni za Kiafrika zinazoandamana na sanaa za maonyesho. Matti alichunguza tohara kwa dhamira ya kudhihirisha kuwa sanaa za

maonyesho ya jadi zilikuwa na sifa kamili za kidrama. Kupitia kwa uchunguzi wake, ilidhihirika kwamba utendaji wa sanaa za maonyesho katika sherehe za tohara ya jamii ya Watharaka uliwawezesha kuendeleza na kuhifadhi utamaduni wao. Utafiti huu ulichunguza jinsi sanaa za maonyesho zilizoandamana na miviga ya tohara na miviga ya aina nyingine zilivyoweza kuchangia katika utunzi na uimarishaji wa fani na maudhui katika tamthilia ya Kiswahili.

Ndungo (1997) alichunguza kuhusu usawiri wa mwanamke miongoni mwa jamii za Waswahili na Wakikuyu kupitia kwa matumizi yao ya methali. Nadharia iliyoongoza utafiti wake ni ile ya Mtazamo-Kike. Matokeo ya utafiti huo wa Ndungo yalidhihirisha kuwa methali hutumiwa na jamii kuwasawiri wanawake kama viumbe duni wakilinganishwa na wanaume. Aidha, utafiti huo uling’amua kwamba Fasihi Simulizi ni chombo muhimu kinachotumiwa na jamii husika katika kuhifadhi mila na desturi zake. Utafiti wetu utashughulikia matumizi na mchango wa methali kama utanzu wa sanaa za maonyesho katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na uimarishaji wa fani na maudhui katika tamthilia.

Marete (1998) katika tasnifu yake ya ujadi katika tamthilia mbili za Emmanuel Mbogo alichunguza tamthilia za *Ngoma ya Ng’wanamalundi* na *Morani* kwa lengo la kuchanganua na kuainisha uamilifu wa ujadi katika tamthilia ya Kiswahili. Ili kuchunguza ujadi katika tamthilia ya Kiswahili, Marete aliangazia vipengele vya utambaji hadithi, uchezaji wa nyimbo na ngoma, utongoaji wa majigambo, urithi wa tamathali za lugha za kijadi, matumizi ya uchawi na imani za kishirikina na asasi zingine za kijadi. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya Sanaa ya Ki-Marx iliyosherehezewa zaidi na Lenin. Utafiti wetu ni wa uchunguzi wa Mwingilianomatini kati ya sanaa za maonyesho ya Kiafrika ya kale na tamthilia ya Kiswahili na mbinu iliyotumika katika uchotaji wa tanzu za sanaa za maonyesho katika kujenga na

kuimarisha tamthilia ya Kiswahili. Nadharia iliyoongoza uchunguzi huu ni ile ya Uhistoria Mpya au Uyakinifu wa Kitamaduni iliyoasisiwa na Mmarekani kwa jina Stephen Greenblatt pamoja na nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na mwananadharia wa Kifaransa kwa jina Julia Kristeva.

## 2.2 Mwingilianotanzu

Simiyu (2015) ameshughulikia mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika hasa katika miviga ya "Embalu" na "Mwaka kogwa" miongoni mwa jamii za Waswahili na Wabukusu wa Magharibi mwa Kenya. Utafiti wake ulilenga kuchunguza nafasi ya fanani, hadhira na muktadha wa utendaji katika ujenzi wa mwingiliano na kupambanua ni kwa namna gani viviga katika miviga ya "Embalu na Mwaka kogwa" miongoni mwa jamii za Wabukusu na Waswahili inaweza kuelekeza uteuzi na utolewaji wa tanzu maalumu katika ujenzi wa mwingilianotanzu. Simiyu vilevile ameshughulikia historia ya uainishaji wa tanzu za Fasihi Simulizi na nadharia ya Mwingilianotanzu. Aidha, Simiyu alieleza umuhimu wa kuainisha tanzu za fasihi ya Kiafrika kwa misingi ya mwingiliano wake kiutanzu badala ya kuzishughulikia kipekee kwa kuitenga kimpaka. Utafiti wetu unakubaliana na wake pale tunapoonyesha kuwa utanzu mmoja wa sanaa za maonyesho ya jadi na Fasihi Simulizi kwa jumla unaweza kutumia tanzu nyingine katika kujenga fani na dhamira zake.

Murimi (2016) amehakiki mwingilianotanzu katika muziki wa Taarabu wa kitengo cha Modern Taarabu mipasho. Utafiti wake ulilenga kudhihirisha taswira mbalimbali za mwingilianotanzu zinazojitokeza katika nyimbo za taarabu mipasho, kuchanganua miktadha mbalimbali ya mwingilianotanzu katika muziki wa taarabu mipasho na kutathmini dhima ya mwingilianotanzu katika muziki wa taarabu ya aina ya mipasho. Utafiti wake kama wetu uliongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa

na Julia Kristeva katika miaka ya sitini baada ya kuiibua upya kutokana na nadharia ya Usemezano iliyoasisiwa na Mikhail Bakhtini. Aidha, Murimi aliongozwa na nadharia ya Umuundo ili kutoa mwelekeo zaidi kuhusu uainishaji wa tanzu za Fasihi Simulizi tofauti na nadharia yetu ya Uhistoria Mpya iliyotuwezesha kuainisha matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika muktadha wa kihistoria.

Macha (2013) alichunguza mtindo na Mwingilianomatini katika fani ya tendi. Malengo ya utafiti wake yalikuwa kuthibitisha ikiwa utanzu wa tendi za Kiswahili huwa na Mwingilianomatini na kubainisha vipengele vinavyoingiliana katika utanzu wa utendi pamoja na dhamira zake. Utafiti wetu umechunguza matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili tofauti na utafiti wa Macha ulioshughulikia Mwingilianomatini katika utanzu wa utendi wa lugha ya Kiswahili. Utafiti wake hata hivyo ulitufaa katika kudhihirisha mbinu ya Mwingilianomatini katika utunzi wa tamthilia andishi ya Kiswahili.

Kenguru (2013) amehakiki Mwingilianomatini katika Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi akizingatia historia na mazingira, wahusika na tamathali za usemi. Utafiti wetu kama utafiti wake umeongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini. Hata hivyo utafiti wetu unajikita katika kuainisha matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili bali si utathmini wa Kimwingilianomatini wa historia, mazingira, wahusika na tamathali za usemi kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. Jukumu letu ni kuchunguza mbinu, taswira na umuhimu wa matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ambayo ni fani ya Fasihi Simulizi katika kujenga tamthilia ya Kiswahili ambayo ni Fasihi Andishi tofauti na tathmini ya vipengele vya historia, mazingira, wahusika na tamathali za usemi vinavyojenga Mwingilianomatini katika tamthilia.

### 2.3 Misingi ya Kinadharia

Uchotaji na matumizi ya motifu ya sanaa za maonyesho ya jadi ni dhana ambayo inadhihirika katika kazi za sanaa za jamii zote ulimwenguni na katika vizazi na ustaarabu wa nyakati mbalimbali (Wellek na Warren, 1949; Leech na Short 1981 na Wafula 1992). Ili kutosheleza mahitaji ya utafiti huu, ilitubainikia ya kwamba nadharia za Uhistoria Mpya au Uyakinifu wa Kitamaduni iliyoasisiwa na mwananadharia kutoka Marekani, Stephen Greenblatt, na nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na Julia Kristeva zilitumiwa kuongoza majaribio ya uchunguzi wetu.

#### 2.3.1 Nadharia ya Uhistoria Mpya

Uhistoria Mpya au Uyakinifu wa kitamaduni ni nadharia ya uhakiki wa fasihi ambayo matumizi yake yalisambaa katika miaka ya arobaini. Wafuasi wa nadharia ya Uhistoria Mpya kulingana na Wamitila (2002) wanaitambua nafasi inayochukuliwa na muktadha wa kihistoria katika usomaji wa kazi za fasihi. Nadharia ya Uhistoria Mpya hutekeleza utunzi au uhakiki wa kazi za sanaa kwa kuleta pamoja mikabala mbalimbali ya kihakiki. Mihimili mahususi ya nadharia ya Uhistoria Mpya ni:

i) Kila tukio la kielezi au kisimulizi hutegemezwa kwenye hali changamano ya matukio ya kiyakinifu.

ii) Tukio lolote la kufichua, kuhakiki, kukosoa au kupinga huishia kuzitumia mbinu inazozipinga. Hivyo tukio hili huweza kutumbukia katika hali inayotaka kufichua au kukosoa.

iii) Kazi za kifasihi na zisizo za kifasihi huingiliana kiMzunguko.

iv) Hakuna usemi wa kibunifu au kinyaraka unaoweza kuelekeza kwenye ukweli usiobadilika au unaoelekeza hali ya Binadamu isiyoweza kubadilishwa.

v) Mtindo wa kihakiki na lugha inayokifu kuueleza utamaduni unaopatikana katika jamii ya kibepari huhusika katika uchumi wa kibepari unaopendelea matajiri.

vi) Katika mfumo wa uhalisia, ujumbe na usawiri wa kazi ya sanaa unazingatiwa badala ya kuzingatia muundo wake. Hivyo dunia huwasilishwa kama mahali penye machukizo, umaskini, mazingaombwe, usiiri (vijisababu vya kutofanya), ugandamizaji, mateso na kuchanganyikiwa.

Wafuasi wa nadharia ya Uhistoria Mpya hueleza ya kwamba kazi za kifasihi ni matokeo ya uhusiano changamano wa Kimwingilianomatini wala si kazi zinazotokana na ubunifu wa mwandishi peke yake. Kulingana na wahakiki hawa Mwingilianomatini uliopo unapatikana kwa kuiangalia jamii pamoja na utamaduni wake wala si lazima kwa mhakiki kujifunga kwenye lugha kama wanavyosema wataalamu Barthes na Derrida (1977). Hivyo katika mazingira haya, ni kosa la kihakiki kuitenga matini ya kifasihi au kazi ya kifasihi na muktadha wa kijamii kwa kuwa maingiliano kati ya muktadha huo na kazi ni muhimu katika kuipa sura na uhai kazi inayohusika. Uhakiki katika mazingira haya hujengewa nguzo na utamaduni na muktadha wa kijamii. Mhakiki hana budi kulizingatia suala hili katika uhakiki wake.

Dhana muhimu ya nadharia ya Uhistoria Mpya ni usukaji. Hapa matukio, wahusika na matendo yanayochotwa kutoka kwa jamii na mengine ya kihistoria huchukuliwa na kufanywa sehemu ya msuko wa hadithi au kazi ya fasihi. Mtindo unaotumiwa katika usukaji wa visa katika kazi ya sanaa unastahili uwe umefichika. Dhana nyingine inayohusishwa na nadharia hii ni ya mzunguko au mabadilishano. Dhana hii hurejelea

mageuzi au matukio ya maana za itikadi au vibuniwa vya kitamaduni ambavyo hutokea katika kazi ya kisanaa moja kwenda kwa nyingine kwa mabadilishano. Hivyo kazi za kifasihi na zile ambazo si za kifasihi huingiliana kwa Mzunguko.

Mihimili ya nadharia ya Uhistoria Mpya inashabihiana na maoni yetu kuwa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika yametumiwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Nadharia ya Uhistoria Mpya iliyotumiwa katika utafiti huu, ilitusaidia kudhihirisha kuwa sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya utamaduni wa Kiafrika zimeweza kutumiwa kimuundo na kimtindo katika sanaa ili kujenga na kuimarisha maana ya kitaswira katika tamthilia za Kiswahili. Aidha, ilidhihirika ya kwamba matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho katika utunzi wa tamthilia na kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili ni sehemu ya utamaduni ambao umekuwepo katika jamii mbalimbali ulimwenguni tangu jadi na huchotwa tu na watunzi katika vipindi mbalimbali katika utunzi wao. Uchotaji wa sanaa za maonyesho ya jadi kwa ajili ya utunzi wa kazi za fasihi umerudiwarudiwa katika kazi nyingi na kwa vipindi virefu katika muktadha wa kihistoria. Uchotaji wa tanzu za sanaa za maonyesho katika utunzi wa tamthilia hushadidia katika kufafanua uhalisia wa maisha ya binadamu kama yalivyo na kuendeleza uhifadhi wa utamaduni wa Mwafrika.

### 2.3.2 Mwingilianomatini

Utafiti huu, vilevile, uliongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini. Nadharia ya Mwingilianomatini imejadiliwa na Kristeva (1980), Allen (2000) na Lemaster (2012). Kristeva (1980), anaeleza kuwa dhana ya Mwingilianomatini inahusu kuathiriana, kuhusiana na kutegemeana kwa kazi za fasihi ambapo matini za kifasihi huingiliana kwa njia ya kuchangiziana fani na matini zenye maudhui mbalimbali ili kukamilishana. Kulingana na Kristeva, si rahisi kuzungumzia uasili au upekee wa

kazi ya fasihi kwani kazi moja huwa imetokana na kazi nyingine za fasihi zilizotangulia au zilizopo. Kimsingi, kazi ya sanaa si zao la mwandishi mmoja bali ni zao la jinsi matini hiyo huhusiana na matini nyingine na miundo ya lugha yenyewe. Mbinu ya Mwingilianomatini husisitiza kuwa matini zote za kisanaa zaweza kuchukuliwa kuwa kama matini moja kuu ambazo zinajibizana kimuundo na kimaana.

Allen (2000) anafafanua Mwingilianomatini kama namna ya kuhusiana na kutegemeana kwa kazi za fasihi. Lamaster (2012) anaongezea kuwa Mwingilianomatini katika fasihi ni pale ambapo kazi moja ya fasihi inarejelea kazi nyingine ya fasihi kwa mujibu wa visa na matukio, wahusika na usimuliaji na matini mbalimbali za kifasihi kama wimbo, hadithi za kitamaduni, filamu, maonyesho ya televisheni na mawasilisho mengine ya vyombo vya habari kutumiwa tena ndani ya kazi nyingine za fasihi.

Wamitila (2003, 2008) anaeleza Mwingilianomatini kama namna ya kuhusiana kwa kazi moja ya fasihi na nyingine iliyoitangulia katika muundo, dhamira, wahusika na mtindo. Mwingilianomatini ni mtazamo uliojengwa kwa misingi kuwa matini ya kisanaa si zao la mwandishi mmoja bali ni zao la jinsi matini hiyo huhusiana na matini nyingine na miundo ya lugha yenyewe. Mtazamo huu husisitiza kuwa matini zote za kisanaa zaweza kuchukuliwa kama matini moja kuu ambazo hujibizana; kila moja ikisemezana na nyingine kwenye usemezano uliotanuliwa (Plotell na Charney, 1978). Matini zinazoingiliana huhusiana kwa njia moja au nyingine na matini zenyewe hutegemeana ili kuzalisha maana. Mihimili ya nadharia ya Mwingilianomatini hujumuisha:

i) Matini yoyote ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingi tangulizi.

ii) Kazi za kifasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali zilizowekwa na kazi tangulizi za kifasihi ambapo taswira za maisha ya kawaida na uhusiano wa kimaana huunganishwa na kubadilishwa.

iii) Matini moja hufafanua usomekaji wa mkusanyiko wa matini zote za kongoo moja ambapo matini tangulizi hufyonzwa na kujibiwa na matini mpya

iv) Matini za kifasihi huwa zimechota, kugeuza, kuiga kwa namna ya kubeza au kurejelea kwa njia moja au nyingine matini nyingine.

v) Kila usomaji wa matini huwa ni kijalizo cha matini tangulizi na hivyo basi hugeuzwa kwa kiwango. Kwa jinsi hii, kauli inayonukuliwa hubadilika na kuelezea upya kauli asili kwa kuiambatanisha na muktadha mwingine wa kiisimu na kijamii.

Mwingilianomatini hurejelea matumizi ya utanzu mmoja wa fasihi katika kujenga umbo au kuwasilishia utanzu mwingine, kwa mfano wimbo ndani ya ngano au hadithi ndani ya hadithi (Senkoro 2011). Mwingilianomatini, vilevile, ni ule uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi nyingine ya fasihi. Hivyo matumizi ya nyimbo, barua, ngoma, masimulizi ya hadithi, misemo na nahau, majibizano, vichekesho na picha ndani ya kazi nyingine za fasihi ni muundo wa Mwingilianomatini.

Kuingiliana na kuathiriana kwa kazi za fasihi kulitupelekea kusaili ni kwa namna gani mwandishi mmoja, wawili au zaidi wa tamthilia ya Kiswahili wameweza kuathiriana na kuwa na uwiano wa kiubunifu katika kazi zao. Hivyo, watafiti wa kazi hii walidhamiria kubaini, ni kwa namna gani mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kudhihirisha mfanano na mabadiliko ya kiubunifu katika utunzi wake kiwakati na kimuktadha katika ujenzi wa vipengele vya taswira ya taashira na dhamira za mtunzi, muundo na mtindo katika kazi zake. Aidha, tunasaili ni kwa namna gani mtunzi

ametumia fani ya sanaa za maonyesho ya jadi katika kujenga na kuendeleza fani na maudhui katika kazi za mwanzo ikilinganishwa na kazi zake nyingine za sanaa za baadaye au za watunzi wengine. Je, kuna ushikamano wa matini moja na nyingine katika kuibua dhamira za mtunzi? Je, mtunzi ametumia vipi fani ya sanaa za maonyesho ya jadi katika vipindi mbalimbali vya kazi yake katika kuibua taswira mbalimbali na kuimarisha umbo la tamthilia yake?

Fafanuzi za wataalamu mbalimbali zinadhihirisha aina mbili za Mwingilianomatini. Kwanza, Mwingilianomatini kuwa namna ya kuathiriana kwa waandishi kupitia kwa kazi zao za fasihi katika vipengele mbalimbali kama jina la kitabu, wahusika, visa na matukio, muundo, usimulizi, mtindo na matumizi ya lugha. Pili, ni kuhusiana, kuathiriana, kuingiliana na kujengana kwa matini mbalimbali za fasihi katika kazi moja ya fasihi. Hivyo vipengele vya sanaa za maonyesho ya jadi kama nyimbo, ngoma, semi, hadithi, ndoto, methali, nahau, hotuba na vingine hujidhihirisha katika kazi moja ya fasihi. Utafiti huu umezingatia aina zote za Mwingilianomatini.

Wataalamu mbalimbali hueleza kwamba matini za kifasihi huhusiana kwa njia moja au nyingine, jambo ambalo huifanya kila matini kukisiwa kuwa na mwingiliano na nyingine (Kristeva 1966, 1981, 1986). Ingawa uhusiano huu hukisiwa kuwa katika tanzu zote za fasihi, utanzu wa riwaya ndio ambao umehakikiwa zaidi kwa misingi ya nadharia ya Mwingilianomatini huku tanzu nyingine kama tamthilia zikikosa kushughulikiwa kwa undani. Ufafanuzi huu wa matumizi ya sanaa za maonyesho katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili, ulitupelekea kuona pengo na kuchunguza ni kwa namna gani kazi za fasihi zinaweza kuathiriana, kuingiliana na kuimarishana kimuundo, kidhamira na kifani?

Kazi hii iliongozwa na maswali yafuatayo:

i) Watunzi wa tamthilia za *Mashetani* (1972), *Pungwa* (1988), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1999) na *Mashetani Wamerudi* (2016) wanadhihirisha mbinu zipi katika matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia zao?
ii) Je, kunao mshikamano wa matini moja na nyingine katika kuibua taswira za kimaana katika tamthilia teule za Kiswahili?
iii) Je, mbinu za utunzi walizozitumia waandishi wa tamthilia ya Kiswahili katika karibu miaka hamsini iliyopita, zimekuwa na maendeleo na mabadiliko yapi katika utunzi wa tamthilia teule kufikia sasa?

Maswali haya yalitusababishia shauku iliyotufanya kutaka kusaili uhusiano ulioko katika kazi za Ebrahim Hussein, Emmanuel Mbogo na Said A. Mohamed na tanzu nyingine za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika na mbinu za utunzi wa tamthilia za watunzi hao katika mapito ya wakati wa karibu miaka hamsini. Aidha, tulinuia kudhihirisha namna tanzu za jadi za sanaa za maonyesho zilivyotumiwa kisanaa katika kujenga taswira na umbo zima la tamthilia teule za Kiswahili na jinsi Mwingilianomatini ulivyojitokeza katika kazi za watunzi hao kama mbinu ya utunzi.

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia tulizoziteua kimakusudi za *Mashetani*, *Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* ambazo zimebuniwa katika vipindi mbalimbali vinavyopishana kwa takribani miaka hamsini. Utafiti huu ulifanywa kwa misingi ya nadharia mbili tofauti ambazo ni nadharia ya Uhistoria Mpya iliyotuwezesha kubaini matukio muhimu yaliyoshughulikiwa na watunzi kwa mkabala wa kihistoria. Aidha, utafiti huu uliongozwa na nadharia ya

Mwingilianomatini iliyotuwezesha kubaini namna watunzi walivyoathiriana katika utunzi wa tamthilia zao katika kipindi cha kihistoria cha karibu miaka hamsini.

### 2.4 Pengo la Maarifa

Tafiti nyingi zimefanywa hasa kuhusu vipengele vya uhusika, fani na maudhui katika kazi mbalimbali za tamthilia. Hata hivyo, hatujasoma kazi zinazodhihirisha ulinganifu wa kazi za watunzi tofautitofauti ili kudhihirisha mbinu za matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na jinsi watunzi huathiriana na kuingiliana katika mbinu zao za utunzi. Tamthilia zilizohakikiwa zinatengana kwa karibu miaka hamsini (miongo mitano): *Mashetani* (1971), *Pungw*a (1988), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1998) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Uchunguzi wa kazi hizi utatuwezesha kubaini jinsi watunzi hao walivyofumbata mbinu zao za utunzi kwa kutumia sanaa za maonyesho na jinsi walivyofumbata mbinu ya Mwingilianomatini. Ulinganisho wa matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho na mbinu ya Mwingilianomatini utatuwezesha kubaini na kudhihirisha mabadiliko yoyote ya kiubunifu katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na kuendeleza uelewaji wa jinsi mbinu hiyo ilivyotumiwa katika kuendeleza dhamira za mtunzi. Kwa njia hii, utafiti huu unakusudia kuziba pengo la mbinu faafu zinazofaa kutumika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Aidha, utafiti huu utachangia katika kuibusha mbinu zinazofaa katika uhifadhi wa tamaduni na tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya Kiafrika.

### 2.5 Hitimisho

Katika sura hii, tumepitia maandishi ya wataalamu mbalimbali waliyoyaandika kuhusu mada yetu ya matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Ilibainika kwamba, matumizi ya tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika ni mbinu ambayo

inadhihirika katika kazi za sanaa za jamii zote ulimwenguni na katika vizazi na ustaarabu wa nyakati mbalimbali.

Katika sura ya pili vilevile, tulishughulikia kiunzi cha kinadharia kilichoongoza utafiti huu. Ilibainika kwamba utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili mtawalia ambazo ni nadharia ya Uhistoria Mpya iliyoasisiwa na mtaalamu na mwananadharia kutoka Marekani ambaye anaitwa Stephen Greenblatt na nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na mtaalamu wa Kifaransa kwa jina Julia Kristeva (1980) katika miaka ya sitini. Hivyo, watafiti walikusudia kubainisha kwamba tamthilia ya Kiswahili na fasihi yenye utamaduni wa Kiafrika kwa jumla imechota vipengele vya tanzu za sanaa za maonyesho ya asili ya Kiafrika na kuvitumia katika utunzi wa tamthilia andishi ya Kiswahili.

Katika sura inayofuata tumeshughulikia suala zima la muundo wa utafiti, mbinu tulizozitumia katika kutekeleza utafiti, mahali pa kufanyia utafiti, sampuli na mbinu zausampulishaji, mbinu za ukusanya data iliyotumiwa katika uandishi wa tasnifu hii, vifaa vya kukusanyia data, uchanganuzi wa data iliyokusanywa na mbinu za uwasilishaji wa data hiyo katika mchakato mzima wa ukusanyaji na uandishi wa tasnifu hii.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia, tulifanya mapitio ya maandishi mbalimbali kuhusu mada yetu ya utafiti yaliyotuwezesha kubainisha pengo la maarifa lililofaa kujazwa. Aidha, katika sura iliyotangulia tuliweza kufafanua misingi ya nadharia zilizoongoza utafiti wetu. Katika sura hii ya tatu tumeshughulikia mbinu ambazo watafiti walizitumia katika kukusanya, kuainisha, kuchanganua na kuwasilisha matokeo ya utafiti huu. Kimsingi, utafiti huu ulikuwa wa ndani na nje ya maktaba. Hivyo, sura hii imeanza kwa kufafanua mahali pa kufanyia utafiti wetu na muundo wa utafiti huu ambao kimsingi ndio msingi mkuu wa tasnifu hii. Njia na vifaa vya kukusanyia data pamoja na uthabiti wa data ni masuala ambayo yameshughulikiwa hapa. Sura hii vilevile imeeleza mbinu zilizotumiwa kuchambua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti kwa kuongozwa na mkabala wa kifasihi.

## 3.1 Muundo wa Utafiti

Muundo uliofaa utafiti wa aina hii ni wa aina ya kifasili na kimaelezo. Hughes (1989), Marriams (1998) na Bryman (2001) wanaeleza utafiti wa kimaelezo kuwa bora katika kuwasilisha maelezo mengi na ya kina hasa kuhusiana na asili ya jambo fulani na habari kwa jumla. Utafiti wa aina hii ulifaa kwa sababu utafiti wa kimaelezo hutoa maelezo halisi ya jinsi jambo lilivyofanyika na kupata taarifa za tafiti za Fasihi Simulizi za Kiafrika ambazo huwasilishwa kwa njia ya mdomo mbali na kutazama utendaji wa wahusika.

Data iliyokusanywa wakati wa utafiti huu ilikuwa ya aina ya kithamano wala si ya kitakwimu. Data ya kithamano kwa kawaida ni data ya maelezo yanayoweza kufafanua na kufasili tabia na mahusiano ya watu katika jamii. Uainishaji wa data ya

kithamano ulitufaa kwa sababu ndiyo mbinu inayoweza kutumiwa katika kufafanua taarifa nyingi tulizozikusanya na zilizopitishwa kwa njia ya maandishi au kupitishwa kwa njia ya mdomo (Mugenda na Mugenda, 1999). Utafiti wa kithamano, vilevile, ulikuwa mwafaka kwa uchanganuzi wetu kwa sababu ndio husisitiza zaidi kuhusu uainishaji wa taarifa za aina ya usemi. Data ya utafiti wetu ambayo ilikuwa ya nukuu za usemi ulioandikwa katika tamthilia andishi ilifaa kuainishwa kwa misingi ya uchanganuzi wa kithamano ili kuweza kufafanua matini nyingi za kiusemi tulizoweza kuzidondoa kutoka kwa tamthilia teule tulizozisoma na kuzihakiki.

Tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia za Kiswahili zilichotwa kutoka kwa tanzu za kiusemi za Fasihi Simulizi na utamaduni wa Kiafrika. Hivyo, data za kiusemi tulizozidondoa kutoka kwa tamthilia andishi teule za Kiswahili, zilichanganuliwa kwa misingi ya data ya kithamano. Uhakiki na uainishaji wa data ya aina ya usemi ulifanywa kithamano kwa kusoma tamthilia nne za Kiswahili, kuzitambua na kuzidondoa data zetu. Data iliyokusanywa ilikuwa ya aina ya semi zilizochotwa na waandishi wa tamthilia zetu teule na kuzitumia kisanaa katika kuumba tamthilia zao. Utafiti wetu vilevile uliainisha kwa mkabala wa kithamano vitendo vyote vya sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika na kufafanua jinsi vilivyoambatanishwa na usemi huo katika tamthilia zilizohakikiwa kupitia kwa maelezo yaliyowekwa ndani ya mabano au kwa maandishi ya mlazo katika tamthilia zenyewe.

### 3.2 Eneo la Kufanyia Utafiti

Utafiti wetu kuhusu matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ulifanywa kwa njia ya usomaji wa maandishi mbalimbali. Ili kutuwezesha kupata data ya utafiti huu, tulisoma na

kuhakiki tamthilia kadhaa zilizoandikwa kwa Kiswahili ili kubaini mbinu ya matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika zilizotumika katika utunzi wa tamthilia teule za Kiswahili. Vilevile, tulisoma tamthilia zetu teule ili kubaini taswira zilizojengwa kupitia kwa matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika. Mbinu zetu za kiuhakiki, ulinganuzi na uchanganuzi zilituwezesha kubaini maendeleo na umuhimu wa matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili kwa mujibu wa malengo yetu ya utafiti huu. Utafiti huu, basi, ulihitaji usomaji wa kina wa tamthilia mbalimbali zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili na hasa zilizodhihirisha matumizi ya motifu inayojirudiarudia ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho ya Kiafrika.

Utafiti huu uliegemea usomaji wa ndani na nje ya maktaba. Mtafiti alitembelea maktaba mbalimbali za Vyuo Vikuu na za kitaifa katika miji mbalimbali na kusoma vyanzo anuwai kuhusiana na mada ya utafiti, nadharia za utafiti na tamthilia nyingi. Usomaji wa maktabani ulituwezesha kupata ufahamu zaidi kuhusu nadharia zilizoongoza uchunguzi huu. Usomaji wetu katika maktaba mbalimbali ulijumuisha usomaji wa vitabu, tasnifu, majarida na maandishi yoyote ambayo yangekuwa na umuhimu kwa utafiti wetu. Aidha, tulifanya usomaji zaidi katika mtandao ili kushadidia data ya maktabani. Usomaji huu ulituwezesha kuelewa vizuri na kulipanua suala letu la utafiti. Usomaji wa maktabani vilevile ulituwezesha kuelewa zaidi kuhusu nadharia za Uhistoria Mpya iliyoasisiwa na Stephen Greenblatt na nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na Julia Kristeva zilizoongoza utafiti wetu kama mbinu mwafaka ya kuchambua, kuchanganua na kuwasilisha matokeo ya uchunguzi wa data ya Fasihi Simulizi na Fasihi Linganishi. Marejeleo mengine yalipatikana kupitia kwa kuazima vitabu, majarida, miswada na nukuu kutoka kwa watu binafsi, wasimamizi, walimu, wahadhiri na marafiki.

Usomaji kupitia kwa njia ya wavuti na mtandao kwa jumla ulitufaa sana katika utafiti wetu kupitia kwa habari muhimu tulizozipata hasa kuhusiana na mada yetu ya utafiti. Kwa jumla, usomaji wa ndani na nje ya maktaba ulituwezesha kukusanya tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho ya Kiafrika kama nyimbo, semi, ngoma, majigambo, malumbano ya utani, pungwa, matambiko, maghani miongoni mwa fani nyingine zilizotumiwa katika utunzi na ujenzi wa dhamira na maudhui katika tamthilia teule ya Kiswahili.

### 3.3 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ya utafiti imeteuliwa kimaksudi kwa misingi ya uteuzi wa malengo maalumu ya utafiti huu. Kabla ya kuanza kukusanya data, tulipitia na kusaili tamthilia na maandiko mbalimbali na kujadili mada zilizoibuka na wataalamu mbalimbali ili kuibuka na tamthilia zilizodhihirisha matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi kutokana na tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Tuliegemeza usomaji na uhakiki wetu wa data katika mbinu ya uchanganuzi wa mbinu za uteuzi na matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia teule za Kiswahili na taswira zilizoibuliwa kupitia kwa matumizi ya tanzu hizo za sanaa za maonyesho. Katika usampulishaji wetu tulichagua kushughulikia kijisehemu cha muundo na taswira za matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ambayo ni sehemu ndogo ya Fasihi Simulizi kuafikiana na maoni ya mtaalamu Kothari (1989: 59) ambaye anaeleza hivi:

> “Watafiti huteua vijisehemu maalumu vya umma lengwa kimaksudi, ili kuunda sampuli ambayo inawakilisha umma mzima” (Tafsiri yetu).

Nadharia za Uhistoria Mpya na Mwingilianomatini zilituwezesha kukusanya, kuchambua na kujadili data ya uchunguzi wetu kutokana na vitabu vya tamthilia

vilivyoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu. Tamthilia zilizoteuliwa kwa ajili ya uhakiki na uchanganuzi wa matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ni zifuatazo:

*Mashetani* (1971) - iliyoandikwa na mtunzi Ebrahim Hussein.

*Pungwa* (1988) - iliyoandikwa na mtunzi Said A. Mohammed.

*Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1998) - iliyoandikwa na mtunzi Emmanuel Mbogo.

*Mashetani Wamerudi* (2016) - iliyoandikwa na mtunzi Said A. Mohammed.

Watunzi wa tamthilia hizi ambao ni Ebrahim Hussein (*Mashetani*), Said A. Mohamed (*Pungwa* na *Mashetani Wamerudi*) na Emmanuel Mbogo (*Ngoma ya Ng'wanamalundi*) wametunga tamthilia nyingi nyingine mbali na kazi nyingine za fasihi. Tamthilia zote hizi ziliteuliwa kimaksudi kwa sababu baada ya usomaji wa awali, ilidhihirika kwamba zote zimechota tanzu za jadi za sanaa za maonyesho ya jadi na kuzitumia katika utunzi wao. Tamthilia ya *Mashetani* iliyotungwa na Ebrahim Hussein ndiyo ya kwanza katika tamthilia zilizoteuliwa za Kiswahili iliyoakisi matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika miaka ya mwanzo ya 1970. Uhakiki wa tamthilia hii ulitoa misingi ya uhakiki wa matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia za Kiswahili za baadaye katika mkabala wa Mwingilianomatini.

Tamthilia ya *Pungwa* iliyochapishwa 1988 karibu miaka ishirini baada ya tamthilia ya *Mashetani* kuchapishwa, iliwakilisha tamthilia zilizochapishwa katika miaka ya 1980 na zilizotumia sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wao. Uhakiki huu vilevile ulichunguza tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* iliyochapishwa na mtunzi Emmanuel Mbogo katika mwaka wa 1998. Tamthilia hii ilichapishwa karibu miaka thelathini baada ya kuchapishwa kwa tamthilia ya *Mashetani*. Uhakiki wake

ulituwezesha kuelewa mbinu za utunzi hasa matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili mwishoni mwa karne ya ishirini.

Mwisho, utafiti wetu ulichunguza tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* iliyochapishwa na Said A. Mohamed katika mwaka wa 2016 zaidi ya miaka arobaini baada ya uchapishaji wa tamthilia ya kwanza ya utafiti huu. Tumezingatia tofauti ya miongo minne katika uchunguzi wetu ili kutuwezesha kuakisi ukuaji, maendeleo na mabadiliko yaliyofikiwa katika matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

Kujumlisha, tuliteua tamthilia *za Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* kwa misingi kwamba watunzi: Ebrahim Hussein, Emmanuel Mbogo na Said A. Mohammed ni watunzi bunifu na wenye umahiri mkubwa sio tu katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili bali pia katika kutumia malighafi asilia ya sanaa za maonyesho ya Kiafrika na mbinu zingine katika kubuni tamthilia zao na kuendeleza utamaduni wa Kiafrika. Hawa wote ni watunzi wakongwe ambao wamestaafu katika kazi zao za umma na ambao wana haiba kubwa katika taaluma ya uandishi. Inaaminika kwamba kazi zao zimeathiri watunzi wengi wa baadaye wa tamthilia kimuundo, kimtindo, kimaudhui na katika usawiri wao wa wahusika.

**3.4 Mbinu za Ukusanyaji Data**

Utafiti huu ulifanywa kwa njia ya usomaji na uhakiki wa maandishi mbalimbali yaliyohusiana na mada ya utafiti. Usomaji wa vitabu, majarida, makala na machapisho mengine kuhusu nadharia na mambo muhimu kuhusiana na mbinu za matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ulifanywa ili kupata dira na mwelekeo mahususi wa kazi. Aidha, maoni na ujumbe wa wataalamu wengine kupitia kwa tahakiki zao ulitambuliwa kuwa

wenye umuhimu usio na kifani. Vitabu vilivyochaguliwa kwa utafiti huu vilisomwa kwa kuzingatia muundo, mtindo na maudhui yaliyosawiriwa kuambatana na motifu ya sanaa za maonyesho ya jadi.

Mtafiti vilevile alikusanya takribani jumla ya tanzu zote za sanaa za maonyesho alizoweza kuzitambua katika tamthilia nne alizoweza kuziteua, kunukuu tanzu hizo na kuziainisha kwa misingi ya vigezo vya nadharia ya Uhistoria Mpya na Mwingilianomatini sawa na anavyosisitiza Kothari (1989:60) mtaalamu wa masuala ya utafiti:

> "Chini ya mfumo wa usampulishaji …, kila kipengele cha umma lengwa huwa na nafasi sawa ya kujumlishwa kwenye sampuli" (Tafsiri yetu).

Tamthilia ya *Mashetani* iliyotungwa na Ebrahim Hussein (k.h.j.) na kuchapishwa 1972 ilichunguzwa mkabala na tamthilia nyingine tatu zilizosalia kama kiongozi cha misingi ya utunzi unaohakikiwa. Kipindi cha utunzi kati ya mwaka 1972 wakati wa utunzi wa tamthilia ya *Mashetani* na mwaka 2016 wakati wa uchapishaji wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, ni kipindi kirefu cha miaka arobaini na nne au karibu miongo mitano hivi kwamba mfanano wowote wa masuala yanayoshughulikiwa katika kazi hizo, dhamira ya watunzi hao na mbinu zao za utunzi unaoweza kubainika hauwezi kuwa wa kiajali wala hauwezi kupuuzwa. Tuliweza kuchunguza na kulinganua tofauti na mfanano wowote uliobainika katika tamthilia teule kwa mujibu wa nadharia ya Uhistoria Mpya na Mwingilianomatini na kwa mujibu wa malengo yetu ya utafiti.

**3.5 Uchanganuzi wa Data**

Baada ya kukusanya data, uchanganuzi wa data hiyo uliendelezwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia za Uhistoria Mpya na nadharia ya Mwingilianomatini. Young (1960:448) anasema kwamba;

> "Utafiti lazima uwe na uhusiano kati ya malengo ya utafiti, data inayochanganuliwa pamoja na mihimili ya nadharia husika. Uwepo wa uhusiano huu tegemezi ndio msingi wa uasilia na uhalali wa matokeo ya utafiti" (Tafsiri yetu).

Data vilevile ilichanganuliwa kwa mujibu wa vipengele vifuatavyo:

i) Namna motifu ya sanaa za maonyesho ya jadi ilivyojitokeza kisanaa katika utunzi wa tamthilia za Kiswahili zilizoteuliwa na fasihi kwa jumla.

ii) Taswira ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilizotumika katika ujenzi na uimarishaji wa maana na dhamira za watunzi wa tamthilia.

iii) Umuhimu na sura mbalimbali za matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho zinavyojitokeza katika utunzi wa tamthilia za Kiswahili zilizoteuliwa katika kipindi cha karibu miaka hamsini.

Lengo kuu la utafiti huu kwa jumla lilikuwa kuthibitisha ikiwa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zimetumiwa na watunzi wa tamthilia teule za Kiswahili katika kujenga ujumi wa kazi hizo, jumbe zinazopitishwa na tanzu za Sanaa za maonyesho ya jadi zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia hizo na athari inavyojitokeza katika kuingiliana kimatini kwa tanzu hizo za Sanaa za maonyesho katika mapito ya wakati wa karibu miongo mitano.

### 3.6 Uwasilishaji wa Data

Matokeo ya uhakiki huu yaliwasilishwa kwa kuzingatia mbinu ya uchanganuzi elezi. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kupitia kwa maelezo ya kimaandishi yaliyoambatana na ufafanuzi wa matumizi ya tanzu hizo. Tulifanya nukuu nyingi za tanzu za jadi za sanaa za maonyesho zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ili kuthibitisha na kushadidia ufafanuzi wa maelezo hayo. Matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho za masimulizi, nyimbo, majigambo, ushairi simulizi, malumbano ya utani, maghani maalumu miongoni mwa tanzu nyingine zilifafanuliwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti.

Uwasilishaji wa matokeo ya data iliyochanganuliwa vilevile ulifanywa kwa njia ya maelezo ya maandishi yaliyofanywa moja kwa moja kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu na kwa misingi ya marejeleo ya data iliyokusanywa kuhusiana na mada ya matumizi ya sanaa za maonyesho za jadi za asili ya Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Kila ilipohitajika, sehemu za maelezo ya waandishi wa vitabu, majarida na machapisho mengine pamoja na fani za sanaa za maonyesho zilinukuliwa.

### 3.7 Hitimisho

Katika sura hii, tumefafanua muundo wa utafiti tulioutumia na mbinu tulizozitegemea katika kuchunguza tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika zilizotumika katika utunzi wa tamthilia teule za Kiswahili. Tulifafanua kuwa utafiti wetu ulifanywa ndani na nje ya maktaba kama mahali pa kufanyia utafiti mbali na kusoma katika wavuti na mitandao mbalimbali. Sampuli yetu ya tamthilia nne zilizoteuliwa baada ya usomiji wa awali uliobainisha kwamba sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika zilikuwa zimetumiwa katika utunzi wa tamthilia hizo ilikuwa ya makusudi. Baada ya kusoma tamthilia zetu teule na maandishi mengine na kudondoa data ya utafiti, tuliweza kuichanganua na kuihakiki kwa mujibu wa malengo yetu matatu ya utafiti ili kuibuka na matokeo ya utafiti huu tuliyoyawasilisha hapa baadaye.

Katika sura inayofuata tumefafanua kwa mapana kuhusu matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika ambazo ni kipengele muhimu cha Fasihi Simulizi kinachotumiwa kama malighafi adimu ya kubuni na kuendeleza umbo la kipekee la tamthilia ya Kiswahili. Katika sehemu hii vilevile tuliweza kuainisha na kufafanua tanzu za aina mbalimbali za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika zilizotumika katika utunzi wa tamthilia.

# SURA YA NNE

# SANAA ZA MAONYESHO YA JADI NA TAMTHILIA YA KISWAHILI

## 4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu, tulifafanua vipengele muhimu vinavyohusiana na muundo wa utafiti na mbinu zilizotumika katika kufanikisha utafiti huu. Kazi hii ni maelezo ya kina yaliyofanywa kwa uhakiki na ufasili wa data nyingi zilizokusanywa kutoka kwa tamthilia nne za Kiswahili yaani, *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* zilizoteuliwa kimakusudi baada ya kudhihirisha matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika katika usomaji wa awali.

Katika sura hii, tulilenga kufafanua dhana za tamthilia ya Kiswahili na sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya utamaduni wa Kiafrika kama njia ya kuweka misingi ya uelewaji wa utafiti wetu na kuweka mipaka kati ya sanaa za maonyesho ya jadi na tamthilia ya ki-Aristotle. Tumeweza kueleza historia ya tamthilia na matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Sura hii vilevile, imeshughulikia uainishaji wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ambazo zilikisiwa kuwa zimetumika kama mbinu ya utunzi wa tamthilia zetu teule za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundindi* na *Mashetani Wamerudi*.

## 4.1 Tamthilia ya Kiswahili na Sanaa za Maonyesho

Tamthilia ni mojawapo ya tanzu za Fasihi Andishi ambazo ni pamoja na, riwaya, ushairi, novela na hadithi fupi. Tamthilia ni neno ambalo asili yake ni lugha ya Kiarabu na lina maana ya kumithilisha au kufananisha kulingana na Matti (2003). Neno hili hurejelea michezo ya kuigiza ambapo ufananishaji hujitokeza kwa njia ya

mwigizaji kujifananisha na mhusika katika mchezo wakati wa uigizaji. Aidha, tamthilia inaweza kuelezwa kuwa utungo ulioandikwa au haukuandikwa na ambao unaweza kuliweka wazo linalowasilishwa katika umbo linaloweza kutendeka au kuigizika mbele ya hadhira. Tamthilia hubuniwa kwa lugha ya mazungumzo yanayosababisha matukio ya kihadithi yanayojenga kisa ambacho huigizwa jukwaani.

Katika matumizi ya kawaida, dhana ya tamthilia hukanganya kwani inaingiliana sana na dhana zingine kama 'drama', uigizaji na sanaa ya utendaji. Wafula (1999), anaeleza kuwa neno drama linarejelea somo linalohusu uigizaji wa hali mbalimbali za vitendo, tabia au hisia za Binadamu kwa kufuata taratibu maalumu. Tamthilia kwa upande mwingine ni utungo hasa ulioandikwa kwa ajili ya kuigiza kama njia ya kumithilisha kupitia kwa njia ya uhaishaji wa matendo, tabia na hisia za wahusika asili. Hivyo, 'drama' ni taaluma inayofafanua mitazamo mbalimbali ya kuhakikia tamthilia. Uigizaji nao unahusu kufuatiza maneno au matendo ya wengine na unafanana sana na sanaa ya utendaji.

Tamthilia ndio utanzu mchanga zaidi kuliko tanzu nyingine za Fasihi Andishi katika Kiswahili, ingawa mbegu yake kwa upande wa sanaa tendaji ndiyo ya kale zaidi. Asili hii inachimbuka katika Fasihi Simulizi hasa katika utambaji wa ngano na hadithi, ngoma za kienyeji, jando, makafara, matambiko, mazishi na maigizo ya aina mbalimbali. Maigizo haya ya kijadi yalishirikisha moja kwa moja msimulizi na hadhira yake katika utendaji na uigizaji katika mashairi ya majibizano, ngoma za watoto na watu wazima, michezo ya sarakasi miongoni mwa masimulizi mengine ambayo yalihusu matukio ya kila siku.

Katika maigizo ya awali, matendo na maneno ya maigizo yalizuliwa papo hapo wala hakukuwa na mgawanyiko katika vitendo na maonyesho. Wachezaji vilevile walivalia

maleba na kubeba vifaa wakati wa uigizaji. Maleba katika sanaa za maonyesho za kijadi yalitegemea tukio lenyewe ilhali vifaa vilivyoandamanishwa na maonyesho vilitolewa katika mazingira asilia. Vita vya kikabila katika jamii za Kiafrika kwa mfano viliigizwa kwa kushirikisha vikundi viwili vya waigizaji ambavyo vilikuwa vimejihami na mfano wa zana za kivita ambapo kimoja kiliwakilisha adui na kingine kinachojitetea au kinachovamiwa. Maonyesho ya matambiko, pungwa na uganga yaliambatana na matumizi ya vifaa kama mafuvu, makopo, ngozi za wanyama, meno, pembe, wanasesere na vyombo vingine vya nyumbani vilivyozua taswira ya uganga.

Watoto, vilevile, waliigiza maisha jinsi walivyoyaona ambapo waliathiriwa pakubwa na mazingira ya nyumbani. Watoto, kwa mfano, waliigiza mchezo wa baba na mama au shughuli zilizofanywa nyumbani kama upishi, ususi, uvuvi, ukulima, tabia na mienendo ya ndugu na wazazi wao. Watoto waliweza kupokezana zamu katika michezo yao na kila mmoja angejibunia maneno na vitendo ambavyo angeviigiza kulingana na nafasi aliyopewa na wenzake.

Maigizo ya awali yalifanywa kwa nuru wakati wa usiku. Kwa sababu hiyo, katika maigizo haya ya jadi moto uliwashwa ili kutoa mwanga au wakati mwingine waigizaji na watazamaji walifaidi mwanga wa mbalamwezi. Maigizo vilevile yalifanyiwa uwanjani ili kushirikisha watu wote katika jamii.

Kiango (1973) anaeleza kuwa awali vilevile kulikuwepo na maigizo ya vichekesho ambavyo vilitokana na hadithi za kienyeji zilizobuniwa kutokana na tajriba za maisha. Vichekesho hivyo vilivyosimuliwa kwa njia ya ucheshi vilidhihirisha ujanja au ujinga wa wahusika mbalimbali katika jamii. Vichekesho vya ujanja wa wanawake katika ndoa ambapo walikuwa na wapenzi wa kando au vichekesho vilivyodhihirisha unafiki kati ya marafiki kwa mfano viliigizwa katika jamii nyingi za Kiafrika. Masimulizi

haya yalikusudiwa kuchekesha na kufurahisha nyoyo. Maigizo hayo vilevile yalifundisha kuhusu maadili ya kijamii kama adabu, heshima, uaminifu, ukarimu miongoni mwa mengine.

Matti (2003), anaeleza ya kwamba katika utamaduni wa Waswahili kabla ya kuja kwa watu wa Ulaya na kuleta drama yao, kulikuwa na utungaji na kughani tendi katika sherehe mbalimbali za utamaduni wa Waswahili. Tendi hizo ziliwasilishwa kwa namna ya maigizo na matendo. Masuala mbalimbali ya utamaduni wa Waswahili yaliwasilishwa katika tendi hizo.

## 4.2 Matumizi ya Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Utunzi wa Tamthilia ya Kiswahili

Kabla ya kuja kwa tamthilia andishi katika eneo la Afrika Mashariki, Waafrika walikuwa na utajiri mkubwa wa sanaa zao za maonyesho ambao tunaurejelea katika utafiti huu kama tanzu za jadi za sanaa za maonyesho. Walipofika Wakoloni katika bara la Afrika na tamthilia yao andishi, Waafrika walikuwa wakiigiza na kufanya maonyesho ya kisanaa kwa ajili ya dhima mbalimbali kulingana na muktadha, wakati, mahali na umuhimu wa tendo linaloigizwa tofauti na Wazungu walioigiza kwa ajili ya kujiburudisha tu. Hivi sasa tamthilia ya Kiswahili ni zao la mchanganyiko wa sifa za sanaa za maonyesho ya jadi yaliyoasisiwa katika utamaduni wa Kiafrika na mwigo ulioambatanishwa na sifa za tamthilia ya Kimagharibi. Ili kufikia hali yake ya sasa, tamthilia andishi ya Kiswahili imepitia vipindi mbalimbali vya utunzi vinavyodhihirisha miundo na maudhui yanayorudiwarudiwa na kubadilika kiwakati.

Kuja kwa wakoloni na wageni wengine katika Afrika Mashariki kuliashiria kuingia kwa Fasihi Andishi katika eneo hili. Topan (1975) alivyoeleza, michezo ya kuigiza yenye umbo la kisasa haikuanzia hapa kwetu Afrika. Umbo la tamthilia na michezo

mingine ya kuigiza kama tuijuavyo sasa ililetwa hivi majuzi tu kutoka ng'ambo. Kipindi cha ukoloni kilishuhudia kuzaliwa kwa aina mpya ya fasihi iliyokuwa na mchanganyiko wa Fasihi Andishi ya Kimagharibi na sanaa za maonyesho za Kiafrika. Zao hilo jipya la mchanganyiko wa sanaa za jadi na za kisasa lilichangia kuzuka kwa sura maalumu ya tamthilia ya Kiswahili.

Maigizo ya kijadi yamechangia katika mafanikio ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ya kisasa. Hivi sasa tamthilia nyingi za Kiswahili zinadhihirisha mwingiliano mkubwa wa Fasihi Simulizi hasa wa sanaa za jadi za maonyesho na mitindo ya tamthilia ya Kimagharibi. Nyingi ya tamthilia za sasa zinadhihirisha matumizi ya matambiko, kafara, nyimbo, ngoma, vitendawili, hadithi, mashairi na sanaa zingine za jadi kama mbinu ya kuziimarisha na kuziendeleza. Tamthilia za awali za Ebrahim Hussein za *Jogoo Kijijini* (1975), *Ngao ya Jadi* (1975) na *Arusi* (1980) na zingine za Kiswahili zilifaidi kutokana na matumizi ya sanaa za jadi kwa kujumuisha katika utunzi wao, hadithi za kimapokeo na tanzu nyingine za sanaa za maonyesho ya jadi ili kusimulia kuhusu matukio mbalimbali katika jamii kama mabadiliko ya mfumo wa kisiasa na kitamaduni, maendeleo ya kiuchumi katika nchi miongoni mwa matukio mengine. Mwandishi Ebrahim Hussein, kwa mfano, anafuata mbinu ya utambaji hadithi katika utunzi wake wa tamthilia ambapo hadhira inashirikishwa katika masimulizi badala ya kukaa kimya kama ilivyo katika tamthilia ya Kimagharibi.

Wakoloni hasa Waingereza walipoingia katika bara la Afrika walianzisha uigizaji (drama) kama njia ya kujistarehesha. Drama hiyo ya mwanzo ya wakoloni ilihusu tamaduni na mawazo ya Kimagharibi. Tamthilia ya Kiswahili kulingana na Mazrui (1992) ilianza kuchukua umbo lake kupitia kwa michezo hii ya kuigiza iliyobuniwa na wanafunzi katika shule wakati wa ukoloni kwa ajili ya kuwaburudisha wazazi na walimu wakati wa sherehe za siku ya wazazi. Michezo iliyoigizwa wakati huo ilikuwa

ya lugha ya Kiingereza hasa zile tamthilia za William Shakespeare kama *Romeo and Juliet, The Merchants of Venice, Macbeth, Julius Caesar* miongoni mwa michezo mingine ambayo ilikuwa imebuniwa kimakusudi kwa ajili ya kuburudisha.

Maigizo ya kijadi katika jamii za Kiafrika kabla ya tamthilia ya Kiswahili ya sasa yalifanyiwa uwanjani na mtazamaji alikuwa na uhuru wa kutoka na kuingia katika mchezo alivyopenda. Aidha, hadhira ingeweza kushiriki katika ngoma na nyimbo jinsi ilivyotaka. Waigizaji walishirikiana na watazamaji katika uwasilishaji wa michezo ya kijadi. Tofauti na maigizo ya kijadi, katika michezo ya Kimagharibi kuliwekwa taratibu kama waigizaji kutoonyesha hadhira mgongo wakati wa maonyesho na sasa michezo ya kuigiza ikawa imeandikwa, kuchapishwa na kugawanywa katika matendo na maonyesho.

Kulingana na mazoea na tamaduni za kijadi na labda tofauti na tamthilia za Kimagharibi, maigizo ya sanaa za maonyesho ya jadi yalilenga zaidi kuadilisha na kuelekeza jamii. Hata hivyo, Waafrika vilevile walijiburudisha kupitia kwa maonyesho yao ya sanaa za kijadi. Majilio ya wakoloni yalibadilisha dhamira ya michezo ya kuigiza na kuifanya kuwa ya kuburudisha na kuchekesha tu. Suala hili pia liliathiri tamthilia za kwanza za Kiswahili kuandikwa kama *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* iliyobuniwa kwa malengo ya kuburudisha hadhira tu.

Mtunzi na mwigizaji wa tamthilia za muundo wa Kimagharibi huwa ni watu tofauti. Hali hii ni tofauti na maigizo ya kijadi katika jamii za Kiafrika ambapo mtunzi alibuni maneno jinsi mchezo ulivyoendelea na alikuwa mwigizaji pia. Maneno ya mtunzi katika tamthilia ya sasa yanabidi yakaririwe jinsi yalivyoandikwa na mtunzi ambaye huwa ametoka na kukaririwa na waigizaji ambao ni watu tofauti na mtunzi huyo. Maigizo ya kijadi katika mila na tamaduni za Kiafrika, yalihusu maisha ya jamii ya

kawaida vilevile. Tamthilia za Kimagharibi hata hivyo zilitungiwa masuala yoyote hata kama yalikuwa ya kigeni na yasiyokuwa na uhusiano na hadhira na utamaduni wao au yale ya kisayansi.

Utawala wa kikoloni ulitumia dini ya Kikristo kupinga maendeleo ya sanaa za maonyesho ya Kiafrika kwa madai kuwa ziliendeleza imani za kishirikina na kutomwamini Mungu mmoja kinyume na mafundisho yao ya Kikristo. Nyimbo za tohara, unyago, ndoa za kienyeji, matambiko, makafara na tamaduni nyingine zilizokuwa na sanaa za maonyesho ya Kiafrika zilipigwa marufuku. Aidha, ilikuwa vigumu kuendeleza sanaa za maonyesho ya Kiafrika kwa siri kwa sababu sanaa hizi zilihusu kucheza ngoma ambayo huwa na mdundo wa sauti kubwa, kuimba kwa sauti, kucheza hadharani na kukusanya makundi makubwa ya watu mahali pamoja mbali na sherehe za kitamaduni zilizoandamana na shughuli hizo kufanywa katika nyakati maalumu zilizojulikana na jamii husika. Vilevile, ilikuwa vigumu kwa Wakristo kuendeleza utamaduni huo bila kuonekana na wamishenari ambao waliishi nao vijijini. Wakati mwingine Waafrika wengine waliojiona kuwa Wakristo bora zaidi kuliko wenzao walipeleka habari kwa Wamishenari ambao walichukua hatua za kuwaadhibu wale “waliofanya kosa” la kushiriki katika utamaduni wao wenyewe. Hali hii ilifanya sanaa za maonyesho kufifia na ngoma za matambiko kukomeshwa kabisa.

Serikali ya kikoloni ilileta mfumo wa elimu wa kuwatenga wazazi na vijana wao ili kukwamiza tamaduni za Kiafrika na sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya Afrika kwa madai ya kuwa za kichawi. Wamishenari na walimu katika shule za kimishenari walifundisha na kuhubiri dhidi ya wanafunzi kushirikishwa katika matukio ya sanaa za maonyesho ya Kiafrika wakichelea wanafunzi hao kuathirika na imani za kishirikina katika tamaduni hizo. Kwa kuwaweka wanafunzi katika shule za bweni,

wanafunzi walizuiwa kushiriki katika ngoma za kienyeji na sanaa zingine za maonyesho ya jadi pamoja na tamaduni nyingine za jamii hizo zilizoendelea vijijini wakati wa masomo. Waliporudi nyumbani wakati wa likizo, wanafunzi waliwekewa askari wa kuwachunga wasishiriki katika sanaa hizo. Kabla ya wanafunzi kuachiliwa kwenda likizo, walihubiriwa na walimu wamishenari kwa nia ya kuwavuruga bongo zao kwa kuwaeleza kwamba nyumbani wangekumbana na Shetani kupitia kwa ngoma, unyago, matambiko na watoto ambao hawasomi. Wanafunzi hao wangeshauriwa washikilie imani yao mpya ya kidini na kwamba wasiyumbishwe na "Shetani hao" bali waepukane nao.

Iwapo ingehofiwa kwamba wanafunzi wangeshiriki katika sherehe za miviga ya jando, unyago na ngoma mbalimbali za kitamaduni za matambiko, pungwa na makafara wakati wa likizo, wangeshauriwa kuimalizia likizo yao shuleni. Kwa kufanya hivi, wakoloni waliharibu na kuvunja asasi ya mila na tamaduni za Kiafrika kama jando, unyago, matambiko na tamaduni nyingine ambapo maonyesho mengi ya sanaa na utambaji yalifanywa. Mkondo huu wa matukio wa wakati wa ukoloni uliathiri tamthilia ya Kiswahili ambayo ilianza kuweka misingi yake wakati huo na kuchukua maudhui na mtindo mpya.

Michezo ya awali kabisa iliyoweza kuandikwa katika eneo la Afrika Mashariki wakati wa ukoloni iliwatumia wanafunzi katika shule za msingi na za upili na waigizaji wengine kuigiza katika miji mikubwa kama Nairobi na Mombasa kwa malengo ya kuwaburudisha wakoloni. Michezo hii ilimbeza Mwafrika, utamaduni wake na tabia zake kwa jumla hasa kwa kutokuwa na uwezo wa kusoma na kuandika. Michezo hiyo ilimdhihaki na kumwonyesha Mwafrika kama asiyestaarabika. Aidha, michezo hiyo ilimsimanga Mwafrika na kumsawiri kama kiumbe duni mbele ya Mzungu. Mfano wa michezo hiyo ni wa "mama mshamba na kioo" aliyekivunja kioo kwa kuona kuwa lile

fumano lake katika kioo ni mke mwingine aliyeolewa na bwanake. Mchezo mwingine ni wa “Bwana na boi” ambapo daima mhusika Bwana alikuwa Mzungu au Mhindi na Boi daima alikuwa Mwafrika. Kwa mfano katika hadithi ya kijana Mwafrika kwa jina Juma na Mhindi, Juma anatumwa na Mhindi kumchukulia bidhaa mbali huko mjini na kwa safari nyingi siku nzima. Kila mara Juma alitimua mbio kwenda madukani kiasi kwamba mwishowe anaishiwa nguvu na kuchoka katika hekaheka zake za kumtumikia na kumfurahisha bwanake. Badala ya kujipumzisha kutokana na maumivu ya uchovu wa kukimbia sana masafa marefu, Juma anajikasirikia kwa kuchoka Mhindi anapomtuma.

Michezo kama hii iliyomdhihaki Mwafrika kwa kumtukuza na kumwabudu Mzungu, na hali ya Mwafrika kukosa hekima na ustaarabu kulimfurahisha na kumburudisha Mzungu wakati wa ukoloni. Wazungu na watawala wa kikoloni walishangilia na kusherehekea hali hii ya Mwafrika ambayo kwao ilikuwa ya udhaifu. Wazungu hao walitumia michezo hii kama kibali cha kuidhinisha na kuimarisha utawala wao wa kikoloni uliolazimishwa juu ya Waafrika na nchi za Kiafrika kwa madai ya kutaka kuleta dini na elimu ili kumstaarabisha Mwafrika.

Michezo ya awali kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili ilikuwa ya kuchekesha na iliigizwa kwa kutumia maleba ya kuchekesha pia. Maleba hayo yalijumuisha nguo kuukuu zilizochanika, kofia kubwa, suruali yenye mguu mmoja mrefu na yenye mifuko iliyotoka nje miongoni mwa hali zingine za umaskini. Licha ya kwamba maleba haya yalidhihirisha hali duni ya maendeleo na umaskini wa Waafrika, Wazungu wakoloni walijiburudisha na kufurahia hali hiyo. Muhando (1983), katika makala ya “Utunzi wa tamthilia katika mazingira ya Tanzania,” anasema kuwa hapo awali tamthilia haikuzungumzia masuala yaliyohusu nchi ya Tanzania moja kwa moja. Tamthilia nchini Tanzania ilitungwa na kutumiwa na serikali ya kikoloni kwa

malengo ya kusisimua wahudumu wa serikali hiyo. Kupitia kwa michezo hiyo, lugha na tamaduni za Kiafrika zililinganishwa na zile za kizungu. Aidha, maisha ya vijijini yalilinganishwa na yale ya mijini kwa Wazungu. Kwa jumla, tamthilia na michezo ya kuigiza ya kwanza ya kikoloni ilimtwaza Mzungu na utamaduni wake na kumtweza Mwafrika na utamaduni wake. Amali na rasilimali asilia za sanaa za maonyesho za jadi zilidunishwa na Mzungu na Waafrika waliokubali kuiga utamaduni wa Kimagharibi.

Tamthilia nyingi zilizobuniwa kabla ya uhuru zilikuwa na athari za kigeni. Nyingi yazo zilikuwa tafsiri na baadhi ya waandishi wa awali wa tamthilia ya Kiswahili walikuwa wageni Wazungu. Dini ya Kikristo kupitia kwa Wazungu Wamishenari ilichangia katika athari ya ugeni katika tamthilia ya Kiswahili wakati wa ukoloni. Wamishenari hawa walitunga na kutafsiri tamthilia kutoka kwa lugha zingine hasa ya Kiingereza kwa mfano *Bwana amekufa* (*The Lord is Dead*) na *Wanawake Wenye Akili* (*Intellingent Girls*). Kama Mazrui (1992) anavyothibitisha, huu ndio uliokuwa mwanzo wa tamthilia ya Kiswahili.

### 4.3 Uwasilishaji wa Sanaa za Maonyesho ya Jadi ya Kiafrika

Sanaa za maonyesho hujumlisha kazi bunifu ambazo huwasilishwa kwa hadhira ana kwa ana kwa njia ya utendaji. Kulingana na Mlama (1983), kuna sanaa za maonyesho za jadi na za mamboleo. Sanaa za maonyesho za jadi zilichimbuka kutokana na jamii za Kiafrika na hujumuisha ngoma, majigambo, miviga, jando na unyago, matambiko, utambaji hadithi, ngoma za kupunga majini na pepo na tanzu nyingine. Katika tanzu hizi za sanaa za maonyesho, watu waliigiza na kufanya vitendo kisanaa kama kucheza ngoma, kuimba, kucheza muziki, kutongoa mashairi, kunengua viungo na miondoko mingine ya mwili, ishara za nyuso miongoni mwa maonyesho mengine. Utendaji wa sanaa hizi uliambatana na maneno yanayosemwa pamoja na matendo ya kimwili.

Sanaa za maonyesho zilikuwa njia nzuri za kuwasiliana baina ya watu, watu na miungu pamoja na mizimu katika juhudi za kuboresha maisha na kuendeleza jamii.

Kucheza ngoma katika utamaduni wa Kiafrika, kulifundisha watoto tabia walizotarajiwa kuwa nazo katika utu uzima wao. Kuimba, kucheza na utendaji mwingine ulitumiwa na jamii kueleza miungu matatizo yao ya magonjwa, njaa, ukame na shida zingine. Utambaji hadithi vilevile ulifundisha vijana historia ya jamii, tabia nzuri, namna ya kuishi na watu wengine na thamani zingine za maisha ya Kiafrika.

Kila jamii ya Kiafrika huwa na aina yake ya sanaa za maonyesho. Kwa sababu ya kuwa na makundi na makabila mengi katika jamii, huwa kuna aina nyingi za sanaa za maonyesho ya jadi hivi kwamba kuna mitindo mingi ya ngoma, matambiko, masimulizi ya hadithi, majigambo na tanzu nyingine. Baadhi ya sanaa za maonyesho zilibadilika kimaumbo ilhali zingine zilipotea au zilifishwa kabisa na mabadiliko yaliyoletwa na utawala wa kikoloni na mitindo mipya ya maisha ya Magharibi. Ukoloni kwa mfano ulikomesha na kupiga vita sanaa za maonyesho kwa kutumia dini na elimu. Hivyo, nyingi ya sanaa za maonyesho hasa zile zilizohusiana na dini za jadi zimepotea. Hata hivyo, kwa sababu watu hukataa kutupilia mbali utamaduni wao, baadhi ya sanaa za maonyesho zimehimili na zimeweza kuchotwa na kutumiwa na waandishi katika utunzi wa tamthilia ya sasa. Sanaa hizo hujitokeza kama ngoma, majigambo, utambaji hadithi, kupunga pepo, miviga ya jando na unyago.

Sanaa za maonyesho mamboleo hujumuisha sanaa zilizotokana na athari za ustaarabu wa kigeni kulingana na Mlama (k.h.j.). Wazungu walileta drama katika eneo la Afrika wakati wa ukoloni kwa dhima kuu ya kujifurahisha, kujiburudisha na kujikumbusha maisha ya nyumbani hasa walipokuwa wakiishi mbali na nyumbani. Kwa

kuwahusisha Waafrika katika uigizaji wa tamthilia na michezo yao ya kuigiza kama tamthilia za Shakespeare, Waafrika waliweza kuathiriwa kiasi cha baadaye kujishirikisha katika utungaji wa tamthilia na kuzionyesha majukwaani.

Matumizi ya Kiswahili katika uigizaji na drama wakati wa ukoloni yalistawisha vichekesho vilivyoibuka kutokana na drama ya Waingereza. Kwa sababu ya urahisi wa uendeshaji na utungaji wa drama ya hapo kwa hapo, hivi leo, vichekesho kwa jina mashuhuri "standing comedy" vimetawala katika tanzu za sanaa za maonyesho kuliko drama yenyewe. Shuleni, vichekesho huigizwa kwa urahisi na kwa wingi kuliko drama inayotegemea tamthilia iliyoandikwa au kuchapishwa. Sababu nyingine ya ukuaji wa vichekesho ni kuwa vichekesho kama tamthilia inayozingatia "hali ya utoto" huwavutia wanafunzi zaidi. Vichekesho ndiyo tamthilia inayoziba pengo la michezo ya tamthilia inayopendwa na wanafunzi na watoto wengine. Vichekesho vilevile huwa na uhuru wa kuchukua maudhui na fani mbalimbali kulingana na mazingira. Mara nyingi hata hivyo, vichekesho havihifadhiwi katika maandishi.

Kimaandishi, tamthilia nyingi zilizotungwa na kuchapishwa hazipati nafasi kuonyeshwa jukwaani kwa sababu hazitiliwi maanani. Kabla ya ukoloni, sanaa za jadi zilithaminiwa na maonyesho yao yalifanywa kila wakati ulipohitaji. Hata hivyo, wakoloni "walileta drama yao ya kujiburudisha tu wakidhani kwamba walileta sanaa za maonyesho kwa mara ya kwanza katika jamii ambayo haikuwa na kitu kama hicho." Wakoloni hawakujali kuchunguza kama kulikuwepo na sanaa yoyote asilia wala hawakuleta ushirikiano wowote kati ya drama yao na sanaa za maonyesho za jadi za Kiafrika. Kwa njia hii, drama ya wazungu na hasa ya kutoka Uingereza ililazimizishwa kwa Waafrika hasa wa Afrika Mashariki kana kwamba ni kitu kipya kilicho huru na ambacho hakina uhusiano na utamaduni wa Kiafrika.

Ili kuiua sanaa za maonyesho za Afrika, wakoloni walitumia dini ya Kikristo kukomesha maendeleo yoyote katika sanaa hii. Waafrika waliotawaliwa na wakoloni walilazimishwa kuchagua kati ya utamaduni wao na ule wa Ukristo ulioambatana na ustaarabu na utamaduni mgeni wa kizungu. Kuzingatia mazingira yaliyowazunguka, mara nyingi Waafrika wengi "walichagua ukristo na kuukataa utamaduni wao" hata kama hawakuufurahia uigizaji wa tamthilia iliyojaa utamaduni wa Kimagharibi. Izingatiwe kuwa wakati wa ukoloni, Waafrika waliteswa na kufanyiwa visa vya "kuwachota akili" kwa kutishwa na kulazimishwa na utawala wa kikoloni kutenda walivyotaka wao bila kuhusishwa katika maamuzi yoyote. Hivyo, Waafrika hao "wapya" walikataa kucheza ngoma za Kiafrika, kuendeleza miviga asili ya Kiafrika, majigambo na pengine kutamba hadithi kwa jina la Ukristo. Waafrika waliokataa utamaduni huo mpya wa Ukristo, walilazimishwa kuukubali kwa kuadhibiwa kila waliposhiriki katika shughuli za utamaduni wao kwa kutolewa katika kitabu cha kanisa, kutengwa na Wakristo wengine au hata kuzuiwa kushiriki katika meza takatifu ya Bwana ili wajihisi kuwa wao hawafai tena katika jamii yao mpya ya Ukristo.

Kuelekea mwisho wa kipindi cha ukoloni hasa katika miaka ya arobaini na hamsini, hata hivyo, Wazungu ambao hapo awali walikuwa wamechukulia sanaa za maigizo za Kiafrika kama sanaa za kishenzi, walianza kuziendeleza. Ngoma na maigizo yakaanzishwa shuleni kwa ajili ya kuwaburudisha wazazi na Waafrika waliokuja katika shughuli za shule. Kwa wakati huu, wamishenari kwa upande mwingine bado walikuwa wakiendeleza dini yao na kutafsiri vitabu ambavyo maudhui yake yalikuwa ya kidini na yalilenga kuadilisha hadhira. Morrison (1945) kwa mfano alitafsiri tamthilia alizozipa majina *Tabibu Asiyependa Utabibu* (1945) na *Imekwisha* (1945) zilizokuwa zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza hapo awali na Frank, C. N.

Sanaa za maigizo zilipigwa jeki wakati mwanajeshi mwigizaji kutoka Uingereza kwa jina Graham Hyslop alipofika Afrika Mashariki katika mwaka wa 1936. Graham alibuni kikundi cha uigizaji cha wanajeshi kilichoitwa "East African Entertainment and Propaganda unit Force" katika mwaka wa 1944. Huu ulikuwa wakati wa Vita vya Pili vya Dunia na wanajeshi walihitaji kujiburudisha wakati wa mapumziko. Maigizo ya kikundi hiki vilevile, yalitumiwa katika kuelimisha jamii za Kiafrika na umma kwa jumla. Kutokana na maigizo hayo, filamu ya *Akilimali* iliweza kutungwa katika mwaka wa 1945.

Mulokozi (1982) anaeleza kuwa, Graham Hyslop aliandika na kuchapisha tamthilia za *Afadhali Mchawi* na *Mgeni Karibu* katika mwaka wa 1957 baada ya kurudi Uingereza kwa ajili ya masomo. Tamthilia ya *Afadhali Mchawi* iliyoigizwa na wanafunzi wa Jeans School alikokuwa akifundisha Graham, inasimulia kuhusu uchumba na ufisadi katika hospitali za umma ambapo daktari asiye mwadilifu anauza dawa za wagonjwa ili kupata faida ya kando. Masimulizi hayo yanaendelezwa kupitia kwa ulinganuzi wa madaktari wawili ambao mmoja ni mwadilifu na mwingine mwizi na fisadi. Tamthilia ya *Mgeni Karibu* inazungumzia dhuluma za kiutawala za ufalme wa Kiarabu, urithi, ufisadi na rushwa miongoni mwa mengine.

Kwa sababu ya hekaheka za vita vya dunia, watunzi hawakupata nafasi ya kutunga kazi za sanaa. Kwa mfano, hakuna tamthilia zilizotungwa na kuchapishwa kati ya 1944 baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia na mwaka 1957 ambapo ni tamthilia mbili tu za Graham Hyslop zilizobuniwa. Kulikuwa na maendeleo machache yaliyokuwa yamefikiwa katika utunzi na uchapishaji wa kazi za usanii kwa lugha ya Kiingereza ambayo ndiyo ilitukuzwa zaidi na wasomi hata na wasomi Waafrika. Katika eneo la Afrika Mashariki, ni tamthilia tatu tu zilizokuwa zimetungwa na kuchapishwa na zote mbili zilikuwa za Graham Hyslop pamoja na tamthilia ya

*Nakupenda Lakini* (1957) ya Henry Kuria, zilizoandikiwa nchini Kenya. Kwa sababu ya upungufu huu, utawala wa kikoloni kupitia kwa shirika la British Council ulianzisha mashindano ya maigizo ambayo yaliendelea hadi 1963 nchi za Afrika Mashariki zilipopata uhuru na msaada huo kukatizwa. Nchi za Afrika Mashariki zilikuwa zimepata uhuru wakati huo na sasa tawala za kikoloni zikakatiza msaada wake wa kifedha. Hata hivyo, kupitia kwa msaada huo, msanii mwingine, Gerishon Ngugi, alitunga tamthilia yake ya *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* katika mwaka wa 1961. Tamthilia zote hizi zilikuwa za kuburudisha na zilikuwa na maudhui mepesi ya kuadilisha na kuwafunza vijana kuhusu mapenzi, uchumba, ufisadi, utamaduni na athari za pesa kwa jamii za Kiafrika.

Ingawa tamthilia ilianza kuigizwa nchini Tanzania katika mwaka wa 1922, hakuna tamthilia ya Kiswahili iliyoandikwa na kuchapishwa nchini humo hadi mwaka 1968. Ebrahim Hussein alitunga na kuziigiza tamthilia zake mbili za *Wakati Ukuta* na *Alikiona* (1968) ambazo zilichapishwa na East African Publishing House katika mwaka wa 1970, miaka kumi na mitatu baada ya tamthilia ya kwanza kuchapishwa nchini Kenya. Kulingana na Mulokozi (1982) katika Kiswahili (Juzuu 49/2), wakati mwingi wa ukoloni nchini Kenya na Tanzania ulishuhudia kuigizwa kwa michezo ya Kiingereza shuleni. Watu wengi wa wakati wa ukoloni hawakujua kwamba ngoma, pungwa, matambiko, majigambo, miviga, utambaji hadithi na tanzu nyingine zilizotupiliwa mbali ndizo hasa sanaa za maonyesho za utamaduni wa Kiafrika.

Hadi mwaka wa 1967, utunzi wa kazi za fasihi kwa jumla uliathiriwa sana na hali ya nchi za Afrika kutokuwa na sera maalumu ya lugha mara tu baada ya kujinyakulia uhuru kwani michezo mingi ya kuigiza ilitungwa kwa lugha za kikoloni hususan lugha ya Kiingereza katika eneo la Afrika Mashariki. Hivyo utunzi ulifanyika kupitia kwa vikundi vya maigizo ambavyo vilidhamiria kuonyesha utukufu wa utamaduni wa

Mwafrika, falsafa, dini, siasa, kasumba, matatizo ya jamii ya Mwafrika miongoni mwa mengine kwa kutumia lugha za Wazungu. Watunzi wachache tu kama Ebrahim Hussein wa tamthilia za *Kinjeketile* (1969) na *Mashetani* (1972), Penninah Muhando wa tamthilia ya *Lina ubani*, Felix Osodo aliyetunga tamthilia ya *Hatari Kwa Usalama* (1979) miongoni mwa wengine waliweza kujitokeza kubuni tamthilia zao kwa lugha ya Kiswahili katika eneo la Afrika Mashariki baada ya uhuru.

Kwa sababu nchi za Afrika zilikuwa zikisherehekea uhuru wao, watunzi walibuni michezo ya vichekesho na tamthilia ya aina ya futuhi punde tu baada ya kujinyakulia uhuru hadi miaka ya 1970. Hali ya kutunga michezo ya kuigiza ya aina hii iliendelea katika eneo la Afrika Mashariki vilevile. Tamthilia hizi zilitumia kichekesho na dhihaka kuwasuta kwa njia ya kuvutia Waafrika walioiga kikasuku mienendo ya Wazungu. Hata hivyo watunzi walianza kufungamanisha utunzi wa tamthilia na mahitaji ya nchi zao kwa kuingiza katika utunzi wao tanzu za jadi za sanaa ya maonyesho.

Nchini Tanzania ambako ndiko tamthilia zetu teule ziliandikiwa na watunzi Watanzania, kulianzishwa mashindano ya uigizaji wa tamthilia za Kiswahili na Kiingereza katika mwaka wa 1967. Vyama vingi miongoni mwao chama cha “Youth Drama Association” vilibuniwa nchini humo ili kushiriki katika mashindano hayo wakati huo.

Maudhui katika tungo za michezo ya kuigiza ya baada ya uhuru yalibadilika vilevile ili kuendeleza dhima ya vichekesho na futuhi. Badala ya kuwasimanga na kuwacheka wanavijiji ambao hawakujua kusema kwa Kiingereza na ambao hawakuuelewa utamaduni wa Mzungu tu kama ilivyokuwa katika michezo ya kuigiza ya wakati wa ukoloni, watunzi sasa walianza kutunga kazi ambazo ziliwakashifu wasomi

waliokengeuka katika mienendo na walioanza kuwaiga wazungu. Mfano mzuri ni ule wa Martin Kayamba uliotungwa na kusimuliwa kuhusu kijana aliyeenda ng'ambo kusoma lakini aliporudi alikuwa ameathiriwa na utamaduni wa ughaibuni hivi kwamba alianza kuwadharau wazazi wake ambao hawakuwa wamesoma. Mwishowe, kijana huyu alizinduka na kutambua makosa yake na akabadilisha mienendo yake na kuwaomba msamaha wazazi wake.

Michezo iliyokashifu wakoloni na utawala wao uliowadhulumu Waafrika, vilevile, ilianza kutungwa. Nchini Tanzania, kulipitishwa Azimio la Arusha katika mwaka wa 1967 ambalo lilitoa changamoto kwa watunzi wa tamthilia kuzikomboa fikra za Mwafrika. Azimio hili likapanua maudhui katika utunzi na tamthilia zikaanza kuwasuta mabepari, mabwanyenye, makupe na watu weusi waliokengeuka na kuwaiga Wazungu. Baada ya Azimio la Arusha, michezo na mashairi mengi hasa ya ngonjera yaliweza kuigizwa ili kuelezea siasa na kuusifu utamaduni wa Mwafrika. Mathias Mnyampala kwa mfano aliigiza ngonjera nyingi nchini Tanzania, akipigia debe sera ya nchi yake na kutangaza maazimio ya Azimio la Arusha kwamba watu warudi vijijini ili wakalime. Mnyampala alikuwa na ujumbe wa kuusuta ubepari na kueneza sera ya Tanzania ya kueneza ujamaa na juhudi za pamoja. Wahusika waliotumiwa katika uigizaji wa michezo sasa wakawa ni watu weusi Waafrika wa kawaida waliotukuzwa wala si wazungu maarufu tu. Maonyesho vilevile yalitenganishwa na pazia na michezo yenyewe ikawa mirefu kuliko ile ya awali.

### 4.4 Mwingilianomatini wa Sanaa za Maonyesho na Tamthilia ya Kiswahili

Uchotaji na matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ni mbinu ya utunzi wa tamthilia kimwingilianomatini. Matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika fasihi, ni mfano wa fasihi ya

kimajaribio ambayo imechota vipengele vya Fasihi Simulizi ya Kiswahili na kuviweka katika Fasihi Andishi ya Kiswahili, kwa lengo la kuleta vionjo vipya katika fasihi ya Kiafrika. Dhana ya fasihi ya majaribio inarejelea kufufua fani za fasihi na tamaduni asili za Kiafrika kwa kutumia mbinu na vipengele vya sanaa za maonyesho ya jadi na Fasihi Simulizi ya Kiafrika kwa jumla katika utunzi wa tanzu za Fasihi Andishi kama riwaya, ushairi na tamthilia. Kwa mujibu wa Noordin (2006), maendeleo ya kitamaduni yanasisitiza kufufua na kuhifadhi mambo ya jadi ili kunufaisha jamii kutokana na yaliyomo.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa tamthilia ya majaribio au tamthilia mpya ni dhana inayotumiwa katika fasihi kuelezea tamthilia ambayo inakiuka kaida za kawaida zinazotumiwa katika utunzi wa tamthilia ya muundo wa ki-Aristotle. Tamthilia hii huwa na msuko, hadithi na wahusika wenye sifa zisizokuwa za kawaida kwa kuchota na kutumia tanzu kochokocho za sanaa asili za jadi.

Matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili yamekuwa yakifanywa tangu mwanzo wa utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na waandishi maarufu wa tamthilia ya Kiswahili kama, Ebrahim Hussein na Penina Muhando. Ebrahim Hussein alitumia mbinu hii katika tamthilia zake za *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*, na Penina Muhando katika tamthilia yake ya *Lina Ubani*. Waandishi hawa na wengine wa tamthilia ya majaribio wamedhihirisha ithibati za kuasi kaida za kijadi za utunzi wa tamthilia na kubuni tamthilia mpya kwa kuchota tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho na kuzitumia katika utunzi wa tamthilia mpya ya Kiswahili. Muundo na mtindo wa utunzi wa tamthilia mpya ya majaribio ya Kiswahili umewezesha hali ya kukabiliana na mabadiliko yanayozikumba jamii nyingi za kisasa za Kiafrika. Utafiti huu unakusudia kuchunguza namna uchotaji na matumizi ya sanaa

za maonyesho ya jadi katika tamaduni za Kiafrika ulivyotumiwa katika kubuni na kuimarisha muundo na maudhui katika tamthilia ya Kiswahili.

### 4.5 Uainishaji wa Tanzu za Sanaa za Maonyesho ya Jadi

Uainishaji wa tanzu za sanaa za maonyesho hurejelea ugawaji wa vipera vya Fasihi Simulizi na uwekaji wake katika makundi mbalimbali kwa misingi ya vigezo maalumu (Ngure, 2003 na Muiruri, 2006). Hivyo, tanzu ni aina ya tungo za fasihi zenye sifa na muundo unaokaribia kufanana.

Sanaa za maonyesho zina vitanzu mbalimbali ambavyo vimechotwa na watunzi wa kisasa ili kuunda tamthilia ya Kiswahili. Wataalamu mbalimbali wa kiasili na wageni wa mataifa ya Kimagharibi wamejaribu kuainisha tanzu za Fasihi Simulizi ili kuweka mipaka dhahiri kati ya tanzu hizi bila mafanikio kwa sababu ya utata unaotokea. Asili ya utata huu anavyoeleza Ndungo (2006) ni ugiligili na mwingilianotanzu unaodhihirika baina ya vitanzu mbalimbali vya Fasihi Simulizi au ukaribiano wa tanzu zinazoainishwa kuwa na muundo unaorandana. Wimbo na ushairi simulizi kwa mfano au nahau na semi, visaviini na visasili, hurafa na ngano miongoni mwa vitanzu vingine hufanana sana kiasi kwamba tanzu hizi hutatiza kutofautisha. Senkoro (1996:2) anasisitiza kuwa kuna utata kubainisha baina ya bembelezi na wimbo kwa kusema ifuatavyo:

> “Wakati mwingine, wanawake wanaotunga na kuimba hizi bembelezi huwa hawawalengi watoto wao kutokana na maudhui yanayobebwa na nyimbo hizi. Hapa ni pale ambapo, utanzu mmoja wa fasihi una fani inayowalenga watoto huku maudhui yakiwalenga watu wazima.”

Asemavyo Simiyu (2015), ni vigumu kuweka mipaka dhahiri kati ya tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiafrika kwa sababu kila utanzu una sifa tofautitofauti za kiutanzu zinazouwezesha kuwekwa katika vikundi zaidi ya kimoja.

Utata mwingine unatokana na mbinu za uainishaji ambazo zinazingatia mitazamo mbalimbali ya kitaaluma na kwa upande mwingine zinazozingatia mitazamo ya kiutamaduni ambayo husisitiza sifa na istilahi za jamii inayochangiza tanzu hizo za sanaa za maonyesho na Fasihi Simulizi kwa jumla. Ingawa kila moja ya mbinu hizi za uainishaji ina manufaa yake, matumizi ya mbinu tofautitofauti huleta utata katika makubaliano ya jina moja kwa aina moja ya utanzu bila kuibuka na majina mengi kwa tanzu za Fasihi Simulizi na sanaa za maonyesho ya jadi zinazokaribiana kuwa za aina moja ya utanzu. Hata hivyo, misingi ya uainishaji wa tanzu za Fasihi Simulizi na sanaa za maonyesho ya kale iliyozingatiwa ni pamoja na tunayoieleza hapa.

Kwanza, ni uainishaji wa tanzu kwa kuzingatia mianzo ya tanzu hizo. Tanzu za sanaa za maonyesho ya Kiafrika ya kale zimepewa majina kutegemea mianzo ya tanzu hizo. Tanzu za masimulizi, semi fupi, mafumbo na vitendawili huwa na namna ya kipekee ya kuzianza. Masimulizi kwa mfano huanza hivi:

1. Msimulizi: Hadithi hadithi. (*Msimulizi hupiga kamusa hii, kabla ya kuanza kusimulia hadithi ili kuvuta nadhari na tafakuri ya hadhira yake)*
   Hadhira: Hadithi njoo. (*Wanaosimuliwa hadithi huitikia kwa kusema njoo kama ishara ya kuonyesha kuwa wako tayari kumsikiliza msimulizi)*

Msimulizi vilevile anaweza kuanza kusimulia kisa chake kwa fomula tofauti kwa kusema paukwa kama ilivyo katika mfano huu:

2. Msimuliaji: Paukwa!
   Hadhira: Pakawa.
   Msimuliaji: Paliondokea chanja gaa
   Kajenga nyumba kakaa
   Mwanangu mwanasiti
   Vijino kama chikichi
   Vya kujengea nyumba na vilango vya kuingia.

Kwa kawaida usimuliaji hadithi au utegaji vitendawili huhusisha makundi mawili ambayo ni ya fanani na lile la hadhira. Vitendawili na mafumbo vilevile huwa na

mbinu maalumu ya kuanza usimuliaji wao unaohusisha makundi hayo mawili. Mtegaji kitendawili au fanani anaweza kuanza utegaji wake kama ifuatavyo:

Mtegaji: Kitendawili!
Hadhira: Tega.
(*Kisha mtegaji husema kitendawili chake*).

Mbinu nyingine ya uainishaji ni ile ya kuzingatia miisho ya tanzu. Nyingi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya kale ya asili ya Kiafrika huwa na namna ya kipekee ya kuhitimisha usimulizi wake. Utanzu wa masimulizi kwa mfano waweza kuishia njia mbalimbali kama ifuatavyo:

: Hadithi yangu inaishia hapo.
: Wakaishi raha mustarehe.

Baada ya kukitegua kitendawili, mtegaji huhitimisha kwa kumweleza mteguaji ikiwa amepata jibu sahihi la kitendawili au la. Ikiwa mteguaji hakulenga ndipo, mtegaji huomba apewe zawadi ambayo inaweza kuwa mnyama au kitu chochote kilicho na thamani. Hata hivyo, zawadi inayotolewa aghalabu huwa mji. Mtegaji akipewa mji na hadhira huweza kusema ujumbe wa salamu kwa watu atakaowatambua na kisha hutoa jibu sahihi la kitendawili. Utoaji zawadi humliwaza mtegaji kitendawili kwa kumfanya ajihisi kuwa mjuzi na bingwa katika kufuma vitendawili vinavyoipiku hadhira yake. Utoaji zawadi ambayo ni itikadi ya jadi katika utamaduni wa Kiafrika hutumika kisanaa katika kuendeleza ushindani katika taaluma ya utegaji vitendawili.

Utamaduni huu vilevile ulisambaa katika ughani wa ushairi wa aina ya ngonjera katika jamii nyingi za Kiafrika hasa miongoni mwa Waswahili pale ambapo manju au malenga wawili wasioonana au hata wasiojuana wangekutana hadharani na kuulizana mafumbo kwa njia ya vitendawili mpaka mmoja wao ashindwe katika itikadi waliyoiita kufunga nyama (Ruo, 1989). Malenga wa kwanza “angefunga nyama,” kwa kufumba fumbo mara nyingi kwa njia ya ushairi. Malenga wa pili vilevile angefumba fumbo na angoje ajibiwe kwa njia ya ushairi hadi afungue nyama

(afumbue fumbo). Malenga wa pili akishindwa kufumbua kitendawili basi atampa mji yule malenga wa kwanza amfumbulie fumbo hilo, yeye pamoja na mashabiki waliokusanyika kama hadhira yake.

Utata mwingine wa uainishaji unatokana na fasili mbalimbali za tanzu na vitanzu vya Fasihi Simulizi. Uainishaji kwa misingi ya nadharia za Kimagharibi huongozwa na mawazo ya Aristotle aliyetoa fasili ya shairi, tamthilia na tanzia (Wellek na Warren, 1949). Aristotle aliamini kuwa tanzu hizi zilikuwa na sifa bainifu ambazo zingetumiwa kuzitofautisha. Akitoa mfano wa utata katika tafsiri ya tanzu za Fasihi Simulizi, Simiyu (k.h.j.) anaeleza kuwa tarihi imefasiriwa kwa njia mbalimbali na wataalamu mbalimbali kwa njia ambayo inaleta utata. Kwa mfano, kwa mujibu wa Mulokozi (1989), tarihi ni ngano zinazofafanua matukio ya kihistoria. Wamitila (2002) naye anaeleza tarihi kuwa hadithi ambazo husimulia na ambazo zimejengwa kwenye matukio ya kihistoria. Tafsili hizi zinazua utata wa uainishaji wa utanzu wa tarihi kwani ilivyo ni kwamba kuna tanzu nyingine ambazo husimulia matukio ya kihistoria lakini haziwezi kurejelewa kuwa za utanzu wa tarihi. Tenzi za *Al Inkishafi, Mwanakupona, Fumo Liyongo* miongoni mwa zingine, husimulia kwa kina matukio ya kihistoria yaliyokumba Waswahili katika eneo la upwa wa Afrika Mashariki kabla ya karne ya ishirini. Uhusishaji wa tenzi hizi na masuala ya kihistoria katika eneo la Afrika Mashariki hauzifanyi kuwa tanzu za Fasihi Simulizi za aina ya tarihi.

Fasili ya wataalamu mbalimbali kuhusu utanzu au kitanzu kimoja cha sanaa za maonyesho jadi, fasihi simulizi au kazi fulani maalumu ya kitaaluma hukinzana. Maelezo yafuatayo ya wataalamu mbalimbali kuhusu utanzu wa methali yanakinzana na kudhihirisha utata ulioko wa uainishaji wa tanzu za Fasihi Simulizi.

i) Methali ni msemo wa kimapokeo ambao una muundo fulani mahususi, unaokumbukika na unaokusudia kueleza, kuadhibu, kusuta na kushauri (Wamitila, 2002).

ii) Methali ni utungo wa kimafumbo unaofananisha dhana mbili kwa wakati mmoja. Neno "methali" linatokana na kitenzi, "mithilisha" linalomaanisha kufananisha vitu viwili au kuhusisha kitu kimoja na kingine, (Kinge'i na Kisovi, 2005).

iii) Methali ni kauli fupi yenye maana fiche inayokubalika na kutumiwa na jamii kama kiashiria cha ukweli na hekima. Methali vilevile inaweza kufasiliwa kama msemo mfupi wenye busara iliyofichika, (Chesaina, 2003).

Maana inayobainika kutokana na fasili hizi chache inadhihirisha utata na ukinzani wa maelezo ya wataalamu. Wamitila anasisitiza ukale, umbo maalumu lenye kukumbukika pamoja na uwezo wa kutekeleza majukumu maalumu ya kijamii katika ufasili wake wa utanzu wa methali. Fasili hii inasababisha maswali mengi kuliko majibu. Kwa mfano, kuna uwezekano wa kubuni methali mpya ikiwa methali ni utanzu wa kale uliopokezwa vizazi katika mapito ya wakati? Ikiwa methali haiwezi kukumbukika inakoma kuwa methali?

King'ei na Kisovi (k.h.j.) kwa upande mwingine wanasisitiza sifa ya umafumbo na ufananishaji katika fasili yao ya utanzu wa methali. Swali linaloibuka hapa ni ikiwa tanzu nyingine zinazotumia mbinu ya mafumbo kama vitendawili na mafumbo yenyewe au tanzu zinazotumia mbinu ya kufananisha kama tashbihi na stiari ni methali. Ikiwa tanzu zinazotumia mafumbo na ufananishaji zote ni methali, kwa nini basi kunazo istilahi mbalimbali zinazojisimamia ikiwa hakuna tofauti kati yao? Kwa

ufupi, fasili zote hizi zinatatiza uainishaji wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na Fasihi Simulizi kwa jumla.

Chesaina (k.h.j.) naye anasisitiza sifa ya methali kuwa fupi na kuwa hifadhi ya busara. Fasili zote za wataalamu hawa na wengine hazilengi kueleza maana wala kubainisha utanzu wa methali na tenzi zingine bali zinajiingiza katika kizungumkuti na kutapatapa katika kueleza sifa za methali. Utata wa fasili ya tanzu za Fasihi Simulizi vilevile unadhihirika katika fasili ya utanzu wa ushairi. Wataalamu mbalimbali wametoa vijelezi vinavyokinzana kuhusu ushairi vilevile. Kwa mujibu wa Abedi (1954: vii) kwa mfano,

> "Shairi au utenzi ni wimbo. Hivyo kama shairi haliimbiki, halina maana kwani ingefaa asiyeweza kutunga mashairi sawasawa aeleze fikra zake kwa maelezo ya desturi kuliko kujitia ndani ya mkorogano wa maneno yasiyoimbika."

Abedi katika Diwani yake ya Ushairi (1954:12) kuhusu utenzi, anaeleza hivi:

> "Utenzi maana yake ni ushairi wenye mizani michache kuliko kumi na mbili."

Maelezo ya wataalamu Abedi, Mulokozi na Kahigi yanatatiza kwani hayaonyeshi tofauti kimaana kati ya shairi, utenzi na wimbo kwani maelezo yao yanarejelea fasili ya misingi ya Aristotle. Maelezo yao yanakanganya uainishaji wa tanzu za sanaa za maonyesho ya Kiafrika ya jadi na Fasihi Simulizi kwa jumla. Maelezo ya wataalamu wengi yanachanganya maana, sifa, namna ya uwasilishaji na wajibu wa shairi katika fasili yao ya mashairi mbali na kueleza kwa Mzunguko unaotanza fasili na maana ya ushairi. Mfano wa ufafanuzi wa aina hiyo ni ule wa Mulokozi na Kahigi (1979: 25) tunaounukuu hapa chini.

> "Ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu wa maneno fasaha na yenye muwala wa lugha ya mkato, picha au stiari au ishara, katika usemi, maandishi, mahadhi ya wimbo ili kueleza tukio au hisi fulani kuhusu maisha au mazingira ya Binadamu, kwa njia inayogusa moyo."

Uainishaji wa utanzu wa hadithi fupi vilevile unakumbwa na utata wa uainishaji unaokubalika kwa sababu ya tafsili mbalimbali zinazokinzana. Mbatia (2000:viii) akifafanua kuhusu utata unaokumba uainishaji wa utanzu wa hadithi fupi anaeleza ifuatavyo:

> "Wataalamu wengi wamekiri kwamba ni vigumu mno kuutolea fasili utanzu huu... hivi leo, wakati wengi wanaamini kwamba haiwezekani kutoa fasili inayokubalika kote juu ya hadithi fupi."

Mbatia anaongezea kwa kusema kuwa:

> "Kuna mambo matatu muhimu yanayoleta ugumu katika ufasili wa utanzu huu ... Hadithi fupi inakaribiana na riwaya na inakaribiana na novela ... ni utanzu mnyumbufu na mbadilifu sana ... utanzu huu huangaliwa kama mazoezi ya utanzu wa riwaya."

Uwasilishaji na utendaji wa tanzu za methali, visasili, tarihi na misemo waweza kuwakilishwa kwa neno moja tu. Aidha, methali, misemo na misimu inaweza kuwakilishwa kupitia kwa maelezo marefu yenye mfumo wa kihadithi na yenye lugha ya kishairi. Kwa misingi ya sababu hizi, ni vigumu kusema kuwa utanzu fulani una muundo au umbo maalumu lisilobadilika.

Ni muhimu kutambua kuwa ni vigumu kusisitiza kwamba utanzu fulani una muundo au umbo maalumu lisilobadilika. Muundo na maana ya utanzu wowote ule wa Fasihi Simulizi hubadilikabadilika kulingana na matumizi yake katika muktadha wa utamaduni wa jamii maalumu. Hakuna fasili moja sahihi ya utanzu wowote ule wa sanaa za maonyesho au Fasihi Simulizi ya Kiafrika iliyoafikiwa na wataalamu kwa sababu maana na muundo wa kila utanzu hubadilika kutegemea utendaji wake. Fasili za Kimagharibi kuhusu tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho ni za kigeni na zimeshindwa kuainisha tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na Fasihi Simulizi ya Kiafrika kwa jumla. Ni wazi kuwa muundo wa tanzu za sanaa za maonyesho ni nyumbufu na huingiliana na kujengana katika kuunda tanzu nyingine za fasihi. Hata hivyo mgawanyo unaotumiwa katika uainishaji wa tanzu za sanaa za maonyesho ya

jadi ya asili ya Kiafrika huwa ni wa kusaidia kuendeleza mjadala. Tanzu za sanaa za maonyesho ya Kiafrika ya kale zimechotwa na watunzi mbalimbali wa tamthilia na kuzitumia katika kubuni upya fani na maudhui ya tamthilia ya Kiswahili.

### 4.6 Sanaa za Maonyesho katika Utunzi wa Tamthilia Kimwingilianomatini

Simiyu (2015) anaeleza mwingilianomatini kuwa uumbaji wa maana kamili ya utanzu mmoja kutokana na tanzu nyingine. Kwa ajili ya kazi yetu, tumesisitiza kuwa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi za asili ya Kiafrika zimetumika katika kujenga na kuimarisha muundo wa tamthilia ya Kiswahili katika fani na maudhui. Hivyo, utunzi wa tamthilia ya Kiswahili umevunja mipaka ya utunzi wa tamthilia ya ki-Aristotle kwa kuchota na kuzitumia tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya Kiafrika na kuyachanganya na mbinu za utunzi za tamthilia ya Kimagharibi wakati wa utunzi ili kubuni tamthilia ya Kiswahili ya kisasa kama inavyodhihirishwa hapa chini.

#### 4.6.1 Utambaji na Usimuliaji wa Kingano

Vitanzu vya hadithi, mafumbo, vitendawili, majigambo, ushairi simulizi na vingine vya Fasihi Simulizi na sanaa za maonyesho huwa na sifa ya utambaji. Mtambaji au fanani ni msanii anayefanya kazi ya kusimulia mbele ya hadhira kama asemavyo (King’ei, 2005). Aidha, ni msanii anayewasilisha kipera chochote cha Fasihi Simulizi kwa hadhira. Usimuliaji hushirikisha kuongoza katika uimbaji, kutamba hadithi, kutega vitendawili, kufumbia watu mafumbo, kujigamba, kughani au kukariri mashairi miongoni mwa mengine. Hizi ni mbinu za sanaa za maonyesho ambazo huwasilishwa ana kwa ana kwa kutumia usanii wa kiutendaji. Katika usimuliaji, msimulizi huwasilisha taaluma yake kwa kutumia mbinu mbalimbali kuteka nadhari ya hadhira yake. Mbinu ya usimuliaji huchotwa na kutumiwa na watunzi wa Fasihi Andishi katika utunzi wa kazi zao katika fasihi ya Kiswahili tutakayoirejelea hapa kwa jina fasihi ya majaribio, tamthilia mpya au tamthilia ya majaribio. Katika

tamthilia ya *Lina Ubani*, mtunzi Muhando (1976), ametumia mbinu hii ya utambaji, pale ambapo mtambaji anasimulia hadithi ya Bibi.

Mtambaji: Paukwa
Hadhira : Pakawa
Mtambaji: Hapo zamani za siku hizi, palitokea huyo Bibi
kama mnavyomuona ...(uk. 2)

Katika usimuliaji huu, mtunzi ametumia mbinu ya kusimulia hadithi kwa kuita kikao au hadhira kwa kutumia fomula au kanuni maalumu ya utunzi wa utanzu wa hadithi. Fomula hutofautiana kutegemea kipera cha utanzu wa sanaa za maonyesho husika.

### 4.6.2 Wimbo, Ngoma na Uimbaji

Wimbo ni utungo wa fasihi unaotumia mahadhi, mdundo, muwala na mapigo ya kishairi ili kuwasilisha ujumbe wake. Wimbo huweza kuimbwa na mtu mmoja pekee au pamoja na wazumi wake wakiitikia (Matteru, 1987). Mawazo katika nyimbo husababishwa na nguvu fulani zinazomsukuma mtunzi kuubuni na kuuwasilisha kwa hadhira kwa ajili ya kuleta athari inayokusudiwa. Msokile (1992) anaeleza wimbo kama ushairi unaoimbwa na kuchezwa.

Katika uimbaji, fanani anaweza kuimba wimbo wote peke yake au anaweza kuimba kitangulizi au mstari mmoja wa wimbo na washiriki wengine katika uimbaji wakaitikia. Utanzu wa wimbo ndio mkongwe zaidi katika taaluma ya fasihi kwani ulianza punde tu binadamu alipopata lugha na kuweza kuzieleza na kuzifumbata hisia zake. Wamitila (2003) anaufafanua wimbo kama utanzu wa sanaa za maonyesho na Fasihi Simulizi wenye mahadhi ya kimuziki yanayopanda na kushuka. Wimbo hubuniwa kwa kutumia lugha ya mkato yenye mapigo ya silabi ambayo ni ya kishairi, matumizi ya taswira na lugha yenye ishara.

Msokile (1992) anaeleza wimbo kama ushairi unaoimbwa, kughaniwa au kuelezwa kuhusu tukio fulani katika jamii. Mazingira ndiyo yanayozalisha hisia na hatimaye

mawazo kwa msanii wa wimbo ili aweze kufanya utunzi wa wimbo. Utunzi wa wimbo hufanywa na watu baada ya kusukumwa na nguvu maalumu. Mawazo ya mtunzi katika wimbo hutolewa kwa hadhira kupitia kwa njia ya sauti ili kuleta athari inayokusudiwa. Sauti zinazotumiwa katika wimbo hutofautiana katika mwendo na mpangilio wa uwasilishaji wake wa kuimbwa. Nyimbo zinapoimbwa hutumia vipengele vingi katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wake kwa hadhira inayolengwa. Vipengele hivyo mbali na maneno huwa na vidokezo, miguno, milio, toni na kiimbo.

Kuna aina nyingi za nyimbo ambazo zimechotwa na kutumiwa na watunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika utunzi wa kazi zao kutegemea dhamira za mtunzi, wahusika, mazingira na muktadha zinamoimbwa. Nyimbo na ngoma tulizozingatia katika utafiti wetu ni zile zilizoasisiwa na zilizoandamanishwa na miviga na sherehe za utamaduni wa Kiafrika.

### 4.6.3 Taswira

Lanham (1991) anaeleza taswira kama kitu kinachowakilisha kitu kingine, kiashiria, kibadala cha au matumizi ya kitu cha pili kinachofanana na cha kwanza. Naye Senkoro (1987), anaeleza taswira kama mbinu ya lugha inayotumiwa kuchorea picha kitu au mahali kwa kutumia ishara. Hivyo, taswira ni mbinu inayotumiwa kuwakilisha ujumbe maalumu kwa njia ya kimafumbo. Matumizi ya taswira ni ya kiishara na ni mbinu inayotumia ishara katika sanaa za maonyesho kuwakilisha wazo kwa hadhira iliyokusudiwa. Dhana hii imetumiwa katika tamthilia ya *Lina Ubani* kwa mfano, ambapo mwandishi amezua taswira ya “zimwi,” kuwakilisha utawala wa mabavu wa aliyekuwa raisi wa Uganda, nduli Idd Amin, kama anavyosema mtambaji:

> ... Mwisho Zimwi likaamua fujo kuzifanya asubuhi na mapema, ukingoni mwa msitu lilisimama, likapiga makelele kuteremsha ardhi - (*Lina Ubani* - uk 18).

Wahusika, na majina ya wahusika waliotumiwa katika tamthilia ya *Lina Ubani*, yanawakilisha binadamu wenye majina halisi ya Kiafrika. Wahusika kama Bibi, Huila, Mwana Hego, Mota pamoja na Mhusika Zimwi ambaye katika jamii za Kiafrika huashiria ubaya. Mtunzi katika tamthilia yake alitumia majina haya kitaswira ili kuwakilisha maana kwa njia fiche. Maana ya kitaswira huhitaji ufasiri ili umfikie msomaji kwa njia ya wazi. Uhakiki wa matumizi ya taswira huwa ni njia mojawapo ya kumsaidia msomaji kuelewa ujumbe kwa njia isiyotatiza. Matumizi ya taswira hulenga kuibua masuala muhimu, nyeti na tata kama ya kisiasa, kidini, kiuchumi na kijamii. Taswira humfikirisha msomaji kwa kumfanya ahusishe taswira yenyewe na tabia, mambo na vitu mbalimbali vinavyojitokeza katika maisha yake.

### 4.6.4 Mwingilianotanzu katika Sanaa za Maonyesho ya Jadi

Mwingilianotanzu au kwa jina lingine utomeleaji ni mbinu ambayo hujitokeza sio tu katika Fasihi Simulizi bali pia katika Fasihi Andishi ambapo vipengele fulani vya fasihi hiyo huingiliana katika njia za matumizi ya fani mbalimbali ili kubuni utanzu mpya wa kisanaa. Katika tamthilia ya *Lina Ubani* kwa mfano, mtunzi ameuingiza utanzu wa sanaa za maonyesho wa hadithi katika utunzi wa tamthilia yake mbali na matumizi ya tanzu za wimbo, ushairi simulizi na ngoma ambazo zimeambatanishwa na ujuzi wa utambaji. Mhusika Bibi katika tamthilia hiyo amesawiriwa akiwa ameketi huku anaomboleza kwa kuimba na kulia. Licha ya hayo, wimbo wenyewe unawasilishwa katika lugha moja ya jadi ya Kiafrika. Wimbo na tafsiri yake kwa lugha ya Kiswahili ni kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| *Ing'oma ii sikuidaha doo ae* | *Ngoma hii siwezi Oooh!* |
| *Woi doo ae aya* | *Woi doo ae aya* |
| *Nimemwitunda dya mele do* | *Nisimame juu ya mlima wa Mele* |
| *Ninange maina baba do* | *Niite baba na mama* |
| *(Lina Ubani - uk 1-3)* | |

Mianzo na miisho ya kifomula ni sifa ya kimsingi katika usimulizi wa hadithi na utambaji wa vitendawili ambazo ni tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika na Fasihi Simulizi ya Kiafrika. Fanani katika uwasilishaji wa tanzu hizi huanza kusimulia hadithi yake kwa kuweka viashiria maalumu katika ufundi wa usimulizi wao ambapo fanani huanza usimulizi wao kwa kusema maneno yafuatayo:

Fanani : *Paukwa*
Hadhira: *Pakawa*

Katika tamthilia ya *Lina Ubani,* mwandishi ameanza utunzi wa tamthilia yake kwa kuelezea kisa chake kwa njia ya matumizi ya utanzu wa hadithi ambao pia ni utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi na Fasihi Simulizi kwa jumla. Mwanzo wa utunzi wake unachukua sura ya mianzo ya utanzu wa hadithi ambao ni utanzu wa Fasihi Simulizi. Mfano wa hapa chini unadhihirisha matumizi ya utanzu wa hadithi katika utunzi wa tamthilia ya *Lina Ubani*:

Mtambaji *: Paukwa*
Hadhira*: Pakawa*
Mtambaji*:* Hapo zamani za siku hizi… (*Lina Ubani* - uk-2).

Mwishoni mwa tamthilia hiyo, mtunzi anamtumia mhusika Mtambaji ambaye amemalizia usimulizi wake kwa kuingiza utanzu mwingine wa Fasihi Simulizi wa kitendawili katika usimulizi wake ambapo anaomba hadhira impe mji ili kuhitimisha hadithi yake kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

Mtambaji: *Akaa!*
*Mwenyewe bibi kajifia*
***Hadithi hakumalizia***
***Mkitaka nimalizie mimi***
***Nipeni mji***
*Lakini mji wenyewe*
*Usiwe na uvundo*
*Kwa sababu ubani wa uvundo*
*Mie siujui.* (*Lina ubani* – uk 2)

Sehemu ya mwisho ya dondoo la hapa juu inajumuisha sehemu ya kuhitimisha kitendawili ambapo mtegaji kitendawili anaomba apewe mji kama zawadi baada ya hadhira ya wateguaji kushindwa kukitegua kitendawili chake, **"Hadithi hakumalizia, Mkitaka nimalizie mimi, Nipeni mji".** Jina la mhusika wa usimulizi katika dondoo la hapa juu (Mtambaji) vilevile ni jina lililochotwa kutoka kwa Fasihi Simulizi na utamaduni wa Kiafrika. Tanzu za usimulizi wa hadithi, uimbaji, kitendawili, ngoma, na tanzu nyingine zimejumuishwa katika utunzi wa tamthilia ya *Lina Ubani* kama mbinu na nyenzo ya utunzi.

### 4.6.5 Imani katika Pepo na Mizimu ya Jadi

TUKI (2014) inaeleza pepo kama anayedhaniwa kuwa ameumbwa kwa moto na ambaye haonekani kwa macho. Pepo au kwa jina lingine mizimu ni neno la Kiswahili linalorejelea viumbe fulani vya ajabu vinavyotokea katika imani ya jamii fulani. Mbithi (1969) anafafanua pepo kuwa vitu vinavyowaadhibu Binadamu kwa kufanya matendo maovu na ambavyo huhusishwa na bahati mbaya na uchawi au mazingaombwe. Noordin (2006) naye anaeleza kuwa mizimu husemwa kuwa wametokana na mababu waliokwishakufa na hivyo kufufuka tena kuja kuwaadhibu watu walio hai wakati wanapokosea. Mizimu hupatikana katika mapango, makaburi, bahari au katika miti mikubwa kama mbuyu unaotajwa katika tamthilia ya *Mashetani* (1971). Ali (1998) anaeleza kuwa pepo hawafanani na yule aliyekufa bali huibuka baada ya kifo chake na kugeuka na kuwa nafsi mbaya yenye kudhuru. Nafsi hizo husemekana kuwa na nguvu fulani ambazo hupaswa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa uteuzi maalumu unaofanywa kupitia kwa njia ya ndoto za kiajabu zinazowatokea wale wanaotokana na ukoo ule. Nguvu hizo aghalabu ni za kiganga na hutumika kuwapunga wagonjwa na kuwatuliza pepo.

Pepo huwa na mahali maalumu wanapoishi au wanapopatumia kuathiri maisha ya kizazi cha leo. Pepo au mizimu huwatumia watu ili kuonyesha nguvu zao. Pepo lazima wawe na mahali au watu maalumu ambao wamewateua wenyewe kuwapanda. Pepo huwapanda watu wanapokusudia kuwaathiri watu kwa njia nzuri au mbaya. Dhima ya pepo na mizimu ni kulinda jamii fulani kutokana na maafa au maangamizo, kulinda kijiji fulani na tamaduni zake dhidi ya athari za kigeni. Pepo hutumiwa kuleta mvua isiyo ya gharika, kuondoa ukame au ugonjwa miongoni mwa mambo mengine mengi. Mila hizi za kitamaduni za asili ya jadi ya Kiafrika ambazo zilipigwa marufuku na wazungu na wamishenari wakati wa ukoloni, hivi sasa zimetumiwa kibunifu katika kutunga tamthilia na kazi nyingine za Fasihi Andishi.

**4.6.6 Tambiko**

Tambiko ni aina ya dawa ya Kiafrika itolewayo kwa pepo kwa ajili ya kurudisha maelewano baina ya watu. Pepo au mizimu kwa mujibu wa Akida (1981), huhitaji aina ya sadaka ili kuirithisha na kuifurahisha kufuatana na mila na desturi za jamii mahususi za Kiafrika. Huu ni utekelezaji wa ada maalumu ili kutuliza mizimu au pepo.

Abdala (1998) anaeleza ya kwamba, tambiko ni utekelezaji wa masharti ya Mashetani kila baada ya muda. Desturi hizi ambazo hupatikana katika mila na desturi nyingi za Kiafrika, hutumika kama nyenzo itumikayo katika ngoma za kupunga mizimu. Tambiko linapofanywa, mnyama au ndege huchinjwa. Kwa mujibu wa Abdala (k.h.j), sherehe yenyewe ya tambiko hufanywa saa za magharibi ambapo pepo huwa wamepumzika.

Mbali na tambiko, pia huwa na dawa ya kafara. Aghalabu, kafara hufanyika ili kujikinga kutokana na vijicho na roho mbaya za mahasidi. Miongoni mwa jamii ya

Waswahili kafara hufanywa kwa kutumia mnyama ambaye mara nyingi huwa mbuzi au kondoo mweusi anayezikwa mbele ya nyumba ya mgonjwa. Wakati mwingine chungu chenye damu ya kuku, ngamia au hata damu ya mgonjwa mwenyewe hufunikwa ili kuwa kafara kutegemea matakwa ya jamii mahususi ya Kiafrika inayojihusisha na kafara hiyo.

### 4.6.7 Kilinge

Kwa mujibu wa tamaduni wa Waswahili ambapo ndipo tamthilia zetu teule ziliandikiwa, kilinge ni mahali maalumu ambapo wagonjwa hufanyiwa uganga au hupungwa. Hivyo kilinge huwa jukwaa ambalo limejengwa na kufunikwa kwa shuka nyekundu zenye ishara ya moyo, nyoka, nyota na ishara zingine za kutisha ambazo pia zimenakishiwa nyuzi nyeupe. Kijumba hiki huwa na dari ambalo huangikwa hirizi mbalimbali. Hapa pia huchomwa udi, ubani, nyasi na majani kutokana na vitu vilivyoangikwa darini humo na wakati huohuo kutiwa ndani ya kilinge. Mtu anapoingia kilingeni hukaribishwa na mandhari au ulimwengu wa kipepo unaotisha na kuogofya. Aidha, hapa hupigwa ngoma za kupunga mizimu na kuchezeshwa na kuimba nyimbo kadha za kuwaridhisha wale pepo au mizimu. Wanaoshiriki tambiko, wote kwa pamoja huimba nyimbo na kupiga makofi na kurudia kibwagizo fulani. Anayefanyiwa uganga huo ndiye huathirika zaidi kwani hupiga kelele na kujizungusha kichwa mpaka akaanguka. Wengi katika hadhira hushikwa na jazba na kuingia katika ngoma na kucheza.

Utafiti huu ni wa uhakiki wa tamthilia nne za Kiswahili ambazo kutokana na usomaji wa awali uliofanywa na mtafiti ulidhihirisha uchotaji wa sanaa za maonyesho ya jadi na kuzitumia katika utunzi wao. Kwa kuzingatia fani, mtindo, dhamira na maudhui katika tamthilia hizi, utafiti huu ulidhamiria kuakisi jinsi watunzi mbalimbali wa tamthilia ya Kiswahili walivyotumia mbinu ya kuchota sanaa za maonyesho ya jadi

katika utunzi wa kazi zao na jinsi mbinu hii inavyotumika kujenga na kuimarisha fani na maudhui ya kazi za sanaa. Aidha, utafiti huu unakusudia kudhihirisha kwamba watunzi wa tamthilia ya Kiswahili wametumia sanaa za maonyesho ya Kiafrika kama malighafi na mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

### 4.7 Hitimisho

Katika sura hii ya nne, tumetofautisha kati ya sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika na tamthilia ya ki-Aristotle. Vilevile, tumebainisha na kufafanua tanzu mbalimbali za jadi za sanaa za maonyesho na kuonyesha jinsi zilivyotumiwa na jamii za Kiafrika kabla ya kupigwa marufuku na Wazungu wakati wa ukoloni. Sifa mbalimbali za sanaa za maonyesho ya jadi ziliweza kuibuka na mipaka kati ya sanaa za maonyesho na tamthilia ya Kiswahili iliweza kudhihirishwa kama mbinu ya kuweka misingi ya utekelezaji wa utafiti wetu.

Katika sura inayofuata tunashughulikia uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti kwa mujibu wa lengo letu la kwanza la utafiti huu ambalo ni kupambanua tanzu za sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika na kufafanua jinsi zilivyotumiwa na watunzi wa tamthilia teule za Kiswahili kama mbinu ya utunzi wa tamthilia zao.

# SURA YA TANO

# SANAA ZA MAONYESHO KATIKA TAMTHILIA YA KISWAHILI

## 5.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia matokeo ya utafiti kwa mujibu wa lengo la kwanza la utafiti huu ambalo ni kuchanganua tanzu za jadi za sanaa za maonyesho zilizotumika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Tuliweza kusoma, kuchambua na kuchanganua kwa lengo la kuvitambua na kuvihakiki kwa undani vitanzu vyote vya sanaa za maonyesho ya jadi vya asili ya utamaduni wa Kiafrika vilivyotumiwa na watunzi Ebrahim N. Hussein, Saidi A. Mohamed na Emmanuel Mbogo katika utunzi wa tamthilia zao teule. Tulifikia lengo hilo kwa kujibu swali: Watunzi wa tamthilia za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* wametumia vipi tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia teule za Kiswahili?

Tamthilia zote zilizochaguliwa zimebuniwa kwa ajili ya kuigizwa jukwaani sababu ambayo inazifanya kuwa tamthilia zenye misingi ya ki-Aristotle. Licha ya misingi hii ya ki-Aristotle, watunzi wa tamthilia tulizozitaja wamechota tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na kuzitumia kisanaa katika kubuni na kuimarisha fani ya tamthilia hizo zao. Matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ulituwezesha kubainisha tanzu zilizochotwa kutoka kwa utamaduni wa Kiafrika na kuchunguza namna watunzi wa tamthilia hizo walivyozitumia kisanaa katika kubuni tamthilia ya Kiswahili ya kisasa kama inavyofafanuliwa hapa chini.

## 5.1 Sanaa za Maonyesho katika Tamthilia ya *Mashetani* – Ebrahim Hussein

Mtunzi Ebrahim Hussein wa tamthilia ya *Mashetani* iliyoteuliwa kwa utafiti huu, alizaliwa mwaka wa 1943 kule pwani ya kusini ya nchi ya Tanzania, mkoani Lindi. Hussein ana tajriba kubwa katika utunzi wa michezo ya kuigiza inayojumuisha sanaa

za maonyesho na maigizo ambayo imempa umaarufu wa kipekee katika kanda ya Afrika Mashariki na katika utunzi wa tamthilia za Kiswahili. Kama msomi aliyehitimu na shahada ya uzamifu katika Kiswahili na Fasihi kutoka Chuo Kikuu cha Humboldt, Ujerumani, Ebrahim Hussein amefundisha maigizo na sanaa za maonyesho katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzia mwaka 1975 hadi 1985 na kustaafu mwaka 1988. Vilevile, Hussein alipata kushinda tuzo ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu wa Tanzania (UWAVITA) kama mwandishi bora wa maigizo ya Kiswahili.

Michezo ya kuigiza ya kwanza aliyoitunga Ebrahim Hussein ilikuwa *Alikiona* (1967) na *Wakati Ukuta* (1969) ambayo imeakisi masuala ya migongano na mabadiliko ya kijamii katika tamaduni za Kiafrika. Hussein alitunga michezo mingine ya kuigiza ya *Kwenye Ukingo wa Thimu* (1988), *Kinjeketile* (1969), *Mashetani* (1971), *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* zote zilizotungwa katika mwaka wa 1976. Kazi zake zote za michezo ya kuigiza zimeshughulikia masuala mbalimbali ya migogoro ya kijamii, ukoloni, utabaka, ukoloni mamboleo, ukombozi, uongozi mbaya, ubadhirifu na ufisadi. Mchezo wake mwingine wa “Sokomoko” haujawahi kuchapishwa.

Katika mapitio ya watafiti, ilibainika kwamba mtunzi Ebrahim Hussein amebuni tamthilia zake zote kwa mtindo na umbo la ki-Aristotle. Hata hivyo, Hussein vilevile alipiga hatua na kuzifanyia majaribio sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika kwa kuziingiza na kuzitumia mbinu mbalimbali za sanaa hizo katika ubunifu wake katika kuibuka na tamthilia zake hususan tamthilia ya *Mashetani*. Mbinu za sanaa za maonyesho ya jadi alizozichota na kuzitumia katika utunzi wake zinadhihirika kupitia kwa sherehe na miviga ya kijamii pamoja na mbinu asili za uzalishaji mali kama matambiko, mazingaombwe, pamoja na shughuli zingine za kijamii na maisha ya kawaida kama jando, unyago, arusi, matanga miongoni mwa tanzu nyingine

zinazowasilishwa kupitia kwa mbinu mbalimbali za sanaa za maonyesho kama majigambo, masimulizi, malumbano ya utani, nyimbo na ngoma (Mbogo 1993). Tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilizodondolewa kutoka kwa tamthilia ya *Mashetani* zinawalishwa katika jedwali 5.1 hapa chini:

**Jedwali 5.1: Tanzu za Sanaa za Maonyesho katika Tamthilia ya *Mashetani***

| | Utanzu wa sanaa za maonyesho | Mfano wa utanzu wa sanaa za maonyesho |
|---|---|---|
| i) | Majigambo | -Majigambo ya Shetani - uk 1 |
| ii) | Maigizo ya Mazingaombwe na miujiza ya Shetani | -Miujiza ya Shetani wakati wa kuigiza mchezo wa Shetani na Binadamu – uk1 |
| iii) | Fumbo la Shetani | -Fumbo la uhusiano wa Shetani na Binadamu –uk 2<br>-Mchezo wa Shetani na Binadamu – uk 2 |
| iv) | Masimulizi | -Uzungumzi nafsi wa Binadamu baada ya kumuua Shetani – kr 8 – 9<br>-Hadithi ya chewa – uk 28 |
| v) | Nyimbo na Ngoma | -Wimbo wa Binadamu chini ya mkuyu kusherehekea kumuua Shetani - kr 9 – 10<br>-Wimbo wa Baba Kitaru wa kusherehekea kununua gari – kr 21 – 22<br>-Shairi la Upweke la Juma - kr 41 - 42 |
| vi) | Malumbano ya utani na mchongoano | -Utani kati ya Mama Kitaru, Kitaru na Juma kr - 14 - 15 |

***Chanzo: Data za utafiti kutoka kwa tamthilia ya Mashetani* – Ebrahim Hussein**

Jedwali 5.1 hapa juu linaonyesha data ya tanzu za majigambo, maigizo ya mazingaombwe na miujiza, fumbo la Shetani, masimulizi, nyimbo na ngoma, malumbano ya utani na mchongoano ambazo ni tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika zilizobainishwa kuwa zimetumiwa katika utunzi wa tamthilia ya *Mashetani*. Tanzu zilizotambuliwa zimefafanuliwa katika uchanganuzi unaofuata hapa chini.

### 5.1.1 Majigambo

Ebrahim N. Hussein amechota utanzu wa majigambo (Jedwali 5.1.) (i) wa sanaa za maonyesho ya jadi na kuutumia katika kubuni tamthilia yake ya *Mashetani*. Majigambo kwa mujibu wa Matei (2011) ni utungo wa kishairi ambao unaweza nusu kukaririwa au kughaniwa na nusu kusemwa. Majigambo yalipokaririwa au kutambwa katika jamii za Kiafrika, yaliambatanishwa na matendo ya uigizaji na mdundo wa ngoma. Katikati ya ngoma, mwanamme anayejigamba anajitokeza mbele ya hadhara, kujigamba na kisha kurudi kucheza ngoma. Aliyejigamba alibeba zana zake za kazi kutegemea kazi aliyoifanya kama ala za kivita ambazo alizitumia kuonyesha jinsi alivyotenda matendo yake ya kishujaa anayojigambia. Aidha, mwanamme aliyejigamba alivaa maleba kuambatana na kazi aliyoifanya au jambo la kishujaa lililomfanya kujisifu. Onyesho la Kwanza la Sehemu ya Kwanza ya tamthilia ya *Mashetani* linamdhihirisha mhusika Shetani akijigamba kwa jinsi ifuatayo;

Shetani: **Unanijua mimi nani?**
**Mimi Shetani.**
**Siyo jini wala kuhani**.
Mimi Shetani.
Uwezo wangu hauhifadhiki.
Wema wangu hauhesabiki.
Wema wangu hausemeki.
**Ninajenga.**
**Ninabomoa.**
**Ninadhalilisha nitakavyo**.
Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi
Mimi ni uwezo na uwezo ni mimi
(*Mashetani – uk. 1*)

Jigambo katika dondoo la hapa juu ni ukariri wa mhusika Shetani aneyetumiwa na Ebrahim Hussein kumbainisha dhalimu anayewadhulumu Waafrika katika mfumo mbaya wa utawala. Hussein anamfanya mhusika huyu kujigamba kwa kujitambua yeye ni nani na kueleza matendo yake ya uovu. Mhusika huyu anajitambulisha kwa kuuliza, "**Unanijua mimi nani? Mimi Shetani. Siyo jini wala kuhani** (*Mashetani –*

*uk. 1*)**.** Hivi ndivyo wahusika wanaojigamba wanavyojitambulisha katika ughani wao. Wahusika hawa huweza kusema majina yao na hata kutambua majina ya ukoo wao. Hutaja jina la baba yake na lile la mama yake mbali na kutaja mahali walikotoka. Mhusika huyu anaeleza kuwa yeye ni Shetani wala si kuhani. Mtunzi amelitumia jina Shetani kistiari na kwa makusudi ili kudhihirisha uovu wa mhusika huyu. Shetani ni stiari aliyoitumia mwandishi ili kumwakilisha mkoloni aliyemdhulumu Mwafrika katika utawala wake wa ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo.

Watu ambao huigiza utanzu wa majigambo hujisahau wanapojisifu na kujigamba kwa sababu ya ubingwa walioupata katika taaluma yao. Shetani katika dondoo hili anajisifu si kwa matendo mazuri bali kwa matendo yake mabaya yanayomwathiri Binadamu mwingine ambaye ni Mwafrika anayemshinda kwa nguvu. Shetani anajitapa na kujigamba kuwa ni yeye mwenyewe aliye na nguvu za kiajabu wala si kiumbe mwingine mwenye uwezo wa kiungu kama jini au kuhani. Shetani anaeleza kuwa uwezo wake hauna kifani na kutaja uwezo wake wa kujenga, kubomoa na kudhalilisha kama inavyoonyeshwa katika maandishi ya wino uliokolezwa hapa juu, "**Ninajenga. Ninabomoa. Ninadhalilisha nitakavyo**" - (*Mashetani, uk -1)* Majigambo ya Shetani). Mkoloni anayewakilishwa na mhusika Shetani anajigamba kwa kiburi kikubwa kwa Mwafrika anayewakilishwa na mhusika Binadamu katika jigambo hili kuwa yeye anazo nguvu na uwezo mkubwa wa kumjenga, kumbomoa au kumdhalilisha anavyotaka. Huu ndio udhalimu ambao wakoloni (Shetani) waliwafanyia Waafrika katika kipindi cha kulitawala bara la Afrika.

Kama tulivyoeleza hapa juu, wakati wa kughani majigambo, mhusika anayejigamba hujitoa mhanga na kuigiza matendo fulani hadharani huku akinengua maungo yake kwa namna ya kufanya maonyesho ya kisanaa. Mhusika Shetani anajigamba kwa

kusema maneno kwa ufasaha ambayo anayawasilisha kwa lugha ya mkato na ya kishairi. Majigambo yalitumiwa na wahusika mashujaa waliofanikiwa katika matendo fulani yaliyoiletea jamii mafanikio ya aina fulani, kwa mfano ushindi katika vita au mieleka miongoni mwa mengine. Licha ya ubahili wa mhusika Shetani, maneno anayoyatumia katika majigambo yake yana mvuto mkubwa. Wanaojigamba katika utamaduni wa Kiafrika huwa ni wahusika mashujaa waliofanya matendo makubwa kwa jamii na wenye kipawa cha ulumbi. Kinyume na hali hii ya utamaduni wa Kiafrika, Hussein alimtumia mhusika Shetani kujigamba kwa lugha fasaha kama wafanyavyo mashujaa wa Kiafrika lakini kwa kuwafanyia Waafrika maovu. Hii imekuwa mbinu mwafaka iliyomwezesha mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* kuwasilisha dhamira zake za udhalimu wa mkoloni kwa njia ya kuvutia.

### 5.1.2 Maigizo na Miujiza ya Shetani

Tamaduni za jadi za Kiafrika zilibarikiwa kuwa na sherehe na matukio mengi ya kijamii ambayo ndiyo kwayo tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilitekelezwa na jamii. Kupitia kwa utekelezaji wa sherehe za pungwa, mahoka, mazingaombwe, miujiza miongoni mwa nyingine wanajamii waliweza kudhihirisha ubunifu wao wa kisanii. Watunzi kama zao la jamii, vilevile waliweza kuzisoma mbinu hizo kupitia kwa maigizo ya kila siku ya sanaa za maonyesho na tungo za Fasihi Simulizi za jamii zao na kuweza kuzijumuisha katika utunzi wa kazi zao za tamthilia andishi.

Ebrahim Hussein amechota mbinu zake za utunzi kutoka kwa tamaduni hizi za Kiafrika na kuzitumia kiubunifu katika utunzi wa tamthilia yake ya *Mashetani* kwa njia ya majaribio ili kubuni tamthilia asili ya Kiswahili. Katika ukurasa wa kwanza wa Onyesho la Kwanza, sehemu ya Kwanza ya tamthilia ya *Mashetani*, mtunzi amechota na kutumia mbinu ya mchezo wa kuigiza kupitia kwa mchezo wa Shetani na Binadamu ambapo kuna mazingaombwe au miujiza ambayo katika jamii zingine za

Kiafrika huchukuliwa kuwa imani za kiuchawi na kuzitumia katika utunzi wake kama inavyoonyeshwa hapa chini:

> Tazama muujiza. (*Anajibadilisha*) Sasa mimi nani?
> BINADAMU: Kama ndege … vile … ndege.
> SHETANI: **Sawa. Nimejigeuza ndege. Ninaweza kadhalika kuwa upepo, nikawa kila mahali. Naweza kuwa nafsi, nikaingia katika roho yako au ya wenzako. Sasa tazama. Unaona nini?**
> BINADAMU: Unarukia tawi.
> SHETANI: Na sasa, unaona tawi?
> BINADAMU: **Tawi limegeuka kiti.**
> SHETANI: **Umeshuhudia miujiza. Nimekuonesha miujiza ili uamini uwezo wangu.** (*Anakaa juu ya kiti kwa upole na huruma*). Usiogope, usiogope. Kwako wewe mimi rafiki. Wala hutapata rafiki kama mimi. (*Anabadilika kwa ukali*). Unaniogopa?
> BINADAMU: Ndiyo.
> SHETANI: Unanicha
> BINADAMU: Ndiyo.
> SHETANI: Unaninyenyekea?
> BINADAMU: Ndiyo.
> SHETANI: Mbona siuoni unyenyekevu wala uoga katika uso wako?
> BINADAMU: Kipitacho moyoni si lazima kionekane usoni.
> SHETANI: Sijali kipitacho moyoni. Ninajali kionekanacho usoni. Onesha kwa dhahiri ninachotaka kukiona *(anacheka)*. Baadaye utafahamu kuwa uso ukizoea kuonesha kinachotakiwa kuonekana, na sicho kinachopita moyoni, basi wakati utauzoea moyo usifarikane na uso wake. Unaelewa nasema nini?
> (*Mashetani - uk 2*)

Maigizo ya mazingaombwe kati ya wahusika Shetani na Binadamu katika dondoo la hapa juu, ni utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi alioutumia mwandishi kwa nia ya kudhihirisha mabadiliko ambayo mkoloni mkongwe anajifanyia na kuwa mkoloni mamboleo anayeendelea kuwadhibiti na kuwadhulumu Waafrika kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mhusika Shetani anasema hivi, "**Sawa. Nimejigeuza ndege. Ninaweza kadhalika kuwa upepo, nikawa kila mahali. Naweza kuwa nafsi, nikaingia katika roho yako au ya wenzako. Sasa tazama. Unaona nini? … Tawi limegeuka kiti … Umeshuhudia miujiza. Nimekuonesha miujiza ili uamini uwezo wangu.**" – (*Mashetani* - uk 2). Mhusika Shetani katika dondoo hili anamweleza mhusika

mwenzake Binadamu kuhusu uwezo wake wa kujibadilisha kimiujiza na kubadilika kuwa vitu mbalimbali. Maelezo ya Shetani yanafanana sana na masimulizi ya kifantasia yanayozungumzia masuala ya ajabu na ya kimiujiza katika sanaa za maonyesho za Kiafrika. Hussein amechota mbinu hiyo ya masimulizi ya Kiafrika na kuitumia katika kuendeleza dhamira yake ya kuonyesha jinsi wakoloni waliobanduliwa Afrika walivyojibadilisha kimiujiza kutoka ukoloni mkongwe na kuingia katika ukoloni mamboleo ili kuendelea kuwatawala Waafrika baada ya kujinyakulia uhuru.

Tamthilia ya *Mashetani* inazungumzia masuala ya kikoloni na ukoloni mamboleo yaliyoikumba nchi ya Tanzania kwa kutumia utanzu wa sanaa za maonyesho wa mchezo wa kuigiza wa *Mashetani* kama njia ya kuyaangazia matatizo yaliyoikumba nchi ya Tanzania na nchi zingine za bara la Afrika kwa jumla. Mchezo wa kuigiza ni utanzu wa maigizo katika sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika. Maigizo au mchezo wa kuigiza hurejelea mfuatizo na uigaji wa maneno au matendo ya watu wengine (King'ei na Kisovi - k.h.j.). Utanzu wa maigizo umetumiwa Kimwingilianomatini na utanzu mwingine unaodhihirisha matumizi ya miujiza tulioueleza hapa juu ili kujenga utanzu mkubwa zaidi wa tamthilia ya *Mashetani* kutika mbinu ya mchezo ndani ya mchezo. Ebrahim Hussein anautumia mchezo wa Shetani ili kudhihirisha hali ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo inayoyakumba mataifa ya Afrika. Kwa kuyamulika matatizo ya nchi za Afrika kwa njia hii, Hussein anakusudia kuyafanya kuwa kichocheo cha kuzingatia usuluhishaji wa masuala fulani ya kimaisha na kueleza kuhusu maisha ya Mwafrika yalivyo hasa baada ya ukoloni mkongwe.

Hussein ametumia Juma na Kitaru ambao ni wahusika vijana walioelimika na wanaoelewana kimawazo ili kuwakilisha mawazo yanayokinzana. Mtunzi huyu hata hivyo anamtumia mhusika Kitaru kuelezea imani yake kuhusiana na uhusiano wa nchi za Afrika na nchi za Magharibi, utabaka na hali ya ukoloni mamboleo uliozikumba nchi za Afrika. Kupitia kwa mhusika Kitaru (*Mashetani* - Kr 24 - 25) Ebrahim Hussein anaeleza dhana ya Shetani kwa kuirejelea kuwa "**nafsi yenye ncha nyingi na kiumbe kinachomwingia Binadamu … na kumzuga akili"** kwa kusema ifuatavyo katika dondoo la hapa chini:

> **Shetani,** hii **ni nafsi yenye ncha nyingi, ni kiumbe kinachomwingia Binadamu kwa namna mbalimbali na kumzuga akili** … hadithi chungu nzima juu ya Shetani na Binadamu zinazoeleza vipi Shetani anavyomjia na kumghilibu kwa sura mbalimbali. (*Mashetani - kr 24 – 25*)

Mhusika Kitaru anadhihirisha kusumbuliwa sana na mawazo fulani wakati babake anapojaribu kumweleza mamake Kitaru kwamba baada ya kujinyakulia uhuru, Waafrika wanafaa kuwa katika mstari wa mbele kwa kufanya kazi nyingi kama yeye wala si kukaa nyuma na kuzembea. Baba Kitaru anapomuuliza Kitaru kuhusu linalomsumbua, Kitaru anaeleza kuwa anafikiri kuhusu mambo mengi pamoja na Mashetani. Licha ya babake kusema kwamba anaelewa Mashetani ni nani na kwamba hayafai kumpatia mtu fikra, Kitaru anamweleza hivi kuihusu athari ya Mashetani kwa Binadamu wa kawaida;

> "… Huoni, lakini kama **leo kila kitendo kina alama ya Shetani na kila mtu ana nafsi ya Shetani.**" *(Mashetani - uk 25*)

Matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya *Mashetani* yalikusudia kudhihirisha kwamba jamii za Kiafrika zinakumbwa na mikasa na matukio ambayo ni magumu kuyasuluhisha. Kama anavyosema Kitaru katika dondoo la hapo juu, matukio yanayozikabili jamii za Kiafrika hayako wazi. Matukio hayo ni yale yanayodhihirisha alama ya Shetani na kila mtu huwa na nafsi ya Shetani, "**leo**

**kila kitendo kina alama ya Shetani na kila mtu ana nafsi ya Shetani"** - (*Mashetani* - uk 25). Katika mazungumzo yao nyumbani kwa Kitaru, Juma na Kitaru wanauzungumzia mchezo wa Shetani na Binadamu walioigiza baina yao;

> KITARU: Acha maneno yako. Maneno ya kiShetani …
> JUMA: Naye kweli, namna gani siku ile? Ukakurupuka tu. Mi nikaogopa …
> KITARU: **Ndivyo unaogopa Mashetani bado? Lo! Hata sikudhani …**
> KITARU: **Unaogopa utakupanda nini?** (*Mashetani – uk 19*)

Binadamu wa kawaida huogopa Mashetani kwani katika tamaduni za Kiafrika yanaaminiwa kuwadhuru watu. Katika dondoo la hapa juu, mhusika Kitaru anamcheka na kumdhihaki Juma kuwa alionyesha kuogopa Shetani wakati walipokuwa wakiigiza mchezo wa Shetani na Binadamu kwa kusema, "**Ndivyo unaogopa Mashetani bado? Lo! Hata sikudhani … Unaogopa utakupanda nini? -** (*Mashetani – uk 19*). Katika jamii za Kiafrika, mashetani huwapanda Binadamu vichwa na kuwasababishia madhara jinsi Kitaru anavyosema katika dondoo.

Mchezo wa Shetani na Binadamu kati ya Juma na Kitaru ni mfano wa uigizaji unaopatikana katika sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika. Matukio mengi ya kijamii yaliigizwa katika fani hii ya michezo kama vita, jando, unyago, matanga, pungwa, kazi mbalimbali pamoja na shughuli ny ingine za kijamii na Ebrahim Hussein amechota utanzu wa mchezo wa kuigiza wa Shetani na Binadamu ili kumwezesha kujenga mawazo yake na kuyafanya kuwa tamthilia yake ya *Mashetani*. Maigizo ya kitamaduni na michezo mingine yalitumiwa na wanajamii kuonyesha jinsi walivyokuwa wakipambana dhidi ya hali mbalimbali za maisha ili kufanikisha maisha yao.

Ebrahim Hussein ametumia kunga ya maigizo na mchezo wa Mashetani katika tamthilia yake ili kudhihirisha tofauti za kimatabaka na kiuchumi zilizoko baina ya

jamii za Kiafrika baada ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru. Wafula (1999) anaeleza kuwa wahusika Kitaru na Juma wanacheza "mchezo wa Mashetani" ili waweze kuusaka uhusiano wa kimaana kati yao. Swali linaloibuka baada ya uigizaji wa mchezo huo ni ikiwa itawezekana kuwa na uhusiano mzuri baina ya Shetani na Binadamu baada ya mchezo wao.

### 5.1.3 Fumbo la Shetani

Hussein ametumia jina "Shetani" kimafumbo katika tamthilia yake ya *Mashetani*. Fumbo kwa mujibu wa Matei (2011) ni kauli zenye maana iliyofichika. Mafumbo hutumia lugha fiche au ya kistiari pamoja na tamathali nyingine za usemi. Matumizi ya mafumbo katika mazungumzo humhitaji anayeambiwa kuyadadisi mazingira yake na kufikiria kwa ndani ili kupata maana yao ya ndani. Kwa kawaida, maana ya kisemantiki ya maneno yaliyotumiwa katika fumbo huwa na maana ya nje ambayo huilaghai hadhira kufikiria maana ya fumbo kijuujuu. Dhana ya Shetani imetumiwa katika tamthilia y*a Mashetani* kuwakilisha kielelezo cha nguvu ambazo huwa pingamizi dhidi ya juhudi za Binadamu kujitawala.

Katika simulizi za asili ya utamaduni wa Kiafrika na kwingineko ulimwenguni, huwa kuna maelezo kuhusu kiumbe huyu dhahania anayeitwa Shetani ambaye humwogofya na kumtisha Binadamu wa kawaida. Vitendo vya kimachachari vya Shetani humfanya kuwa kiumbe wa ajabu aliye na uwezo wa kufanya mambo ya kimiujiza. Mhusika Shetani katika tamthilia ya *Mashetani* anajieleza kuwa kiumbe chenye maajabu mengi kama inavyodhihirika katika dondoo la hapa chini:

> Shetani: Unashuhudia miujiza
> Nimekuonyesheni miujiza ili
> Uamini uwezo wangu …
> … unaniogopa? - (*Mashetani -uk 2*)

Shetani huelezwa kuwa kiumbe katili aliyejaa matendo maovu kwa Binadamu. Uhusiano kati ya Binadamu na Shetani, kila wakati huwa mbaya. Shetani hawezi kutendewa uovu na Binadamu bali yeye ndiye humtendea Binadamu uovu. Katika tamthilia ya *Mashetani*, Shetani anamtendea uovu Binadamu ambaye amemtawala kisiasa, kiuchumi na kijamii. Katika ukatili wake, Shetani hawezi kutawaliwa na Binadamu bali yeye ndiye humtawala Binadamu. Maongezi baina ya Shetani na Binadamu yanadhihirisha uhusiano mbaya ulioko baina yao.

> Shetani: Unashuhudia miujiza
> Nimekuonyesheni miujiza ili
> Uamini uwezo wangu …
> … unaniogopa?
> Binadamu: Ndiyo.
> Shetani: Unanicha?
> Binadamu: Ndiyo.
> Shetani: Unaninyenyekea?
> Binadamu: Ndiyo.
> Shetani: Mbona siuoni unyenyekevu wako?
> Binadamu: Kipitacho moyoni si lazima kionekane usoni.
> Shetani: Sijali kipitacho moyoni. Ninajali kionekanacho usoni. Onesha kwa dhahiri ninachotaka kukiona. (Anacheka). Baadaye utafahamu kuwa uso ukizoea kuonyesha kinachotakiwa kuonekana, na sicho kinachopita moyoni, basi wakati utauzoeza moyo usifarakane na uso wake. (*Mashetani -uk 2*)

Sehemu ya kwanza ya maigizo haya kati ya Shetani na Binadamu ina maswali na majibu ambayo yanalenga kuonyesha jinsi Shetani anavyofanya jitihada kumtamalaki na kumnyanyasa Binadamu. Uhusiano kati ya Shetani na Binadamu katika sehemu hii ya mazungumzo ni ya bwana (Shetani) na mtumwa wake (Binadamu) ambao unawakilisha uhusiano wa nchi za Magharibi na nchi za Afrika. Nchi za Magharibi zinakusudia kuzidhibiti nchi za Afrika katika uhusiano wao wa kiuchumi ambapo zinakuza unyanyasaji. Katika uhusiano huu, nchi za Afrika zinazinyenyekea, kuziabudu na kuziogopa nchi za Magharibi kwa kufanya wanavyotaka wao.

Pamoja na namna Binadamu anavyoweza kunaswa kwa urahisi na hila za Shetani, maigizo kati ya wahusika Shetani na Binadamu yanasawiri uwezekano wa Binadamu kutawaliwa kimawazo na Shetani au nchi maskini za Afrika kutawaliwa na nchi tajiri za Magharibi. Binadamu ni stiara inayoigiza jinsi mtu anavyojizatiti kukabiliana na matatizo ya kiuchumi na kihisia. Shetani kwa upande mwingine ni taashira ya nguvu zinazomkinza Binadamu kutimiza malengo yanayomwainisha kama Binadamu.

### 5.1.4 Masimulizi

Utunzi wa tamthilia ya *Mashetani* umejumuisha mbinu ya usimulizi tendaji katika mbinu za utunzi wa tamthilia hiyo. Mara kwa mara kuna wahusika wanaosimulia mawazo yao moja kwa moja wakiwa mkabala na hadhira kama ilivyo katika sanaa za maonyesho ya jadi na Fasihi Simulizi kwa jumla. Vitanzu kama hadithi, mafumbo, vitendawili, majigambo, ushairi na vingine vilivyoshirikishwa katika utunzi wa tamthilia hii vina sifa ya usimuliaji unaopatikana tu katika sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika. Usimuliaji hushirikisha kuongoza katika uimbaji, kutamba hadithi, kutega vitendawili, kufumbia watu mafumbo, kujigamba, kughani au kukariri mashairi kama asemavyo King'ei (2005). Katika Sehemu ya kwanza, Onyesho la Kwanza la tamthilia ya *Mashetani*, Ebrahim Hussein anaanza utunzi wa tamthilia yake kwa kumfanya mhusika Juma kuisimulia hadhira litakalofuata katika mchezo wao kama inavyoonyeshwa katika dondoo la hapa chini:

> JUMA: **Wananchi; kwa mara nyingine chini ya mbuyu huu mimi Juma, na rafiki yangu Kitaru**, **tutakuonesheni mchezo wa Shetani na Binadamu**. Mimi nitakuwa Shetani na Kitaru atakuwa Binadamu. (*Mashetani - uk 1)*

Katika dondoo la hapa juu, mhusika Juma anaisimulia hadhira yake ambayo imekaa mkabala na yeye kwa kuihutubia katika nafsi ya kwanza kuhusu mchezo wa Shetani na Binadamu yeye Juma na rafiki yake Kitaru waliokusudia kuuigiza mbele yao.

Katika masimulizi hayo, Juma anaeleza hivi; "**Wananchi; kwa mara nyingine chini ya mbuyu huu mimi Juma, na rafiki yangu Kitaru" -** (*Mashetani - uk 1).* Katika usimulizi wake, Juma anaita jina la hadhira yake iliyo mkabala na yeye kwa kutaja jina, **Wananchi**, kujirejelea yeye na Kitaru kwa kusema, "**mimi Juma, na rafiki yangu Kitaru"** na kutaja mahali usimulizi wao unakofanyikia kwa kusema, "**chini ya mbuyu huu."** Aidha, katika usimulizi huo, Juma anataja mada ya usimulizi wao kwa kusema, "**tutakuonesheni mchezo wa Shetani na Binadamu."** Vishazi hivi vya maneno vilivyotumiwa na mhusika Juma vinatoa ithibati ya matumizi ya mbinu ya usimulizi tendaji alioutumia mwandishi Ebrahim Hussein katika utunzi wa tamthilia yake. Mbinu ya usimulizi wa mhusika Juma imechotwa na mtunzi kutoka kwa tanzu mbalimbali za usimulizi za sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya utamaduni wa Kiafrika.

Masimulizi ya Juma kwa hadhira katika dondoo la hapa juu, yanafanywa kwa namna ya maelezo ya moja kwa moja ya mtunzi kuhusu namna jukwaa linavyofaa kutayarishwa ila mabadiliko ni kwamba huyu ni mhusika anayeizungumzia hadhira na kuieleza litakalofuata jukwaani. Mtunzi ameitumia mbinu hii ya sanaa za maonyesho ya jadi ili kuishawishi hadhira iendelee kuutazama au kuusoma mchezo hadi mwisho ili kufikia matokeo ya matendo ya uigizaji. Baadaye katika mchezo huohuo wa Shetani na Binadamu, mtunzi vilevile anadhihirisha mbinu ya usimuliaji wa wahusika kwa kuwafanya kuzungumza na hadhira moja kwa moja. Baada ya kumuua mhusika Shetani, mhusika Binadamu katika uzungumzi nafsi anasimulia hivi;

> **Amekufa, nimemuua! Nimemuua!**
> Nimemuua, au alitaka nimuue?
> Umepata kumsikia nani akajichinja mwenyewe? Aakh, mawazo gani …mawazo mabovu kabisa. Nimemuua nimemuua, basi. Fikira mbovu hizi za kazi gani? Alikuwa anacheka huku akifa! Kuna mtu akacheka huku anakufa? Alijua, siyo alijua, aliamini kama hafi.

> Maana ukisema alijua ina maana kuwa kweli kitendo kimetokea kama alivyofikiria. Aliamini bora. Aliamini kama hafi.
> Fikira gani hizi zinazonijia? Ninagombana na kuzungumza na nafsi yangu kama mwenye wasiwasi, nisiye na imani na kitendo nilichofanya? (*Kimya*) Kisu … nani alinipa kisu, yeye? (*Fikira zinazomjia zinamuogopesha*)
> Ina maana … haiwezi kuwa … Nikiamini hivyo … basi yeye hakufa …! Hata kidogo! Ina maana kuwa huu wote ulikuwa mchezo tu. Stihizai. Shere. Ngoja, ngoja. Hebu jidhubutu kwanza. Weka akili yako juu ya kitu kimoja – **kisu! Kweli kisu kanipa yeye.** Lakini kanipa kwa sababu alikuwa hana njia ila anipe tu. Kama hangenipa, alijua, ningekichukua kwa nguvu. **Ndiyo maana kanipa. Hapana! Hakuniingia katika hali yangu, wala katika nafsi yangu. Wala kifo chake hakikuwa stihizai. Yeye amekufa, nimemuua. Na mimi niko hai, nimejidumisha. Mimi ni mimi, mimi mtupu wala si mimi ganda, au kiti cha Shetani, hata kidogo.** Mimi siyo kivuli, wala sanamu, wala bandia, bali mimi ni mimi mtupu – ngozi, damu na mfupa.
> (*Mashetani* - *kr 8 – 9*)

Binadamu kumuua Shetani katika masimulizi ya dondoo la hapa juu (**Amekufa, nimemuua! Nimemuua!**), ilikuwa taashira ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru kutoka kwa Wazungu mabepari. Kwa muda mfupi, nchi za Afrika zilijinyakulia uhuru lakini hazikuweza kujisimamia. Huu ulikuwa uhuru wa bendera tu lakini Waafrika hawakujinyakulia mamlaka na madaraka kamili ya kujifanyia mambo yao ya ndani bila kuomba msaada wa mawazo, hali na mali kabla ya kuyatekeleza majukumu yao wenyewe. Mtunzi ametumia mbinu ya usimulizi wa nafsi ya kwanza katika dondoo la hapo juu kuelezea jinsi Mwafrika alivyopigania uhuru wake au alivyopewa uhuru kutoka kwa mkoloni na akadhani kwamba amejisimamia na Mzungu mbeberu kurudi kwao Ulaya. Badala yake, Mwafrika anagundua kuwa Mzungu anayerejelewa kijazanda kwa jina Shetani hakufa wala hakutoka Afrika licha ya kumkabidhi uhuru kwa mikono yake mwenyewe (**kisu! Kweli kisu kanipa yeye - *uk 9***), bali alijibadilisha kama Shetani na kurudi kwa njia ya ukoloni mamboleo. Mwafrika pia anajigamba kuwa mkoloni hakumzuga na kumwingia akilini kwa nia ya kumteka mawazo - **Hakuniingia katika hali yangu, wala katika nafsi yangu. Wala kifo**

**chake hakikuwa stihizai. Yeye amekufa, nimemuua. Na mimi niko hai, nimejidumisha. Mimi ni mimi, mimi mtupu wala si mimi ganda, au kiti cha Shetani, hata kidogo – *uk 9*.** Ukweli ni kwamba Afrika imetekwa na kutawaliwa na nchi za Kimagharibi kimawazo na kamwe Afrika haiwezi kujitegemea yenyewe. Mtunzi ametumia usimulizi wa Binadamu vilevile kwa ajili ya kuonyesha msimamo wake kuhusu uhuru waliojinyakulia Waafrika wakidhani wamejisimamia na kujifanyia mambo yao wenyewe.

Ili kusherehekea uhuru waliojinyakulia kutoka kwa mabeberu waliowatawala, kwa haraka nchi za Afrika zilibuni nyimbo na ngoma na kuziandamanisha na michezo ya kuigiza ili kuelezea furaha yao. Waafrika hawakuanza kufanya kazi mara moja punde tu baada ya kujinyakulia uhuru ili kujiendeleza kiuchumi na kuwawezesha kujitegemea, bali walianza kufanya tamasha za ngoma na nyimbo ili kusherehekea uhuru wao. Nyimbo na ngoma hizi pia zimepata nafasi katika utunzi wa Ebrahim Hussein ambaye amezitumia kiubunifu kutunga tamthilia yake na kuwadhihaki Waafrika kwa jinsi walivyoupokea na kuusherehekea kwa anasa uhuru walioupata kwa tabu kama ilivyoelezwa baadaye hapa chini.

Mtunzi vilevile amevuma tamthilia yake kwa kuingiza usimulizi wa aina ya hadithi. Hapa Hussein amemfanya mhusika wake kusimulia kisa kupitia kwa kuwapa wahusika wake lugha, matendo ya kuiga na kuwavisha uhalisia ili kusimulia kisa kama mtunzi mwenyewe (Mutembei, 2010). Akimweleza mama yake kuhusu hadithi moja ambayo Bibi yake Juma alikuwa amewasimulia, mtunzi Ebrahim Hussein katika sehemu ya II, onyesho la III la tamthilia yake ya *Mashetani* anamfanya Kitaru kuisimulia hadithi hiyo ya mnyama hatari anayeitwa Chewa na anayeishi kule mbali katika bahari saba kama ifuatavyo:

> KITARU: Nilikuwa nafikiri hadithi.
> MAMA: Hadithi!
> KITARU: …
> MAMA: Hadithi! Hadithi gani?
> KITARU: Hadithi ya chewa. Mbali sana, ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa. Chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake. **Anaweza kutoka huko aliko, kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa tu na mkondo wa maji, akitaka asitake**. Na huyu chewa siyo chewa bali Shetani. (*Mashetani - uk 28. Msisitizo ni wetu*)

Kupitia kwa hadithi ya chewa katika dondoo la hapa juu, ambaye ni mnyama aishiye katika bahari ya mbali, mtunzi anawezeshwa kusimulia kuhusu mkoloni ambaye alivuka "bahari saba" ili kufika Afrika kuja kumtawala na kumdhulumu Mwafrika. Hadithi ya Kitaru inaandamana na fomula ya ufunguzi pale jina "hadithi" linarudiwa mwanzoni mwa usimuliaji wa hadithi hiyo kama ilivyo katika utanzu wa hadithi za kimapokeo za sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika. Fomula ya ufunguzi ya hadithi hii imebadilishwa na mtunzi kwa kuifanya kuwa swali linalojibiwa na mhusika wa pili ambaye anafaa kuwa hadhira ya msimuliaji ili kuafiki muundo wa tamthilia na mtindo wake wa utunzi na uwasilishaji wa hadithi hiyo. Kupitia kwa hadithi hii, mtunzi anasimulia kuhusu ulafi wa mkoloni wa kuwanyang'anya Waafrika mali yao kwa nguvu na kuipeleka kwao ughaibuni ***(… akivuta pumzi … maji yote yanaingia kinywani mwake)*** huku akimdhibiti na kumlazimisha mtawaliwa wake kutenda anavyotaka yeye bila hiari yake. Uwezo mkubwa alionao mkoloni kama ule wa chewa unamwezesha kumlazimisha mtawaliwa Mwafrika kukubali mahitaji yake kwa lazima au hata kumwangamiza katika kumlazimisha kukubali masharti yake - (*Anaweza kutoka huko aliko, kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa tu na mkondo wa maji, akitaka asitake*). Mkoloni analinganishwa na Shetani ambaye haeleweki na ambaye ana nguvu za kiajabu.

### 5.1.5 Nyimbo na Ngoma

Mtunzi Ebrahim Hussein ametumia tanzu za nyimbo na ngoma za sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia yake ya *Mashetani*. Baada ya kumng'oa mbeberu kutoka bara la Afrika na kujinyakulia uhuru wao, Hussein anazionyesha kwa njia ya kuzidhihaki jinsi nchi za Afrika zilijitungia nyimbo na kucheza ngoma ili kusherehekea uhuru wao. Wimbo wa Binadamu katika kurasa za tisa hadi kumi za tamthilia ya *Mashetani* ni mfano wa nyimbo na ngoma ambazo Waafrika walijitungia na kucheza ili kusherehekea uhuru wao inavyodhihirishwa katika dondoo lifuatalo:

> (*anapiga vigelegele vya furaha. **Anarukaruka na kuizunguka maiti kwa furaha kubwa**. Anacheka mpaka michozi inamtoka. Anacheka mpaka furaha na kicheko vinamlevya. Anauendea ule mbuyu kwa haraka na huku anacheka. Anaimba*) - (*Mashetani* - kr 9 – 10).

Mtu kwa kawaida hachezi na kurukaruka kwa furaha kubwa huku akiizunguka maiti kama inavyodhihirishwa katika dondoo la hapa juu, "***Anarukaruka na kuizunguka maiti kwa furaha kubwa."*** Hussein anaonyesha kijazanda jinsi Waafrika walivyotunga nyimbo na kucheza ngoma huku akiizunguka "maiti." Maiti ni jina la kistiari alilolitumia mtunzi kurejelea wakoloni walioshindwa na Mwafrika katika vita vya kupigania uhuru. Mkoloni aliyetoka Afrika baada ya ukoloni amemithilishwa na maiti. Maiti haina tena uwezo wa kulitawala bara la Afrika kwa sababu haina uhai. Kwa misingi hiyo, Mwafrika anasherehekea kupata uhuru baada ya kifo cha mkoloni kwa kuimba na kucheza ngoma kama Waafrika wafanyavyo baada ya kufanikiwa kutenda jambo kubwa.

Katika stiari ya mchezo wa Shetani na Binadamu katika Onyesho la Kwanza la Sehemu ya Kwanza ya tamthilia ya *Mashetani*, Binadamu anamuua Shetani kwa kumchoma kisu katika mabavu yake ishara ya Mwafrika kumshinda Mzungu mkoloni na kumwondoa barani Afrika na hivyo kujinyakulia uhuru. Kifo cha mhusika Shetani

kinaashiria mwisho wa utawala wa kikoloni katika nchi za Afrika. Mkoloni anakufa kimwili kuwakilisha Mwafrika kujinyakulia uhuru wa bendera. Baada ya ushindi huo dhidi ya Shetani, Binadamu anayemwakilisha Mwafrika aliyejinyakulia uhuru wake kutoka kwa mkoloni, anaimba chini ya mbuyu kama inavyoonyeshwa katika dondoo la hapa chini:

(…*Anauendea ule mbuyu kwa haraka na huku anacheka. Anaimba*)
Binadamu: Wako wapi walio wakijitapa?
Sasa twawataka.
Wako wapi walio wakijitapa?
Sasa twawataka.
Tumekwisha (*anacheka*) wakamata
Wakamata.
Tumekwisha wabwatabwata.

Wako wapi waliokuwa juu jana?
Sasa twawataka.
Wako wapi waliokuwa juu jana?
Sasa twawataka.
Tumekwisha waangusha
Waangusha.
Tumekwisha wasagasaga.

Tumekwisha wakamata
Wakamata.
Tumekwisha wabwatabwata

Tumekwisha waangusha
Waangusha.
Tumekwisha wasagasaga.
(*Mashetani - kr 9 – 10*)

Ushindi wa nchi za Afrika katika kujinyakulia uhuru, kulizifanya nchi hizo kujitungia nyimbo za kusherehekea ushindi wao ambapo walijitapa na kujigamba kuhusu mafanikio yao kwa maneno "*wako wapi walio wakijitapa … tumekwisha wakamata … wako wapi waliokuwa juu jana … tumekwisha waangusha … tumekwisha wasagasaga … tumekwisha wabwatabwata*." Mtunzi anatumia mbinu ya kurudiarudia ujumbe wa kuwashinda mahasimu wao katika mapambano ya kujinyakulia uhuru wao. Baada ya kusherehekea kujinyakulia uhuru wao kwa nyimbo na ngoma za

furaha na vigelegele kwa muda mrefu, nchi za Afrika zinatambua ukweli kwamba haziwezi kujitawala na kujitegemea kiuchumi zenyewe.

Kila mara baada ya nchi za Afrika kushindwa kujisimamia na kujitegemea kama alivyofanya Shetani alipojigeuza na kujirusha juu ya tawi la mti, nchi hizo zilimlaumu Mzungu kuwa ndiye anayesababisha kuanguka kwao. Ukweli ni kwamba punde tu baada ya kujinyakulia uhuru wao, Waafrika wengi waliingiwa na unafiki wa mabepari waliokuwa wametoka na kuanza kujilimbikizia mali kwa njia ambazo si halali huku wakitumia mali kwa njia ya ubadhirifu kwa mawazo potovu kwamba huu ulikuwa wakati wa Mwafrika kula kama alivyoeleza mhusika MTU 1 katika dondoo la hapa chini:

> MTU 1: Wewe … wewe sijui namna gani unajiweka nyuma kama mkia. Bwana huu sasa wakati wetu. Mwafrika sasa ale vizuri, akae mahali pazuri, avae vizuri … nataka tuwaone Waafrika wana ndege, mali zao wenyewe.
> (*Mashetani - kr 43 – 44*)

Mawazo haya ndiyo yaliyowaongoza wafanyakazi wengi wa Kiafrika kuanza kuibia serikali za nchi zao ili kujinyakulia mali ambayo hawakufaa kuwa nayo. Baada ya nchi ya Tanzania kujinyakulia uhuru, mali iliyokuwa inamilikiwa na wazungu na mabwanyenye wengine ilitwaliwa na kutaifishwa na serikali. Mabadiliko haya katika mfumo wa siasa, utawala na uchumi wa jamii ya *Mashetani* yaliifanya familia ya Juma inayosimuliwa na Hussein katika tamthilia yake na iliyokuwa juu kiuchumi kabla ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru (wakati wa ukoloni mkongwe) kuwa chini kiuchumi, ilhali familia ya Kitaru ambayo ilikuwa chini kiuchumi wakati wa ukoloni ikajibadilisha kama Shetani na kupanda ngazi kijamii, kisiasa na kiuchumi na kuwa katika upeo wa matabaka. Baba ya Kitaru katika mfumo huo mpya, anakuwa mbadhirifu wa mali ya umma ambapo anajilimbikizia mali anavyopenda kwa kujinunulia magari mapya ya bei ghali. Baada ya kununua gari jipya, Baba Kitaru

anacheza na kuimba kwa kiburi na majitapo mbele ya mke wake, Kitaru na Juma ambao kiubunivu Ebrahim Hussein anawafanya hadhira kwa namna ifuatayo;

BABA KITARU: (*anaimba*)
Papa pa pa pa pa
I like some money
Papa pa pa pa pa
I like some money.
Papa pa pa pa pa
(*Mama Kitaru anaingia*)
A very good life.
Papa pa pa pa pa
(*Anamchukua mkewe kucheza*)
A very beautiful wife.
…
A very good life …
BABA KITARU: Njooni hapa dirishani. Unaiona nini?
MAMA KITARU: Gari mpya! Benz!
BABA KITARU: Yangu! Naam! Mali yangu, jasho langu. Kitaru, njoo uitazame. Juma, njoo. Mnaiona? Tazama ilivyotulia. Basi pale itoneshe tu – waaaah, linaruka kama ndege. Twendeni tukatembee, mnasemaje? Twendeni, twende, twende.
(*Mashetani - kr 21 -22*)

Wimbo huu wa Baba Kitaru unaiga usimulizi tendaji unaotekelezwa na fanani jukwaani akiwa ana kwa ana na hadhira yake katika sanaa za maonyesho ya jadi. Katika utendaji wa wimbo huu, Baba Kitaru anaongoza katika kuimba wimbo wa kusherehekea kwake kununua gari jipya linalobadilisha maisha yake kuwa “mazuri” kama anavyosema mwenyewe katika wimbo huu. Matumizi ya lugha ya Kiingereza katika wimbo wa Baba Kitaru unatumiwa na mtunzi kudhihirisha utabaka katika jamii za Kiafrika baada ya watu wachache kujinyakulia mali ya wizi na kupanda ngazi kazini mwao. Uwasilishaji wa wimbo huu wa kisasa unafanywa kwa njia zinazopatikana tu katika sanaa za maonyesho ya Kiafrika.

### 5.1.6 Tamthilia kama Utanzu wa Ushairi

Tamthilia ya *Mashetani* imeandikwa kwa mfumo wa kishairi kama zilivyo tamthilia za ki-Aristotle. Tamthilia ya ki-Aristotle ilihitaji kuimbika wakati wa uigizaji wake.

Hivyo tamthilia yenyewe iliandikwa kwa mishororo mifupimifupi ambayo ingeweza kuimbika kishairi. Mbali na kujumuisha sifa za ushairi simulizi katika utunzi wa tamthilia zao, watunzi pia hujumuisha nyimbo na mafungu ya mashairi mwanzoni na mwishoni mwa kila onyesho la tamthilia ili kuivutia na kuinasa nadhari ya hadhira katika uwasilishaji wao. Katika kuzungumzia matatizo yaliyozikumba nchi za Afrika baada ya kujinyakulia uhuru wao, Ebrahim hussein anamtumia mhusika wake Juma kusema shairi lifuatalo:

JUMA: Upweke.
Upweke una mbawa
Unarusha nyoyo za Binadamu juu kabisa.
Chini linabakia ganda.
Macho yanaona, akili inafikiri …
Lakini …kiwiliwili hakihisi.
(*Anacheka polepole*)
Bibi anapuliza sumu.
Sumu au mapenzi?
Jaribu kupambanua:
Mapenzi hugeuka sumu ...
(*Mashetani - kr 41- 42*)

Mtunzi anautumia ushairi wake katika dondoo la hapa juu kusimulia na vilevile kuhakiki hali sambamba inayotokea kati ya maonyesho mawili katika meza mbili mkahawani ambapo wahudumu wawili Waafrika wanajaribu kufafanua hali ya Waafrika inavyofaa kuwa baada ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru wao. Hali ni kinyume na hiyo katika meza nyingine inakobainika kupitia kwa maelezo ya wahusika ambao ni wahudumu wa pale mkahawani kuwa mashirika mengi yanayoongozwa na Waafrika baada ya uhuru yanafilisika baada ya viongozi wao kuiba na kujilimbikizia mali ya umma. Matumizi ya utanzu wa ushairi katika utunzi wa tamthilia ya *Mashetani* yanadhihirisha usanii unaohusisha mwingiliano wa tanzu. Mtunzi vilevile anatumia lugha ya kishairi ili kuwasilisha ujumbe wake kwa ajili ya kuivutia hadhira yake.

### 5.1.7 Malumbano ya Utani na Mchongoano

Mtunzi ametumia tanzu za malumbano ya utani na mchongoano katika utunzi wa tamthilia ya *Mashetani*. Malumbano ya utani kama wasemavyo King'ei na Kisovi (k.h.j.) ni kipera cha utanzu wa mazungumzo katika sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika ambacho kina maana ya kumfanyia mtu dhihaka, stihizai, mzaha au masihara bila kukusudia kumkera. Utani kama kiungo cha mila na tamaduni za jamii nyingi za Kiafrika huwawezesha wanajamii kutaniana bila ya kuogopa kukaripiwa au kufanyiwa mashtaka. Mtunzi ametumia malumbano ya utani katika Onyesho la Kwanza la Sehemu ya Pili pale ambapo Kitaru na Juma wanafanyiana utani mbele ya Mama Kitaru ambaye kulingana na mila na tamaduni za jamii ya mtunzi hawafanyiani utani. Malumbano ya utani huwa na miiko yake kutegemea jamii inayohusika. Mazungumzo ya Juma, Kitaru na Mama Kitaru yanafanyika ifuatavyo kudhihirisha matumizi ya utanzu wa malumbano ya utani:

> MAMA; **Mwenziyo anakuita huku. (*kwa Juma*) Basi alikuwa kalala hivyo. Kila saa mtoto yuko chumbani. Sijui anafanya nini huko chumbani peke yake. Amegombana na wakwe zetu nini huko nje?** (*Wanacheka*)
> KITARU; Ah, Mheshimiwa.
> JUMA; Unasemaje chief. Ninasikia unalala tu. ***Holiday*** inakupa ***time*** kidogo.
> KITARU; Acha bwana na wewe. Njoo ukae. Unasimamasimama nini? (*Anatoa soda katika friji*)
> JUMA; I say, bure unafungua …
> KITARU; Huachi. Sasa ulitaka kuniambia nini?
> JUMA; Haya basi, nitakunywa.
> KITARU; Mpaka ubembelezwe. Ma, hebu muandikie kadi Mheshimiwa ***umualike aje katika party***. Maana hivi hivi hainywi hii soda.
> MAMA; (*Anacheka*) Hebu niacheni. Hamna watani nini? Mwanifanya mimi mtani wenu, kwa nini?
> (*Mashetani - uk 15. Msisitizo ni wetu*)

Katika mazungumzo ya dondoo la hapa juu, Juma na Kitaru wanajaribu kujenga uhusiano mwema na kuondolea mbali uhasama na chuki yoyote ambayo inaweza

kuweko kati yao. Kama inavyodhihirika katika mazungumzo yao, kuna matumizi ya ucheshi yasiyodhamiria kuudhi katika kujenga malumbano hayo ya utani. Kitaru hapa anajaribu kumuumbua Juma mbele ya mama yake kwa kumwita "mheshimiwa" na kumwambia mamake amwandikie kadi ya mwaliko wa kuja kunywa soda ilhali wako pamoja chumbani. Ucheshi huu waweza kufanywa tu baina ya marafiki wanaofahamiana wenyewe. Katika hali kama hii, hakuna anayemkasirikia mwingine. Ingawa mama ya Kitaru anawakataza wasimwingize katika utani wao, mwenyewe anapomkaribisha Juma nyumbani kwake anamtania mwanaye Kitaru ambaye amekuwa akishinda akilala kutwa kwa njia ya kumzomea na kumrudi, "**Mwenziyo anakuita huku. (*kwa Juma*) Basi alikuwa kalala hivyo. Kila saa mtoto yuko chumbani. Sijui anafanya nini huko chumbani peke yake. Amegombana na wakwe zetu nini huko nje?** (*Wanacheka*)." Mzaha wa aina hii unaofanywa na mama hutumiwa kwa makusudi ya kumrudi yeyote ambaye ana mazoea mabaya kama mtoto ili afuate maadili ya kijamii. Wanaofanyiana utani huelewa mipaka yao. Wanaofanyiana utani vilevile ni wale wanaoelewa maana yake na wanajua kuweka heshima kati yao hata wakati ambapo utani unatumia ubeuzi mkali.

Utani ukiwa mkali kiasi kwamba unamuumbua mtu anayetaniwa hadi anafedheheshwa na kudunishwa, basi huo unakuwa ni mchongoano. Vijana wa rika moja ndio huweza kuchongoana. Mtu huweza kumchongoa mwingine kwa sababu ya kumwonea wivu, kumchukia au kwa sababu ya kutaka kumfanyia mzaha. Wakati mwingine utani haukusudii kumuudhi anayefanyiwa utani. Hata hivyo, mchongoano huudhi na unaweza kumfanya anayechongolewa kuudhika au hata kutokwa na machozi. Mchongoano unaweza kutokea kwa kuzingatia sio tu maumbile au wasifu wa nje wa mtu huyo bali pia tabia yake.

**5.2 Sanaa za Maonyesho katika Tamthilia ya *Pungwa* - Said A. Mohamed (2016)**

Tamthilia ya *Pungwa* imetungwa na mtunzi mashuhuri Said A. Mohamed aliyezaliwa Pemba, kisiwani Zanzibar tarehe 12 Desemba 1947. Said A. Mohamed alisomea shule ya wavulana ya Wete - Pemba na baadaye Kiembe Samaki kule kisiwani Unguja. Said A. Mohamed pia alisomea shule ya watoto wenye vipaji ya Darajani iliyokuwa kisiwani Unguja ambapo alihitimu na kujiunga na shule ya sekondari ya Gulioni ambayo hapo mbeleni ilikuwa inaitwa, "King George the VI" ambapo mapinduzi ya Zanzibar yalifanywa akiwa katika kidato cha pili. Said A. Mohamed alijiunga na Chuo cha Taaluma ya Ualimu cha Nkrumah TTC mjini Zanzibar katika mwaka wa 1966 baada ya kuhitimu masomo ya shule ya sekondari.

Katika tajriba yake ya kazi baada ya kuhitimu chuo cha ualimu, Said A. Mohamed alifundisha katika Shule ya Msingi ya Kizimbani kwa muda wa wiki mbili na Shule ya sekondari ya Utaani kuanzia 1969 hadi 1974 ambapo alifundisha Hesabu, Sayansi ya Viumbe Hai au Bayolojia, Kemia na Lugha ya Kiswahili. Ingawa masomo ya kidato cha tano na sita yalipigwa marufuku na rais wa mapinduzi wa Zanzibar wakati huo, hayati Sheik Abeid Karume, punde tu baada ya mapinduzi, Mohamed alipata nafasi ya kujiendeleza katika masomo hayo akiwa anaendelea na kazi. Kwa sababu ya kukosa maabara na vifaa vya kufanyia majaribio ya kisayansi kwa ajili ya masomo ya sayansi ya kidato cha tano na sita, Said A. Mohamed aliamua kusomea taaluma ya sanaa ambapo alisomea Lugha ya Kiswahili na Fasihi.

Mohamed alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika mwaka wa 1976 kusomea shahada yake ya kwanza ya Ualimu ambapo tena alibobea katika masomo ya Isimu na Fasihi ya Kiswahili. Shahada yake ilimwezesha kuajiriwa kama mwalimu mkuu wa shule za msingi na upili za Hamamni kule Unguja. Miaka mitatu baadaye, Said A. Mohamed alijiuzulu kazi yake ya ualimu na kujiunga tena na Chuo Kikuu cha

Dar es Salaam kusomea shahada ya uzamili katika Isimu Tekelezi. Ni wakati huu alipotambuliwa na mtaalamu wa Historia na Isimu Linganishi wa Kijerumani kwa jina Sigmund Bruner aliyemsaidia kupata fursa ya kusomea shahada ya uzamifu katika Chuo Kikuu cha Karl Marx Leipzig cha kule Ujerumani mwaka wa 1981 aliyoikamilisha mwaka wa 1985.

Baada ya masomo yake ya juu nchini Ujerumani, Said A. Mohamed alirudi nyumbani kwao Zanzibar ambapo aliteuliwa na Bw. Idris Abdul kuwa mkurugenzi wa pili wa Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (TAKILUKI) iliyobadilika baadaye na kuwa Chuo Kikuu cha Zanzibar – Suza. Kwa sababu za kisiasa,, Said A. Mohamed aliwacha kazi yake ya ukurugenzi chuoni nchini Zanzibar na kuhamia nchi ya Kenya ambapo alifundisha na kuwa mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Moi kuanzia mwaka wa 1987. Aidha, Said A. Mohamed alifundisha katika Chuo Kikuu cha Nairobi hadi 1990 alipoamua kuondoka Kenya kwa sababu za kibinafsi na kujiunga na Chuo Kikuu cha Osaka nchini Japan katika idara ya lugha za kigeni ambapo alipandishwa cheo hadi hadhi ya uprofesa katika chuo hicho. Baadaye alihama Osaka Japan katika mwaka wa 1999 na kujiunga na Chuo Kikuu cha Bayreuth nchini Ujerumani ambapo pia alifundisha hadi 2012.

Mohamed alishiriki mashindano ya kuandika hadithi fupi kwa lugha ya Kiswahili yaliyoandaliwa na Idhaa ya Kiswahili ya BBC. Hadithi zilizoshinda, zilichapishwa na kuwa vitabu. Hadithi iliyoibuka kuwa maarufu zaidi, ilikuwa hadithi ya "Sadiki Ukipenda" ambayo ilichangia katika kuenea na kukua kwa umaarufu wa Said A. Mohamed. Said A. Mohamed vilevile ana kipawa ambacho anadai alikirithi kutoka kwa mama yake mkubwa aliyemlea na ambaye alikuwa nyakanga na bingwa wa kuimba nyimbo za unyago na mafundisho ya dini ya Kiislamu. Said A. Mohamed ameandika vitabu vya kubuni zaidi ya hamsini na vitano vikijumuisha vifuatavyo:

**Tamthilia**

| | |
|---|---|
| *Pungwa* | (1988) |
| *Kivuli Kinaishi* | (1990) |
| *Amezidi* | (1995) |
| *Kitumbua Kimeingia Mchanga* | (2004) |
| *Mashetani Wamerudi* | (2016) |

**Hadithi Fupi**

| | |
|---|---|
| *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine* | (2002) |

**Ushairi**

| | |
|---|---|
| *Sikate Tamaa* | (1980) |
| *Kina cha Maisha* | |
| *Jicho la Ndani* | (2001) |

**Riwaya**

| | |
|---|---|
| *Asali chungu* | (1989) |
| *Babu Alipofufuka* | (2001) |
| *Utengano* | (1980) |
| *Tata za Asumini* | (1990) |
| *Dunia Mti Mkavu* | (2006) |
| Kiza katika Nuru | (1988) |
| Dunia Yao | (2006) |

Vitabu viivyoorodheshwa hapa juu ni baadhi tu ya vitabu vingi alivyoviandika na kuvichapisha mwandishi Said A. Mohamed katika maisha yake ya ubunifu. Said A. Mohamed ana umahiri mkubwa katika kubuni tanzu zote za Fasihi Andishi na ameweza kujumuisha sanaa za maonyesho na tajiriba zingine za Fasihi Simulizi katika utunzi wake wa kazi za Fasihi Andishi. Uteuzi wetu wa tamthilia ya *Pungwa* na *Mashetani Wamerudi* kutumiwa katika utafiti huu ulikuwa wa kimakusudi kwa sababu mwandishi wetu ana mkusanyiko mkubwa wa kazi alizoziandika na hatungeweza kuzichagua zote.

### 5.2.1 Tanzu za Jadi za Sanaa za Maonyesho katika Tamthilia ya *Pungwa*

Tanzu za jadi za sanaa za maonyesho ya asili ya utamaduni wa Kiafrika zilizotumiwa na mwandishi Said A. Mohamed katika utunzi wa tamthilia yake ya *Pungwa* zimewasiliswa kwa ufupi kwa njia ya jedwali hapa chini.

**Jedwali 5.2: Muhtasari waTanzu za Sanaa za maonyesho katika Tamthilia ya *Pungwa***

| Utanzu wa sanaa za maonyesho | Mfano katika tamthilia |
|---|---|
| i) Ufunguzi na mbinu ya usimulizi | -Usimulizi wa kingano – uk 1<br>-Wimbo usiojulikana unakotoka uk 1 |
| ii) Ngomezi | -Chanzio cha kamusa – uk 1 |
| iii) Matumizi ya nyimbo | -Wimbo usiojulikana unakotoka uk 1 |
| iv) Majigambo | -Majigambo ya mzuka katika chanzio – uk 1 |
| v) Jadi ya pungwa | -Tamthilia nzima imeegemezwa katika utamaduni wa Kiafrika wa pungwa |

Tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilizoorodheshwa katika jedwali (5.2) la hapa juu zilibainishwa kuwa zimetumika katika utunzi wa tamthilia ya *Pungwa* na zimefafanuliwa kwa ufasaha katika uchanganuzi wa hapa chini.

### 5.2.2 Ufunguzi na Mbinu ya Usimulizi

Mwandishi ameanza tamthilia yake kwa ufunguzi ambao ameuita chanzio. Hii ni mbinu ya utunzi wa tamthilia ya ki-Aristotle ambapo mtunzi anaanza utunzi wa tamthilia yake kwa wimbo. Katika chanzio cha tamthilia hii, mwandishi ametumia mbinu ya usimulizi katika wimbo katika ufunguzi (Jedwali 5.2 kipengele i). Mwandishi kupitia kwa mhusika kwa jina Mzuka anatumia mbinu ya usimulizi wa kingano kutanguliza hoja muhimu anazokusudia kuzishughulikia katika tamthilia yake kupitia kwa usimulizi wa kingano. Usimulizi ni mbinu inayotumika katika utongoaji wa ngano. Ngano ni utanzu wa sanaa za maonyesho ambao ni sanaa asili ya Kiafrika. Kama ilivyo katika ngano, usimulizi huu ni wa kifomula. Katika tamaduni za Kiafrika, usimulizi wa ngano ulifanywa wakati wa usiku katika mwanga hafifu na wakati mwingine uwanjani katika mbalamwezi. Katika maelezo ya jukwaa ya

mwandishi wa tamthilia ya *Pungwa* ambayo ndiyo maandishi ya kwanza kabisa katika tamthilia hiyo, mwandishi anaeleza hivi kupitia kwa maelezo ya jukwaa:

> "**usiku wa manane… katika mwangaza hafifu … pazia li wazi** ... chumba cha kulalia … fahari ya chumba … bwana na bibiye; watu wenye ulwa wao, wamelala kwenye tanda la kujimwaya kwa usingizi mnono wa raha …" (*Pungwa - uk 1*).

Kama katika usimulizi wa utanzu wa ngano za Kiafrika katika sanaa za maonyesho ya jadi, mtunzi anatuelezea na kutuonyesha kitaswira mandhari ambako tukio analolisimulia katika tamthilia yake ya *Pungwa* linafanyika (**usiku wa manane… katika mwangaza hafifu … pazia li wazi) -** *Pungwa - uk 1***.** Maelezo ya mandhari aliyoyatoa mtunzi katika tamthilia yake yanafanana sana na yale yanayopatikana katika masimulizi ya tanzu za masimulizi ya sanaa za maonyesho ya kale hasa ya utanzu wa ngano. Masimulizi ya jukwaa ambayo ni ya muundo wa masimulizi ya kingano kuhusu mahali ambapo tukio linalosimuliwa linafanyika, yanamwezesha mtunzi kujenga kibunifu taswira ya nchi ambapo linalozungumziwa linafanyika. Masimulizi haya katika wimbo yametumiwa na mtunzi Kimwingilianomatini kwa sababu hizi ni tanzu za sanaa za maonyesho zinazojisimamia ambazo hata hivyo zimetumiwa sambamba kuwasilisha ujumbe mmoja kwa njia ya kujengana na kuimarishana.

Said A. Mohamed vilevile ameanza tamthilia yake kwa wimbo usiojulikana unakotoka anavyosema mwenyewe, katika sehemu ya mwanzo ya ufunguzi wa tamthilia yake ya *Pungwa.* Katika sehemu hiyohiyo ya chanzio cha tamthilia yake, mtunzi anaanza wimbo wake kwa kupiga kamsa katika ufunguzi na kuimba kama inavyoonyeshwa hapa chini:

> **Aaaaa, a-a, a-a, a-a ---.**
> Aaaaa, a-a, a-a, a-a
> Aaaaa, a-a, --- (*Pungwa* - uk 1)

Kamsa ya sauti ambazo ni, **Aaaaa, a-a, a-a, a-a --- ,** za hapa juu, ni mfano wa kilio kinachofanywa kwa sauti katika jamii za Kiafrika. Kilio cha aina hii hufanyika wakati wa kuomboleza mtu anapokufa au wakati mtu anapohatarishwa na tukio fulani baya. Vilevile ni njia ya Kiafrika ya kuwaita watu wakusanyike katika mahali pa mkasa unaotokea au ni njia nyingine ya kuwaita watu waje kutoa msaada wakati kuna shida ya aina fulani. Mtunzi Said A. Mohamed ametumia mbinu ya kupiga kamsa si kwa ajili ya kuomboleza bali kwa ajili ya kuwatahadharisha watu wajue kuwa wanakabiliwa na hatari ya aina fulani. Hii ni njia ya kiubunifu aliyoitumia mtunzi kuvuta nadhari ya wasomaji, watazamaji na hadhira nyingine ya tamthilia ya *Pungwa* ili watie makini kuhusu jambo analolizungumzia mtunzi.

Kama inavyoonyeshwa katika maelezo ya jukwaa, ujumbe wa wimbo unawasilishwa kutoka mahali pasipojulikana kama ifanyikavyo katika matangazo ya habari ya redio yanayosambazwa na vyombo vya habari vya kisasa ambavyo licha ya kuvimiliki kwa kuwa navyo uso kwa uso, hatuwaoni watangazaji wenyewe wala hatuoni mahali ambapo wanatangazia. Mwandishi amechanganya kiubunifu mbinu za kisasa za kurusha matangazo na mbinu za kale za kupiga kamsa ili kuanza usimulizi na utunzi wa tamthilia yake.

Usimulizi ni mbinu yenye mshabaha katika utunzi wa tamthilia ya *Pungwa*. Usimulizi wa mhusika Sauti ya Mzuka ni katika nafsi ya kwanza inayoupatia usimulizi huo mwonjo wa kitawasifu. Mtunzi ametumia usimulizi katika chanzio cha tamthilia ya *Pungwa* ili kutanguliza mawazo anayodhamiria kuyashughulikia baadaye katika tamthilia yake na kuipa tamthilia hiyo mwelekeo wa kidhamira na kiumbo inaouchukua baadaye. Kamsa hiyo ya utanzu wa wimbo wa sanaa za maonyesho ya

jadi inayoanza katika mwanzo wa tamthilia, inazua taswira ya matumizi ya utanzu mwingine wa jadi wa sanaa za maonyesho wa ngomezi unaojadiliwa hapa chini.

### 5.2.3 Ngomezi

Ngomezi (Jedwali 5.2 kipengele ii) ni utanzu wa sanaa za maonyesho unaotumia ngoma na ulitumiwa na jamii nyingi za Kiafrika kupitisha ujumbe wa dharura kwa haraka (King'ei k.h.j.). Jamii hizo zilipiga ngoma kwa njia maalumu iliyowakilisha maneno fulani ambayo yalieleweka tu na wanajamii wenyewe wala mgeni hangeweza kuelewa maana iliyowakilishwa na mapigo hayo ya ngoma, wimbo au muziki. Ngoma hiyo ilipigwa na kuhusisha usemaji wa maneno, uimbaji au muziki wa aina fulani pamoja na uchezaji wa viungo vya mwili kuambatana na mapigo ya ngoma na muziki.

Utanzu wa ngomezi ulitumiwa kuiarifu jamii kuhusu matukio muhimu yaliyohusu jamii kama kuzaliwa kwa mtoto, kufa kwa mtu mashuhuri, kuwakusanya watu katika mikutano au kuwaita kuja kwa sherehe za jamii, kuanzisha, kuhitimisha au kukomesha kufanya makafara na matambiko, kufungua sehemu za matambiko na makafara, kutahadharisha jamii kuhusu majanga yaliyofanyika kama mafuriko, misiba iliyoifika jamii wakati huo, mikasa ya radi au volikano miongoni mwa mengine. Ngomezi ilikuwa njia mwafaka ya kufanya matangazo katika jamii za Kiafrika kwa ajili ya ukosefu wa teknolojia ya kupaaza sauti kubwa au kufikia eneo kubwa kwa mpigo. Kamsa ya Sauti ya Mzuka katika wimbo usiojulikana ulikotoka inakupa taswira ya tangazo lililofanywa na watawala wa jamii za Kiafrika kwa kutumia wapiga kamsa "criers."

Mwanzo wa tamthilia ya *Pungwa* vilevile umechukua muundo wa utanzu wa sanaa za maonyesho wa ngomezi. Mtunzi amechota utanzu huu wa sanaa za maonyesho pale anapoanza utunzi wake kwa kupiga kamsa inayofuatwa na karima. Kamsa ni mbinu

iliyotumiwa na wapiga mbiu waliowekwa na watawala fulani wa jamii za Kiafrika katika kila kijiji ili kuzunguka na kupiga mbiu tofautitofauti iliyofungamana na ujumbe mahususi uliokusudiwa kupitishwa kwa jamii hiyo na mtawala wake:

> **Aaaaaa, a – a, a – a, a –a ---**
> Aaaaaa, a – a, a – a, a – a,
> Aaaaaa, a – a … (*Pungwa - uk 1*)

Kamsa kama hii ni jambo la kawaida katika jamii nyingi za Kiafrika za jadi ambazo hazikuwa zimeendelea kiteknolojia na hata sasa ambapo mawasiliano hufanywa kupitia kwa njia hii ili kupitisha ujumbe. Mhusika Mzuka unapopaza sauti hii unavuta tafakuri ya taswira ya ngomezi ya kutoa tahadhari na onyo kuhusu jambo baya au zuri litakalotokea katika jamii (**Aaaaaa, a – a, a – a, a –a …** ) kama inavyodhihirishwa katika dondoo la hapa juu. Mtunzi amechota utanzu wa ngomezi ili kwanza, aweze kujenga na kuimarisha umbo la tamthilia yake, na pili, aweze kuimarisha dhamira ya kuonya jamii kuhusu ukoloni mamboleo uliozivamia jamii za Kiafrika kupitia tamthilia yake. Mtunzi ametumia utanzu wa ngomezi ili kuiarifu hadhira kwa mdokezo kuhusu nchi za Afrika kutawaliwa na nchi za kigeni katika mfumo mpya wa utawala wa ukoloni mamboleo baada ya ukoloni mkongwe kuondolewa. Ukoloni mamboleo ndiyo mada inayotawala baadaye katika tamthilia yenyewe baada ya kamsa hii kwa kuifuatiza na utongoaji wa kishairi unaosimuliwa katika wimbo wa Sauti ya Mzuka isiyojulikana inakotoka. Mtunzi anatanguliza mada ya ukoloni mamboleo kwa njia ifuatayo:

> SAUTI YA MZUKA …
>
> Nipo hamnioni,
> Naishi, siishi,
> Machoni mwenu siishi,
> **Niko mbali kumbe niko karibu,**
> **Niliondoka kumbe bado nipo,**
> Nimeselelea, nimelowea,
> Na kwamba hamnioni, si kama sipo,
> **Najigeuza nitakavyo …** (*Pungwa – uk 1)*

Uwasilishaji wa hapa juu umefanywa kwa njia ya kishairi. Mhusika Sauti ya Mzuka anaghani na kunuiza maneno kwa lugha ya kishairi inayovutia. Kama katika sanaa za maonyesho za Kiafrika na kwa mapigo ya kishairi Sauti ya Mzuka inaimba, "**Nipo hamnioni, Naishi, siishi, Machoni mwenu siishi, Niko mbali kumbe niko karibu, Niliondoka kumbe bado nipo, Nimeselelea, nimelowea, Na kwamba hamnioni, si kama sipo"**, - ***Pungwa – uk 1.*** Sanaa za maonyesho katika utamaduni wa Kiafrika zilikuwa kazi ambazo zinavutia hadhira. Mtunzi amechota na kuutumia utanzu huu wa sanaa za maonyesho kama njia ya kurembesha na kuifanya kazi yake kuwa ya kuvutia wasomaji na watazamaji wa mchezo.

Sauti ya Mzuka isiyojulikana inakotoka inatanguliza kwa mdokezo dhamira ya mtunzi kuhusu uwepo wa walowezi wa kikoloni ambao walikuwa wakidhaniwa kuwa walikuwa wameondoka baada ya kushindwa katika makabiliano ya vita vya uhuru na nchi za Afrika na nchi hizo kujinyakulia uhuru. Ingawa haonekani, mkoloni bado yupo (**Niko mbali kumbe niko karibu, Niliondoka kumbe bado nipo)**. Huyo mkoloni amejibadilisha kwa kujigeuza atakavyo na kurudi katika mataifa ya Kiafrika katika muundo na mtindo mpya wa utandawazi (**Najigeuza nitakavyo …** ***Pungwa – uk 1)***. Wimbo huu ni wa kuwatahadharisha Waafrika wajichunge na udhalimu wa mkoloni unaokuja katika umbo jipya la ukoloni mamboleo

### 5.2.4 Matumizi ya Wimbo

Wimbo au kwa wingi nyimbo (Jedwali 5.2. kipengele iii) ni utanzu mmoja wa sanaa za maonyesho ya jadi ya utamaduni wa Kiafrika na Fasihi Simulizi kwa jumla ambao umechotwa na mtunzi na kutumiwa katika utunzi wa tamthilia ya *Pungwa*. Wimbo ni utungo wenye mpangilio maalumu wa maneno yaliyo na mahadhi ya kupendeza. Wimbo unaweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi cha watu. Maelezo ya mtunzi

katika chanzio cha tamthilia ya *Pungwa* yamefanywa kwa njia ya usimulizi kupitia kwa wimbo. Uwasilishaji wa wimbo huu wa Mzuka umejumuisha mbinu zaidi ya moja Kimwingilianomatini kama ilivyoelezwa kwingineko hapo juu. Usimulizi wa Sauti ya Mzuka unaanza kwa "sauti kali ya kuogofya inayokuja kwa "wimbo", na isiyojulikana inakotoka" kama inavyoonyeshwa hapa chini.

**SAUTI YA MZUKA (*kali ya kuogofya … inakuja kwa wimbo, haijulikani inakotoka*).** (*Pungwa* – Uk 1)

Dondoo la hapa juu ni maelezo ya mtunzi kuhusu hali ya jukwaa na hali ya uwasilishaji wa wimbo wa Sauti ya Mzuka. Maelezo haya ya jukwaa yanajenga taswira na hali halisi ya utendaji wa sanaa za maonyesho. Katika sehemu ya chanzio cha tamthilia hii, mtunzi amechota utanzu wa sanaa za utendaji wa wimbo ili kujenga umbo la tamthilia yake kama inavyodhihirishwa katika dondoo la hapa juu: (**SAUTI YA MZUKA (*kali ya kuogofya … inakuja kwa wimbo, haijulikani inakotoka*)** (*Pungwa* – Uk 1)**.** Kwa kuimba wimbo wa kutisha na kuogofya, hadhira inahamasishwa kuwa suala linalozungumziwa katika wimbo ni nyeti na la dharura na kwamba linahitaji umaakini fulani wa kulishughulikia.

Pamoja na kutimiza mapendekezo ya Aristotle kuhusu umbo la tamthilia ya Kiswahili, Said A. Mohamed anatumia utanzu huu wa wimbo kuendeleza umbo la tamthilia yake ya *Pungwa*. Dhamira ya mtunzi wa tamthilia pia inajitokeza kupitia kwa maelezo ya jukwaa kuhusu wimbo wa Sauti ya Mzuka inaposema kuwa ni - ***kali ya kuogofya.*** Mwandishi anaanza tamthilia yake kwa sauti kali ya kuogofya kama njia ya kudhihirisha hasira na kiburi cha mzuka unaoimba. Mzuka kwa mujibu wa TUKI (2014) kwa majina mengine ni Shetani, pepo au kiumbe anayedhaniwa ameumbwa kwa moto na ambaye haonekani kwa macho. Basi Sauti ya Mzuka inarejelea sauti ya Shetani, pepo au kiumbe hatari ambaye haonekani.

Pepo katika tamaduni za Kiafrika hutokana na roho za watu waliokufa kitambo ambazo hufufuka na kurudi duniani tena kuja kuwahangaisha Binadamu walio hai. Mwandishi wa *Pungwa* anakusudia kuonyesha kwamba wale waliodhaniwa kuwa wamekufa na kuondoka wamerudi tena wakiwa wakali zaidi na wakiwa wanaogopesha zaidi - **SAUTI YA MZUKA (*kali ya kuogofya*).** Mzuka unaorejelewa na Said A. Mohamed katika wimbo wa ufunguzi wa tamthilia ya *Pungwa* ni mkoloni aliyeshindwa na Mwafrika katika vita vya kupigania uhuru na ambaye anarudi kwa siri kama mzuka asiyeonekana kwa ukali unaoogofya kuja kuwadhuru tena Waafrika katika hali mpya ya ukoloni mamboleo.

Katika tamaduni asili za Kiafrika, nyimbo ziliimbwa kutegemea shughuli na uamilifu wake kwa jamii. Wimbo wa Sauti ya Mzuka unaimbwa kwa sauti kali na ya kuogofya kama ilivyoonyeshwa hapo juu. Mwandishi anaanza wimbo kimakusudi kwa hali hiyo ya ukali na inayoogopesha kwa dhima ya kuonya na kuwatahadharisha Waafrika kuhusu mkoloni ambaye "amefufuka" tena kijazanda kuja kumwangamiza katika hali ya ukoloni mamboleo. Hii ndiyo sababu wimbo wenyewe unaanza kwa kilio cha kamsa au mbiu ya kuhatarisha.

Mtunzi wa *Pungwa* amechota utanzu wa wimbo na kuutumia pamoja na tanzu nyingine katika kuumba sio tu chanzio cha tamthilia ya *Pungwa*, bali pia na umbo zima la tamthilia hiyo. Mtunzi ametumia mbinu hii na kujumuisha tanzu nyingi pamoja kwa njia ya Mwingilianomatini kwa ajili ya ubunaji wa tamthilia yake si tu katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira bali pia katika kujenga na kuimarisha ujumi na umbo la tamthilia yake ya *Pungwa*. Katika sanaa za maonyesho ya jadi, nyimbo ziliimbwa wakati wa sherehe ili kutambuisha hadhira. Nyimbo za kidini ziliimbwa wakati wa kuabudu miungu, kutoa makafara au kufanya matambiko.

Vilevile, nyimbo ziliimbwa wakati wa utendaji wa miviga kama tohara au jando, unyago, pungwa miongoni mwa mengine kutegemea shughuli ya kijamii iliyokuwa inashughulikiwa.

### 5.2.5 Majigambo

Katika sehemu za 5.2.2, 5.2.3 na 5.2.4 za hapa juu tulitanguliza kueleza kwamba Said A. Mohamed ametumia tanzu za ngomezi na nyimbo katika kusimulia matukio mbalimbali katika tamthilia yake. Katika sehemu hii, tunaendeleza maelezo kuhusu matumizi ya utanzu wa majigambo (Jedwali 5.2. kipengele iv) kama mbinu ya utunzi ya kusimulia matukio katika tamthilia ya Kiswahili. Usimulizi wa sauti ya mhusika Sauti ya Mzuka katika tamthilia ya *Pungwa* vilevile unafanyika kupitia kwa muundo mwingine wa utanzu wa majigambo. Majigambo ni sanaa ya maonyesho inayowasilishwa kupitia kwa aina fulani ya utendaji wa kitamaduni ambao pia husimuliwa na jamii nyingi za Kiafrika katika kujisifu. King'ei na Kisovi (2005) wanaeleza majigambo kama utanzu wa Fasihi Simulizi ambao upo katika kundi la sanaa za maonyesho. Fanani au mtambaji anapotamba katika sanaa hii kwa kawaida huwa na tabia ya kujivuna. Katika kianzio au chanzio kama Said A. Mohamed anavyouita utangulizi wa tamthilia yake, mtunzi kupitia kwa masimulizi ya Sauti ya Mzuka anachota utanzu wa majigambo na kuutumia katika kutunga tamthilia yake kama ifuatavyo:

> … Nani ajuaye ayajuayo Mzuka?
> Vipawa vyangu vimewakalia juu wanadamu
> Macho yamepakwa ukungu
> Masikio vipande vya chuma,
> Pua vitomeo vya vijiti,
> Hisia imezimwa kwa ganzi
> Na bongo limetomelewa tope … vyote
>         Vyote maradufu
> Mimi ndiye mimi,
> Mpiga – mbizi …
> Mpiga mbizi pasi ukomo wa pima

Huzamia kuliko mkizi.
Na kufika kusiko fikwa – vina vya ajabu
Mimi mzuka wa bahari saba na mgaagaa fukwe saba
Mhodhi wa miamba saba, mkwepa mawimbi saba
        na mfika mafu …
*(Pungwa - uk 1)*

Jigambo hili katika chanzio cha tamthilia linachukua muundo wa kishairi. Ingawa halina migawanyo ya beti kama katika shairi la kimapokeo, jigambo hili limepangwa katika mistari yenye mapigo ya silabi na mizani ya kishairi. Silabi hizi vilevile hazilingani kama katika shairi la kiarudhi. Mshororo wa kwanza una mizani kumi na nne, wa pili kumi na saba, wa tatu na wa nne tisa na kumi mtawalia, almradi mishororo yote katika jigambo hili haina ulinganisho wa urari wa mizani. Aidha, jigambo la sauti ya mzuka halina vina vyovyote (vya kati na vya mwisho) bali linazua takriri za maana, takriri za maneno na taswira ambazo zinarudiwarudiwa.

Katika takriri ya maana, jigambo la mzuka linaghani maneno yafuatayo yanayodhihirisha msisitizo wa maana inayojirudiarudia:

Nani ajuaye ayajuayo mzuka
Vipawa vyangu vimewakalia juu wanadamu
Macho yamepakwa ukungu,
Masikio vipande vya chuma,
Pua vitomeo vya vijiti
Hisia imezimwa kwa ganzi
Na bongo limetolewa tope …
Sifi hata nikiuliwa
Nyundo hainivunji, mkuki haunitoboi
Mshale haunitumbui, haunirarui … (*Pungwa* - uk 1)

Ughani huu unasisitiza uzito wa binadamu kuelewa mazingira yake kama afanyavyo mzuka. Ili kuonyesha uziwi na upofu wa binadamu katika kuelewa yanayomzunguka, mzuka unaeleza hivi kuwahusu binadamu; "*Macho yamepakwa ukungu, masikio yamezibwa na vipande vya chuma … na pua vitomeo vya vijiti*." Mtunzi ametumia mbinu ya uhuishaji wa mzuka kwa kuufanya kusema na kuupa sifa ya kutenda na kuelewa mambo ambayo binadamu anashindwa kuyaelewa. Dhana ya binadamu

kutoweza kutumia vizuri uwezo wake wa kuona, kuelewa, kunusa na kuyafahamu mazingira yake kwa jumla umeelezwa kwa lugha ya kitaswira ambayo imefumbwa na inayohitaji ufumbuzi na uelewa wa ndani ili kung'amua analolieleza mtunzi.

Mtunzi vilevile amechota utanzu huu wa majigambo ili kumwezesha kupitisha dhamira yake kwa kueleza kuwa baada ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru wa bendera, mkoloni hakuweza kutoka kabisa, wala nchi za Afrika hazikuweza kujinyakulia uhuru wa kujisimamia wenyewe. Waafrika bado wanaishi na mkoloni lakini hawamtambui licha ya kuwa na macho ya kuona, pua ya kunusa na masikio ya kusikia. Sauti ya Mzuka katika wimbo wa chanzio cha tamthilia yake unaeleza hivi;

> Iwapo hamnioni
> Naishi, siishi
> Machoni mwenu siishi
> Niko mbali kumbe niko karibu
> Niliondoka kumbe bado nipo.
> Nimeselelea, nimelowea
> Na kwamba hamnioni, si kama sipo
> Najigeuza nitakavyo …
> Pengine ni miongoni mwenu
> Ndani ya damu zenu n…
> Sifi hata nikiuliwa … (*Pungwa* - uk 2)

Uwepo wa mkoloni katika nchi za Afrika na nchi zingine za ulimwengu wa tatu si wazi. Wazungu walibadilisha utawala wao wa ukoloni mkongwe kimiujiza afanyavyo Shetani na kuleta utawala wa ukoloni mamboleo ambao upo lakini hauonekani wazi kwa wenyeji wa nchi hizo. Kupitia kwa utanzu huu wa majigambo, mtunzi anamzindua na kumtanababhisha Mwafrika kuhusu hali yake ya kutawaliwa na kwamba hajitambui wala kujielewa akiwa katika hali hiyo ya kunyanyaswa na mlowezi.

Said A. Mohamed vilevile amechota mbinu za utendaji wa sanaa za maonyesho kutoka kwa Bibilia takatifu kupitia kwa mazungumzo kati ya wahusika Bwana na Bibiye ambapo mhusika Bwana alitaka kueleza Shetani ni nani. Dhana Shetani

imetumika kijazanda kuzua taswira ya mkoloni. Mtunzi vilevile anamwita Shetani pepo aliyempanda mwele kichwa. Shetani na pepo katika tamaduni za Kiafrika ni dhana dhahania inayorejelea kiumbe hatari anayemwathiri Binadamu kwa kumtendea maovu. Mashetani na pepo katika utunzi wa tamthilia ya *Pungwa* huweza kuwapanda watu vichwa alivyompanda mhusika Bwana na kumsababishia maradhi. Katika jigambo la mhusika Bwana, mtunzi anasisitiza dhana ya pepo aliyesafiri kutoka ng'ambo kuja kumhangaisha Mwafrika kuwa mkoloni kupitia kwa maelezo yafuatayo;

> …
> A -a, a-a, Aaaaaa
> **Mimi ndiye mimi** … (*Anayongoyea*)
> Mimi ni pepo,
> Niliyesafiri ng'ambo saba
> Kuja hapa kulowea … ( *Pungwa - kr 8 – 9 msisitizo ni wetu*)

Maneno haya vilevile yalitumiwa na Mungu katika Bibilia takatifu katika Mlima wa Sinai alipotaka kumtuma Musa kwenda Misri ili awakomboe wana wa Israeli waliokuwa wamedhulumiwa na kunyanyaswa na utawala wa nchi hiyo. Wana wa Israeli walikuwa wametekwa kutoka nchi yao kama mahabusu wa kivita kwa kumsahau Mungu wao na kupelekwa Misri ambako walikuwa wamewekwa na kutumikizwa kama watumwa. Musa alikuwa akilisha mbuzi na kondoo wa Jethro, baba mkwe wake alipowavusha mifugo hao kutoka jangwa na kuwaelekeza malishoni katika mlima mtakatifu wa Sinai. Alipokaribia kichaka kilichokuwa kinawaka moto, Mungu alimwamrisha aende Misri kuwakomboa wana wa Israeli waliokuwa wanateseka utumwani huko. Musa alipomuuliza Mungu amwelekeze jinsi ambavyo angemweleza mfalme wa nchi ya Misri kuwa Mungu wa mababu wa Waisraeli Abramu, Isaka na Yakobo ni nani ili akaweze kuwaachilia huru wana wa Israeli waliokuwa utumwani kwake, Mungu alizua taswira ambayo mtunzi pia ameitumia

Kimwingilianomatini katika tamthilia yake ya *Pungwa.* Kitabu cha Kutoka 3:14 cha Bibilia takatifu kinasema hivi:

Mungu akasema, "**Mimi ndiye mimi**"

Mtunzi anasisitiza kwamba anayemtawala Mwafrika katika nchi yake ni mkoloni aliyesafiri kutoka ng'ambo kupitia kwa njia ya bahari. Said A. Mohamed akitumia mbinu ya mdokezo, anaashiria kuwa asili ya matatizo ya nchi za Afrika ni mgeni aliyehama kwake ng'ambo na kuja kwa meli kupitia bahari saba. Mgeni huyo ni mlowezi aliyekuja kama mkoloni akazitawala nchi za Afrika kimabavu. Mlowezi ndiye Shetani na ndiye pepo aliyewapanda vichwa viongozi wa nchi za Afrika na kuwafanya kiti chake kama inavyoelezwa katika imani za kichawi za pungwa zipatikazo katika tamaduni za Kiafrika ambazo tumefafanua matumizi yake katika jamii hapa chini.

### 5.2.6 Jadi ya Tamaduni za *Pungwa*

Tamthilia ya *Pungwa* imebuniwa vilevile kupitia kwa matumizi ya tamaduni za jadi za Kiafrika hasa katika jamii za pungwa za pwani ya Afrika Mashariki (Jedwali 5.2 kipengele v). Mwandishi Said A. Mohamed anaeleza kuwa tamthilia yake ya *Pungwa* inadhihirisha njia mojawapo ya tamaduni asili za jadi za Kiafrika inayotumiwa kuwatoa watu Mashetani au pepo waliowakumba na ambao husemekana kukaa vichwani mwao ambamo wamejiwekea viti na kufanya vilinge vyao humo. Matumizi ya pepo wanaowapanda watu vichwa katika utunzi wa tamthilia ya *Pungwa* ni mbinu ya kisanaa ya mtunzi kuzua taswira za kijazanda katika kazi ya fasihi. Kwa kutumia hali ya kweli ya utamaduni wa Kiafrika wa kupandwa na kupungwa kwa pepo katika mazingira ya Kiafrika kunamwezesha Said A. Mohamed kueleza dhana fulani muhimu katika kazi yake. Mazungumzo kati ya wahusika Bwana na mganga Mahoka yanadhihirisha kwamba Bwana katika tamthilia ya *Pungwa* amepandwa na pepo:

> BWANA: (*Anapiga kelele*) Biye … Biye … Biye …Biye … naona wingu linaanza kunigubika kichwani. Naona wimbi linaingilia nyumbani mwangu na wewe unaliruhusu, wimbi litatugharikisha …
>
> SAUTI: (*Haijulikani inakotoka*). **Muwele wangu, huyu mumeo, naona anataka kubawibiwa na kuliwa akili. Kiti changu, kiti changu bibiye, kihifadhi kisichukuliwe.** Kihifadhi kisije kikaliwa. Mkinihifadhi nitakuhifadhini. Sote tuwe wahifadhina; wenye kuhifadhiana na kusaidiana, la si hivyo, hiari yenu … sitaki mganga mimi, sitaki kupungwa. (*Pungwa* - uk 15)

Sauti isiyojulikana inakotoka katika dondoo la hapa juu ni ya Shetani aliyempanda Bwana kichwa na kumfanya kiti chake, "**Muwele wangu, huyu mumeo, naona anataka kubawibiwa na kuliwa akili. Kiti changu, kiti changu bibiye, kihifadhi kisichukuliwe" -** (*Pungwa* - uk 15). Kwa sababu hiyo, Shetani anamuuliza Bibiye amtunze mhusika Bwana ambaye ni bwanake asiweze kuwa na Mashetani wengine. Jamii nyingi za Kiafrika zinaamini katika uwepo wa pepo na Mashetani na imani za kishirikina au uchawi. Mtunzi Said A. Mohamed na watunzi wengine wa Kiafrika wa tamthilia za Kiswahili wamechukua nafasi hii kutumia imani za pungwa na ushirikina kiubunifu kama mbinu ya utunzi na nyenzo ya kujenga maana na dhima katika kutungia tamthilia zao. Mhusika Bibiye anapomuuliza Burhani mganga wa kupunga pepo ni nani anayeamini katika imani hiyo ya pungwa, Burhani anaeleza kuwa ni watu wengi. Mazungumzo yao yanaendelea ifuatavyo:

> Burhani: **Wengi tu, hasa wakulima**. **Wao husema Nairuzi huambatana na miongo**; kwamba kutanyesha mvua kubwa au la., kama ukame utatawala au la, kama wajawazito watajifungua au la, kama vifo vya kuchawiana vitazidi au la, kama ndege na nzige watakuwa wengi au la, kama samaki na matunda yataenea na biashara itashamiri …(*Pungwa - uk 28*)

Dondoo hili linaonyesha kwamba imani katika uchawi na tamaduni za pungwa zinahifadhiwa na kuendelezwa na watu wengi katika jamii za Kiafrika. Katika kumjibu Bibiye kuhusu nani na idadi ya watu wanaoamini katika uchawi na utamaduni wa pungwa, mhusika Burhani anamweleza kuwa kuna watu wengi hasa

wakulima, "**Wengi tu, hasa wakulima. Wao husema Nairuzi huambatana na miongo" -** *Pungwa - uk 28.* Watu wengi katika jamii za Kiafrika hasa wakulima huwa na misimu na sherehe (nairuzi) ambazo huambatana na miongo. Shughuli zote za kijamii kama kunyesha kwa mvua, kuwa na au kutokuwepo kwa ukame, kama wanawake watajifungua au la, kuzuka au kutozuka kwa nzige na kuwepo kwa mambo mengine mabaya ya kichawi zilitegemea imani katika miungu na pepo ambazo zinachukuliwa kuwa utamaduni na uchawi wa Kiafrika.

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kwamba mwandishi kama zao la jamii, hawezi kujitenga na matukio ya jamii yake. Imani za pungwa zimetawala katika jamii ya mtunzi Said A. Mohamed ya Zanzibar na yeye ameichota amali hiyo ya utamaduni wa Kiafrika na kuitumia kiubunifu kama mbinu ya utunzi na nyenzo ya kujenga dhima katika tamthilia yake. Kama asemavyo mhusika Burhani katika dondoo la hapa juu, watu walio na imani za pepo na Mashetani wanaohitaji kupungwa ni wengi. Kidini, pepo na Mashetani ni viumbe wa ajabu walio na uwezo mkubwa wa kutenda maovu kimiujiza mara nyingi dhidi ya Binadamu. Jamii zote ulimwenguni huwa na imani za pepo na Mashetani na hulaani na kushutumu matendo yoyote maovu ambayo wanaamini husababishwa na viumbe hao. Mashetani yanadaiwa kumwingia kichwani mhusika Bwana na kumhangaisha, "**BIBIYE: … Mume wangu anaumwa – amekumbwa na Shetani."** Bibiye anamweleza Mahoka kuwa Bwanake amepandwa na Shetani na Bwana anasisitiza kwamba yeye mwenyewe ni Shetani kama ifuatavyo:

> **BIBIYE: … Mume wangu anaumwa – amekumbwa na Shetani.**
> …
> **BWANA: Sina Shetani. Mimi mwenyewe Shetani**. Mimi mwenyewe pepo, mimi mzuka, *(anayongoyea. Yupo palepale alipoachwa*) (*Pungwa – uk. 11)*

Kuna mbinu nyingi zinazotumiwa katika kuwapunga au kuwatoa pepo na Mashetani kutoka kwa wari kama wanavyoitwa watu waliokumbwa pepo na Mashetani. Katika

nchi ya Zanzibar, genge la waganga na wasaidizi wao pamoja na watu ambao kitambo walipandwa na pepo kisha wakapungwa na sasa hawasumbuliwi tena na pepo wala Mashetani hao, hukusanywa pamoja katika sherehe ya kupunga Mashetani na pepo (Mohamed, k.h.j.). Katika sharehe hiyo, watu hawa hubeba vibao ambavyo huvitumia kupiga makofi yaliyorandana vizuri na mdundo maalumu wa ngoma ya kupunga pepo na Mashetani. Mohamed anaendelea kueleza kuwa, mdundo wa ngoma ya pungwa ulichezwa kutegemea pepo au Shetani aliyempanda mtu kichwani. Ngoma zilizochezwa pungwani kutegemea pepo aliyempanda mwele zilijumuisha ngoma ya “rubamba, kumbwaya, kibuki, kiluwa na madogori” zilizochezwa huko Zanzibar kwa ajili ya kutekeleza utamaduni huo wa kupunga waliopandwa na pepo. Ngoma mbalimbali za kuwatoa watu pepo na Mashetani ziliandaliwa kwa ajili ya matayarisho ya kuwapunga waliopandwa na pepo. Ngoma hizo ziliandamanisha na ngao za aina mbalimbali kama kaniki za rangi nyeusi na nyeupe, vyakula vya matoleo ya Shetani na vile vitakavyotumiwa kufanyia makafara wakati wa kumpunga mwari pamoja na zana za uganga, majani, marashi na dawa mbalimbali zilizoandaliwa kwa ajili ya shughuli hiyo. Katika tamthilia ya *Pungwa,* mhusika Bwana aliyepandwa na pepo anaaguliwa na kupungwa na waganga mbalimbali kama Mahoka na Burhani. Utekelezaji wa pungwa uliandamanishwa na uchezaji wa “ngoma ya rubamba,” uigizaji, unuizaji wa maneno na maonyesho fulani ya kisanaa ya jadi yaliyochukuana vizuri na shughuli hiyo. Anapomwagua Bwana, “Mahoka anapiga makelele mengi kama anayewaita watu na kujitikiza huku akicheza ngoma ya rubamba,” kama ifuatavyo:

> MAHOKA: Mafundi wa baba (***Anapiga kelele kama waita watu),*** **mafundi wa baba taireni … taire taaaai … aaaah. (*Anajitikiza mwili mzima*), mafundi wa baba anzeni ngoma, anzeni rubamba. (*Rubamba inaanza kupigwa, kwanza inasikika taratibu na halafu inasikika waziwazi*)*.* Nipe ruhusa, nipe ruhusa bibiye.**

BIBIYE: Nimekupa … nimekupa ruhusa …
MAHOKA: Hujanipa ruhusa …
BIBIYE: Nikikupa?
MAHOKA: **Uingie mashindoni na wewe udemke. (*Mahoka na Bibiye wanademka pamoja na mdundo wa rubamba unaoendelea*).**
MAHOKA: Aaaaaa – aaaaa, ho, ho ho, … haha-haha-haha (*Anachagawa huku anamsogelea Bwana ambaye pia alikuwa akichagawa)* - (*Pungwa* - uk. 12)

Pungwa ilihusisha mgonjwa, mganga kama Mahoka au Burhani na watu wengine waliohusiana na mwele huyo. Mahoka katika dondoo la hapa juu anamwomba ruhusa mhusika Bibiye aweze kumwagua Bwana kwa mwenyewe kushiriki katika kucheza ngoma ya kienyeji ya rubamba inayochezwa wakati wa shughuli yenyewe ya pungwa, "**Nipe ruhusa, nipe ruhusa bibiye … Uingie mashindoni na wewe udemke. (*Mahoka na Bibiye wanademka pamoja na mdundo wa rubamba unaoendelea*).** Pungwa katika jamii za Kiafrika za pwani ilikuwa shughuli ya kijamii iliyohusisha wanajamii wote ili kuifanikisha.

Pepo na Mashetani ambao hawangeweza kuondolewa na waganga, wasaidizi wa waganga na watu ambao wamepungwa si kitambo kupitia kwa njia ya kupiga ngoma mbalimbali na makofi, wangepungwa pia kupitia njia zingine tofauti zilizokuwa za kiimani. Wanajamii pia wangetumia mbinu ya kutoa sadaka, kufanya makafara, kujifungia sihiri ya kuwafukuza, dhikiri, maulidi ya homu au kwa kuzinguliwa kwa kisomo fulani kilichofanywa na watu maalumu katika jamii ya Waswahili. Katika tamthilia ya *Pungwa*, mtunzi anamtumia mhusika Burhani kumpunga Bwana kwa kutumia kisomo cha aina fulani cha maandishi matakatifu au mara nyingi bao la ramli na elimu ya nyota kama afanyavyo Burhani katika dondoo la hapa chini anapomwagua mhusika Bwana:

BIBIYE: Ulilolikujia mbona hulifanyi?
BURHANI: Nd'o nimo hivi n'nafanya (*Anaendelea kupiga ramli*). Kamar … Zohar … Mushtar … A-a! **Lo! Nimeona … Ah,**

> **Shetani au pepo … Pepo ndiye anayemsumbua Bwana. Pepo anayeitwa Mfakamizi. Lo! Hatari pepo huyu. Hula kila kitu … shaba, chuma makaa, dhahabu, karafuu, katani, karanga …** (*Pungwa – uk 29*)

Baada ya kuaguliwa na mganga mwingine kwa jina Burhani, inabainika kwamba Bwana anasumbuliwa na pepo hatari wa tamaa na ulafi wa kula kila kitu kilichopo katika nchi yake. Bwana ni kiongozi katika nchi moja maskini ya Kiafrika. Mtunzi ametumia utamaduni wa Kiafrika wa pungwa ili kuonyesha kwamba viongozi wa Kiafrika wanaugua kutokana na tamaa ya kutaka kujilimbikizia mali yote katika nchi zao kupitia kwa njia ya wizi wa mali ya umma. Burhani anamweleza hivi mhusika Bibiye baada ya kumwagua Bwana, "**Lo! Nimeona … Ah, Shetani au pepo … Pepo ndiye anayemsumbua Bwana. Pepo anayeitwa Mfakamizi. Lo! Hatari pepo huyu. Hula kila kitu … shaba, chuma makaa, dhahabu, karafuu, katani, karanga …** (*Pungwa – uk 29*). Matendo ya viongozi kama Bwana ni hatari kwa sababu wanaiba shaba, chuma, makaa na rasilimali zingine za umma kwa matumizi yao binafsi.

Mashetani na pepo walichukuliwa kuwa hatari na wanaotishia maisha ya Binadamu wanayempanda, majirani wake, watu wa ukoo wake na watu wanaomkaribia. Katika tamthilia ya *Pungwa*, mganga wa kupunga watu waliopandwa na pepo anamwambia mhusika Bwana kuwa amepandwa na Shetani anayemhangaisha na ambaye atawahangaisha watu wengine. Mahoka anamweleza Bwana hivi:

> MAHOKA: Una Shetani bwana mkubwa. Una pepo … una mzuka. Usidhani atatula sisi ndugu zako tu. Usidhani anatunyanyasa sisi tu, lakini atawanyonya damu nyinyi mlionenepeana … tafauti … tafauti ni ya kiwango: baina ya kunyonya mfu na alo hai. Wenzetu husema tafauti hiyo ni tafauti ya kumuua tena mauti na kumwonjaonja mzima. Nipe ruhusa … nipe ruhusa bibiye. (*Pungwa - uk 13*)

Hivyo watu wa aila yake wangefanya njia zote chini ya ardhi pamoja na kutumia mali yao yote ili kumpunga mtu aliyepandwa na pepo na Mashetani. Katika jamii ya

Waswahili, iliaminika kuwa pepo na Mashetani wangesababisha hasara kubwa ya magonjwa yasiyopona, ndoto mbaya, wasiwasi, majinamizi na mambo ambayo yangeleta upotevu wa mali pamoja na maisha ya watu. Pepo na Mashetani waliogopwa na wanajamii kwa matatizo ambayo wangeyasababishia watu. Akimuagua mhusika Bwana aliyekuwa amekumbwa na pepo, mganga Burhani anaeleza hivi baada ya kutazama kwa tunguli za ramli:

> BIBIYE: Endelea kumwagua.
> BURHANI**: Kamar … Zohar … Mushtar … Lo! Naona kiza … kiza … kiza … moto mmoja. Kiza … kiza maana yake nini?**
> BIBIYE: Kiza cha Mzimu wa Watu wa Kale.
> BURHANI: Ata! Hiki si kiza cha wafu. Si kiza cha watu waliokufa. Hiki ni kiza cha walio hai. **Cha wenye kwenda na kurudi. Cha wanaokwenda bila ya hadhari ya kutaka kuona nyuma wanakotoka na mbele wanakokwenda**. Cha wanaokwenda mpaka wajigonge, waanguke ndio warudi nyuma kuona kwamba wamekosea. (*Pungwa – kr 29 – 30. Msisitizo ni wetu*).

Kwa kupiga ramri kama inavyofanyika katika uaguzi wa Kiafrika wa utamaduni wa pungwa; **Kamar … Zohar … Mushtar … Lo! Naona kiza … kiza … kiza … moto mmoja. Kiza … kiza maana yake nini?** (*Pungwa* - uk 29), mwandishi Said A. Mohamed anakusudia kutafuta suluhu la matatizo ya nchi za Afrika kwa kutumia mbinu za kiasili. Burhani ni aina ya mganga wa kiasili ambaye huwaagua wagonjwa ili kubaini na kutibu matatizo yao. Mhusika Bibiye ambaye ni bibi wa mhusika Bwana ambaye ni kiongozi wa moja ya nchi za Kiafrika na anayeugua, anamwomba Burhani achunguze na kubaini matatizo ya kiongozi huyo kwa njia ya kumwagua ili aweze kupata tiba ya matatizo yake. Hii ndiyo sababu Bwana ana wasiwasi kwamba kwa kutaka aaguliwe Bibiye anaanika matendo yake ya uongozi mbaya.

Kwa kuzirejelea tamaduni za Kiafrika za pungwa katika utunzi wa tamthilia yake, mwandishi anakusudia kutafuta suluhu la matatizo ya nchi za Afrika kijazanda.

Utamaduni huu wa pungwa umetumika kijazanda ili kudhihirisha dhamira ya kutafuta suluhisho la kiasili kwa matatizo ya nchi za Afrika.

Pepo aliyempanda mhusika Bwana ni hatari anavyosema mganga Burhani. Bwana ni kiwakilishi cha viongozi wa Afrika "**wanaopandwa kichwa na pepo hatari**". Pepo huyu hatari ambaye amewapanda Waafrika ni pepo wa ulafi mwenye tamaa mbaya anayekula kwa pupa kila kitu ikijumuisha madini yote katika nchi yake kama vile dhahabu, shaba na almasi, kawi ya makaa, mimea kama vile kahawa, karafuu, njugu, miongoni mwa vitu vingine vinavyokuzwa katika bara la Afrika. Huyu ni pepo anayewafanya watawala kuwa na tamaa ya kunyakua mali ya umma ili kuishi maisha ya anasa. Akiendelea kumuagua, mganga Burhani anaongezea kuwa walio na pepo wa aina hii huwa hawana aibu yoyote kwani wao huharibu kila kitu bila kuangalia hasara waliyoisababisha wala madhara ya hasara waliyoisababisha kwa kizazi kijacho. Kama anavyosema Burhani, hiki ni kiza, "**cha wenye kwenda na kurudi. Cha wanaokwenda bila ya hadhari ya kutaka kuona nyuma wanakotoka na mbele wanakokwendea**" (*Pungwa* - uk 30). Viongozi wa Afrika ni watu wasiojali maendeleo ya nchi walizopewa jukumu la kuziongoza na wananchi wa nchi zao kwa imani kwamba wangezitunza vizuri. Viongozi wa nchi hizi ni watu wanafiki wanaojithamini wao wenyewe na wabadhirifu wenye pupa wanaotumia mali ya nchi zao vibaya.

Matumizi ya tamaduni ya pungwa katika utunzi wa tamthilia ya *Pungwa* vilevile ni kwa dhima ya kujenga na kuendeleza umbo la tamthilia hiyo. Akiiga utendaji wa tamaduni za pungwa, Said A. Mohamed anataja majina mahususi yanayonuizwa na waganga na Burhani ambao hutekeleza pungwa kwa kuandika hivi; **Kamar … Zohar … Mushtar … Lo! Naona kiza … kiza … kiza … moto mmoja. Kiza … kiza maana yake nini?** Waganga na mahoka kutaja maneno kamar, Zohar, Mushtar na

mengine ili kuelewa matatizo yanayomkumba mgonjwa ni njia ya kimiujiza na kimaajabu ya kugangua na kuagua matatizo ya watu. Hii ni mbinu ya Kiafrika ya kutafuta suluhu la matatizo yao. Kimwingilianomatini, maneno yanoyonuizwa na waganga, mahoka na Burhani hapa juu ni majina ya nyota yanayotajwa na wataalamu wa elimu ya nyota katika tamaduni za Kiarabu, Kihindi na Asia kwa jumla ili kutabiri yatakayotokea mbeleni. Kwa kuiga utendaji wa tamaduni za pungwa, mwandishi anazitumia tamaduni hizi katika kuendeleza umbo la tamthilia yake ya *Pungwa* na kupamba ujumi wa kazi yake.

### 5.3 Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* – Emmanuel Mbogo (1999)

Sehemu hii imeshughulikia tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya tamaduni za Kiafrika zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Uchanganuzi huu ulidhamiria kudhihirisha mbinu za matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* kwa mujibu wa lengo la kwanza la utafiti huu.

Mwandishi Emmanuel Mbogo ni mzaliwa wa mji wa Kongwa, mkoani Dodoma nchini Tanzania aliyezaliwa katika mwaka wa 1947. Baada ya masomo yake ya shule za upili katika mwaka wa 1967, Mbogo alijiunga na Chuo cha Ualimu wa Shule ya Msingi cha Morogoro ambapo aliandika kazi yake ya kwanza ya kisanii iliyoweza kuchapishwa katika jarida la chuo hicho la "Morani." Kazi hiyo ya aina ya hadithi kwa jina, "James I die of love" ilikuwa kama kifungua macho kwa ubunifu wa baadaye aliokuja kuwa nao. Baada ya kuhitimu chuo cha ualimu, Mbogo alifundisha katika shule za msingi za wilaya ya Dodoma kwa miaka mitatu. Katika mwaka wa 1973, Mbogo alijiuzulu ualimu na kujiunga na Chuo Kikuu cha Elimu ya Taifa, Chang'ombe ambapo tena katika mwezi wa Juni, mwaka wa 1974 alihitimu na Cheti

cha stashahada ya ualimu na hapohapo akaajiriwa kufundisha katika Chuo cha Ualimu cha Katoke cha huko Bukoba ambako alifundisha hadi mwisho wa mwaka huo. Baadaye alijiuzulu tena kazi hiyo ya ualimu ili kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kusomea shahada ya B.A. katika masomo ya sanaa ambapo alihitimu katika mwaka wa 1979 na kuajiriwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili (TUKI). Mbogo alisomea shahada yake ya uzamili (M.A.) aliyohitimu 1980 akiwa bado anafanya kazi katika taasisi hiyo ya TUKI.

Ujuzi wa matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya Kiafrika katika utunzi wa kazi za sanaa hususani tamthilia ya Kiswahili, alianza kuudhihirisha alipokuwa mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo alibobea katika taaluma ya sanaa za maonyesho. Aidha, alinoa kipawa chake cha sanaa za maonyesho ya jadi alipokuwa mwajiriwa wa taasisi ya TUKI ambapo alikuwa mtaalamu katika Kitivo cha Sanaa za Maonyesho. Mbogo aliendeleza taaluma yake katika Chuo Kikuu cha Humbolt huko Ujerumani kwa kujiunga na masomo ya shahada ya uzamifu (Ph.D) ambako pia alifanya utafiti katika uwanja wa sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika katika eneo la Afrika Mashariki. Matokeo ya utafiti wake yanajidhihirisha vizuri katika tamthilia na riwaya alizoziandika.

Baada ya kuhitimu na shahada ya uzamifu katika mwaka wa 1985, Mbogo alirudi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama mhadhiri. Katika kazi zake kama mhadhiri wa chuo kikuu, alishikilia vyeo mbalimbali kazini vikiwemo uenyekiti wa chama cha CHASAMATA (Chama Cha Sanaa za Maonyesho Tanzania) na kuwa mkurugenzi wa kundi la uigizaji la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Dar es Salaam University Drama Group). Baadaye katika mwaka wa 1988, Mbogo alihamia Chuo Kikuu cha Moi nchini Kenya katika kiwango cha mhadhiri ambapo pia aliendeleza

fani ya fasihi na kuongoza makundi mbalimbali ya uigizaji. Katika mwaka wa 1990, ustadh Mbogo alihamia Chuo Kikuu cha Maseno (wakati huo kikiwa Chuo Chandamizi) ambapo alianzisha idara ya Lugha ya Kiswahili na Lugha nyiingine za Kiafrika. Baada ya kuhitimisha wakati wake katika Chuo kikuu Cha Maseno, Ustadh Mbogo vilevile aliweza kufundisha katika vyuo vya Kenyatta na Kigali, Rwanda ambapo alikuza uigizaji wa sanaa za maonyesho.

Pamoja na tamthilia ya Ngoma ya Ng'wanamalundi, Mbogo ameandika na kuchapisha kazi zifuatazo:

**Tamthilia**
Giza limeingia (1980 TPH)
Tone la Mwisho na Watoto Wetu (1981, Up)
Morani (1993: Dup)
Sundiata (1994: Lake Publishers)
Isinyango
Ndoto za Joseph
Exodasi
Nebukadineza
Visa vya Ayubu
**Riwaya**
Bustani la Edeni (1993)
Vipuli vya Figo (1992)
Watoto wa Mama Nitilie (Up)
**Vitabu vya watoto**
Mfululizo wa Hadithi za Manu (Juzuu 6)
Chemshabongo I na II

Kwa mujibu wa tahakiki ya takribani kazi nyingi za mwalimu Mbogo, ni wazi kuwa ameathiriwa na hali ya sanaa za maonyesho ya Kiafrika ya jadi pamoja na tamaduni na maendeleo ya jamii za Kiafrika. Yeye ni mmoja wa watunzi na wahakiki wa tamthilia ya Kiswahili wanaoonyesha matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya Kiafrika katika utunzi wa kazi zao kuanzia miaka ya 1970. Wole Soyinka na Chinua Achebe wa Afrika Magharibi ni mfano mzuri wa watunzi wa Kiafrika waliochota na kutumia maarifa ya sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika na kuyaoanisha na misingi ya drama ya Kimagharibi katika kutunga tamthilia, riwaya na

hadithi fupi. Kazi za Emmanuel Mbogo zina muonjo na ladha kamili ya utamaduni wa Kiafrika.

**Jedwali 5.3: Tanzu za Sanaa za maonyesho katika Tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi***

| | Utanzu wa sanaa za maonyesho | Mifano katika Tamhtilia |
|---|---|---|
| i) | Nyimbo na ngoma | i) Ngoma ya Nyamiti - uk 8<br>ii) Ngoma ya Sindimba – uk 11<br>iii) Ngoma ya Chidama – uk 27<br>iv) Ngoma ya Ng'wanamalundi - kr 48 - 49 |
| 2. | Mazungumzo / hotuba | i) Hotuba ya Chidama – uk 31 na kr – 32 – 33 Uzungumzi nafsi wa Chibuba – uk 34<br>ii) Ulumbi - Uzungumzi nafsi wa Chidama – kr 28 - 29<br>iii) Malumbano ya utani - kr 4 – 5<br>iv) Soga - kr 4 - 5 |
| 3. | Majigambo | i) Majigambo ya Chidama - uk 24<br>ii) Majigambo ya Ng'wanamalundi – kr 48 - 49 |

**Chanzo: Data kutoka kwa tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* – Emmanuel Mbogo (1999)**

Jedwali 5.3. la hapa juu linaonyesha kwa muhtasari tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilizodondolewa kutoka kwa tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Tumeeleza tanzu hizo mbalimbali na kufafanua mbinu za matumizi yao katika utunzi wa tamthilia yenyewe katika sehemu ya uchanganuzi wa hapa chini.

### 5.3.1 Nyimbo na Ngoma katika Tamthilia ya Ngoma ya *Ng'wanamalundi*

Emmanuel Mbogo ametumia tanzu za nyimbo na ngoma mbalimbali katika kujenga na kuimarisha umbo na dhamira katika tamthilia yake ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Ngoma ni utanzu wa sanaa za maonyesho na Fasihi Simulizi kwa jumla ambao unapatikana katika takribani tamaduni za jadi za jamii nyingi za Kiafrika. Nyimbo huhusisha upigaji ngoma, uimbaji, uchezaji viungo vya mwili, upigaji mbija na vigelegele na uigizaji wa namna fulani kutegemea shughuli inayoimbiwa au kuchezewa ngoma. Uchezaji ngoma na uimbaji huandamana na uvaliaji wa maleba na vizuizui maalumu vinavyochukuana na muktadha wa wimbo/ngoma inayowasilishwa.

Ngoma na nyimbo vilevile huandamana na ubebaji wa vifaa mahususi kwa mujibu wa nyimbo zinazoimbwa na kuchezwa na jamii mahususi za Kiafrika kwa mujibu wa tukio maalumu linalohusishwa na jamii hiyo. Ngoma vilevile hurejelea nyimbo na dansi za tamaduni za kiasili. Ngoma na nyimbo alizozichota mtunzi Emmanuel Mbogo kutoka kwa sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika na kuzitumia kibunifu katika kujenga tamthilia yake ni pamoja na ngoma ya Nyamiti, ngoma ya Sindimba, ngoma ya Chidama na ngoma ya Ng'wanamalundi tunazozibainisha hapa chini na kufafanua mbinu na namna ya matumizi yao katika miktadha mbalimbali.

#### 5.3.1.1 Ngoma ya Nyamiti

Ngoma ya Nyamiti ndiyo utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi wa kwanza wa aina ya ngoma alioutumia mtunzi katika kutunga tamthilia yake. Ngoma ya Nyamiti inachezwa wakati wa sherehe ya arusi ya mwanamwali Nyamiti anayeandaliwa na somo yake anayeitwa Seche kwa ajili ya kuozwa. Ngoma hii huimbwa na kuchezwa tu wakati wa tukio la sherehe ya kumwandaa mwanamwali kwa ajili ya kuolewa wakati wa unyago. Ngoma inachezwa hivi:

**Seche: (*Anaimba*)**
Leo mambo mtaona
**Leo mambo mtaona**
**Tumembadili kijana**
Tumembadili kijana.
*(Ngoma ya Ng'wanamalundi* - *uk 8)*

Dondoo la wimbo wa hapa juu alioutumia Emmanuel Mbogo katika utunzi wa tamthilia yake ni la utanzu wa aina ya wimbo na ngoma ya arusi. Ngoma ya arusi kwa kawaida ni ngoma ya furaha kama ngoma ya unyago na jando inayochezwa wakati wa sherehe ya arusi yenyewe katika utamaduni wa Kiafrika. Hivyo, ngoma na nyimbo za arusi huimbwa katika muktadha wa tukio la arusi yenyewe. Ngoma na nyimbo nyingi mbalimbali za arusi huimbwa wakati wa jioni na wakati wa mchana kutegemea jamii ya Kiafrika na utamaduni wake na matakwa ya hadhira. Katika jamii ya

Ng'wanamalundi, ngoma na nyimbo za arusi hutumiwa kutumbuiza, kuelimisha na kufahamisha hadhira kuhusu shughuli yenyewe ya arusi.

Ingawa ngoma hii inaitwa Ngoma ya Nyamiti, ngoma yenyewe haichezwi na kuimbwa na mhusika Nyamiti mwenyewe kama inavyotarajiwa kwa kuitwa kwa jina lake. Ngoma ya Nyamiti inaanzishwa na kuimbwa na Seche ambaye ni somo yake Nyamiti anayefanya kazi ya kumtayarisha mwanamwali Nyamiti akiwa unyagoni kwa ajili ya arusi. Kama katika jando ambapo ngariba huanzishia vijana wimbo baada ya tohara, kungwi katika unyago na arusi huanzisha wimbo kama inavyodhihirishwa katika wimbo huu, **Seche: (*Anaimba*) -** *Ngoma ya Ng'wanamalundi - uk 8.* Seche ndiye kiongozi na mwimbaji wa pekee wa ngoma ya Nyamiti inayotumika kusherehekea arusi ya Nyamiti. Ngoma hii ni ngoma ya kitamaduni ya Kiafrika inayoimbwa na kuchezwa wakati wa arusi.

Nyimbo na ngoma za arusi ni nyenzo ya kuzungumza na maarusi na kuwapa mawaidha kuhusu maisha ya ndoa. Nyamiti ambaye ni msichana aliyebalehe na aliyekuwa tayari kuolewa, alikuwa amefungiwa ndani katika unyago kama ilivyo kawaida katika utamaduni wa Kiafrika ili kupewa mafundisho ya utu uzima yatakayomwezesha kuishi vyema katika ndoa yake. Katika kumbadilisha kutoka utoto kwenda utu uzima, mhusika Seche ambaye ndiye kungwi wake Nyamiti anaanzisha ngoma hiyo ya arusi kwa kuimba na kusema hivi katika dondoo, "**Leo mambo mtaona, Tumembadili kijana", - (***Ngoma ya Ng'wanamalundi - uk 8*). Haya ni maneno ambayo ni thibitisho la kumkomaza na kumchachawisha kijana kwa majukumu ya utu uzima yatakayofuata baada ya kufunga arusi. Jukumu muhimu la ngoma ya arusi kama ngoma ya Nyamiti linapatikana katika maneno ya ngoma yenyewe, "**Tumembadili kijana."**

Akieleza kuhusu dhima ya nyimbo za arusi, Muhando na Balisdya (1976) wanaeleza ya kwamba katika jamii ya Wakaguru nchini Tanzania, nyimbo za arusi huimbwa na wanawake walioolewa au waliopitia tohara ya unyago ili kutoa mafundisho kwa mwanamwali aliye unyagoni kuhusu jinsi atakavyomtunza mumewe, kuitunza familia pamoja na jamii yake. Mbali na kuitumbuiza hadhira, ngoma na nyimbo za arusi ni mbinu mwafaka ya jamii za Waafrika ya kutolea maarusi mawaidha na mafundisho adimu kuhusu asasi ya ndoa. Kwa kawaida hakuna wakati maalumu uliotengwa wa kuketi kitako na vijana na kuzungumza nao kuhusu maisha yao ya ndoa katika jamii za Kiafrika ila katika mviga wa unyago. Katika jamii nyingi za Kiafrika, wakati huu, vijana, hasa wanawali hutengwa unyagoni na kupewa mawaidha maalumu kuhusu maisha yao ya baadaye ya ndoa kupitia kwa walimu wao wanawake wanaoitwa makungwi katika utamaduni wa Kiafrika. Pamoja na maelezo yao ya kuwatayarisha wanawali hao, ngoma hupigwa, hucheza na kuimba nyimbo ambazo huandamana na utoaji wa mawaidha.

Emmanuel Mbogo vilevile, ametumia mbinu ya nyimbo na ngoma wakati wa ndoa za jadi kuonyesha na kusaili utayarishaji wa vijana wa sasa kwa maisha yao ya baadaye ya ndoa. Kwa jinsi alivyomsawiri, mtunzi anaitumia ngoma hii ya unyago na ya arusi kuonyesha jinsi Nyamiti alivyokuwa tayari kuolewa na mwanamume ampendaye kwa jina Chibupa badala ya kuponzwa na utajiri wa mwanamume asiyempenda kwa jina Chidama. Wengi wa vijana wa sasa labda wangekimbilia mali ya mzee Chidama bila kujali kuhusu furaha yao wenyewe katika maisha ya ndoa au athari ya uovu wa mzee mchimvi kama Chidama ambaye anaendeleza madhila kwa wengine kupitia kwa nguvu zake za kichawi. Nyimbo na ngoma katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ni nyenzo mwafaka aliyoichagua kuitumia mtunzi katika kujenga na kuimarisha umbo la tamthilia yake pamoja na fani na maudhui katika tamthilia hiyo.

Arusi ya Nyamiti ni mfano alioutumia mwandishi Mbogo ili kudhihirisha kijazanda utayari wa nchi za Afrika kujitawala kiuchumi, kisiasa na kijamii chini ya uongozi wa watawala waliowachagua kidemokrasia wenyewe baada ya kujinyakulia uhuru. Vita vya kupigania uhuru ni mbinu kama sherehe ya unyago na arusi katika utamaduni wa Kiafrika wa kuzifyaza nchi za Afrika kwa ajili ya kujitawala na kujitegemea zenyewe baada ya kujinyakulia uhuru. Hata hivyo, mataifa ya nchi za Magharibi yanazinyemelea kiujanja na kuzinyakua kupitia kwa njia laghai kama alivyofanya mganga Chidama kumroga mrembo Nyamiti na kuzitawala nchi za Afrika katika mfumo wa ukoloni mamboleo.

Mbogo anaitumia ngoma ya Nyamiti mwanzoni mwa tamthilia kama kivutio cha kunasa nadhari ya wasomaji. Kwa kupandisha ari ya wasomaji ya kutaka kujua ni lipi litakalotokea baada ya Nyamiti kujipaka mafuta ya uchawi kichwani, mtunzi anakuza mbinu ya taharuki. Kinyume na furaha inayoandamana na uchezaji wa ngoma na sherehe ya arusi, Nyamiti anapochemka na kuingia katika ngoma, joto kali linampanda mwilini kwa sababu ya mafuta ya uchawi aliyojipaka wakati wa kuirembesha nywele yake. Ngoma ya Nyamiti inafikia upeo wake pale Nyamiti anapokata "roho." Mtunzi anatumia ngoma hii kutuonyesha ila za wenye wivu na mahasidi wa ndoa na mbinu za Kiafrika wanazozitumia katika kuleta maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

#### 5.3.1.2 Ngoma ya Sindimba

Ngoma hurejelea nyimbo na dansi zenye misakato ya kiasili inayochezwa kuambatana na midundo ya ala za muziki. Kubo na wenzake (2013) wanaeleza kuwa ngoma au ngomezi ni fasihi ya ngoma na ala za muziki ambapo maneno hayasemwi. Milio au mapigo ya ngoma yaliwasilisha ujumbe unaofahamika tu na jamii husika inayocheza ngoma hiyo. Jamii vilevile ilitumia ngoma na nyimbo za kitamaduni ili kuweza

kuwasiliana miongoni mwa jamii na kusambaza ujumbe katika majira na wakati tofauti. Ngoma katika jamii za Kiafrika zilitumiwa kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, ngoma zilitumiwa kuarifu jamii kuhusu matukio muhimu katika jamii kama kuzaliwa kwa mtoto, tukio la ndoa, uvamizi wa kivita, matangazo ya mabaraza ya viongozi wa jamii, tukio la hatari au tangazo la kifo miongoni mwa taarifa zingine. Ujumbe wa ngoma vilevile uliweza kutambulisha habari za wafalme, machifu, mashujaa, waganga na viongozi wengine katika jamii.

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (k.h.j.) inaeleza ngoma kwanza kabisa kama ala ya muziki iliyotengenezwa kwa kuwamba ngozi katika mzinga na pili, kama mchezo wa kuvutia unaoandamana na ala ya muziki. Ngoma za kiasili hutawala katika utamaduni wa Mwafrika na mtunzi Emmanuel Mbogo amechota malighafi hii adimu ya jadi na kuitumia kujenga na kuimarisha tamthilia yake ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Anwani ya tamthilia hii vilevile imechimbuka kutokana na **Ngoma ya Ng'wanamalundi** iliyotumiwa kujenga tamthilia yenyewe.

Nyimbo za arusi katika jamii za Kiafrika huambatana na mdundo wa ngoma. Ngoma hii ya arusi ni kama utanzu mwingine wowote wa sanaa za maonyesho wa ngomezi ambao unatumiwa na jamii nyingi za Kiafrika kwa ajili ya kuiarifu jamii kuhusu matukio maalumu na muhimu kwa jamii. Mdundo wa ngoma ya Sindimba iliyokuwa inasikika kwa mbali kwa mfano ilitumika katika jamii ya Ng'wanamalundi kwa ajili ya kuwaarifu wanajamii kuhusu arusi iliyokuwa inatarajiwa kufanywa karibuni:

> ***… Mirindimo ya ngoma ya arusi inaongezeka; Sasa tunasikia wanabadili mapigo na kunasikika mirindimo ya Sindimba.*** **Nyamiti anaruka kwa furaha Ee! Sindimba – Unyago! Wote huko arusini wanachemka ila mie tu.** (*Mirindimo ya Sindimba inaongezeka*). Iko wapi kanga (*anachukua kanga*). Heri nicheze leo, kesho chambilecho somo yangu, niweke soni usoni! ***(kesha jifunga kanga mbili kiunoni sasa anaanza kucheza. Kwanza ni polepole huku akiimba pamoja na waimbaji wa nje. Sasa mirindimo ya Sindimba inapamba moto, nae Nyamiti anapamba moto.***

> ***Vigelegele vinasikika; naye anachemka zaidi*** *… anapepesuka – anachoka, anajibwaga chini kwa furaha)*
> *(Ngoma ya Ng'wanamalundi - Uk 11)*

Emmanuel Mbogo ametumia ngoma kumhusisha mhusika Nyamiti anayefanya arusi katika ngoma ya Sindimba. Kama utanzu wa ngomezi, ngoma ya Sindimba inalia kutoka mbali kuiarifu jamii ya Ng'wanamalundi kuhusu tukio hilo muhimu la arusi ya Nyamiti (***Mirindimo ya ngoma ya arusi inaongezeka; Sasa tunasikia wanabadili mapigo na kunasikika mirindimo ya Sindimba*****)** – (*Ngoma ya Sindimba - Uk 11)*. Emmanuel Mbogo hawezi kuirekodi milio ya ngoma hiyo ya sindimba inapochezwa, bali kupitia kwa matendo na maelezo ya mhusika Nyamiti anayefanya arusi tunaelewa ngoma hiyo ya sindimba ni ya kutekeleza wajibu gani (**… Nyamiti anaruka kwa furaha Ee! Sindimba – Unyago! Wote huko arusini wanachemka ila mie tu).** Anapoinuka na kucheza kwa furaha, tunaelewa kwamba Sindimba ni ngoma ya furaha. Ni wakati Nyamiti anapocheza na kuruka ndipo tunapoelewa umuhimu wa ngoma hii. Sindimba ni ngoma ya arusi inayochezwa mchana na usiku katika jamii za Kiafrika kusherehekea ngoma. Tunapata ujumbe huu wakati Nyamiti mwenyewe anapotamka maneno **Sindimba – Unyago! Wote huko arusini wanachemka ila mie tu.**

Nyamiti anapousikia mdundo wa ngoma ya Sindimba kule kwake anakofungiwa unyagoni, naye anachemka na mara anainuka na kujifunga kanga mbili tayari kuanza kucheza. Mtunzi Emmanuel Mbogo anamtumia mwanamwali Nyamiti kutuelezea jinsi ngoma ya Sindimba inavyochezwa. Nyamiti ***…(kesha jifunga kanga mbili kiunoni sasa anaanza kucheza. Kwanza ni polepole huku akiimba pamoja na waimbaji wa nje. Sasa mirindimo ya Sindimba inapamba moto, nae Nyamiti anapamba moto Vigelegele vinasikika; naye anachemka zaidi…)*** - (*Ngoma ya Sindimba - Uk 11)* Sindimba ni aina nyingine ya ngoma ya arusi ambayo huchezwa

miongoni mwa jamii za Tanzania katika sherehe za arusi kwa ajili ya kutumbuiza hadhira. Kama Nyamiti, Marete (1998) anaeleza kwamba mirindimo na mapigo ya ngoma ya Sindimba huwapa waimbaji, wachezaji na hadhira mchemko ambao huwapa hamasa na ari ya kutaka kucheza ngoma. Waimbaji na wachezaji wa Sindimba huimba, hunengua viungo vya mwili, kupiga vigelegele na mbinja huku wakiigiza miondoko ya aina fulani.

Wakati wa sherehe ya arusi katika jamii za Kiafrika, watu hujumuika pamoja usiku na mchana wakiimba na kusherehekea kwa vyakula na vinywaji. Wanajamii husherehekea kwa njia hii kama dhihirisho la kupokezana mwali kwa pande mbili zinazoshiriki katika ndoa. Ngoma hii ya arusi vilevile iliwashirikisha wanajamii wote pamoja na kuwapa vijana ambao hawajaoa nafasi ya kukutana na kuchumbiana. Ngoma za kiasili zilikuwa njia nzuri ya kuwakutanisha wanajamii na kukuza umoja uliokuwa kiungo muhimu cha kudumisha amani na utulivu katika jamii.

Katika hali ya kawaida ya utamaduni wa jadi wa Kiafrika, mchezo wa ngoma ya arusi ni mchezo unaohusisha wanajamii wote katika kuucheza. Hata hivyo, katika sehemu hii ya tamthilia yake, mtunzi Emmanuel Mbogo ameleta mabadiliko ya kimakusudi kupitia kwa matumizi ya utanzu wa ngoma katika kujenga na kuimarisha tamthilia yake ili yaweze kumfaa katika utunzi. Hivyo, Emmanuel Mbogo ameifanya ngoma hiyo ya arusi kusikika kutoka mbali na kumfanya Bi Arusi (Nyamiti) kuwa mchezaji wa pekee mbele ya hadhira ya mchezo wa *Ng'wanamalundi.* Emmanuel Mbogo vilevile anamfanya mhusika Nyamiti kuwa msimulizi na mhakiki wa ngoma hiyo katika jukwaa la tamthilia hii yenye misingi ya ki-Aristotle. Katika mabadiliko aliyoifanyia ngoma hiyo, mtunzi vilevile, ameitenga hadhira ya mchezo na wachezaji wa ngoma ya arusi ya Sindimba ambao hawawezi kutagusana katika ngoma hiyo kama ilivyo katika misingi ya uchezaji wa ngoma ya arusi katika tamaduni na mila za

Kiafrika. Ngoma ya arusi ni ngoma ya furaha inayowahusisha wanajamii wote. Nyamiti anasema, "… ***anaruka kwa furaha Ee! Sindimba – Unyago! Wote huko arusini wanachemka ila mie tu.*"** Nyamiti, katika mabadiliko hayo anatumika kama msimulizi na mhakiki anayeifahamisha hadhira kuhusu yaliyokuwa yanafanyika katika matayarisho ya arusi yake. Mtunzi amemtumia mhusika Nyamiti katika tamthilia yake mbali na maelezo ya jukwaa kama kiunzi cha kufafanua matukio kati ya waigizaji na watazamaji, hisia na mawazo mbalimbali yanayoigizwa.

Mbali na ngoma ya Sindimba, Emmanuel Mbogo vilevile ametumia ngoma nyingine ya Chidama na Ng'wanamalundi katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* kimakusudi kwa ajili ya kujenga fani na kuimarisha umbo la tamthilia yake kwa ajili ya kuzitoa dhamira zake vizuri.

### 5.3.1.3 Ngoma ya Chidama

Katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, ngoma ya Chidama inaimbwa na kufundishwa na mganga mwenye wivu na anayetumia uganga wake kwa njia mbaya kuwaathiri watu wasio na hatia, wasiokubaliana na mawazo yake au wale anawaona kama wanashindana naye katika jamii yake. Mganga mwenyewe ambaye ni Chidama anamtumia mfuasi na mtumishi wake kwa jina Mahube kuwafundisha wimbo huo watu aliowaroga na kuwabadilisha kuwa vizuu. Kwa mujibu wa mganga huyu, jina lingine la ngoma ya Chidama ni "dansi ya Tilantiki". Jina "tilantiki" limetumiwa kimakusudi na mtunzi wa tamthilia kuonyesha kuwa hii ni ngoma yenye mdundo wa kisasa ulioigwa kutoka nje ya bara la Afrika au ambao asili yake ni ughaibuni. Dansi ya "Tilantiki" inaimbwa na kuchezwa na vizuu wakiongozwa na Mahube, kijakazi wa mganga Chidama kama inavyoonyeshwa katika dondoo la hapa chini:

MAHUBE: **Wote mko tayari?**
VIZUU: Oooo!

MAHUBE: Kweli!
VIZUU: Ooooo!
MAHUBE: Dansi ya nani?
VIZUU: **Chi-chi-chi-chii! (***Ngoma ya Ng'wanamalundi* - uk 26)

Katika kuanzisha ngoma ya Chidama, kiongozi wa ngoma hiyo ambaye ni Mahube kama tunavyoonyeshwa katika dondoo la hapa juu anawauliza vizuu kama wako tayari, "**Wote mko tayari?"** Hii ni ngoma inayochezwa na wengi na huweza kuwa na kiongozi anayeelekeza namna ya kuimba au kuicheza. Ngoma inaweza kuchezwa na mtu mmoja, wawili au watu wengi. Vizuu ni watu wa kawaida waliofanyiwa uchawi wa aina fulani na mchawi Chidama wakabadilishwa kuwa mazuzu wasiojitambua wala kujielewa. Vizuu hubadilishwa kwa njia hiyo ya uchawi na mganga laghai ili waweze kumtumikia kwa lazima katika kazi zake bila kulalamika wala kuelewa kuwa anawanyanyasa katika hali ya utumwa. Hii ndiyo sababu ngoma hii inaitwa ngoma ya Chidama, "**Chi-chi-chi-chii!", (***Ngoma ya Ng'wanamalundi* - (uk 26). Ngoma ya Chidama ni ngoma inayochezwa na vizuu katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ili kumtukuza bwana wao mchawi Chidama.

Ngoma na nyimbo huchezwa kwa ajili ya dhima maalumu kutegemea utanzu wa ngoma hiyo na hadhira inayoimbiwa au kutegemea wachezaji wa ngoma au wimbo unaoimbwa. Emmanuel Mbogo alitumia ngoma hii kuonyesha hali ya udhibiti na unyanyasaji unaofanyiwa maskini wengi na matajiri wachache ili waweze kuwatumikia wao wenyewe. Ngoma ya Chidama ni aina ya dansi ya "kiuchawi" inayobuniwa na kufundishwa vizuu na kijakazi Mahube ili kuchezwa na vizuu hao wa mchawi Chidama kwa dhima maalumu ya kichawi ya kuwapumbaza na kuwatia ari ya kufanya kazi kwa nguvu, kama asemavyo mchawi Chidama katika dondoo la hapa chini;

"… **Kuwafanya wakakamavu wa mwili lakini mazimbwezimbwe wa roho na bongo.** Dansi ya kutia mbolea nyongo ya unyonge wao.

> Dansi ya kurutubisha nidhamu katika kazi zao …" (*Ngoma ya Ng'wanamalundi* - uk 26)

Wimbo huu ni wa kisasa na si wa Kiafrika kwa sababu umenaswa katika ukanda wa muziki na huweza kuchezwa kwa mitambo kisha vizuu wanaucheza. Kwa jinsi jina lake lilivyo, "Tilantiki", ngoma hii ni ya Kimagharibi na haieleweki na vizuu wanaoicheza. Ni ngoma ya kuwateka mawazo wanaoicheza kama anavyosema mhusika Chidama, "**Kuwafanya wakakamavu wa mwili lakini mazimbwezimbwe wa roho na bongo"** – (*Ngoma ya Ng'wanamalundi* - uk 26)**.** Ngoma hii ya "Tilantiki" inadokeza kwamba ni ngoma ngeni iliyoletwa na wageni walowezi na kulazimishwa kuchezwa na wenyeji wa Afrika. Ngoma ya Chidama inachezwa kwa namna ya mdundo unaoendeleza hali ya ukoloni mamboleo. Hali hii inawaweka vizuu katika hali ya utumwa unaowafanya mazuzu walio na uwezo wa kuwatumikia mabwana wao lakini wasiokuwa na uwezo wa kubaini ukweli kuwa wao ni watumwa. Watumwa wasioweza kujikomboa kimawazo ili kupigania haki zao na kujisimamia wenyewe katika fikira na matendo yao wenyewe. Ngoma yenyewe inaenda hivi:

> VIZUU: *(wanaitikia)* **Ooooooo!**
> MAHUBE: Wote mko tayari.
> VIZUU: Oooo!
> MAHUBE: Kweli!
> VIZUU: Ooooo!
> MAHUBE: Dansi ya nani?
> VIZUU: **Chi-chi-chi-chii!**
> MAHUBE: Nani?
> VIZUU: **Da-da-da-daaaa!**
> MAHUBE: Nani?
> VIZUU: **Ma-ma-ma-maaa!**
> MAHUBE: *(Muziki kidogo unaanza)* o.k! o.k. o.k!
> ONE: TWO: THREE: GO!
> *(Ngoma ya Ng'wanamalundi - uk 2)*

Ngoma ya Chidama ya dondoo la hapa juu vilevile inaitwa ngoma ya "Tilantiki". Tilantiki ni jina alilolitohoa mwandishi Emmanuel Mbogo kutoka kwa jina "Atlantic" ambalo ni jina la bahari kuu. Mwandishi amelitumia jina hili kijazanda ili kuficha

ukweli kuwa ngoma hii imevuka bahari ya *Atlantic* ikiwa inaletwa kutoka ng'ambo ughaibuni. Hata hivyo, hii ni ngoma ya Chidama kwa sababu inaimbiwa na mganga Chidama. Ngoma hii labda ingeitwa ngoma ya vizuu kwa sababu inaimbwa na vizuu wanaomilikiwa na Chidama. Maneno yanayosemwa na vizuu katika ngoma hii hayaeleweki kwani ni mdundo wa sauti za kimuziki zisizoleta maana kwa vizuu wanaoicheza lakini zinazosisimua na kufurahisha wanaozicheza. Sauti, "**Ooooooo! … Chi-chi-chi-chii! … Da-da-da-daaaa! … Ma-ma-ma-maaa!"** (*Ngoma ya Ng'wanamalundi* – uk 27) zinazoimbwa na vizuu ni mwigo wa sauti za ngoma inayochezwa na vizuu na kuongozwa na Mahube, Kijakazi wa Chidama. Vizuu wanapocheza ngoma hiyo, wanasisimukwa kama watu waliotumia dawa za kulevya au waliovuta bangi na kupata nguvu nyingi za kumfanyia Chidama kazi bila kulalamika ingawa hawalipwi.

Mazingira wanakofanyia kazi vizuu ni mabaya na yaliyojaa mateso ambayo hayafai hata kwa wanyama. Ngoma ya Chidama ni ngoma ya kuwalainisha watu wa kawaida kama hawa vizuu ili waweze kukubali hali ya kunyanyaswa. Ngoma hii vilevile inawafanya vizuu kukubali mahali wanapofanyia kazi ambapo kuna mazingira mabaya, ambapo hawapati malipo yoyote wala chakula kinachofaa. Ngoma ya Chidama kwa jinsi ilivyochezwa ni ya kuwapumbaza na kuwalainisha vizuu wasijitambue na kuelewa hali yao mbaya kama wafanyakazi. Ngoma ya Chidama inamwezesha mtunzi kuendeleza dhima ya unyanyasaji katika tamthilia yake ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi.*

Emmanuel Mbogo, vilevile, ametumia utanzu wa ngoma ya Chidama kijazanda kudhihirisha jinsi mataifa, mashirika, matajiri na waajiri wanavyotumia mbinu mbalimbali kuwapumbaza wananchi na wafanyakazi wasijitambue ili wasiweze

kulalamikia hali mbaya ya kufanyia kazi. Wimbo kwa jinsi ulivyobuniwa ni wa kisaikolojia wa kuteka hisia za vizuu wafanya kazi kwa nia ya kuwapumbaza tu. Muziki huu una umuhimu tu kwa mwasisi na mdhamini wake ambaye ni tajiri, mnyanyasaji, mchawi na mganga Chidama. Wachezaji wa ngoma hii hutaja jina la Chidama katika wimbo bila kuelewa maana ya maneno wanayoyasema. Ni ngoma ya kuteka mawazo na kuwapumbaza wanaoshiriki katika kuicheza ngoma hiyo. Vizuu wamefanyiwa uchawi na kutekwa mawazo na hawatambui wao ni nani. Kupitia kwa ngoma ya Chidama, mtunzi Emmanuel Mbogo anaionyesha hadhira mbinu wanazozitumia matajiri kuwadhibiti na kuwanyamazisha wanyonge wafanyakazi wasilalamike wanaponyanyaswa.

Katika mbinu hii ya uzungumzi nafsi au usimulizi katika nafsi ya kwanza katika dondoo la hotuba la hapa chini, Mbogo anadhihirisha jinsi matajiri mabwanyenye huwatumikiza wafanyakazi wao bila wao kutambua wala kuelewa kuwa haki zao zimekanyagiwa chini. Chidama mwenyewe anaeleza namna wanavyoendeleza unyanyasaji wa wafanyakazi kwa kusema maneno yafuatayo;

> **CHIDAMA: (*peke yake*).** Watoto wangu hawana gharama. Hawana gharama watoto wangu. Hawana makuu wala mahitaji. **Watoto wangu watiifu. Hawana kelelekelele kama za wale wenzao mjini. Wale vijakazi na watwana wa viwandani hububujika maneno toka ndimi zao ndefu kama za kinyonga.** Domokaya zao hutokota fosi kama taka machinjoni zikachafua mitima ya waungwana. **Kila kiwanda ukiingia vurumai, ghasia. Ati wenyewe wameunda vikundi vyao vya ujambazi na madai chungu nzima. Madai ya kugoma kazi. Madai ya chakula. Si wazimu? Utagomeaje kazi halafu udai chakula?** *(anafikiri*). Mimi hapa kwangu nimeisha kata kilimilimi. Hakuna mdudu anayeweza kufurukuta. Nikimwona mmoja: namfua sawasawa kabla sijamuanika juani…
> *(Ngoma ya Ng'wanamalundi - uk 28*

Kupitia kwa dondoo la hotuba la hapa juu, mtunzi anawatambulisha vizuu kama wafanyakazi ambao ni tofauti na wale wengine wanaolalamikia hali mbaya ya kufanya kazi kupitia kwa vyama vya wafanyakazi. Katika kuthibitisha madai haya,

Chidama anahutubia hivi katika hotuba yake, "**Watoto wangu watiifu. Hawana kelelekelele kama za wale wenzao mjini. Wale vijakazi na watwana wa viwandani hububujika maneno toka ndimi zao ndefu kama za kinyonga" –** **(***Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 28)***.** Vizuu katika hotuba ya Chidama wanazua taswira ya kihistoria ya watumwa walionyakuliwa kwa nguvu na wazungu kabla ya wakati wa kabla ya ukoloni. Watumwa hao walilazimizwa kufanya kazi kwa nguvu ughaibuni katika mashamba ya waarabu na wazungu ambapo hawakupewa malipo yoyote. Watumwa wa Kiafrika kama vizuu hawangeweza kulalamikia hali yao mbaya ya kufanyia kazi kwa sababu hawakuwa na uhuru wowote.

Katika kufurahia alivyowanyamazisha vizuu wafanyakazi katika shamba lake ikilinganishwa na "**vurumai"** za malalamiko ya wafanyakazi katika viwanda na mashamba ya matajiri wengine, mhusika Chidama anaeleza hivi katika dondoo la hapa juu, **"Kila kiwanda ukiingia vurumai, ghasia. Ati wenyewe wameunda vikundi vyao vya ujambazi na madai chungu nzima. Madai ya kugoma kazi. Madai ya chakula. Si wazimu? Utagomeaje kazi halafu udai chakula?" - (***Ngoma ya Ng'wanamalundi* - uk 28). Wafanyakazi katika viwanda vya matajiri wengine huwa kuna uhuru kwa wafanyakazi kugoma na kulalamikia hali yao ya kufanya kazi ikiwa mbaya. Chidama hana uvumilivu wa kuwaona wafanyakazi wake wakilalamikia hali mbaya ya kazi katika shamba lake kwani anayaona kama uwazimu. Vitisho na mizungu anayoifanya Chidama kwa vizuu ili kuwafanya waache kushughulikia masuala yao wenyewe ya kawaida na kuanza kumtumikia yeye bila faida yoyote kwao inalinganishwa na mtunzi Emmanuel Mbogo na uchawi wa mganga Chidama ambaye ni mnafiki na katili. Utamaduni wa Kiafrika wa "uchawi" ni suala la kihistoria lililokita mizizi katika jamii za Kiafrika na ambalo Emmanuel Mbogo amelichota kisanaa kudhihirisha matatizo ya ufanya kazi katika nchi za Kiafrika.

"Uchawi" aliowafanyiwa vizuu ulikuwa na nia ya kuwanyamazisha na kuwapumbaza vizuu wasijue haki zao. Emmanuel Mbogo anayatumia masimulizi ya Chidama ya aina ya hotuba kuionyesha hadhira jinsi mabwanyenye huwatumikiza wafanyakazi wao vibaya na kuwanyamazisha ili wasiweze kulalamika wala malalamiko yao kujulikana na umma wa nje.

Dondoo la hapo juu vilevile ni mfano mwingine wa utanzu wa uzungumzi nafsi katika fani ya sanaa za maonyesho ya jadi. Chidama akiwa pekee - **CHIDAMA; (*peke yake*)** amejihusisha katika uzungumzi nafsi ambapo anahutubia hadhira akiwa mhusika wa pekee jukwaani kuzungumzia kuhusu alivyopunguza gharama katika shamba lake kwa kuwanyamazisha kwa vitisho vya kuwakata ndimi na kuwaadhibu tofauti na mashamba mengine ambapo wafanyakazi wanagomea chakula na hali zingine mbaya za kufanya kazi na kufanya gharama ya kuliendesha shamba kuwa ghali. Kama katika wakati wa utumwa na okoloni, waafrika walinyakuliwa kwa nguvu na kufanyishwa kazi kwa nguvu katika hali mbaya ya kufanya kazi na bila wao wenyewe kupata faida yoyote. Mazungumzo yake yana usanifu mkubwa kama yale ya utanzu wa mazungumzo ya ulumbi. Mazungumzo ya hotuba katika dondoo la hapa juu yana ubunifu na ufasaha mkubwa unaopatikana tu katika ulumbi. Mtunzi ameutumia utanzu huu wa uzungumzi nafsi wenye ufasaha na ulumbi wa hali ya juu ili kujenga na kuimarisha ujumi wa umbo la kipekee la tamthilia yake mbali na kupitisha ujumbe wake kwa hadhira.

### 5.3.2 Mazungumzo katika Tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*

Emmanuel Mbogo vilevile ametumia tanzu za mazungumzo ambazo ni fani ya sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia yake ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Kuna mazungumzo ya aina mbalimbali yaliyotumiwa na

Emmanuel Mbogo katika utunzi wa tamthilia yake. Mazungumzo ni utanzu wa fani ya sanaa za maonyesho na Fasihi Simulizi kwa jumla ambayo hufanywa kwa maongezi ya mdomo na yenye usanii mkubwa. Katika mazungumzo ya sanaa za maonyesho kama wanavyosema King'ei na Kisovi (2010), uhalisia haunakiliwi moja kwa moja bali humithilishwa kitamathali kwa kutumia jazanda, chuku, kejeli, tashbihi miongoni mwa mbinu zingine. Mazungumzo katika sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya utamaduni wa Kiafrika hujumuisha tanzu za hotuba, malumbano ya utani, soga, mawaidha, ulumbi miongoni mwa zingine ambazo tumezibainisha kuwa zimetumiwa katika utunzi wa tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na kufafanua hapa chini katika tasnifu hii namna zilivyotumiwa;

#### 5.3.2.1 Mbinu ya Hotuba

Katika uzungumzi nafsi wa Chidama uliorejelewa hapo juu, mhusika Chidama anatoa hotuba kwa hadhira katika mbinu ya uzungumzi nafsi. Katika maisha ya kawaida, hotuba ni maelezo yanayotolewa na msemaji aliyeteuliwa ili kuwasilisha ujumbe kwa wasikilizaji kuhusu mada fulani aliyoiteu mwenyewe au aliyopewa na mdhamini. Katika fani ya sanaa za maonyesho, hotuba hutolewa kwa usanii wa juu na kwa njia isiyokera na hutumia msamiati unaolingana na mada, tajriba na uelewa wa hadhira. Mtunzi Emmanuel Mbogo ametumia utanzu wa hotuba katika sehemu mbalimbali za kazi yake kama tunavyoonyesha katika ufafanuzi wa hapa chini.

Akizungumzia kuhusu watumwa wake ambao kupitia mbinu za uchawi amewafanya vizuu, Chidama mhusika mnafiki, anajigamba na kujipiga kifua kuwa ana wafanyakazi ambao hawalalamiki, hawadai chakula wala kumgharimu chochote. Katika hotuba yake ya uzungumzi nafsi iliyofanywa katika nafsi ya kwanza akiwa peke yake, anasema hivi:

> Watoto wangu hawana gharama. Hawana gharama watoto wangu. Hawana makuu wala mahitaji. Watoto wangu watiifu. Hawana kelelekelele kama za wale wenzao mijini. Wale vijakazi na watwana wa viwandani hububujika maneno toka ndimi zao ndefu kama za kinyonga. Domokaya zao hutokota fosi kama taka machinjoni zikachafua mitima ya waungwana. Kila kiwanda ukiingia vurumai, ghasia. Ati wenyewe wameunda vikundi vyao vya ujambazi na madai chungu nzima. Madai ya kugoma kazi. Madai ya chakula. Si wazimu? Utagomaje kazi halafu udai chakula? (anafikiri) Mimi hapa kwangu nimeisha kata kilimilimi. Hakuna mdudu anayeweza kufurukuta. Nikimwona mmoja: namfua sawasawa kabla sijamuanika juani (kimya) Lakini …
> *(Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 28)*

Mtunzi ametumia mbinu ya mazungumzo ya aina ya hotuba katika dondoo la hapa juu ili kuwasilisha ujumbe wake kwa njia mwanana inayopatikana tu katika sanaa za maonyesho ya kijadi. Hotuba ya Chidama ambayo ni mojawapo ya utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi inatolewa na mganga mashuhuri ambaye amebuniwa kisanii na mtunzi Emmanuel Mbogo. Hotuba ni mbinu aliyoichagua mtunzi kimakusudi sio tu kwa ajili ya kupitisha ujumbe wake, bali pia kuimarisha muundo wa tamthilia yake. Kama ilivyo katika mihimili ya nadharia ya Uhistoria Mpya, hotuba hii haitolewi katika mazingira ya kawaida. Chidama vilevile si mhusika wa kawaida bali ni mhusika aliyebuniwa kibunifu kwa kummithilisha na wathalimu katika jamii za Kiafrika za hapo mbeleni hasa wakati wamiliki watumwa na wakoloni waliowadhulumu wafanyakazi Waafrika. Chidama ni mhusika maalumu anayepewa nafasi maalumu ili kutoa ujumbe mahususi wa udhalimu.

Chidama anarudia mazungumzo ya hotuba yake akiwa peke yake tena pale anapojigamba kuhusu uwezo wake wa ajabu wa kuwageuza binadamu na kuwafanya vizuu wasiojielewa ambao anawatumikiza kama watumwa katika kazi zake katika dondoo la hotuba na uzungumzaji nafsi katika kurasa 32 – 33. Wafanya biashara wa utumwa na mabwanyeye wa kikoloni kama mchawi Chidama katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* waliwabadilisha wafanya kazi wao na kuwafanya vizuu

wasio na gharama kali na wasiojua haki zao kazini. Mhusika Chidama anatumiwa na Emmanuel Mbogo kudhihirisha matatizo ya kihistoria ya unyanyasaji na haki za wafanya kazi.

### 5.3.2.2 Mbinu ya Ulumbi

Ulumbi ni aina mojawapo ya sanaa za maonyesho ya jadi na Fasihi Simulizi ambayo aghalabu huwasilishwa hadharani na mhusika mwenye umahiri na ufasaha wa usemaji mbele ya hadhira kwa malengo ya kuishawishi jamii kufuata mkondo fulani wa kimaisha au kufanya mambo kwa njia fulani. Emmanuel Mbogo amemtumia mhusika Chidama katika utunzi wa tamthilia yake kusema moja kwa moja na hadhira yake katika mbinu ya ulumbi kama ilivyo hapa chini:

> CHIDAMA: **Kazi kidogo tu. Lakini wajinga wengine watakwambia ni sihiri. Hakuna sihiri yoyote bali ufundi, utaalamu, ujuzi (***kimya kidogo***). Jambo kubwa hapa ni kuyateka na kuyafuga mawazo ya watu wako. Kuwapumbaza, kuwatia ubozi, ubwege ili wasijijue. Uweze kuwatumia utakavyo. Na hawawezi kusema lolote la maana kwani tayari uwezo wao wa kufikiri umo mikononi mwako.** Hivyo ndivyo **sisi watu wenye ujuzi tunavyofinyanga udongo ili kuumba vijakazi na vitwana** vyetu. **Kizuu hana makuu hahitaji kitanda. Kama nguruwe anaweza kulala topeni. Hahitaji blanketi wala shuka. Kama kima hujifunika viganja vya mikono yake. Hana gharama ya chakula kizuu. Ukimpa maganda ya ndizi atakula. Ukimkorogea maungaunga, yawe ya njano au meusi, yawe ya uchungu au chachu – kizuu atakula, tena kwa furaha. Hasemi, hakatai. Bali hukushukuru wewe bwana wake. Wakati mwingine huna haja ya kuwapa chakula hapa nyumbani. Unaweza ukawaacha wakajilia chochote wakiwa gizani. Vizuu, kama ng'ombe au mbuzi, hujichungia wenyewe huko mashambani kwangu, wakalima huku wakiokota minyoo na panzi wakashibisha matumbo yao na kwa kweli hakuna chakula kinachotia nguvu katika mishipa yao kama minyoo, panzi na nzi** warukao juu ya vinyesi vyao. **Nakwambieni, ukiwa na akili na ukajua namna ya kuzitumia, kutajirika ni kama mchezo wa kitoto.** Lakini, tuwache hayo. Sasa nitazame … (*Nyamiti bado kalala pale kitandani. Chidama anamwendea akiwa na tunguri zake mbili. Akimwimbia nyimbo za uchawi. Wakati huo huo*

> *anaingia Melo na kuweka chupa ya dawa upande wa kushoto mwa jukwaa, na jembe upande wa kulia mwa jukwaa, kisha anatoweka. Sasa uchawi wa Chidama unamfanya Nyamiti aamke taratibu na kutembea katika mangazibwe ya usingizi akielekea, polepole kunako chupa ya dawa. Anaishika, kwa taabu anaikunywa yote. Hivyo hivyo akiwa kwenye usingizi anaelekea kunako jembe, analiinua, analiweka begani taratibu na kutokea mlango wa kushoto…*)
> CHIDAMA: (*anapasua kicheko*) Kazi kidogo tu! - *(Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 31)*

Hotuba katika dondoo la hapa juu, inamdhihirisha mhusika Chidama kama mlumbi mkubwa kwa jinsi anavyojitapa kwa kiburi kikubwa kuhusu jinsi ilivyo kazi ndogo kuwabadilisha binadamu wa kawaida wa taifa lake na kuwafanya watumwa wake binafsi wanaomfanyia kazi bila malalamiko yoyote licha ya kwamba anawanyanyasa na kuwatumia vibaya. Hotuba ya Chidama imewasilishwa kwa ulumbi mkubwa wenye ufasaha.

Walumbi kama Chidama huhusisha viziada lugha na mbinu zingine za kurudiarudia usemi ili kusisitiza ujumbe na kuhakikisha kuwa wameishawishi jamii husika kukubaliana na maoni yao kama wasemavyo King'ei na Kisovi (k.h.j.). Anapoelezea jinsi ilivyo rahisi kuwafanya watu kuwa watumwa wake wanaomtumikia bila malalamiko, Chidama anarudiarudia maneno kusema hivi, "**Kazi kidogo tu. Lakini wajinga wengine watakwambia ni sihiri. Hakuna sihiri yoyote bali ufundi, utaalamu, ujuzi.** *(kimya kidogo)* **Jambo kubwa hapa ni kuyateka na kuyafuga mawazo ya watu wako. Kuwapumbaza, kuwatia ubozi, ubwege ili wasijijue. Uweze kuwatumia utakavyo. Na hawawezi kusema lolote la maana kwani tayari uwezo wao wa kufikiri umo mikononi mwako" – (***Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 32).* Akijitapa kuwa ujuzi wake wa kufanya watu kuwa watumwa vizuu si uchawi, Chidama anarudiarudia maneno ufundi, utaalamu na ujuzi kuwa ndiyo mbinu kubwa anayoitumia. Aidha, anarudiarudia maneno "kuwapumbaza, kuwatia ubozi, na ubwege" ili wasijijue ili kuelezea kuwa jambo kubwa katika kuwafanya watu kuwa

watumwa ni kuyateka na kuyafuga mawazo ya watu wako. Hii ndiyo mbinu kubwa iliyotumiwa na wamiliki wa utumwa katika karne na kumi na nane na kumi na tisa na wakoloni katika karne ya ishirini. Mbogo aliyachota maarifa haya ya dhuluma za kihistoria na kuyatumia kisanaa kueleza matatizo ya sasa ya wafanya kazi.

Katika usemi wao wa kifasaha, walumbi huweza kutumia mifano fulani kama vielelezo vya kusisitiza ujumbe wa maelezo yao. Chidama anatumia mfano wa mfinyanzi kama kielelezo kufafanua ujuzi wake wa kuwabadilisha watu na kuwafanya watumwa kwa kusema hivi, "**sisi watu wenye ujuzi tunavyofinyanga udongo ili kuumba vijakazi na vitwana vyetu" – (***Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 32).* Kwake Chidama, huku ndiko kuwa na akili na kuelewa jinsi ya kuzitumia akili hizo ili kuwa tajiri. Jambo hili ambalo ni gumu kwa watu wa kawaida, Chidama analiona kuwa mchezo wa kitoto. Chidama mwenyewe ndiye anayeelewa namna ya kuwafanya watu mazuzu au vizuu ambao hawaelewi namna wanavyonyanyaswa na kutumiwa vibaya na mabwana na waajiri wao katika mfumo mahususi wa uzalishaji mali.

Mwandishi Emmanuel Mbogo alimtumia mhusika Chidama kuhutubu kwa ufasaha wa mlumbi kwa nia makusudi ya kueleza na kuonyesha vizuu ni nani katika tamthilia yake ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi.* Akionyesha kwamba vizuu ni wafanyakazi ambao hawana gharama yoyote katika kazi ya uzalishaji mali, Chidama anaeleza ya kwamba," **Kizuu hana makuu hahitaji kitanda. Kama nguruwe anaweza kulala topeni. Hahitaji blanketi wala shuka. Kama kima hujifunika viganja vya mikono yake. Hana gharama ya chakula kizuu. Ukimpa maganda ya ndizi atakula. Ukimkorogea maungaunga, yawe ya njano au meusi, yawe ya uchungu au chachu – kizuu atakula, tena kwa furaha. Hasemi, hakatai. Bali hukushukuru**

**wewe bwana wake. Wakati mwingine huna haja ya kuwapa chakula hapa nyumbani. Unaweza ukawaacha wakajilia chochote wakiwa gizani. Vizuu, kama ng'ombe au mbuzi, hujichungia wenyewe huko mashambani kwangu, wakalima huku wakiokota minyoo na panzi wakashibisha matumbo yao na kwa kweli hakuna chakula kinachotia nguvu katika mishipa yao kama minyoo, panzi na nzi …" – (*Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 32)*.**

Ulumbi wa kifungu kilichorejelewa hapa juu ni mfano wa utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika anaoutumia mtunzi Emmanuel Mbogo ili kuionyesha hadhira ya tamthilia yake jinsi walowezi wanavyowashawishi walowezi wengine wenzao kunoa maarifa yao ya kuwafanya Waafrika kuwa watumwa. Hii ndio mbinu wanayoitumia walowezi waweze kujiimarisha ili kuendelea kuwafanyia Waafrika na watawaliwa wengine wa dunia ya tatu madhila na unyanyasaji wa aina hii. Chidama ana ufasaha wa hali ya juu anapohutubia hadhira kuhusu uwezo wake wa kuwafanya binadamu wa kawaida kuwa vizuu, mizuka na watumwa ambao hawalalamiki wanaponyanyaswa na kupokonywa haki zao za kibinadamu.

#### 5.3.2.3 Mbinu ya Malumbano ya Utani

Emmanuel Mbogo ametumia utanzu wa sanaa za maonyesho wa malumbano ya kutaniana katika utunzi wa tamthilia yake. Malumbano ya utani kwa jina lingine ni mchongoano. Mchongoano ni utanzu wa sanaa za maonyesho ambao hujumuisha mazungumzo ya kutaniana kwa kujibizana kati ya marafiki, mashemeji, makundi au makabila tofauti. Katika malumbano ya utani, anayetaniwa hutoa jibu kwa utani aliofanyiwa papo kwa papo kwa kutumia dhihaka vilevile isiyodhamiriwa kuudhi kwa vile ni kati ya watu wanaojuana na kuzoenaa kwa muda mrefu. Mfano mzuri wa malumbano ya utani katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ni ule kati ya

mwanamwali Nyamiti na somo yake Seche wakati wa maandalio ya arusi ya Nyamiti (*Ngoma ya Ng'wanamalundi* kr 4 - 5). Seche anamuuliza Nyamiti kama Bwana arusi alikuwa amefika nyumbani. Mazungumzo yao yanabadilika na kuwa malumbano ya utani kwa njia ifuatayo:

> SECHE: … Shemeji alifika?
> NYAMITI: *(kwa manung'uniko kidogo)* Sijamwona mie, sijui kwa nini …
> SECHE: *(kwa mzaha)* **"Sijamwona mie!" Unaanza wivu na kumwaya mara! Mwanamke ukiwa na wivu hukai na bwana, nikwambie basi!**
> NYAMITI: Namwaya ama yeye ndo aliyoahidi? Mimi nam …
> SECHE: (*akimkata*) **Basi, basi! Usije ukachachua hiyo sura kwa mchozi kabla ya arusi**.
> SECHE: Kesho shemeji akikutia machoni - Pu! Mbona atatamani akumeze mzimamzima ….
> NYAMITI: **Usianze kuniletea uchimvi mie!**
> SECHE: Uchimvi akufanyie nani mtoto…
> *(Ngoma ya Ng'wanamalundi - kr 4 – 5)*

Ingawa Nyamiti anamjibu Seche kwa unyenyekevu kuwa hakuwa amemwona mchumba wake na kwamba hakujua ni kwa nini hakuwa amefika nyumbani kwao kama alivyokuwa ameahidi, Seche anamtania kwa ukali ifuatavyo: "**Sijamwona mie!" Unaanza wivu na kumwaya mara! Mwanamke ukiwa na wivu hukai na bwana, nikwambie basi!"** Nyamiti vilevile anatoa jibu papo kwa papo bila kungoja. Jibu la Nyamiti kwa utani huo linakuwa na ukali kama ulivyo utani wa Seche: "**Usianze kuniletea uchimvi mie!"**

Kuna mpaka mwembamba kati ya malumbano ya utani na mchongoano. Malumbano hufanana sana na mchongoano. Kama malumbano, mchongoano humuumbua mtu kwa lengo la kumfedhehesha, kumdunisha au kumrekebisha tabia. Kama ilivyo katika dondoo la hapo juu kati ya Seche na Nyamiti, aghalabu mchongoano hutokea kati ya vijana kama Nyamiti na Seche. Mchongoano hutokea kwa nadra sana kati ya watu wazima na hasa wanaume. Mchongoano unaweza kutokea vilevile kwa misingi ya maumbile ya wanaochongoana, wasifu wao au hata kwa misingi ya tabia yao.

Mchongoano ukizidi ubeuzi kwa mtu anayechongolewa, wakati mwingine unaweza kuzuka na kuwa kisababishi cha vita kati ya wanaochongoana.

Mbali na kuendeleza na kuimarisha umbo la tamthilia yake, mtunzi wa tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* alitumia utanzu wa malumbano ya utani ili kumwezesha kutoa mafundisho muhimu ya kuweka unyumba na kudumisha ndoa kwa wasichana wanaobaleghe kama Nyamiti na Seche. Nyamiti anaponung'unika kuwa hajui ni kwa nini mchumba wake hakuwa amefika ilhali ndiye mwenyewe aliyeahidi kuwa angefika wakati huo, Seche anamdhihaki na kumrekebisha kwa kumwambia kuwa, "**Mwanamke ukiwa na wivu hukai na bwana, nikwambie basi!."** Kwa kumwambia kuwa yeye hataki uchimvi, Nyamiti anadhihirisha kuwa alipata ule ujumbe na kwa kutumia dhihaka kama aliyoitumia Seche anamfundisha kutotumia lugha yenye ukali katika mazungumzo.

**5.3.2.4 Mbinu ya Soga**

Soga ni mazungumzo ya kupitisha wakati kati ya watu wawili au zaidi yasiyozingatia muda au mada maalumu ya matumizi. Mazungumzo haya hugusia masuala ibuka, masuala ya zamani kuhusu siasa au masuala yanayohusu jinsia miongoni mwa mengine. Soga mara nyingi hufanyika baina ya watu wa rika moja ambao pia hufanyiana udamizi au chuku. Kwa kufanya hivyo, hufanyiana kebehi ya namna fulani. Mara nyingi soga huwa ya watu wanaozungumza kujiburudisha na kujichangamsha wenyewe. Mazungumzo ya soga huwa na ubunifu mkubwa. Mtunzi Emmanuel Mbogo ametumia mbinu ya soga katika utunzi wa tamthilia yake ya *Ngoma ya Ng'wanamalund*i, kama ifuatavyo;

> SECHE: … Shemeji alifika?
> NYAMITI: *(kwa manung'uniko kidogo)* Sijamwona mie, sijui kwa nini …

SECHE: ***(kwa mzaha)* "Sijamwona mie!" Unaanza wivu na kumwaya mara! Mwanamke ukiwa na wivu hukai na bwana, nikwambie basi!**
NYAMITI: Namwaya ama yeye ndo alivyoahidi? Mimi nam …
SECHE: (*akimkata*) **Basi, basi! Usije ukachachua hiyo sura kwa mchozi kabla ya arusi. Kama alisema atakuja (*kashika heleni*). Tazama heleni. Basi njewe moja heleni, njewe nyingine heleni. Hizi ndo zitachukuzana na shela lako jeupe, sio zile za mwanzo**.
NYAMITI**: Ama kweli somo unajua kuchagua. (*akivaa na ya pili akivalishwa na Seche*)**
**SECHE: Mambo si hayo! (*analeta kioo*) Hebu jilole mwenyewe …, pasua kicheko ati!**
NYAMITI: (*akicheka*) Mm! Naye huyu!
SECHE: **Kesho shemeji akikutia machoni - Pu! Mbona atatamani akumeze mzimamzima**.
NYAMITI: **Usianze kuniletea uchimvi mie!**
SECHE: Uchimvi akufanyie nani mtoto! (*Akisosonea kwa kidole cha shahada*) **Manake kesho nataka tuwakate watu vilimilimi. Na (*anastuka*) He! Mwenzangu!**
NYAMITI: Nini!
SECHE: Mjini!
NYAMITI: Kitu gani basi?
SECHE: **Nimekutana naye**.
NYAMITI: Nani?
SECHE: **Makubwa! Tena kanipa na salamu zako**.
NYAMITI: **(*Kwa hasira*) Chidama!**
SECHE: Mwenyewe huyo.
NYAMITI: Simtaki mie!
*(Ngoma ya Ng'wanamalundi - kr 4 – 5)*

Pamoja na dondoo la hapo juu kuwa malumbano ya utani kama ilivyokwisha kuelezwa katika **5.3.2.3** hapa juu, dondoo hili pia limeendelezwa kupitia kwa mbinu ya mazungumzo ya kupitisha wakati - maarufu kwa jina soga. Seche na Nyamiti ni wasichana waliobaleghe na wa rika moja. Kila wakiwa pamoja, wao hujichangamsha wenyewe katika mazungumzo au soga ya wanawake isiyokuwa na mada mahususi mbali na kufanyiana mzaha.

Wakiwa katika mazungumzo yao wenyewe mara Seche anamuuliza somo yake mwanaharusi Nyamiti kama alikuwa amemwona mchumba wake Chibupa. Katika kumjibu Seche anamwambia Nyamiti awache wivu kwani akiendelea hivyo ndoa

yake haingedumu kama inavyodhihirika katika mazungumzo yao: (***kwa mzaha***) **"Sijamwona mie!" Unaanza wivu na kumwaya mara! Mwanamke ukiwa na wivu hukai na bwana, nikwambie basi!**, (*Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 4).* Kauli ya Seche kwa Nyamiti ni ya ukweli mtupu lakini imetolewa kwa mzaha. Mzaha kati ya marafiki hauleti kero au chuki yoyote. Nia ya Seche katika maneno yake ya mzaha kwa Nyamiti si kumdhihaki bali ni ya kumrekebisha bila kumuudhi. Kupitia kwa soga kati ya Nyamiti  na Seche, vilevile, mtunzi anapata nafasi ya kupitisha ujumbe kwa hadhira kuhusu umuhimu wa mviga wa unyago katika jamii za Kiafrika. Wanawali wakiwa wamefungiwa unyagoni kabla ya ndoa yao, wanapewa mafundisho muhimu kuhusu taasisi ya ndoa. Seche katika soga hii amebadilishwa na kuwa kungwi ambaye anampa mafundisho mwanamwali Nyamiti ambaye alikuwa amebaleghe na ambaye alikuwa tayari kuolewa katika ndoa ya arusi ya hivi karibuni.

Nyamiti anapoonyesha kutofurahishwa na utani wa somo yake, Seche tena anamkaripia kwa kufanya hasira kwa maneno makali lakini yasiyoudhi na yanayoandamana na ucheshi fulani. Soga huweza kuwa na ukweli unaochoma lakini unaofumbatwa na kupunguzwa makali kupitia kwa matumizi ya vichekesho kama afanyavyo Seche kwa Nyamiti katika dondoo hili: **Basi, basi! Usije ukachachua hiyo sura kwa mchozi kabla ya arusi. Kama alisema atakuja** – *Ngoma ya Ng'wanamalundi uk 5.* Wakati mwingine katika soga huwa kuna hadithi ya kufurahisha, vichekesho au hata dhihaka ya aina fulani ili kupunguza makali ya ile kejeli.

Soga vilevile huwa na sifa ya kubadilisha mada ya uzungumzi kila baada ya muda mfupi au sentensi chache. Kabla ya kukamilisha uzungumzi wake, Seche anabadilisha mada ya mazungungumzo kwa kusema hivi: **Kama alisema atakuja *(kashika***

***heleni*). Tazama heleni. Basi njewe moja heleni, njewe nyingine heleni. Hizi ndo zitachukuzana na shela lako jeupe, sio zile za mwanzo. NYAMITI: Ama kweli somo unajua kuchagua. (*akivaa na ya pili akivalishwa na Seche*) SECHE: Mambo si hayo! (analeta kioo) Hebu jilole mwenyewe …, pasua kicheko ati! – (**Ngoma ya Ng'wanamalundi uk 5).* Mazungumzo ya aina ya soga hayafuati mada moja maalumu kwa kawaida. Mada huweza kubadilika wakati wowote katikati ya mazungumzo ya soga. Soga kati ya Seche na Nyamiti inagusia mambo mengi yanayowazunguka wasichana wa rika moja kama mavazi mbalimbali na mitindo mipya ya mavazi, porojo kuwahusu wanaume wanaowatongoza na hisia zao kuwahusu wanaume hao. Kama inavyodhihirika katika dondoo la hapa juu, mazungumzo yao huandamana na uigizaji na matendo ya kujiangalia kwa kioo na kujitazama jinsi wanavyoonekana, kusuka nywele na kufanya masuala mengine ya jinsia ya kike huku wakiambiana jinsi wanavyoonekana katika mavazi yao mapya au mtindo mpya wa ususi.

Ingawa Mbogo ameingiza mazungumzo ya aina ya soga katika utunzi wa tamthilia yake ili kuifurahisha hadhira, ametumia utanzu huu wa soga kimakusudi ili kujenga na kuimarisha ujumi na umbo la tamthilia yake. Utanzu wa soga umetumika Kimwingilianomatini na kwa njia ya kuondoshana na tanzu nyingine za sanaa za maonyesho ya jadi kama malumbano ya utani, hotuba na ulumbi ili kuendeleza umbo la tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*.

### 5.3.3 Mbinu ya Majigambo ya Chidama na Ng'wanamalundi

Emmanuel Mbogo ametumia mashairi ya aina ya malumbano na majigambo ya sanaa za maonyesho ya jadi kujenga fani ya tamthilia yake ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Chidama na Ng'wanamalundi ni wahusika wakuu katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ambao wana majukumu yanayokinzana. Ng'wanamalundi ndiye

mhusika nguli ambaye mtunzi anamtumia kuendeleza dhamira na falsafa yake ya maisha. Chidama kwa upande mwingine ni mhusika mkuu mkinzani ambaye mtunzi anamtumia kuonyesha uovu katika jamii. Wote ni wahusika bapa kwa sababu wanaendeleza sifa moja tu ya wema au ya uovu katika jamii. Mbogo anawatumia kujenga fani ya tamthilia yake kwa kuwafanya walumbane na kujigamba wenyewe kuhusu uwezo wa matendo yao.

Chidama anajigamba kuhusu ubahili wake kwa wananchi wa Ng'wanamalundi na kwa mwenzake Ng'wanamalundi kwa kumrushia joka la vichwa saba. Chidama katika majigambo yake anaghani kwa kujigamba mwenyewe na kujibandika majina mbalimbali kama "**Joka la vichwa saba, Lakini ni joka moja tu"** na kuonyesha namna mbalimbali za ukatili wake. Chidama anajigamba na kueleza ifuatavyo:

> CHIDAMA: Vizuri. **Sasa wakati umefika wa kumtumia Ng'wanamalundi joka hili la vichwa saba, liende likamfundishe adabu na heshima.** (*anaanza tena kunuiza kimyakimya. **Baadaye anaingiza mkono ndani ya kibuyu au kapu na kumtoa nyoka wa vichwa saba. Anamlisha dawa mdomoni huku akiimba kisha anasema nuizo huku angali amemshika)***
> **… Joka la vichwa saba**
> **Lakini ni joka moja tu**
> **Moja katika saba na saba katika moja,**
> **Ewe mtambaa chini,**
> **Mwenye meno ya sumu**
> Mwenye kinywa kilichojaa misumari na miiba ichomayo
> Na kurarua bila kuruma, bila kusita …
> **Haya nawende, nakutuma.**
> **Enda ukatumbukize ukucha wako**
> **Wako wa chuma ubavuni mwake,**
> **Ukamfutue na kumfumua matumbo yake**
> **Ukamzingire na kumzingara figo zake**
> **Umkamue anye na kujinyea**
> **Umuminye akojoe na kujikojolea**
> Ajue kuwa Chidama ni Chidama kweli.
> (*Anamtemea mate kichwani kisha anamrusha nje kupitia dirishani).*
> *(Ng'wanamalundi, - uk 24. Msisitizo ni wetu)*

Majigambo kama ilivyoelezwa kwingineko hapa juu ni utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi ambao unaweza kukaririwa, kughaniwa au kusemwa. Majigambo yaliyokaririwa yaliambatanishwa na utendaji ambapo fanani mtendaji aliigiza, kunengua viungo vyake vya mwili pamoja na kucheza ngoma huku akijigamba kwa kughani au kusema tu. Katika ukariri wa majigambo, mhusika au fanani aliyejigamba alibeba zana zake za kazi kutegemea kazi aliyoifanya. Katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi,* Chidama ambaye ndiye fanani anayejigamba alibeba tunguli zake za uchawi kama inavyoonyeshwa katika maelezo ya jukwaa ya mwandishi Emmanuel Mbogo akinuiza maneno ya majigambo, "*anaanza tena kunuiza kimyakimya.* ***Baadaye anaingiza mkono ndani ya kibuyu au kapu na kumtoa nyoka wa vichwa saba. Anamlisha dawa mdomoni huku akiimba kisha anasema nuizo huku anghali amemsika*** *" Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 24.* Chidama anabeba zana za uganga ambazo ndizo anazozitumia kuwafanyia wengine uovu na ukatili katika jamii ya Ng'wanamalundi huku akijigamba kuhusu ubahili na ukatili wake kwa wananchi wa Ng'wanamalundi.

Emmanuel Mbogo anatumia utanzu wa majigambo katika dondoo la hapa juu ili kuonyesha ubahili wa mhusika Chidama ambaye anachukuliwa kuwa mfano wa kiongozi katika jamii ya Ng'wanamalundi. Maneno ya jigambo la Chidama katika dondoo la hapa juu yamefumbwa na maana yake ya ndani haieleweki moja kwa moja. Aidha, maneno haya yametumiwa kijazanda ili kuwakilisha dhana fulani ambayo haieleweki kwa uwazi bila kuidadisi kwa undani. **… Joka la vichwa saba; Lakini ni joka moja tu; Moja katika saba na saba katika moja; Enda ukatumbukize ukucha wako, (***Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 24).* Joka la vichwa saba ni taswira ya kijazanda inayomrejelea mtawala dhalimu ambaye anasukumwa na tamaa yake ya kinafiki ili kuwanyanyasa na kuwadhulumu watu wengine ambao kwa kawaida ni

wanyonge wa hali fulani. Katika ukatili wake, Chidama anamtumia Ng'wanamalundi joka la vichwa saba ili liweze kumdhuru kama anavyosema katika jigambo lenyewe; **Ewe mtambaa chini,; … Haya nawende, nakutuma.; Enda ukatumbukize ukucha wako; Wako wa chuma ubavuni mwake,; Ukamfutue na kumfumua matumbo yake; Ukamzingire na kumzingara figo zake; Umkamue anye na kujinyea; Umuminye akojoe na kujikojolea (***Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 24)***.** Maneno anayoyatumia Chidama katika majigambo yamerudiwarudiwa kama inavyoonyeshwa katika dondoo la hapa juu. Mtindo wa kurudiarudia maneno ni kwa ajili ya msisitizo wa ukatili wa joka la vichwa saba ambao umefanywa kimakusudi na uliodhamiriwa na mwandishi kudhihirisha ubabe na ukatili wa viongozi. Mwandishi Emmanuel Mbogo ameutumia utanzu huu wa sanaa za maonyesho ya Kiafrika kuendeleza dhamira yake ya kuweka wazi ukatili wa matajiri na viongozi wa nchi za Kiafrika dhidi ya wananchi wa kawaida wanaowaongoza licha ya kupewa mamlaka na wananchi haohao.

Majigambo huwa ni usemi wa kishairi ambao huwa na mishororo mifupimifupi yenye mapigo ya kishairi na yenye ujumbe uliofumbwa. Chidama katika majigambo yake anasema; **… Joka la vichwa saba; Lakini ni joka moja tu; Moja katika saba na saba katika moja; Ewe mtambaa chini; Mwenye meno ya sumu**. Maneno haya katika majigambo ya Chidama yamesemwa kwa lugha ya kishairi yenye mvuto na inayonata. Hata hivyo, mtunzi hajazingatia matumizi ya sheria za utunzi wa mashairi ya kimapokeo. Majigambo ya Chidama yaliyoko katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ni ya aina ya shairi huru ambalo halifuati sheria za kimapokeo katika utunzi wake.

Ughani au ukariri katika utanzu wa majigambo hudhihirisha msimulizi mwenye sifa za umahiri wa utambaji anayechochea hisia za msikilizaji, huamsha ari ya msikilizaji na mtazamaji wa mchezo wa kuigiza ili kuleta athari ambayo inakusudiwa na mtunzi. Kupitia kwa ufasaha na ufundi wa maneno anayoyakariri mhusika Chidama, Msanii Emmanuel Mbogo anafanikiwa kudhihirisha uovu na ukatili wa mhusika huyo Chidama. Mbali na kumwezesha mtunzi kujenga na kuendeleza umbo la tamthilia yake, utanzu wa majigambo ulimwezesha kufaulisha malengo ya utunzi wake katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi.*

Matendo ya ukatili ya Chidama kwa Ng'wanamalundi yalimfanya Ng'wanamalundi kujigamba pia na kutenda mambo fulani katika hali ya kujikinga na madhara ya uchawi wa huyo hasimu yake kwa njia ya kumrudishia uovu wake. Mbinu ya mtunzi Emmanuel Mbogo kujibu majigambo ya Chidama kupitia kwa majigambo ya mhusika mwingine ambaye ni Ng'wanamalundi Kimwingilianomatini kunayafanya majigambo haya mawili kuwa ya aina ya malumbano. Katika majibizano yake ya majigambo kwa Chidama, Ng'wanamalundi analumbana na Chidama kwa kumrudishia ifuatavyo:

NG'WANAMALUNDI: (…*anampiga yule nyoka kwa mgwishu wake. Nyoka anatulia. Sasa anamkamata na kuanza kunuiza na kusema naye*)

**Najua aliyekutuma**
**Lakini huyo si mlume sawasawa**
**Wewe ni tonga, hujawa tui bado.**
**Hu'chochote bali garasa,**
**Shushu la nyoka mgonjwa,**
**(*anamtemea mate*)**
Lakini nakutambua wewe nani.
Najua ndiye wewe yule unukae damu ya maskini.
Huwezi kunizuga na mavazi uliyovaa.
Kwani sabuni na manukato
Havitoshi kutoharisha nuksi
Iliyoko ndani ya kichwa,
Roho, na matendo yako.
Kwani nani hajui kuwa
Wewe ni mchawi wa *msukule*?
Nani hajui kuwa wewe hupika

Vitumbua kwa maji ya
Kuoshea wafu ili vitoke?
Nani hajui kuwa wewe
Hutumia kiganja cha mtoto
Aliyekufa kuchotea na
Kuuzia vitumbua hivyo?
Nani hajui kuwa:
Wewe hutumia vipara
Vya Binadamu kuvulia
Matanga kwa matanga
Ya samaki …
Ukanadi, ukachuma ndarahimu?
(*kimya*)
Lakini saa wakati umefika wa kucheza Ngoma ya Ng'wanamalundi!
*(Ngoma ya Ng'wanamalundi - kr 48 – 49)*

Kwa mtazamo wa nje, tungo za hapa juu **Majigambo ya Chidama na Majigambo ya Ng'wanamalundi** *Ngoma ya Ng'wanamalundi* – uk 24 na kr 48 - 49) zinadhihirisha muundo wa ushairi wa aina ya malumbano. Kawaida katika mashairi ya malumbano, mtunzi mmoja huchangamki a utunzi wa kishairi wa mwenzake baada ya muda kwa kujibu swali alilouliza mshairi wa kwanza au kwa kufafanua masuala fulani ambayo mshairi wa kwanza aliyaibua kwa njia ya kuyahakiki. Mashairi ya malumbano yanaweza kuchapishwa katika magazeti au katika vitabu mradi kuna majibizano ya aina fulani baina ya washairi wawili au zaidi kuhusu mada moja inayowaathiri. Mwandishi Emmanuel Mbogo amechota bahari hii ya ushairi na kuitumia katika utunzi wa tamthilia yake. Kwa kumfanya mhusika Ng'wanamalundi kumjibu mshairi Chidama kishairi katika tamthilia yake baada ya muda, kunafanya majibizano na ushairi huu kuwa wa aina ya malumbano.

Tungo za kishairi za madondoo ya hapa juu vilevile ni za aina ya majigambo. Majigambo kama ilivyoelezwa kwingine ni utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi ambao hujumuisha maigizo na ughani wa kujisifu kwa mhusika fanani mwenyewe anayejigamba kuhusu matendo yake fulani ya kishujaa au kuhusu mafanikio yake katika maisha. Wote Chidama na Ng'wanamalundi wanajigamba kwa mafanikio ya

matendo yao wenyewe. Chidama anajigamba kwa ubahili na uovu wake wa kuwaua na kuwafufua watu aliowaroga na kuwafanya watumwa vizuu wake wa kumtumikia katika shamba lake bila malipo yoyote na bila wao kulalamika. Ng'wanamalundi kwa upande mwingine anaonyesha ubingwa wake wa kumshinda mganga mwovu Chidama kwa jinsi anavyomdunisha na kumdhihaki jatu aliyetumwa na Chidama – "**Najua aliyekutuma, Lakini huyo si mlume sawasawa, Wewe ni tonga, hujawa tui bado. Hu'chochote bali garasa, Shushu la nyoka mgonjwa, (*anamtemea mate)*." Ng'wanamalundi hajigambi kuhusu uwezo wake wa kuzuia maovu ya Chidama, maneno na vitendo vyake vinadhihirisha ubingwa wake ambao angekuwa anajigambia kwao juu ya Chidama. Majigambo ya wahusika hawa wawili yanamwezesha mtunzi kujenga mgogoro wa tamthilia yake na wakati huohuo kuimarisha dhamira ya utunzi wake.

## 5.4 Sanaa za Maonyesho katika *Mashetani Wamerudi* - Said A. Mohamed (2016)

Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* iliyoandikwa na Said A. Mohammed ni mfwatilizo wa kazi ya kihistoria ya Ebrahim Hussein katika tamthilia yake ya *Mashetani* (1972). Hussein katika tamthilia yake ya *Mashetani* alijikita katika nadharia ya Mpito wa Ukoloni kuelekea ukoloni mamboleo ambapo wakati huo kihistoria aliakisi mwelekeo wa nchi za Afrika kuchukua mifumo mibaya ya kiuchumi, kijamii, kisiasa, kielimu, kisayansi, kiteknolojia na kitamaduni. Wakati huo ulikuwa wakati wa kuondoshwa "ukoloni halisia na kuelekea uhuru wa bendera" kama asemavyo Said A. Mohamed katika dibaji ya tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* (k.h.j.). Kwa maoni yake Said A. Mohamed, Hussein amechukua muda mrefu kuandika tamthilia nyingine ambayo inafumbata hali mpya ya usasa ya utandawazi wa siasa, uchumi, usafiri, biashara, uhaulishaji wa fedha wa kasi, uanahabari ugenini, vita, migongano ya kidini, ukimbizi na uhamiaji wa makundi ya watu kwenda nchi za ng'ambo tangu aandike tamthilia

yake ya *Mashetani* karibu miongo mitano iliyopita. Said A. Mohamed alisukumwa kuandika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* baada ya kuona kwamba hakuna tamthilia inayoakisi masuala ya utandawazi kwa namna alivyoyashughulikia Ebrahim Hussein katika tamthilia ya *Mashetani*. Kwa maoni yake, huenda tamthilia ya aina hiyo, ikapitwa na wakati kwani hakuna tamthilia iliyondikwa "kufikia sasa" kufuatiliza tamthilia ya *Mashetani* wakati Ebrahim Hussein haandiki tena. Kwa mujibu wa misingi hii, Said A. Mohamed akachukua hatua ya kuandika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Kwa maneno yake mwenyewe, Mohamed anasema:

> "*Mashetani Wamerudi* imelazimika kushikamana na tamthilia asili ya *Mashetani* ili iweze kwenda katika usasa na upya kwa kushonana katika wakati uliopita na wakati wa sasa" (*Mashetani Wamerudi* - uk vi).

Akimtabarukia Ebrahim Hussein tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi*, Said A. Mohamed anamshawishi mtunzi huyu wa zamani kuinuka na kurudi tena katika ulingo wa utunzi wa kazi za sanaa ili kukichachawisha, kukiongoza na kukionyesha kizazi kipya njia ya utunzi wa tamthilia kwa mawimbi ya tajriba yake pana ili kuchukua hatamu za utunzi. Said A. Mohamed alimunuizia Ebrahim Hussein maneno ya busara yafuatayo yaweze kumwaamusha;

> *Ewe Profesa Ebrahim Hussein*
> *Mpuliza upepo na mawimbi*
> *Inuka! Simama ewe gwiji!*
> *Simama utuonyooshee mkono*
> *Kuzifinyanga dhamira za dhati*
> *Zitazotetea wananchi (Mashetani Wamerudi - uk vii)*

Tamthilia ya *Mashetani* ambayo inafuatilizwa na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, inaakisi mitazamo ya nchi za Afrika Mashariki punde tu baada ya kujinyakulia uhuru ambao ilizitumbukiza nchi hizi na zingine za Afrika kwa jumla katika ukoloni mamboleo. Mtunzi alikerwa na mfumo wa kisiasa uliotumiwa kuonyesha jinsi Waafrika walivyogawanyika kimatabaka na kuendeleza siasa za kukemea ukoloni mamboleo kwa mdomo tu, huku wakoloni wakiendeleza faida zao za kukamata

mikononi mwao kila sekta za nchi za Afrika kwa njia zisizo wazi, yaani, “remote controlled” kwa lugha ya utandawazi na usasa kama asemavyo Said A. Mohamed. Kama anavyoonyesha katika dondoo la hapo juu, tangu kuandika tamthilia ya *Mashetani*, Hussein mpaka sasa hajaandika au hajatoa tamthilia nyingine ya baadaye inayogonga ndipo kwenye usasa mpya wa utandawazi. Tanzu za jadi za sanaa za maonyesho ya Kiafrika zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* zinabainishwa na kufafanuliwa hapa chini.

### 5.4.1 Wimbo katika Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*

Mwandishi Said A. Mohammed ameanza utunzi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kwa kujumuisha tanzu mbalimbali za nyimbo na ngoma ambazo zote zinawasilishwa na mhusika ambaye ni mfano wa fanani mahiri mcheza ngoma, na mwimbaji na anayepatikana katika sanaa za maonyesho ya jadi. Nyimbo zilizowasilishwa katika tamthilia yenyewe ni za aina ya mashairi huru ambayo licha ya kutofuata sheria za utunzi wa mashairi ya kimapokeo, zimeandikwa kwa lugha ya kishairi. Ushairi wenyewe ni wa mishororo kumi na minne unaojulikana kama “sonnet” kwa lugha ya Kiingereza. Indangasi (1991) katika *Notes on William Shakespeare’s Romeo and Juliet* anaeleza kuwa “sonnet” ni aina ya shairi la mishororo kumi na minne, lenye wizani unaoimbika vizuri kwa mfumo wa *abcb cbcd, efef gg* na ambalo lina sauti ambazo zinafanana na kufahamika mwishoni mwa kila mshororo. Katika enzi ya akina Aristotle kama Wamitila (2002) anavyoeleza, maigizo yote ya wakati huo yaliimbwa. Nyimbo pia zilitumiwa kutanguliza maonyesho ya maigizo mbalimbali. Said A. Mohammed vilevile ametumia mbinu hii ya utunzi wa tamthilia ya Kimagharibi kutunga tamthilia yake kwa kutanguliza kila onyesho la mchezo huo kwa wimbo.

Wimbo wa kwanza - Mchezo mpya: “Roho Haifi” (*Mashetani Wamerudi* - uk 1) katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni shairi huru lenye mishororo kumi na minne na linachukuana vizuri kwa sifa na mashairi ya aina ya “sonnet” yaliyotungwa na mtunzi mashuhuri wa michezo ya kuigiza kwa lugha ya Kiingereza kwa jina William Shakespeare. Said A. Mohammed amelitunga shairi hilo kama lilivyo hapa chini:

> Mwanambele: (*Anaimba. Anapiga ngoma. Anacheza karibu na hadhira!*)
> Walitumia na wanatumia ndimi,
> Ndimi za uwongo,
> Ndimi zilizoshikamana na lugha yao’ sisi tunatumia lugha zetu,
> Na wengine wanatumia Krioli na Pijini,
> Kuwa lugha zao – Sawa kabisa!
> Lugha hizo huianisha simulizi za historia!
> Historia ya lugha zetu,
> Lugha kama Kiswahili,
> Na zile zinazoitwa Krioli au Pijini,
> Lugha hizo husimulia ukoloni,
> Na baada-ya-ukoloni,
> Yenye ladha ya mapigo ya vita,
> Ukoloni na ukoloni-mamboleo!
> (*Mashetani Wamerudi - uk 1*)

Wimbo wa *Mchezo mpya: Roho Haifi* uliodondolewa hapa juu ni aina ya shairi huru ambalo halifuati sheria za utunzi wa mashairi ya kimapokeo. Ushairi simulizi ni utanzu unaojumuisha tungo zote zenye mapigo ya kimuziki. Mawazo, hisia na hoja katika utanzu huu huwasilishwa kwa njia ya mdomo kwa kutumia lugha ya mkato yenye mpangilio maalumu wa maneno katika mishororo. Ushairi huru kama ushairi wa kimapokeo huimbwa, hughaniwa au hukaririwa. Kama inavyoonyeshwa katika maelezo ya jukwaa, fanani Mwanambele anaimba, anapiga ngoma na anacheza karibu na hadhira. Hizi ni sifa muhimu za uwasilishaji wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi. Mwandishi amemtumia mhusika wake Mwanambele ili kutanguliza suala la

kihistoria analotaka kulishughulikia ambalo ni ukoloni na ukoloni mamboleo unaoziathiri nchi za Kiafrika.

Mwandishi anatumia jumla ya nyimbo kumi na mbili (12) zinazoimbwa na mhusika wake Mwanambele ambaye ni mfano wa fanani mtendaji katika sanaa za maonyesho ya jadi mwanzoni mwa maonyesho yote ya baadaye ya tamthilia yake ili kutanguliza mawazo yake katika kila onyesho. Nyimbo hizi kama Brecht (1948) anavyoeleza katika utangulizi wa tamthilia yake ya *The Caucasian Chalk Circle*, zinamwezesha mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kutanguliza kwa mdokezo na kuwasilisha mawazo yake katika hali halisi hata kabla mchezo wenyewe haujaanza. Nyimbo kumi na mbili zinazotanguliza maonyesho ya baadaye katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ambazo ni pamoja na zinazofuata hapa chini, zinatumiwa na mtunzi kuakisi hali halisi ya matatizo ya nchi za bara la Afrika na ulimwengu wa tatu kwa jumla:

**Jedwali 5.4.1: Nyimbo/Mashairi katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi***

| | Kichwa cha Wimbo/Shairi | Aina ya Wimbo/ Shairi |
|---|---|---|
| i) | Mchezo Mpya: "Roho Haifi" – Sehemu ya kwanza Onyesho la 1 – uk 1 | Shairi huru la aina ya sonnet linazoeleza historia ya lugha zinazotumiwa kama Kiswahili, Krioli na Pijini barani Afrika na athari yao katika kusababisha mfumo wa utawala wa ukoloni mamboleo ulioko katika nchi za Afrika. |
| ii) | Wimbo wa ngoma – Onyesho la 2 uk 10 | Wimbo unaoimbwa na fanani kwa jina Mwanambele unaoeleza sura mpya mbalimbali za ukoloni mamboleo. |
| iii) | Mazingaombwe: Vuta nikuvute – Onyesho la 3 uk 15 | Shairi huru linaloeleza kwamba ukoloni mamboleo umerudi ukiwa na sura mpya. |
| iv) | Ya jana si ya leo – Sehemu ya Pili: Onyesho 1 uk 22 | Shairi huru linaloeleza kuwa mazungumzo kuhusu ukoloni mamboleo bado yako na kuomba kila mtu achangie ili kukana ubwana wa wazungu na madai yao kuwa Waafrika ni mabwege. |
| v) | Kipimo cha usawa: Wakubwa na wadogo … Sehemu ya Pili: Onyesho 2 uk 28 | Shairi huru linalohimiza watu wa nchi za bara mbalimbali kama Waasia, Wakarebiani na Waamerika ya Kusini na wafuasi wa wanaharakati wa vita vya uhuru wa kale kama Mahatima Ghandi, Patrice Lumumba na Amilear Cabral waamke wapiganie uzalendo, uhuru na utaifa wao. |
| vi) | Mpandangazi na Mshuka ngazi … - Sehemu ya Pili: Onyesho 3 uk 39 | Wimbo unaozungumzia sheria walizoziwacha wakoloni zinazowanyanyasa Waafrika katika ugavi wa mali na kandarasi. |
| vii) | Vijana wanachachamaa - Sehemu ya Tatu : Onyesho 1 uk 46 | Wimbo wa kejeli na kucheza ngoma unaowachachawisha vijana kusimama imara kuupiga vita ukandamizaji mambo maovu yanayohusiana na ukoloni mamboleo. |
| viii) | Watu na hoja! - Sehemu ya Tatu: Onyesho 2 uk 54 | Wimbo wa urazini unaoimbwa na kucheza ngoma na kueleza kuhusu ushirika kati ya viongozi Waafrika na Wazungu wenye ukoloni mamboleo kuwafanyia njama watawaliwa wao kukubali kupewa kidogo. |
| ix) | Umoja - Sehemu ya Nne: Onyesho la 1 uk 63 | Wimbo wa umoja unaotoa wito kwa Waafrika kushikana mikono na kuungana pamoja ili kuvikabili vishindo vinavyokuja. |
| x) | Mchezo wa ukweli - Sehemu ya Nne: Onyesho la 2 uk 69 | Wimbo wa kutia moyo kwamba umoja umefika wa kuwachochea Waafrika kutenda wala si kusema maneno matupu kwa ukoloni mamboleo hauwalilizi tena. |
| xi) | Barabarani … Sehemu ya Nne: Onyesho 3 uk 74 | Wimbo wa barabarani ni mchezo wa usanii unaowapongeza Waafrika kwa kuchukua njia nzuri ya kuwa huru na kuwapa wosia waende kote nchini kwa ukakamavu na kwa amani. |
| xii) | Mtu hafi, huzaliwa tena … - Sehemu ya Nne: Onyesho la 4 uk 77 | Wimbo wa mwisho na ngoma ya usanii inayowahimiza watu wa ulimwengu wa tatu washikane mikono na kuungana kama kitu kimoja ili kupigania uhuru wao na kwamba watafanikiwa katika azimio lao. |

**Chanzo: Data kutoka kwa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi***

Jedwali 5.4.1 linaorodhesha jumla ya nyimbo zilizotumika katika utunzi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi.* Mbali na kufuata mbinu za ki-Aristotle katika kutunga tamthilia yake, mtunzi vilevile ameingiza tanzu za sanaa za maonyesho ya kale katika utunzi wake. Mwanambele ni mfano wa mhusika mtendaji anayepatikana tu katika sanaa za maonyesho ya jadi. Katika jumla ya nyimbo zote alizoziwasilisha katika tamthilia yake, mtunzi amezichanganya kimwingilianomatini na mbinu za uimbaji na uchezaji wa ngoma katika utunzi wake pamoja na mbinu ya utambaji katika mbinu ya uandishi wa kidrama ya Kimagharibi inayomwezesha kuibuka na tamthilia yenye mvuto wa kisanaa.

### 5.4.2 Usanii wa Fanani katika Sanaa za Maonyesho

Mhusika kwa jina Mwanambele anayetumiwa na mtunzi katika kuwasilisha nyimbo mwanzoni mwa kila sura ya tamthilia yake ni mfano mzuri wa fanani wanaopatikana katika tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho ya jadi. Kwa kumbuni mhusika Mwanambele kwa jinsi alivyofanya, mtunzi amechota ufundi huu wa kisanaa kutoka kwa sanaa za maonyesho ya jadi yaliyoasisiwa katika tamaduni za Kiafrika na kuutumia katika utunzi wa tamthilia yake. Kwa mujibu wa Kubo na wenzake (2013), fanani ni mtu yeyote anayewasilisha kipera chochote cha sanaa za maonyesho na fasihi kwa jumla. Katika usimulizi na utambaji, fanani huwasilisha masimulizi yake kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kuteka nadhari ya hadhira. Fanani huweza kusimulia, kughani, kuimba, kuchezesha viungo vya mwili na mabega, kuigiza, kukonyeza na kufanya ishara za mwili na nyuso na kucheza ala za muziki. Katika maelezo yake ya jukwaa, Said A. Mohamed anatujuza hivi:

> Mwanambele: *(anaimba. Anapiga ngoma. Anacheza karibu na hadhira. Anaimba)*
>
> *(Mashetani Wamerudi – u.k1)*

Mhusika Mwanambele ni mfano wa fanani ambaye ni kiungo muhimu katika uwasilishaji wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi. Kwa kawaida katika uimbaji, fanani anaweza kuimba wimbo mzima peke yake na wakati mwingine anaweza kuimba kitangulizi au kuimba mstari mmoja na waimbaji wengine katika kikundi chake wakaitikia. Tunaambiwa kwamba, "Mwanambele anaimba huku akicheza ngoma," kumaanisha kwamba fanani huyu ana uwezo wa kuimba huku akicheza ala ya muziki na kuiandamanisha na kuchezesha viungo vya mwili na kuucheza muziki wenyewe.

Mhusika Mwanambele vilevile anadhihirisha sifa za fanani wa sanaa za maonyesho ya jadi kwa kushirikisha hadhira katika uwasilishaji wake wa wimbo. Katika nyimbo zote zinazoanzisha maonyesho yote ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, fanani Mwanambele anaipigisha hadhira makofi, kuichezesha, kuiimbisha na kuiuliza maswali. Mtunzi Said A. Mohamed katika ukurasa wa kwanza wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, anaeleza hivi katika maelezo yake ya jukwaa:

> Mwanambele: Pigeni makofi (*anaimbia hadhira. Makofi yanasikika kutoka kwa hadhira. Kisha polepole anatoweka Mwanambele. Halafu kimya. Kimya kirefu kidogo …*) *(Mashetani Wamerudi – uk.1)*

Tofauti na tamthilia ya ki-Aristotle ambapo hadhira huwa tuli, mwandishi Said A. Mohamed anashirikisha mbinu za sanaa za maonyesho ya jadi ya utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wake kwa kumfanya fanani kushirikiana na hadhira kwa kupiga makofi na kucheza ala na ngoma huku akiimba wimbo. Kwa njia hii kama asemavyo King'ei na Kisovi (k.h.j), mtunzi amefanya hadhira kuwa wahusika katika tamthilia yake kupitia kupiga makofi, kuimba na wakati mwingine kujibu maswali yanayoulizwa na fanani.

Uhodari wa uwasilishaji nyimbo na ngoma wa fanani ambao unaihusisha hadhira unatumiwa sambamba kimwingilianomatini na mbinu ya usimulizi. Ingawa fanani anawasilisha mawazo yake kwa kuimba, wimbo wenyewe umesimuliwa. Mawazo yote anayoyakusudia kuyaeleza, mtunzi ameyasimulia katika nafsi ya tatu katika nyimbo zake zote alizoziingiza katika tamthilia yake. Mbinu hii inajitokeza vizuri katika tangazo la Mtu asiyejulikana na asiyeonekana.

> Sauti ya mtu: Hapa na pale. Hapa uwanjani panapo kiti cha siasa. Tumesimama katika kitovu cha siasa ya kisasa. Siasa isiyokwisha. Siasa ya misinga na mabomu. Siasa ya mabomu ya kufa na mabomu ya machozi. Huna ruhusa ya kwenda barabarani kwa amani. Huko utaona na kujitupa kama mzoga au utatiririka machozi. Hapa na pale. Hapa na pale ndani ya dunia ya ukandamizaji. *(kimya. Halafu ...*) **MNASEMAJE HADHIRA? SIKILIZENI MIDOMO INAYOTUAMBIA**. Hata hivyo uwanja lazima uwe wazi. Mazingira yanakubali kwa siri. MNASEMAJE HADHIRA? MNASEMAJE? … (*Mashetani Wamerudi - uk 2) Msisitizo ni wetu.*

Kupitia kwa mhusika Sauti ya Mtu inayosimulia katika dondoo hili, mtunzi anaihusisha hadhira katika utunzi wake kwa kuiuliza hadhira, “**MNASEMAJE HADHIRA? SIKILIZENI MIDOMO INAYOTUAMBIA**. … Si mnajua majumba makubwa ya kifahari yanayojengwa na mtu mmoja? Majumba ya kiasi cha sabini na tatu …”. Mtunzi wa tamthilia anajaribu kuihusisha hadhira sio tu katika usimuliaji wake bali pia kuvuta nadhari ili iweze kuyatafakari anayoyaelezea ambayo kwake ni maajabu kwa mtu mmoja kujenga majumba makubwa ya kiasi hicho. Mtunzi vilevile anaitumia mbinu hii ili kushirikisha hadhira katika kuyajadili masuala ya ukoloni mamboleo, ufisadi, ubadhirifu na anasa ya viongozi yanayozikumba nchi za Afrika baada ya kujinyakulia uhuru wao. Katika tamthilia ya ki-Aristotle kwa kawaida, hadhira huwa tuli na ambayo inashiriki tu kupitia labda kucheka na kushangilia kwa vificho na nderemo kama njia ya kuonyesha furaha au kupitia kwa kutokwa na machozi na kuwa na huzuni ikiwa mchezo wenyewe unazua hisia za mtakazo bali

haishirikishwi katika mchezo kupitia kwa kushiriki katika usimuliaji. Kwa kuitumia mbinu hii jinsi alivyofanya mtunzi, anapata aina ya mvuto na mwitikio kutoka kwa hadhira anaokusudia kuupata.

### 5.4.3 Usimulizi wa Kingomezi

Kwa mujibu wa King'ei na Kisovi (k.h.j), ngomezi ni utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi unaotumia ngoma na ambao hutumiwa katika jamii nyingi za Kiafrika katika miaka ya kale kihistoria kutangaza ujumbe wa aina fulani. Katika jamii hizo, ngoma hupigwa kwa mapigo maalumu yanayowakilisha maneno fulani ambayo yanaeleweka tu na wanajamii wenyewe. Hata hivyo, mgeni kutoka jamii nyingine hawezi kufahamu au kuelewa maana ya mapigo hayo ambayo hufanywa kwa njia ya kuweka siri. Ngomezi ni utanzu uliotumiwa katika jamii za Kiafrika ili kupasha ujumbe kwa jamii kuhusu uvamizi wa adui, wizi wa mifugo, kuwaalika watu kuja kwa mikutano ya viongozi, kupiga marufuku au kufungua madhabahu ya kufanyia makafara miongoni mwa shughuli zingine za kijamii. Kwa hivyo, wakati mwingine mawasiliano ya aina hii yalihitaji usiri mwingi ili ujumbe usivuje kwenda jamii zingine.

Wakati mwingine utanzu wa ngomezi huhusisha uchezaji wa viungo vya mwili kama kupinyanga mabega, kuchezesha viuno kuambatana na mapigo ya ngoma iliyotumiwa kutuma ujumbe. Vijumbe waliotumwa kupeleka ujumbe kwa umma ndio tena walikuwa fanani waliopiga ngoma na kucheza wakituma ujumbe. Vijumbe ni watu waliomtumikia mtawala wa kikabila au jamii ndogo iliyokuwa na mpangilio wa utawala. Ujumbe uliopashwa na ngomezi ulikuwa wa dharura na ulihitaji kuchangamkiwa na umma kwa dharura.

Matumizi ya utanzu wa ngomezi yamebadilishwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* pale mtunzi anapotumia tangazo badala ya kupiga ngoma yenyewe kupitia kwa "sauti ya mtu asiyejulikana na asiyeonekana" katika ukurasa wa pili. Mtunzi anaeleza kwamba tangazo linafanywa na mtu asiyejulikana na asiyeonekana. Kama ishara ya mabadiliko ya kiteknolojia na wakati, mtunzi anatumia sauti ya mtu asiyeonekana wala kujulikana kana kwamba inatoka kwa redio ila mfumo ni wa kingomezi. Matangazo yanayofanywa kutoka mbali husababishwa na maendeleo ya kiteknolojia ambayo huendeleza utandawazi. Televisheni, redio, magazeti na mtandao ni miongoni mwa njia nyingine za kiteknolojia za kisasa zinazotumika katika kuwasilisha ujumbe. Kupitia kwa tangazo hili, mtunzi anakusudia kupitisha ujumbe wake wa aina fulani. Kihistoria katika tamaduni za Kiafrika za jadi, matangazo yalifanywa kupitia kwa tanzu za ngomezi. Ngoma ingepigwa ili kuwasilisha ujumbe wa hatari, uvamizi, tanzia ya mtu mashuhuri, kuanza au kukamilika kwa shughuli za kijamii miongoni mwa matangazo mengine muhimu ya kijamii. Sauti ya mtu asiyejulikana na asiyeonekana (*Mashetani Wamerudi* uk 2) inatangaza kauli ya mtunzi kwa hadhira (umma) kupitia mbinu ifuatayo:

> (*Mara sauti ya mtu asiyejulikana na asiyeonekana inasikika. Inatoka mbali. Inatangaza kauli ya umma*)
>
> Sauti ya mtu: …
>
> > *(kimya. Halafu …*) mnasemaje hadhira? Sikilizeni midomo inayotuambia. Hata hivyo uwanja lazima uwe wazi. Mazingira yanakubali kwa siri.
> >
> > Mnasemaje hadhira? Mnasemaje? Si mnajua majumba makubwa ya kifahari yanayojengwa na mtu mmoja? Majumba ya kiasi cha sabini na tatu. Majumba makubwa aliyoyajenga mtu mmoja. Kisha

> tazameni kibanda kile kidogo. Kimesimama tisti. Ndani atatoka mtetezi. Anakuja Profesa Hafi-Leo-Wala-Kesho mtetezi. Polepole ataingia uwanjani – uwanja wa utandawazi. Katika ya uwanja, karibu na kibanda, lipo shina la mbuyu. Linaanza kutoa chipukizi. Zinazoota chipukizi. Miaka mingi imepita. Kumbukeni *U-colony!* Ambao upo mpaka leo. Ukoloni! Au kifungo cha maisha … (*sauti inacheka kwa ufupi. Halafu sauti inakuwa kali. Kisha kimya. Baadaye inaendelea sauti*). Sikilizeni sana. Shina la mbuyu lilikatwa mapema baada ya ukoloni, tena hapohapo uwanjani. Nguvu zetu zilipungua, lakini sasa zinaanza kufufuka! (*kimya. Sauti imefifia na kupotea*) – (*Mashetani Wamerudi – uk 2)*

Tangazo la hapo juu kupitia kwa mhusika Sauti ya Mtu ni mbinu ya kisasa ya kufanya matangazo kupitia kwa magazeti, redio, runinga, mtandao, simu, miongoni mwa njia za kisasa za kurushia matangazo. Kama kawaida, matangazo hufikia umma bila umma yenyewe kuona matangazo hayo yanatoka wapi. Ikilinganishwa na mbinu asilia za Kiafrika za ngomezi za kupitisha matangazo kwa jamii, tangazo hili la Sauti ya Mtu asiyejulikana na asiyeonekana ni mabadiliko yaliyofanywa na mtunzi kimakusudi kama mbinu za kupitisha ujumbe kwa umma. Tangazo hili linafanana na linatumia mbinu za upitishaji ujumbe zinazopatikana katika utanzu wa ngomezi wa sanaa za maonyesho.

### 5.4.4 Semi kama Mbinu ya Sanaa za Maonyesho

Mtunzi wa *Mashetani Wamerudi* ametumia semi za aina mbalimbali katika kubuni na kuimarisha muundo na maudhui ya tamthilia yake. Baadhi ya semi alizozitumia ni mafumbo, methali, semi na nahau kama zinavyoelezwa hapa chini:

#### 5.4.4.1 Mafumbo

Mafumbo ni utanzu mmojawapo wa tanzu za sanaa za maonyesho zilizotumiwa na mtunzi katika kuendeleza umbo la tamthilia yake. Mtunzi vilevile ametumia utanzu wa mafumbo ili kujenga maudhui katika tamthilia yake. Moturi (2006) anaeleza

mafumbo kuwa maelezo yaliyoficha maana ambayo mara nyingine hutumika kama chemsha bongo ya kufikirisha wanaofumbiwa. Mafumbo husheheni maelezo ya kina yanayoficha kitu kilichofumbwa. Mafumbo ni utanzu wa sanaa za maonyesho ambao huhusisha mtendaji na hadhira tendaji. Mafumbo hujumuisha utendaji wa fanani mbele ya hadhira tendaji inayoshiriki katika kufikiria kwa dhati na kwa haraka ili kutoa majibu yanayohitajika. Mhusika Kijana 1 katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* anapomuuliza Prof. ni kwa nini ni hatari kumfukuza, kumkamata au kumkaribia jogoo anayewika nyuma ya kibanda, Prof. anamweleza hivi kimafumbo:

> Prof.: **Kwa sababu Waswahili wameimba. (*Profesa anaimba kwa usanii*)**
>
> **Msegeju ana ng'ombe,**
> **Nami nina ng'ombe wangu**
> **Kanambia nichanganye**
> **Sebu nakwenda zangu**
> (*kimya tena, kitambo cha kimya*)
>
> Kijana 1: **Sikufahamu Prof. na wimbo wako.**
>
> Prof.: Huwezi kunifahamu kwa dakika chache hizi. Utanifahamu baadaye kijana.
>
> Kijana 1: (*Anaondosha mikono kichwani mwake. Ananyanyua kichwa na kumtazama Prof. uso kwa macho*) kwa nini maprofesa husema kwa mafumbo? (*Mashetani Wamerudi – uk 13)*

Wimbo wa mhusika Prof. wa dondoo tulilolinukuu hapa juu ni mfano wa shairi simulizi unaoimbwa unyagoni na ambao tena ni fumbo. Ushairi huu simulizi unamdhihirisha msimulizi mwenye sifa za umahiri wa utongoaji wa kimafumbo na utendaji, anayechochea hisia za msikilizaji. Prof. anaimba hivi; **Kwa sababu Waswahili wameimba. (*Profesa anaimba kwa usanii*); Msegeju ana ng'ombe; Nami nina ng'ombe wangu; Kanambia nichanganye; Sebu nakwenda zangu.** Maneno yaliyobuniwa katika wimbo na mhusika Prof. yameteuliwa kimakusudi ili kuleta athari ya kusisimua na kufikirisha aliyoitarajia Said A. Mohamed. Kwa sababu ya ufundi wa uimbaji na utendaji unaodhihirishwa na Prof. katika uwasilishaji wa kuchochea hisia, kuamsha ari, kusisimua na kuzindua, wimbo huu unakuwa utanzu

tendaji wa sanaa za maonyesho ya jadi wa shairi simulizi. Ufundi wa fanani Prof. wa kuwasilisha ushairi huu simulizi katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* unamwezesha mtunzi Said A. Mohamed kufaulisha dhamira ya utunzi wa tamthilia yake.

Wimbo wa mhusika Prof. hapa juu vilevile ni fumbo katika wimbo wa unyago ambao ni utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika. Mtunzi ametumia mbinu ya Mwingilianomatini kulibadilisha fumbo lake kuwa wimbo, au kwa maneno mengine utanzu wa wimbo kuwa fumbo. Kwa maneno ya kawaida, wimbo unaeleza jinsi mwenzake Msegeju ambaye ana ng'ombe kama yeye anamhadaa wachanganye ng'ombe wao. Mwenyewe mhusika Prof., anadinda kuchanganya ng'ombe wake na wa Msegeju na kutoka kwenda zake kwa sababu anakataa kuhadaiwa kuchanganya ng'ombe wake na ng'ombe wa aina ya sebu. Wimbo unatongoa hivi; **Msegeju ana ng'ombe; Nami nina ng'ombe wangu; Kanambia nichanganye; Sebu nakwenda zangu.** Maneno ya wimbo huu ni fumbo ambalo mbali na kusisimua kwa mvuto wa uteuzi wa maneno yake ya kishairi unaifikirisha hadhira ili kupata jawabu mwafaka kwa fumbo hilo.

Prof. anahusisha utendaji katika utunzi wa fumbo lake na anatumia lugha ya kimafumbo katika utunzi wake ambao unamfanya mhusika Kijana 1 asipate maana ya fumbo analolisema kwa mara moja. Prof. vilevile anaimba kwa usanii mkubwa kama mbinu ya utendaji wa sanaa za maonyesho na uwasilishaji wa fumbo lake. Katika tamati ya wimbo-fumbo lake, Prof. anakimya kwa mtuo kabla ya kuhitaji jibu kudhihirisha usanii na uwezo wake wa utendaji ili kufanya hadhira kufikiria na kuwezesha ujumbe kutua na kueleweka vizuri. Hata hivyo, mhusika Kijana 1 ambaye ndiye hadhira ya mhusika Prof. anayefumba fumbo, hana jibu kwa fumbo hilo kama

inavyodhihirika katika dondoo la hapo juu; "**Sikufahamu Prof. na wimbo wako."** Kama ilivyo kanuni ya kutega vitendawili na kufumba mafumbo katika itikadi za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika, Kijana 1 anamfahamisha mfumbaji wake ambaye ni mhusika Prof. kuwa hafahamu jibu la fumbo hilo.

Utegaji wa vitendawili na kufumba mafumbo kwa kawaida huhitaji jibu papo kwa hapo, hadhira ikishindwa kutoa jibu kwa fumbo walilofumbiwa, hadhira hiyo inalazimika kutoa zawadi kwa kumtajia mji mfumbaji au mtegaji ikiwa ni kitendawili ili kumliwaza kwa ubingwa wake wa kutega vitendawili au kufumba mafumbo na aweze kulifumbua mwenyewe. Katika fumbo hili, baada ya kushindwa kufumbua fumbo, hadhira ikiwakilishwa na Kijana 1 haitoi mji wala mfumbaji (fanani) ambaye ni mhusika Prof. hatoi jibu mara moja bali anamweleza kwamba atafahamu jibu baada ya muda wala si baada ya dakika chache. Katika tamaduni za sanaa za maonyesho, mafumbo hubuniwa papo kwa papo na mfumbaji ambaye huhitaji majibu mara moja. Majibu ya mafumbo yanaweza kuwa maelezo marefu, maelezo mafupi au hata neno moja tu. King'ei na Kisoi (k.h.j) wanaongezea kuwa hiki kipera cha semi hufumba swali ambalo humhitaji anayelifumbua kufikiria kwanza kabla ya kulijibu. Kwa mhusika Prof. kueleza kuwa hadhira itabaini maana ya fumbo baadaye, mtunzi anatoa muda kwa hadhira kuvuta tafakuri ili kufikiria kwa tabasuri na kupata jawabu mwafaka kwa fumbo hilo. Ucheleweshaji wa utoaji wa jibu kwa fumbo la Prof. ni mbinu ya utunzi wa kimakusudi inayomwezesha mtunzi tamthilia, Said A. Mohamed, kurefusha kisa chake na kumwezesha kuichanganya mbinu hiyo ya fumbo na zingine ili kuipa tamthilia yake umbo analokusudia pamoja na kufanikisha upashaji wa ujumbe wake. Mafumbo hutumiwa kuelimisha na kukuza uwezo wa kutafakari na kufikiria uamuzi wa mambo mazito katika jamii.

#### 5.4.4.2 Lugha ya Kimafumbo na Tamathali za Semi katika *Mashetani Wamerudi*

Mtunzi Said A. Mohamed vilevile ametumia vitanzu vya tashbihi, stiari na jazanda katika utunzi na uimarishaji wa muundo na ujumi katika tamthilia yake. Tamathali za usemi ni matamko ya kufananisha dhana moja na nyingine tofauti au zinazofanana. Said A. Mohamed kama msanii ametumia tamathali za usemi katika utunzi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ili kumwezesha kupitisha na kusisitiza ujumbe kwa njia yenye mvuto kwa hadhira mbali na kuimarisha umbo la tamthilia yake. Matumizi ya mbinu ya tamathali za usemi hujumuisha tashibiha, stiari, tashihisi, taniaba, taashira, majazi, lakabu, tabaini, tashtiti, chuku, kinaya na dhihaka miongoni mwa mbinu zingine ambazo zimejadiliwa kwingine katika tasnifu hii.

#### 5.4.4.3 Utanzu wa Jazanda

Jazanda ni utumiaji wa maneno kimafumbo ambapo neno moja au zaidi hutumiwa kuwakilisha taswira au maana nyingine. Matumizi ya "jogoo" na "Mashetani" katika utunzi wa Said A. Mohamed ni wa kijazanda. Jazanda ni utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika. Mtunzi ametumia jazanda ya jogoo katika dondoo lifuatalo:

> Kijana 1: *(anashangaa ... Halafu mbio anaondoka kitini kwenda nyuma ya kibanda.* ***Jogoo anaendelea kupaparika na kupiga mashuzi***)
> Prof.: Si jogoo huyo.
> Kijana 1: Enh, si jogoo kumbe? (*Anasema nyuma ya kibanda*)
> Prof.: Si jogoo nakwambia.
> Kijana 1: Nimfukuze? …
> Prof.: Wewe husikii? Nakwambia si jogoo huyo ndio maana hapatikani! (*Bado anahaha*)
> Kijana 1: Kwani nani huyu**, si jogoo tu**? (Anauliza kibabe)
> Prof.: **Shetani huyo**!
> Kijana: Shetani gani?
> Prof.: **Shetani aliyepo ingawa hayupo, yaani hayupo na sasa yupo**. (*Mashetani Wamerudi* - kr 10 – 11)

Kijana anapomuuliza mhusika Prof kama anaweza kumfukuza jogoo na kumshika ili amchinje, Prof anamweleza kwamba, ndege anayepaparika na kupiga mashuzi ni Shetani na kwamba hawezi kumkamata mwenyewe hasa akiwa peke yake. Taashira ya jogoo na Shetani imechotwa kimakusudi na mtunzi kutoka kwa sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika na kuitumia kijazanda katika utunzi wa tamthilia yake. Said A. Mohamed anatumia jazanda ya jogoo na Shetani kurejelea Wazungu na utawala wao wa kikoloni; "**Shetani aliyepo ingawa hayupo, yaani hayupo na sasa yupo" (*Mashetani Wamerudi* -** uk 11). Mhusika Kijana anapomweleza mhusika Prof. anayewawakilisha raia wa nchi za ulimwengu wa tatu kwamba anataka kumshika jogoo huyo, Prof anamtahadharisha kwamba hilo ni tendo la hatari ambalo linaweza kumdhuru kwani hana uwezo wa kumdhibiti mkoloni.

Kupaparika na kupiga mashuzi kwa jogoo ambaye pia mtunzi anamrejelea kwa jina Shetani (mhusika Sheta) ni jazanda ya madhara ambayo nchi za Kimagharibi na sasa za Mashariki kama Uchina na Japan zinazisababishia nchi za Afrika na zingine za ulimwengu wa tatu. Nchi za Magharibi zinazitawala na kuzinyanyasa nchi za Afrika kupitia kwa mbinu za ukoloni mamboleo ambazo nchi zenyewe hazizielewi. Viongozi wa Kiafrika kwa kawaida hawahusishwi katika mikakati ya kuzitawala vyema nchi zao, bali nchiza Kimagharibi hutumia viongozi vibaraka wa Kiafrika wenye tamaa ya uongozi ili kuwasaidia kuingia uongozini. Kupitia kwa njia hiyo, nchi za Kimagharibi zinapata nafasi kuleta ukoloni mamboleo barani Afrika na kuzisababishia nchi za Afrika madhara ya udhalimu wao.

Shetani katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* anamwambia Prof. kwamba Mashetani huwasababishia Waafrika ugonjwa wa kizunguzungu; "**Tena ni wepesi kuwapa watu ugonjwa wa kizunguzungu" – (***Mashetani Wamerudi* - uk 10).

Ugonjwa wa kizunguzungu ni jazanda ya madhara yanayoletwa kwa Mwafrika na Mzungu mkoloni. Mashetani ambao ni Wazungu kutoka nchi za Magharibi husababishia nchi za Afrika madhara yanayowakilishwa kijazanda na jina ugonjwa. Mhusika Shetani anaeleza hivi kuhusu uwezo wao wa kuwasababishia Waafrika madhara:

> **Sheta**: Sisi unajua kwamba tuna mazingaombwe. **Tena ni wepesi kuwapa watu ugonjwa wa kizunguzungu**. Ndio maana mmetupa jina la kizunguzungu. (*Mashetani Wamerudi* – uk 20)

Jina la kimajazi "**Sheta"** au Shetani na "**jogoo"** ni msamiati alioutumia mtunzi kuwakilisha ukoloni mamboleo ambao upo katika jamii za Kiafrika baada ya ukoloni mkongwe kuondoka. Baada ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru, wakoloni walewale waliotoka walirudi katika sura tofauti isiyodhihirika wazi kuja kuendeleza udhalimu wao. Kama asemavyo Said A. Mohamed kupitia kwa mhusika wake kwa jina Prof. mkoloni alitoka baada ya kupigwa vita na Mwafrika lakini amerudi tena Afrika katika sura tofauti ya ukoloni mamboleo. Prof. anaeleza hivi; "**Shetani aliyepo ingawa hayupo, yaani hayupo na sasa yupo,***" (Mashetani Wamerudi – uk 11).* Katika ukurasa wa 5, mhusika Prof. anaeleza hivi kuhusu kurejea kwa wakoloni kwa njia tofauti:

> Prof.: **Tokea Shetani alipojidai anaondoka tukadhani eti hatarudi? Kumbe alituchezea shere kwa mchezo wa maneno.** Ndani ya miaka mingi ya dhuluma tumegundua kile tulichotiwa vichwani mwetu … (*Mashetani Wamerudi – uk 5*)

Kwa njia ya kurejelea utabiri wa Ebrahim Hussein katika kisa cha mchezo wa Shetani na Binadamu katika tamthilia ya *Mashetani,* Said A. Mohamed anafafanua utabiri huo kwa kueleza kwamba mkoloni alituhadaa kwamba ameng'atuka na kuondosha ukoloni kutoka kwa bara la Afrika pale alipokubali kudungwa kisu na Binadamu (Mwafrika) na kuaga dunia ambapo walisherehekea kifo chake kwa dansi ya *waltz*

katika tamthilia ya *Mashetani*. Ukweli ni kwamba mkoloni (Shetani) hakuondoka kutoka kwa bara la Afrika kama ilivyowakilishwa kupitia kwa kifo chake baada ya kuchomwa kisu ubavuni na Binadamu. Mkoloni alijibadilisha kama afanyavyo Shetani na kurudi Afrika ambako anaendeleza unyanyasaji na udhalimu wake kwa njia ya ukoloni mamboleo. Kwa usemi wa kinahau wa mhusika Prof., mkoloni, "**alituchezea shere.**" Mhusika Kijana 1 anasisitiza kurejea kwa wakoloni kwa kuuliza maswali ya balagha kama ifuatavyo; **Sasa wamerudi au siyo? Wako tayari kucheza mchezo mwingine mpya au sivyo? Na sisi tunaukubali mchezo wao mpya**. Said A. Mohamed kupitia kwa mhusika Kijana 1 anaeleza hivi katika dondoo lifuatalo:

> Kijana 1: **Sasa wamerudi au siyo? Wako tayari kucheza mchezo mwingine mpya au sivyo? Na sisi tunaukubali mchezo wao mpya** … (*anasema kwa kejeli huku anakwenda na kurudi pale penye shina la mbuyu butu*) - **(***Mashetani Wamerudi – uk 5)*

Mtunzi Said A. Mohamed anaunganisha mbinu ya jazanda na tanzu nyingine za maswali ya balagha, dhihaka, kejeli na semi kueleza kwamba ukoloni umerudi katika sura mpya ya ukoloni mamboleo. Maswali aliyoyauliza hapa juu yanajumuisha kejeli na dhihaka kusisitiza kwamba Wakoloni wamerudi na wako tayari kucheza mchezo mpya ambao si ule wa zamani wa ukoloni mkongwe bali wa ukoloni mamboleo kama asemavyo mhusika Kijana 1. Uwepo wa wakoloni barani Afrika ni suala ambalo Waafrika wanafaa kulizamia ili kuelewa sura ya uwepo wao. Kwa kutoa kauli yake kwa nguvu kuwa wakoloni wamerudi Afrika, mtunzi anakusudia kuwazindua Waafrika na kuwahamasisha kuhusu hatari inayowakabili ya kunyanyaswa na kudhulumiwa na Wazungu wakoloni ambao wamerudi tena Afrika katika umbo na sura tofauti.

Mohamed vilevile ametumia kijazanda dhana ya mbuyu katika utunzi wa tamthilia yake - S**hina la Mbuyu -** (*Mashetani Wamerudi – uk 7)*. Matumizi ya dhana ya

mbuyu yanazua taswira ya imani za Kiafrika inayojengwa na methali, "kila mbuyu na Shetani wake." Kwa mujibu wa imani za Kiafrika, Mashetani huishi juu ya miti na mibuyu ndiyo masikani mwafaka kwa pepo hao katika mazingira ya Uswahilini. Tayari imeishaelezwa kuwa Shetani ni dhana ya kijazanda iliyotumiwa kisanaa na mtunzi ili kuwakilisha suala la kihistoria la ukoloni mkongwe na viongozi ambao ni vibaraka wao katika nchi za Kiafrika na ulimwengu wa tatu. Said A. Mohamed ametumia dhana ya mbuyu kijazanda kurejelea bara la Afrika ambalo lilitawaliwa na wakoloni na linatawaliwa kiukoloni mamboleo hata sasa katika mfumo nyanyasaji wa utandawazi.

> Prof.: *...((kimya kizito. Mwangaza unawafuata wahusika. Prof. anasimama. Anakwenda kwenye shina la mbuyu. Kijana anamfuata Prof. analikagua shina la mbuyu kila kipande. Kisha anatazama juu mbinguni)*
>
> Kijana 1: Mbona unatazama **shina la mbuyu** na kisha unaelekezaje jicho mbinguni?
>
> Prof.: Shina la mbuyu, shina la mbuyu – **walilibadilisha jiti kubwa lenye virutubishi. Wakalifanya tanda la kulalia na kisha pahala pa kurukia katika maendeleo yao**. (*Mashetani Wamerudi – kr 6 -7- msisitizo ni wetu)*

Shina la mbuyu katika dondoo hili linarejelea nchi za bara la Afrika ambazo kihistoria wakoloni walijinyakulia na kuzitawala kwa nguvu. Wakoloni walinyonya bara la Afrika wakati wa ukoloni na kupeleka kwao maliasili ya bara la Afrika kama malighafi ya kudumisha viwanda na maendeleo yao. Wazungu waliokuwepo Afrika wakati wa ukoloni walilinyanyasa bara hili mpaka likawa jiti tupu lisilokuwa na manufaa kama hapo awali. Kwa kufanya hivi, Afrika ikabadilishwa kuwa msingi wa maendeleo ya nchi za Kimagharibi. Katika kuchora taswira ya unyanyasaji, mwandishi Said A. Mohamed kupitia mhusika Prof. anaeleza hivi; **"walilibadilisha jiti kubwa lenye virutubishi. Wakalifanya tanda la kulalia na kisha pahala pa kurukia katika maendeleo yao."** Wizi wa kihistoria wa wakoloni ndio asili ya

matatizo yanayozikumba nchi za Kiafrika katika wakati wa sasa kama yanavyodhihirishwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

### 5.5 Muhtasari wa Matumizi ya Tanzu za Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Utunzi wa Tamthilia Teule za Kiswahili

Matokeo ya utafiti wetu katika sura hii ya tano yalifafanuliwa kwa mujibu wa lengo letu la kwanza la kupambanua tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika na namna tanzu hizo zilivyotumika katika utunzi wa tamthilia teule za Kiswahili. Iliibuka ya kwamba tanzu nyingi za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika zilitumiwa na watunzi wote teule kwa njia inayofanana au inayokaribia kufanana kusimulia visa mbalimbali vilivyotumiwa kubuni tamthilia. Kuna mfanano wa mbinu za utunzi miongoni mwa watunzi wa tamthilia za *Mashetani*, *Pungwa*, *Ngoma ya Ng'wanamalundindi* na *Mashetani Wamerudi* unaojirudiarudia katika kipindi cha karibu miaka hamsini ambao si wa kubahatisha tu. Katika sehemu hii, tunarejelea vipengele muhimu vya utunzi wa tamthilia za Kiswahili zilizoteuliwa vinavyoleta tofauti na mfanano huo wa utunzi.

Mbinu za uigizaji na utendaji wa Kiafrika, usimulizi wa kingano, nyimbo, ngoma, ngomezi, ushairi simulizi, majigambo, malumbano ya utani, semi za kimafumbo, kijazanda na methali, mazungumzo ya hotuba, soga na ulumbi, tamaduni za Kiafrika za uchawi, pungwa na miujiza miongoni mwa tanzu nyingine muhimu zimedhihirishwa na kufafanuliwa jinsi zilivyotumika kiubunifu katika utunzi na ujenzi wa umbo mahususi la tamthilia zetu teule za Kiswahili.

Ebrahim Hussein alianza utunzi wa tamthilia yake ya *Mashetani* kwa mchezo wa kuigiza wa Shetani na Binadamu ili kumwezesha kuangazia masuala ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Kisa cha wahusika Bwana na Bibiye katika tamthilia

ya *Pungwa* ni maigizo na utendaji wa kimchezo ndani ya tamthilia hiyo ili kumwezesha kuakisi masuala ya uongozi mbaya miongoni mwa nchi za Kiafrika yanayosababishwa na viongozi wenyewe na ukoloni mamboleo. Kisa cha mwanamwali Nyamiti aliyeuawa kikatili na dhalimu Chidama akipanga arusi na mpenziwe Ciupuba ni mfano mzuri wa mbinu ya uigizaji kwa ajili ya kuibua dhamira ya ukatili, unyanyasaji na udhalimu wa wenye nguvu katika jamii kwa misingi ya unyanyasaji kiuchumi na kiutawala.

Tamthilia zote nne zimejengwa juu ya misingi ya sherehe na miviga ya tamaduni za Kiafrika kuwezesha watunzi wa kazi hizo kuwasilisha dhamira zao. Mhusika Shetani katika tamthilia ya *Mashetani* anajigeuzageuza kuwa vitu mbalimali kama kiti, tawi na hewa kwa njia ya kimiujiza isiyoeleweka ila tu kupitia mbinu za tamaduni za Kiafrika alizozitumia mtunzi. Tamthilia ya *Pungwa* imepewa anwani yake kutokana na sherehe ya mviga wa kiutamaduni wa Kiafrika wa kuwatoa au kuwapunga pepo watu waliopandwa vichwa na pepo hao wabaya kupitia kwa waganga wanaoitwa mahoka au Burhani. Utamaduni wa uchawi wa Kiafrika anaofanyiwa Nyamiti na mchawi Chidama kupitia kwa mviga wa unyago na arusi ni mbinu mwafaka ya utunzi inayomwezesha mtunzi Emmanuel Mbogo kutalii na kuweka wazi mawazo kuhusu ukandamizaji na unyanyasaji wa wananchi wanyonge kama wahusika Nyamiti na vizuu walionyanyaswa katika shamba la Chidama katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*.

Usimulizi wa kingano unatawala katika tamthilia zote nne tulizoziteua kwa uchunguzi wetu. Licha ya kwamba tamthilia huumbwa kwa kujenga mazungumzo baina ya wahusika, wakati mwingine mtunzi wa tamthilia hubuni watunzi wanaosimulia visa fulani katika kazi zao katika nafsi ya kwanza kama ilivyo katika usimulizi wa ngano.

Ebrahim Hussein anamtumia mhusika Kitaru kusimulia hadithi kuhusu ukatili wa chewa anayeishi mbali katika bahari ya saba na ambaye huwasababishia manahodha bughudha wanapoabiri baharini. Kisa cha mhusika mkuu Ng'wanamalundi katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ni masimulizi ya chagina katika utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi ya visakale.

Nyimbo na ngoma ni tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika zilizotawala katika utunzi wa tamthilia zetu teule nne za Kiswahili. Waafrika walipojinyakulia uhuru wao kutoka kwa wakoloni katika tamthilia ya *Mashetani* walijitungia wimbo ulioandamana na usakataji wa ngoma ya aina ya *waltz* ili kuusherehekea uhuru huo. Tamthilia ya *Pungwa* inaanza kwa sauti kali ya mhusika Sauti ya Mzuka inayokuja kwa njia ya wimbo. Said A. Mohamed anatumia wimbo wake huo kutanguliza dhamira anazotarajia kuzishughulikia. Tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* imejengwa kwa misingi ya ngoma mbili zinazokinzana katika malengo ili kujenga umbo la tamthilia hiyo pamoja na dhamira alizozikusudia kuzishughulikia. Ngoma ya Ng'wanamalundi na ngoma ya Chidama ni ngoma muhimu alizozitumia Emmanuel Mbogo katika kuwasilisha dhamira zake. Said A. Mohamed wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* vilevile ametumia jumla ya nyimbo kumi na mbili ambazo vichwa vyao vilidokeza dhamira ya mtunzi katika sura aliyozitanguliza nyimbo katika tamthilia hiyo.

Kuna tanzu za mashairi simulizi na majigambo zilizotumiwa na watunzi wote wanne katika utunzi wa tamthilia zote teule. Majigambo ya mhusika Shetani mwanzoni mwa tamthilia ya *Mashetani* yanamwezesha Ebrahim Hussein kumtambulisha mkoloni na kufafanua udhalimu wake kwa Waafrika. Jigambo la Shetani ni aina ya shairi huru lisilofuata sheria za utunzi wa mashairi ya kimapokeo kama lilivyo shairi la mhusika

Juma katika tamthilia hiyohiyo linalofafanua mitazamo duni waliyonayo wafanyakazi Waafrika baada ya kujinyakulia uhuru kutoka kwa wakoloni. Mhusika Sauti ya Mzuka vilevile anajigamba katika tamthilia ya *Pungwa* kusisitiza dhamira ya mtunzi kuwa mkoloni mamboleo ni yuleyule mkoloni ambaye hakutoka bali ameselelea ili kuwakandamiza Waafrika. Nyimbo alizozitumia Said A. Mohamed katika utunzi wa tamthilia ya *Mashetani wamerudi* zinasisitiza kuwa ukoloni mamboleo bado upo Afrika na kwamba ulileta huku kupitia kwa mbinu laghai za utandawazi

Msamiati wa kijazanda unaowakilisha maana nyingine tofauti na ile inayojulikana umetumiwa katika utunzi wa tamthilia zote nne zilizochunguzwa katika utafiti huu. Majina waliyopewa wahusika fulani au majina waliyobandikwa wahusika fulani kama pepo, chewa, Shetani, jogoo, mchawi, mganga, miongoni mwa mengine yametumiwa kurejelea mkoloni na mkoloni mamboleo aliyetawala nchi za Afrika kimabavu na kuzidhulumu kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutawala. Maana ya msamiati huu uliopewa wahusika katika tamthilia zetu teule inapanuliwa na watunzi wa kazi hizo ili kuibua maana mpya.

Utafiti huu umefanikiwa kudhihirisha kwamba uigizaji na utendaji wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika katika kuendeleza umbo la tamthilia ya Kiswahili ya sasa ni mbinu ya utunzi wa tamthilia teule za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi.* Wahusika wanaosimulia matukio mbalimbali katika tamthilia hizi kupitia kwa tanzu za sanaa za maonyesho ni wasanii mabingwa waliopambwa kwa kuwarundikia sifa za fanani wa sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika. Wahusika na fanani waliowatumia katika tamthilia wanaweza kuimba, kuimba na kucheza ala ya muziki huku wakinengua viungo vya mwili, kuongoza katika kuimba kiitikio, kusimulia, kughani

na kuhadithia wakifanya ishara za mwili na nyuso kama ilivyo katika sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika.

Tanzu za hotuba, malumbano ya utani, soga, ulumbi miongoni mwa tanzu nyingine za mazungumzo vilevile zilitumika katika utunzi wa tamthilia. Licha ya kuwasilishwa kwa njia ya mazungumzo, uhalisia haunakiliwi moja kwa moja bali humithilishwa kitamathali, jazanda, chuku, kejeli na tashibihi. Wahusika Chidama na Ng'wanamalundi katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* wanatoa hotuba katika nafsi ya kwanza. Hotuba ya Chidama kwa mfano kuhusu vizuu wanaomfanyia kazi katika shamba lake kuhusu anavyowadhibiti wasilalamike na kugomea hali mbaya ya kufanya kazi, anadhihirisha ulumbi wa hali ya juu na ufasaha wa usemaji kwa jinsi anavyochagua msamiati wake na kutumia tamathali za usemi. Mhusika Juma katika tamthilia ya *Mashetani* anahutubia watazamaji wa mchezo wao kuhusu mchezo walioukusudia kuwaonyesha chini ya mbuyu. Mamake Kitaru, Juma na Kitaru mwenyewe wanafanyiana utani usiodhamiria kuudhi. Seche na Nyamiti vilevie katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* wanalumbana na kufanyiana utani. Mazungumzo baina ya wahusika wengi katika tamthilia teule yanaendelezwa kwa njia ya mazungumzo ya kawaida yenye usanii na soga ya kawaida baina yao.

Watunzi wa tamthilia waliweza kuzijumuisha tanzu za sanaa za maonyesho zilizobainishwa hapa juu pamoja na zingine nyingi ili kusimulia visa mbalimbali ambavyo kwa pamoja vilichangia katika kukamilisha na kuimarisha umbo zima la tamthilia zilizobuniwa mbali na kujenga dhamira zilizokusudiwa.

## 5.6 Hitimisho

Katika sura hii, lengo la kwanza la utafiti huu limeshughulikiwa ambapo imedhihirishwa kwamba tanzu za sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika za

uigizaji na utendaji wa Kiafrika, usimulizi wa kingano, nyimbo, ngoma, ngomezi, ushairi simulizi, majigambo, malumbano ya utani, semi za kimafumbo, kijazanda na methali, mazungumzo ya hotuba, soga na ulumbi, tamaduni za Kiafrika za uchawi, pungwa na miujiza ambazo ni tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika zimetumika kisanaa katika kutunga na kuimarisha umbo la tamthilia ya Kiswahili ya kisasa. Kila moja ya tanzu za sanaa za maonyesho zilizotumiwa kisanii katika tamthilia za *Mashetani*, *Pungwa*, *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* zilizoteuliliwa kuchunguzwa katika utafiti huu zilidondolewa na mtafiti na kufafanuliwa kwa undani jinsi zilivyotumiwa kimuundo katika utunzi na uimarishaji wa umbo la tamthilia teule za Kiswahili.

Katika sura inayofuata tumechunguza taswira na maana zinazoibushwa na tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia za *Mashetani*, *Pungwa*, *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* zilizoandikwa na waandishi Ebrahim Hussein, Said A. Mohamed na Emmanuel Mbogo kwa mujibu wa lengo letu la pili.

.

# SURA YA SITA

## TASWIRA YA TANZU ZA SANAA ZA MAONYESHO YA JADI ZILIZOTUMIWA KUTUNGA TAMTHILIA YA KISWAHILI

### 6.0 Utangulizi

Katika sura ya tano, tulitambua na kudhihirisha tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho zilizotumiwa na watunzi wa tamthilia za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* katika kujenga na kuimarisha umbo la tamthilia hizo kwa mujibu wa lengo letu la kwanza la utafiti huu. Sura hii imeshughulikia matokeo ya utafiti huu kwa mujibu wa lengo la pili ambalo ni kudhihirisha taswira zinazoibushwa na tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika zilizotumiwa kama mbinu ya utunzi wa tamthilia hizo teule kama mbinu ya kuendeleza dhamira za watunzi. Tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika zilizotumiwa katika kuunda tamthilia hizi zilichunguzwa zilivyotumiwa ili kudhihirisha taswira zilizoibuliwa. Tamthilia zote teule zimebuniwa kwa ajili ya kuigizwa jukwaani sababu ambayo inazifanya kuwa tamthilia zenye misingi ya ki-Aristotle. Licha ya misingi hii ya ki-Aristotle, watunzi wa tamthilia hizi wamechota amali ya sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika na kuzitumia Kimwingilianomatini katika kubuni na kuimarisha umbo na dhamira katika tamthilia zao. Matumizi ya tanzu hizi katika utunzi wa tamthilia zetu teule ulituchochea kuchunguza taswira inayojengwa kupitia kwa makusudio ya watunzi hao na maana inayoibushwa kwa hadhira kupitia kwa matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi kama malighafi na mbinu ya kutungia tamthilia zao.

### 6.1 Taswira ya Sanaa za Maonyesho katika Tamthilia ya Mashetani - Ebrahim Hussein

Sehemu hii ya utafiti ilichunguza matumizi ya tanzu za jadi za maigizo ya mchezo wa Shetani na Binadamu, usimulizi wa kihadithi hususani hadithi ya chewa, uwakilishaji kupitia kwa jazanda mbalimbali, mbali na matumizi ya motifu ya safari na nyingine katika kujenga taswira za ukoloni mamboleo, ukandamizaji, utandawazi, unafiki, ubadhirifu, unyanyasaji na utabaka uliodhihirika katika tamthilia ya *Mashetani*. Ilikuwa imekisiwa kwamba Ebrahim Hussein ametumia tunzu anuai za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za jadi za Kiafrika katika kujenga na kuibua taswira mbalimbali za kimaana katika tamthilia yake ya *Mashetani* ambazo ilibidi tuzibainishe na kuzijadili kwa ufasaha kwa mujibu wa lengo letu la pili la utafiti huu.

#### 6.1.1 Taswira ya Ukoloni Mamboleo katika Mchezo wa *Shetani na Binadamu*

Taswira ya ukoloni mamboleo ilidhihirishwa mwanzoni mwa tamthilia ya *Mashetani* kupitia kwa utanzu wa mchezo wa kuigiza wa Shetani uliohusisha wahusika Shetani na Binadamu kupitia maelezo yao kama ifuatavyo:

> JUMA: Wananchi; kwa mara nyingine chini ya mbuyu huu mimi Juma, na rafiki yangu Kitaru, **tutakuonesheni mchezo wa Shetani na Binadamu. Mimi nitakuwa Shetani na Kitaru atakuwa Binadamu.** (*Mashetani - uk 1)*

Ebrahim Hussein anatumia utanzu wa maigizo au mchezo wa kuigiza kupitia wahusika wake Juma na Kitaru ili kumwezesha kujenga taswira ya ukoloni mamboleo. Katika dondoo la hapa juu, Juma anaeleza hivi, "**tutakuonesheni mchezo wa Shetani na Binadamu. Mimi nitakuwa Shetani na Kitaru atakuwa Binadamu" -** (*Mashetani - uk 1)***.** Ukoloni mamboleo ni namna ya utawala wa nchi zilizoendelea hasa za Kimagharibi kuendeleza mfumo wa kibepari unaoathiri maamuzi muhimu kuhusu uchumi, siasa na utawala wa nchi zinazoendelea. Katika

mfumo huu, nchi zilizoendelea huzidhibiti nchi changa zinazoendelea kupitia kwa mbinu ambazo si wazi.

Tangu mwanzo wa utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ya *Mashetani* (1971), kupitia kwa kipindi cha kati cha utunzi cha akina Said A. Mohamed wa tamthilia ya *Pungwa* (1988) na Emmanuel Mbogo wa tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1999) hadi kipindi cha utunzi cha sasa cha Said A. Mohamed wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016), ukoloni mamboleo ni dondandugu linalodhihirika katika vipindi vyote. Watunzi wote hawa wamedhihirisha kwamba mataifa ya Kiafrika yangali yanadhibitiwa na mataifa ya Kimagharibi kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutawala. Watunzi wa tamthilia hizi wametumia tanzu za sanaa za maonyesho zinazorejelea matukio ya nchi za Afrika kukosa uhuru wa utawala wa ndani, uchumi na siasa licha ya nchi zenyewe kujinyakulia uhuru wa bendera. Hivyo mataifa yaliyoendelea huathiri maendeleo katika nchi changa za Kiafrika mbali na kumiliki nyenzo za uzalishaji mali katika nchi hizo.

Tamthilia ya *Mashetani* (k.h.j.) iliyoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu imeshughulikia masuala ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo kupitia kwa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilizotumiwa kama nyenzo ya utunzi wa tamthilia hii ili kuyamulika matatizo katika nchi za bara zima la Afrika. Utanzu wa mchezo wa maigizo kupitia kwa mchezo wa **Shetani na Binadamu** (*Mashetani – uk 1*) kwa mfano, umetumiwa kijazanda na Ebrahim Hussein katika tamthilia ya *Mashetani* na kurejelewa na Said A. Mohammed katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* Kimwingilianomatini katika mazungumzo baina ya wahusika Prof. na Kijana 1 kuwakilisha dhuluma za ukoloni mkongwe na kudhihirisha ukoloni mkongwe kama asili ya matatizo yanayomkumba Mwafrika anayewakilishwa na mhusika Binadamu.

Ebrahim Husein kama mwandishi mkongwe ni miongoni mwa watunzi waasisi na wa awali kabisa kutumia tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi za asili ya utamaduni wa Kiafrika kuwakilisha dhima ya ukoloni na ukoloni mamboleo katika eneo la Afrika mashariki katika mwaka wa 1971 kupitia kwa utunzi wa tamthilia ya *Mashetani*. Kupitia mhusika Kitaru katika Onyesho la 1 katika Sehemu II, Hussein anatumia stiari ya Shetani kuelezea jinsi ukoloni mamboleo unavyozinyemelea na kujijenga katika nchi za ulimwengu wa tatu kama nchi za Afrika. Kwa kuulinganisha ukoloni mamboleo na Shetani, Hussein anaeleza kuwa ukoloni mamboleo kama Shetani huwa na nafsi yenye ncha nyingi, "**Shetani … mjia Binadamu na kumghilibu kwa sura mbalimbali – (***Mashetani, iv) Ufafanuzi wa Kitaru kuhusu Mkoloni – kr 24 – 25*), humwingia Binadamu kwa namna au sura mbalimbali na kumzuga akili.

> KITARU: **Shetani**, hii ni nafsi yenye ncha nyingi, **ni kiumbe kinachomwingia Binadamu kwa namna mbalimbali na kumzuga akili**. Shetani hufahamu? **Hadithi chungu nzima juu ya Shetani na Binadamu** zinazoeleza vipi **Shetani anavyomjia Binadamu na kumghilibu kwa sura mbalimbali**.
> (*Mashetani – kr 24 – 25*)

Ukoloni mamboleo hunyemelea na kuzitawala nchi za Afrika na zingine za ulimwengu wa tatu kishetani bila nchi zenyewe kutambua jinsi Shetani anavyofanya anapomwingia Binadamu kama inavyoelezwa katika visasili na tamaduni chungu nzima za Kiafrika (**Hadithi chungu nzima juu ya Shetani na Binadamu** – *Mashetani* - uk 24**)**. Masimulizi ya visasili katika tamaduni za Kiafrika yamejaa taswira za Mashetani wanaomkumba Binadamu kwa njia nyingi mbalimbali na kumwathiri. Ebrahim Hussein amechota taswira hizi ambazo zimetumiwa kijazanda ili kujenga dhamira yake ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo katika nchi huru za Afrika.

Akieleza kuhusu dhana ya Mashetani, mhusika Kitaru anaeleza hivi: **Shetani … ni kiumbe kinachomwingia Binadamu kwa namna mbalimbali na kumzuga akili** – (*Mashetani* - uk 24). Ukoloni mamboleo hujikita katika karibu kila kitu anachokifanya Mwafrika. Baba Kitaru anapomuuliza Kitaru kuhusu linalomsumbua kuhusiana na Mashetani, Kitaru anaeleza hivi:

> KITARU: **Huoni, lakini, kama leo kila kitendo kina alama ya Shetani na kila mtu ana nafsi ya Shetani** - (*Mashetani* - uk 24).

**Shetani** ni stiari aliyoitumia Ebrahim Hussein kumwakilisha mkoloni aliyekuja Afrika na kuzitawala nchi za Afrika kimabavu, kuyaingilia maisha ya Waafrika kichumi, kisiasa na kijamii. Wakoloni hawa waliingilia maisha ya Waafrika kwa kila njia kwa namna inayoathiri uhuru wao. Ukoloni umeingia katika kila kipengele cha maisha ya Binadamu kama anavyosema mhusika Kitaru katika dondoo la hapa juu: **Huoni, lakini, kama leo kila kitendo kina alama ya Shetani na kila mtu ana nafsi ya Shetani -** (*Mashetani* uk 25). Katika hali ya kurejelea tamthilia ya *Mashetani* Kimwingilianomatini, mtunzi Said A. Mohamed naye anasisitiza kuwa tatizo la Mashetani la miaka 1970 bado lipo Afrika katika miaka ya sasa ya 2020 pale anaposisitiza kuwa "**Pana Mashetani hapa"** – (*Mashetani Wamerudi*- uk 7) katika dondoo la hapa chini na pale anapotumia maneno "**waltz na mchezo**" yaliyotumiwa na mwandishi Ebrahim Hussein katika tamthilia yake ya *Mashetani* (1972) kurejelea ukoloni mkongwe uliokita mizizi na kukataa kuondoka abadani bara la Afrika hata baada ya nchi za Afrika kupata uhuru wao. Said A. Mohamed ameandika hivi katika tamthilia ya *Mashetani wamerudi* (2016):

> Kijana: **Pana Mashetani hapa.**
> **Prof.: Walewale waliotuchezesha mchezo wa maneno na dansi ya *waltz* huku wakijidai kwamba wangeondoka kwenda kwao.** Kumbe wangerudi na sisi tumewaita na **kudhani ni wakweli**. (*Mashetani Wamerudi – uk 7*)

Matamshi ya wahusika Kijana na Prof katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kuwa; **Pana Mashetani hapa… Walewale waliotuchezesha mchezo wa maneno na dansi ya *waltz* huku wakijidai kwamba wangeondoka kwenda kwao** *(Mashetani Wamerudi – uk 7*), ni thibitisho la madai ya Ebrahim Hussein kwamba wakoloni waliobanduliwa Afrika katika vita vikali vya kung'angania uhuru (kupitia kwa jazanda ya Binadamu kumdunga Shetani kisu katika mchezo wao ) hawakutoka kamwe bali walijibadilisha na kurudi katika mfumo mpya wa ukoloni mamboleo. Ajabu ni kwamba Waafrika wenyewe ndio wamewaita warudi Afrika "**wakidhani kuwa ni wakweli'** na wenye nia nzuri ya kusaidia nchi maskini za Afrika.

Mashetani hutisha na kuiogopesha umma kama anavyosema Kitaru katika dondoo la hapa chini, "**Ndivyo unaogopa Mashetani bado? Lo!" - (*Mashetani* - uk 17)**. Katika masimulizi ya ngano za mazimwi na utamaduni wa Kiafrika, Mashetani huchorwa kuwa viumbe hatari wenye maumbo ya kiajabu wanaohusishwa na mambo mabaya ya kutisha ambayo huhatarisha amani na mfumo wa kijamii. Katika mazungumzo yao nyumbani kwao Kitaru, Juma na Kitaru wanauzungumzia mchezo wa Mashetani waliouigiza awali baina yao ambapo wanaeleza ifuatavyo kuhusu Mashetani.

> Kitaru: Acha maneno yako. Maneno ya kiShetani
> …
> Juma: Naye kweli namna gani siku ile? Ukakurupuka tu. Mi nikaogopa.
> ….
> Kitaru: **Ndivyo unaogopa Mashetani bado? Lo!** Hata sikudhania.
> Kitaru: Tuachilie mbali maneno haya.
> Kitaru: **Unaogopa atakupanda nini?**
> (*Mashetani – uk 17. Msisitizo ni wetu*)

Ukoloni mamboleo kama Mashetani ni hatari kwa usalama wa Mwafrika. Ukoloni mamboleo umenyemelea na kuzitawala nchi za Afrika afanyavyo Shetani anapowapanda kichwa wahusika Bwana katika tamthilia ya *Pungwa* na Binadamu

katika tamthilia ya *Mashetani*. Kitaru akimwakilisha Shetani ambaye ni mkoloni anamuuliza Juma anayemwakilisha mwananchi wa kawaida katika nchi maskini za Afrika kama anaogopa atapandwa na Mashetani, "**Unaogopa atakupanda nini?"** (*Mashetani* - uk 17**)**. Nchi za Kimagharibi zimezidhibiti nchi za Kiafrika kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kwa namna inayomithilishwa na kupandwa kichwa na Shetani. Dhana ya kupandwa kichwa ambayo imetumiwa kimwingilianomatini katika tamthilia tatu za *Mashetani, Pungwa* na *Mashetani Wamerudi,* ni stiari inayomaanisha kwamba nchi zilizopandwa na pepo hazina tena uhuru wa kujiamulia mambo yao wala kujitegemea kiuchumi bila kuathiriwa kwa njia mbalimbali na nchi za Kimagharibi. Kiuhalisia, haya ndiyo madhara yanayosababishwa na nchi za Kimagharibi zinazowakilishwa kijazanda na Shetani na jogoo katika tamthilia za *Mashetani, Pungwa* na *Mashetani Wamerudi* kwa nchi za Afrika na ulimwengu wa tatu ambazo pia zinawakilishwa na mhusika Binadamu. Nchi za Afrika zinafaa kuogopa na kumwambaa Mzungu anayeendeleza ukoloni mamboleo kama wanavyoambaa majini katika utamaduni wa Kiafrika kwa sababu athari zake ni mbaya na hatari kwa uhuru wao.

### 6.1.2 Taswira ya Ukandamizaji na Utandawazi katika Jazanda ya Hadithi ya Chewa

Ebrahim Hussein ametumia utanzu wa hadithi kusimulia kuhusu dhuluma na unyanyasaji unaofanyiwa nchi maskini za Afrika na ulimwengu wa tatu na nchi tajiri kupitia kwa hadithi ya chewa. Chewa ni mnyama mkubwa ajabu aliye na uwezo wa kiungu na wa kipepo wa kumeza kila kitu kilichomo baharini. Chewa anaweza kubadili mwelekeo wa meli na mashua kwa kuvuta mkondo wa maji na kulazimisha chombo hicho kwenda asikotaka nahodha. Mnyama huyu chewa amepewa nguvu za ajabu kama zile za pepo wanaosimuliwa katika ngano na tamaduni za Kiafrika.

Katika mila na tamaduni za Kiafrika, inaaminika kuwa pepo wanaowapanda Binadamu kichwa hutoka baharini. Pepo hao wana uwezo wa kuangamiza na kuwavuruga watu akili wasiweze kufikiria kwa njia razini. Ebrahim Hussein ametumia jazanda ya bahari kurejelea nchi zinazodhibitiwa na nchi za Kimagharibi kiutandawazi katika siasa, uchumi na katika masuala ya kijamii kupitia kwa mfumo huo wa utandawazi unaozikutanisha nchi zilizoendelea na zinazoendelea. Kitaru anamweleza mama yake kuhusu mnyama mkubwa ambaye ni hatari na anayeishi mbali katika bahari kubwa katika hadithi aliyosimuliwa na nyanyake Juma:

> KITARU: **Hadithi ya chewa**. Mbali sana, ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa, **chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake**. **Anaweza kutoka huko aliko, kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa na mkondo wa maji, ikitaka isitake.** Na huyu **chewa si chewa bali ni Shetani**. (*Mashetani* – uk 28)

Hussein anatumia jazanda ya bahari katika masimulizi ya mhusika Kitaru ya "**hadithi ya chewa"** ili kuzua taswira ya maisha halisi katika ulimwengu wa kiuchumi katika nchi za Kiafrika na ulimwengu wa tatu unaomilikiwa na kudhibitiwa na mabepari. Chewa ni mnyama mkubwa kama papa anayeishi ndani ya maji hasa baharini. Katika dondoo la hapa juu, mtunzi anadhihirisha uwezo mkubwa alio nao chewa kwa kueleza kwamba, "**chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake" -** (*Mashetani* – uk 28)**.** Chewa ametumiwa kijazanda na mtunzi kuvuta taswira ya nchi tajiri za ulimwengu wa kwanza ambazo huzidhulumu na kuziathiri nchi changa za Afrika na ulimwengu wa tatu jinsi wafanyavyo chewa na papa kwa kuwameza samaki wadogo. Kitaru anaendelea kusimulia kuhusu uwezo wa ajabu wa chewa kwa kusema kuwa, "…**Anaweza kutoka huko aliko, kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa na mkondo wa maji, ikitaka isitake," -** (*Mashetani* – uk 28)**.** Kama mnyama wa ajabu anayesimuliwa

katika hadithi, chewa anayeabiri kutoka maeneo ya mbali kuja kuimeza mashua yoyote anayoitaka, mkoloni vilevile alisafiri kutoka kwao mbali kuja katika bara la Afrika na kuitwaa nchi yoyote anayoitaka. Nchi hiyo ya Kiafrika inavamiwa, kunyakuliwa na kudhibitiwa kwa nguvu ipende isipende.

Chewa anayesimuliwa katika hadithi katika dondoo la hapa juu, anaweza kuvuta maji yote baharini na kuifanya mikondo yote ya maji kuelekea kinywani mwake, ametumiwa kijazanda na Ebrahim Hussein ili kuonyesha tabia ya ulafi na nguvu na athari ya ukoloni katika mfumo wa ukoloni mamboleo. Nchi za Kimagharibi katika mfumo huu wa ukoloni mamboleo zinamiliki njia za kiuchumi, kisiasa, kiteknolojia na kijamii na kwa kutumia nguvu zao za 'kimkondo' huamua ni upande gani nchi zinazokua zitauchukua kama asemavyo Kitaru katika dondoo **"…Mashua inavutwa na mkondo wa maji, ikitaka isitake"**. Kupitia kwa njia hii ya kusukumwa kwa nguvu, nchi changa hazina uhuru wa kujiamlia mipango ya maendeleo na ustawi wao wenyewe kwa sababu wamedhibitiwa na mkoloni mamboleo anayeuvuta kwake mkondo wa maendeleo kupitia kwa mbinu za utandawazi.

Viongozi wa nchi huru maskini za Afrika kama nahodha wa meli kwenye bahari ya mawimbi makubwa ya "wakoloni", hawana udhibiti wa nchi zao tangu nchi hizo kujinyakulia uhuru kutoka kwa wakoloni. Viongozi wan chi za Afrika wanaelekezwa tu waende wapi na nchi tajiri kama asemavyo Kitaru katika ukurasa 21:

> KITARU: … toka tumepata uhuru, sisi Waafrika hapa imekuwa tumeingia … ehe, mfano mzuri … **imekuwa kama tumeingia … katika jahazi moja zuri na jina letu limeandikwa lakini … nahodha … nahodha nani?** … Je mkondo ukiwa unavuta upande mwingine na nahodha anataka kupeleka jahazi upande mwingine? *(Mashetani – uk 21).*

Kama katika jahazi, nchi za Afrika na ulimwengu wa tatu zimepata utambulisho wa kuwa huru lakini ziko katika mkondo unaozivuta kuelekea zisikokutaka; "**imekuwa**

**kama tumeingia … katika jahazi moja zuri na jina letu limeandikwa lakini … nahodha … nahodha nani?"** Nchi hizi zimedhibitiwa na nguvu za kibepari zinazomiliki njia za uzalishaji mali, biashara, vyombo vya habari, mfumo wa kuhawilisha pesa na njia zingine wanazozitumia kudhibiti nchi changa za Afrika. Utekelezaji wa shughuli hizi zote hauongozwi na tawala za nchi huru za Afrika bali zinadhibitiwa na nchi za ulimwengu wa kwanza "*ki-remote control*" kama asemavyo Said A. Mohamed katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi.*

### 6.1.3 Taswira ya Unafiki, Ubadhirifu na Unyanyasaji katika Ngoma na Nyimbo

Ebrahim Hussein ametumia tanzu za majigambo, nyimbo na ngoma katika kuzua taswira ya unafiki, unyanyasaji na ubadhirifu wa utawala na viongozi wa nchi za Afrika. Baada ya kumng'oa mbeberu kutoka bara la Afrika na kujinyakulia uhuru wao, nchi za Afrika zilijitungia nyimbo na kucheza ngoma ili kusherehekea uhuru wao kwa njia ya kiburi. Katika stiari ya mchezo wa Shetani na Binadamu katika Onyesho la Kwanza la Sehemu ya kwanza ya tamthilia ya *Mashetani*, Binadamu anamuua Shetani kwa kumchoma kisu katika mabavu yake, ishara ya Mwafrika kumshinda mkoloni na kumwondoa barani Afrika na hivyo kujinyakulia uhuru wa kujitawala. Kifo cha mhusika Shetani kinaashiria mwisho wa utawala wa kikoloni katika nchi za Afrika. Mkoloni anakufa kimwili kuwakilisha Mwafrika kujinyakulia uhuru wa kiutawala unaowakilishwa na bendera ya nchi huru za Afrika. Baada ya ushindi huo dhidi ya Shetani, Binadamu anayemwakilisha Mwafrika aliyejinyakulia uhuru wake kutoka kwa mkoloni, anaimba chini ya mbuyu (*Mashetani* - kr 9 – 10) katika tamthilia hiyo

> (*anapiga vigelegele vya furaha. Anarukaruka na kuizunguka maiti kwa furaha kubwa. Anacheka mpaka michozi inamtoka. Anacheka mpaka furaha na kicheko vinamlevya. Anauendea ule mbuyu kwa haraka na huku anacheka. Anaimba*)
>
> **Wako wapi walio wakijitapa?**

Sasa twawataka.
**Wako wapi walio wakijitapa?**
Sasa twawataka.
**Tumekwisha (*anacheka*) wakamata**
Wakamata.
Tumekwisha wabwabwata.

Wako wapi waliokuwa juu jana?
Sasa twawataka.
Wako wapi waliokuwa juu jana?
Sasa twawataka.
**Tumekwisha waangusha**
Waangusha.

**Tumekwisha wasagasaga.**

**Tumekwisha wakamata**
Wakamata.
**Tumekwisha wabwatabwata**

**Tumekwisha waangusha**
Waangusha.
**Tumekwisha wasagasaga.**

(*Mashetani - kr 9 – 10*)

Baada ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru wao, waliingiwa na kiburi na kujitapa kwa ushindi wao dhidi ya kaburu. Waafrika hao walisherehekea ushindi wa uhuru wao kwa kuimba nyimbo na kufanya sherehe kubwa. Kiburi kiliwafanya Waafrika kujipiga kifua na kuwakejeli Wazungu waliokuwa wametoka kwa kuwauliza maswali ya kuwadunisha na kuwadhihaki ifuatavyo katika nyimbo za; **"Wako wapi walio wakijitapa? Tumekwisha (anacheka) wakamata. Wakamata. Tumekwisha wabwabwata" -** (*Mashetani – uk 9)*. Kwa Waafrika, huu sasa ndio uliokuwa wakati wao wa kuwa juu kama walivyokuwa wakoloni. Ukweli ni kwamba huu ndio uliokuwa wakati wa Mwafrika kuwa juu kwa kujitawala, kujitegemea na kujifanyia mambo yake mwenyewe. Kujinyakulia uhuru ulifaa kuwa wakati wa furaha na kujinyakulia utawala wao wa ndani wala si wakati wa kuwaruhusu watu kutoka nje kuja kuwatawala.

Katika kurejelea mbinu zinazopatikana tu katika utanzu wa majigambo wa sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika, Mwafrika (Binadamu) anayataja mambo aliyofanikiwa kuyatekeleza wakati wa kupigania uhuru wake. Binadamu ambaye anamwakilisha Mwafrika katika wimbo wa Binadamu wa dondoo la hapa juu, anajisifu na kujigamba kuhusu matendo makubwa aliyokuwa ameyatenda kwa kusema maneno yafuatayo; **Tumekwisha waangusha … Tumekwisha wasagasaga … Tumekwisha wakamata … Tumekwisha wabwatabwata … Tumekwisha waangusha … Tumekwisha wasagasaga.** Ingawa Waafrika walikuwa wameupata uhuru wao kwa shida kubwa na mahangaiko, walisahau matatizo hayo yote na wakaanza kujitapa kwa kiburi kama inavyodhihirika katika majitapo na majisifu yake katika dondoo la wimbo la hapo juu.

Baada ya kusherehekea kujinyakulia uhuru wao kwa majigambo, nyimbo na ngoma za furaha na vigelegele kwa muda mrefu, nchi za Afrika zinatambua ukweli kwamba haziwezi kujitawala na kujitegemea zenyewe kiuchumi, kisiasa na kijamii. Baada ya muda mfupi wa kujinyakulia uhuru, nchi za Afrika zilianza kutegemea misaada ya mawazo, uongozi na mali kutoka nchi za Magharibi kupitia kwa taashira ya Mwafrika kujirusha juu ya tawi na kuanguka. Baada ya wimbo katika dondoo la hapo juu **(Wimbo wa Binadamu**), Binadamu anajaribu kujirusha juu ya tawi la mti kama alivyofanya Shetani alipojirusha juu ya tawi la mti kimiujiza akitarajia kushikilia bila kuanguka. Kwa mara zote tatu Binadamu anajirusha juu ya tawi na anaanguka kama inavyodhihirishwa katika dondoo la hapa chini ambapo mtunzi anaeleza hivi; "***Anajitupa juu ya tawi, huku anacheka. Mara anaanguka chini. Anajaribu tena, anaanguka."*** Mwandishi Ebrahim Hussein anaandika hivi katika tamthilia ya *Mashetani:*

> (***Anajitupa juu ya tawi, huku anacheka. Mara anaanguka chini. Anajaribu tena, anaanguka. Mara ya tatu vilevile. Ulevi umemtoka***) - *( Mashetani - uk 10).*

Kujitupa juu ya tawi kwa mhusika Binadamu na kuanguka ni taashira ya nchi za Afrika kujaribu kujisimamia na kujitawala kwa kujifanyia mambo yao wenyewe. Nchi za Afrika hata hivyo haziwezi kujisimamia kama nchi za Magharibi zilizozitawala wakati wa ukoloni. Punde tu baada ya kujinyakulia uhuru nchi za Afrika zinaanguka tena na tena kama anavyoeleza mtunzi katika dondoo la hapa juu, ***"Anajitupa juu ya tawi, huku anacheka. Mara anaanguka chini. Anajaribu tena, anaanguka. Mara ya tatu vilevile"*** **(uk 10).** Kuanguka kwa nchi za Kiafrika zinapojaribu kujitegemea kwa kujitawala kunaziingiza nchi hizo katika shimo la utegemezi wa misaada, maarifa, utawala, mbinu za kujiamulia na kujifanyia mambo yao wenyewe. Licha ya nchi za Afrika kufurahia kujinyakulia uhuru wao kwa nyimbo na sherehe, ukweli wa hali ya utegemezi wao katika nchi za Magharibi unazibainikia kama mlizamu na mwandishi anaeleza kuwa "**ulevi umemtoka,"** (*Mashetani – uk* 10). Kuanguka kwa Binadamu kutoka kwa tawi ni taashira ya nchi za Afrika kushindwa kujitawala kama nchi huru na hivyo hatimaye kutoweza kujitegemea.

Kila mara baada ya nchi za Afrika kushindwa kujisimamia na kujitegemea kama Shetani alivyofanya alipojigeuza na kujirusha juu ya tawi la mti, nchi hizo za Afrika zinamlaumu Mzungu kuwa ndiye aliyesababisha kuanguka kwao. Hivyo Waafrika wanaanza kutafuta visababu vya kueleza asili ya kuanguka kwao. Binadamu anasema hivi katika mchezo wake na Shetani baada ya kumuua Shetani, "**Wewe hapo ndiye unayesababisha kuanguka kwangu**":

> Hukufa! Uko hai!
> **Najua umo humu mtini. Wewe hapo ndiye unayesababisha kuanguka kwangu**. Jibu. Unacheka? **Nakuhisi unanicheka**. **Ila sasa siusikii tena mcheko wako, lakini ninauhisi. Sikuoni lakini,**

> **lakini ninakuhisi** … Ninajua kuwa ni wewe tu unayeniangusha. **Unaniangusha kisirisiri huku unac**heka … (*Mashetani* - uk 10)

Ingawa mkoloni alishindwa na Mwafrika na kuondolewa kwa nguvu na Mwafrika kujipatia uhuru wake, Mzungu hakuondoka kama Binadamu anavyoeleza mashaka yake katika dondoo la hapa juu, "**Najua umo humu mtini. Wewe hapo ndiye unayesababisha kuanguka kwangu**". Wazungu walirudi Afrika na kuendelea kuwatawala Waafrika kwa njia tofauti ambazo Waafrika hawakuzielewa. Kwa Binadamu (Mwafrika) hakuelewa hali yake ya kutawaliwa na nchi za Magharibi zilizokuwa zimerudi kisisiri baada ya uhuru. Mhusika Binadamu anasema, "…**Nakuhisi unanicheka. Ila sasa siusikii tena mcheko wako, lakini ninauhisi. Sikuoni lakini, lakini ninakuhisi,** (*Mashetani* – uk 10). Hii ndiyo sababu Binadamu anasema kwamba anajua Shetani yumo humo mtini walikokuwa wakicheza. Mtini ni maskani ya Mwafrika ambapo Wazungu walikuja na kumtawala Mwafrika wakati wa kihistoria wa ukoloni katika hali iliyowakilishwa kisanaa na Ebrahim Hussein kupitia kwa mchezo wa Binadamu na Shetani. Binadamu anamlaumu Shetani kuwa ndiye anayesababisha kuanguka kwake anapojirusha juu ya tawi la mti. Nchi huru za Afrika za wakati wa sasa kihistoria zinaanguka kimaendeleo na kushindwa kujisimamia kama nchi huru kwa sababu ya kudhibitiwa katika nyanja zote za maisha. Hali hii inasababisha utegemezi wa nchi za Afrika katika nchi za Magharibi katika hali zote za maisha kisiasa, kiuchumi na kitamaduni na hatimaye kuanguka kwao.

Punde tu baada ya kujinyakulia uhuru wao, Waafrika wengi waliingiwa na unafiki wa mabepari waliokuwa wametoka na kuanza kujilimbikizia mali kwa njia ambazo si halali huku wakitumia mali kwa njia ya ubadhirifu kwa mawazo potovu kwamba huu ulikuwa wakati wa Mwafrika kula, kama anavyosema mhusika Mtu 1, "**Bwana huu sasa wakati wetu**. **Mwafrika sasa ale vizuri, akae mahali pazuri, avae vizuri … nataka tuwaone Waafrika wana ndege, mali zao wenyewe"** :

MTU 1: Wewe … wewe sijui namna gani unajiweka nyuma kama mkia. **Bwana huu sasa wakati wetu**. **Mwafrika sasa ale vizuri, akae mahali pazuri, avae vizuri … nataka tuwaone Waafrika wana ndege, mali zao wenyewe**.
(*Mashetani - kr 43 – 44*)

Mawazo haya potovu ndiyo yaliyowaongoza wengi wa wafanyakazi wa Kiafrika kuanza kuibia serikali za nchi zao ili kujipatia mali ambayo hawakufaa kuwa nayo. Baada ya nchi ya Tanzania na nchi zingine za Afrika kujinyakulia uhuru, mali iliyokuwa inamilikiwa na Wazungu na mabwanyenye wengine ilitwaliwa na kutaifishwa. Huu ndio wakati ambapo familia ya akina Juma ilikuwa juu kiuchumi kabla ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru (wakati wa ukoloni mkongwe) na mali yao kutaifishwa na kuwafanya kuwa maskini wa tabaka la chini sasa. Familia ya Kitaru ambayo ilikuwa chini wakati wa ukoloni badala yake ilijibadilisha kimiujiza kama alivyofanya Shetani katika mchezo wa Shetani na Binadamu na kupanda ngazi kiuchumi na kuwa katika upeo wa kimatabaka. Baba ya Kitaru katika ubadhirifu huo anabadilisha magari anavyopenda kwa kujinunulia magari mapya ya bei ghali. Baada ya kununua gari mpya, Baba Kitaru anacheza na kuimba na mke wake hivi;

BABA KITARU: (*anaimba*)
**Papa pa pa pa pa**
**I like some money**
**Papa pa pa pa pa**
**I like some money.**
**Papa pa pa pa pa**
**(Mama Kitaru anaingia)**
**A very good life.**
**Papa pa pa pa pa**
**(Anamchukua mkewe kucheza)**
**A very beautiful wife.**
Papa pa pa pa pa
A very good wife
Papa pa pa pa pa
A very good life …

BABA KITARU: Njooni hapa dirishani. Unaiona nini?
MAMA KITARU: Gari mpya! Benz!
BABA KITARU: Yangu! Naam! Mali yangu, jasho langu. Kitaru, njoo uitazame. Juma, njoo. Mnaiona? Tazama ilivyotulia. Basi pale

> itoneshe tu – waaaah, linaruka kama ndege. Twendeni tukatembee, mnasemaje? Twendeni, twende, twende.
> (*Mashetani* - kr 21 -22)

Baba Kitaru anaongoza wimbo wa kusherehekea kununua kwake gari jipya linalobadilisha maisha yake kuwa "mazuri" kama anavyosema katika wimbo wenyewe. Wimbo wa Baba Kitaru unaimbwa kwa lugha ya Kiingereza. Baada ya kujinyakulia uhuru, Waafrika wengi walioingia uongozini, walikengeuka na kubadilisha mienendo yao ya maisha kwenda ile ya Kimagharibi pamoja na kusema kwa lugha ya Kiingereza kama anavyofanya Baba Kitaru katika wimbo anapoimba, **"*Papa pa pa pa pa; I like some money; Papa pa pa pa pa; I like some money; Papa pa pa pa pa; A very good life*" -** (*Mashetani* – uk 21*)*. Baba Kitaru katika wimbo huu anaeleza kwamba, kuwa na pesa na mke mzuri ndiyo mambo ambayo yanamfanya kufurahia maisha yake licha ya kwamba pesa hizo amezipata kupitia kwa njia ya wizi uliochangia katika kuanguka kwa mashirika mengi ya serikali. Matumizi ya lugha ya Kiingereza katika wimbo huu ni mbinu ya kudhihirisha mkengeuko na utabaka ulioko miongoni mwa jamii za Kiafrika baada ya kujinyakulia uhuru.

Viongozi wa nchi za Afrika walidhani kwamba, wao kuwa na maisha mazuri ni kujinyakulia mali na kununua magari mapya kwa bei ghali baada ya kuibia serikali yao. Haya ni maisha ya ubadhirifu ambapo pesa nyingi zinaharibiwa na Waafrika katika kufadhili maisha ya anasa. Wizi wa mali ya umma unaleta umaskini katika nchi za Afrika ambao unazifanya kukimbilia nchi za Magharibi ili kwenda kuomba misaada. Uwasilishaji wa wimbo huu unafanywa kwa njia zinazopatikana tu katika sanaa za maonyesho ya Kiafrika.

Kutoelewa maana ya kuwa huru kunadhihirika mkahawani katika Sehemu III, Onyesho la II la tamthilia ya *Mashetani* pale ambapo wahudumu wanang'ang'ania wateja Wazungu na matajiri ambao wanatoa bahashishi, yaani "tip" na kuwabagua na

kuwadharau wateja Waafrika wanaonekana kuwa maskini na ambao hawawezi kutoa "tip" baada ya kuhudumiwa. Wateja Waafrika wanalalamika kuwa wanapuuzwa na hawasikizwi wanapoweka maombi yao ya vyakula kwa wahudumu hao mkahawani, tofauti na wanavyowafanyia wateja Wazungu. Kama inavyodhihirika katika mazungumzo yao, wahudumu hao hao hubishana na wateja Waafrika kwa njia ya dharau, jambo ambalo hawathubutu kulifanya kwa wateja Wazungu.

Wateja wakingoja vyakula walivyoviagiza katika onyesho tulilolitaja hapa juu, wanazungumzia kuhusu wizi na ubadhirifu wa mali ya umma unaofanywa na wafanyakazi wa serikali. Kwamba mashirika ya serikali yalikuwa yanafungwa baada ya wafanyakazi waliochukua uongozi wao baada ya uhuru kuyapora pesa walizozitumia kinafiki kujinunulia majumba makubwa, magari ya bei ghali mbali na kuishi maisha ya anasa. Mhusika Juma akiwa kando katika meza nyingine mkahawani, anahitimisha hali hiyo ya Waafrika kwa shairi lifuatalo:

JUMA: upweke.
Upweke una mbawa
Unarusha nyoyo za Binadamu juu kabisa.
Chini linabakia ganda.
Macho yanaona, akili inafikiri …
Lakini …kiwiliwili hakihisi.
(*Anacheka polepole*)
**Bibi anapuliza sumu.**
**Sumu au mapenzi?**
**Jaribu kupambanua:**
Mapenzi hugeuka sumu.
Naam, mara nyingi
Mapenzi hugeuka sumu
*(Mashetani – kr 41 – 42)*

Wakati wa mazungumzo kati ya wahudumu wa mkahawa na wateja wao katika Sehemu ya III Onyesho la II, mtunzi anabadilisha mbinu ya uwasilishaji kutoka kwa mawasiliano kupitia kwa mazungumzo ya moja kwa moja kwenda kwa uwasilishaji wa tamthilia yake kupitia kwa mbinu ya ushairi wa dondoo la hapa juu. Ushairi pia ni

utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi ambao msanii ameutumia kiubunifu katika kuwasilisha ujumbe wake. Mtunzi, kupitia kwa mhusika Juma, katika kifungu cha ushairi wa hapo juu anafafanua jinsi Waafrika wanawabagua na kuwanyanyasa Waafrika wenzao kwa manufaa yao ya kinafiki. Waafrika hawajithamini wenyewe. Mhusika Juma anajaribu kusawiri hali hiyo kimafumbo kupitia kwa shairi lake la hapa juu anapoghani kwamba, "**Bibi anapuliza sumu. Sumu au mapenzi? Jaribu kupambanua,** (*Mashetani – uk 42)***.*** Hii ndiyo sababu wanabaguana hata katika mikahawa na kutamani kuwahudumia Wazungu na matajiri wanaotoa bahashishi. Kupitia kwa kifungu hicho vilevile, inadhihirika kwamba Waafrika hawafanyi bidii kujitosheleza wenyewe bali huwangoja matajiri wawape misaada inayokuja kama "tip" baada ya kutoa huduma ambayo ni jukumu lao.

### 6.1.4 Taswira ya Utabaka katika Jazanda za Ugonjwa wa Kitaru na Kumea Manyoya

Suala la utabaka linachipuka wakati familia ya Kitaru iko nyumbani kwao wakingoja chakula cha jioni na kuzungumzia kuhusu kilichokuwa kinamfikirisha Kitaru. Wakati huo Kitaru alikuwa anafikiria sana kiasi kwamba alikuwa na wasiwasi mwingi uliomfanya kuonekana kuwa mgonjwa. Baba Kitaru alibadilisha mazungumzo na kuuliza kuhusu asili ya familia ya Juma ambaye ni rafiki yake Kitaru **(*anajaribu kubadilisha mazungumzo*) Rafiki yako Juma anatoka wapi?** (*Mashetani – Uk 26*). Kitaru mwenyewe anawaeleza Baba na Mama yake kuwa Juma alitoka katika familia iliyokuwa tajiri kabla ya uhuru na ambayo ilikuwa maskini wakati wa uhuru wa nchi yake. Kwamba, kwa sababu mali ya familia ya Juma ilitaifishwa na nchi yake baada ya kujinyakulia uhuru, walikuwa maskini na hali yao ilikuwa inaendelea kudidimia, "**Wazee wake walikuwa wana mashamba ya karafuu. Lakini baada ya mapinduzi serikali ikayachukua."** Mazungumzo yao yanafanyika hivi:

BABA: (*anajaribu kubadilisha mazungumzo*) **Rafiki yako Juma anatoka wapi?** Ninafahamu anatoka Unguja. Lakini wapi? Sehemu gani? Wazee wake walikuwa wanafanya nini huko?

KITARU: **Wazee wake walikuwa wana mashamba ya karafuu. Lakini baada ya mapinduzi serikali ikayachukua.**

BABA: **Kumbe ndio waliokuwa mabwanyenye hawa! Loo! Salale si ajabu babu yake alikuwa na watumwa. Loo!** (*Mcheko wa nguvu. Kitaru anakurupuka anaondoka. Baba na mama wanatazamana. Anapoondoka Kitaru mcheko unapungua pole pole hausikilikani tena. Punde mama anaondoka anamtafuta Kitaru. Baada ya muda anarudi.*) Je ana nini? Kama mgonjwa tumpeleke hospitali. (*Mashetani – Uk 26*)

Ukoloni uliwezesha watu wachache waliokuwa uongozini kujilimbikizia mali katika mfumo wa ubwanyenye uliokuwepo katika jamii. Watu wachache walimiliki vitega uchumi na watu wengi walikuwa watumwa katika nchi yao na hivyo kukosa usawa wa kiuchumi, kijamii na kisiasa katika jamii yao. Mfumo huu wa kijamii ulisababisha kuwepo na matabaka mawili; tabaka la mabwanyenye, yaani matajiri ambao pia walikuwa watawala wa jamii hiyo na tabaka la watwana, maskini lililojumuisha watumwa na wafanyakazi waliokuwa wengi. Tabaka la mabwanyenye lilinyang'anywa mali yao baada ya nchi kunyakua uhuru wa kujitawala kutoka kwa wakoloni ambapo mali hiyo ilitaifishwa na utawala wa nchi. Juma alikuwa anatoka katika familia kama hiyo na Baba Kitaru anatahamaki na kueleza hivi kuihusu familia hiyo, "**Kumbe ndio waliokuwa mabwanyenye hawa! Loo! Salale si ajabu babu yake alikuwa na watumwa" –** (*Mashetani – uk 26).*

Awali ugonjwa wa Kitaru katika tamthilia ya Mashetani ulielezwa na wale waliokuja kumtibu kuwa ugonjwa wa Mashetani, mizuka, wasiwasi, machovu ya akili au kuendekeza akili. Ugonjwa huu ni jazanda inayoashiria mgongano wa nafsi zake mbili zinazokinzana. Hali yake inamwingiza katika mtafaruku wa akili na kumfanya awe na fikra zinazogongana na kuzozana. Ugonjwa wa Kitaru ni fikira alizonazo kuhusu vile anavyoweza kutoka katika hali ya ukabaila ili aweze kujenga uhusiano

mwema na watu wa tabaka lingine. Ugonjwa wa Kitaru katika tamthilia ya *Mashetani* unakusudiwa kuangazia shida zinazozisumbua jamii za nchi za ulimwengu wa tatu na nchi za bara la Afrika zikiwemo zinazowakilishwa na jamii ya Mashetani kwani ugonjwa wenyewe unatokana na mifumo ya kibepari inayoifunga jamii yake. Kitaru anasumbuliwa na fikra nzito ambazo zinaitatiza hadhira kama inavyoonyeshwa hapa chini:

> *Nyumbani kwa Kitaru. Kitaru anafikiri yuko peke yake. Muda mama yake anaingia.*
> MAMA: Kitaru. (*Kimya*)
> KITARU: (*Anashtuka)*. Naam.
> MAMA: **Mbona umeshika tama baba**.
> KITARU: Hata. Hapana kitu.
> BABA: Unaumwa? *(Mashetani - Uk - 27*)

Ugonjwa wa Kitaru ni wa kijazanda kwani inavyodhihirishwa na mtunzi, Kitaru yuko mbioni kujaribu kuelewa ubepari uliopo katika jamii yake. Aidha, Kitaru anataka kuelewa ukweli kuhusu asili ya tofauti za kiuchumi, kijamii na kisiasa baina ya tabaka la maskini na lile la matajiri sababu inayomfanya kuwa na wasiwasi mpaka mamake anamuuliza, "**Mbona umeshika tama baba?**" - (*Mashetani* - 27). Kitaru anajaribu kufikiria jinsi anavyoweza kutoka katika hali ya ukabaila na kujenga uhusiano ulio na usawa. Kwa kurejelea hadithi waliyosimuliwa na bibi yake Juma akiwa na Juma, Kitaru anazua taswira ya tabaka lenye nguvu linalonyanyasa tabaka lisilokuwa na nguvu kwa uwezo wake mkubwa. Kitaru anamweleza mama yake hivi:

> KITARU: Nilikuwa nafikiri tu … Nilikuwa nafikiri hadithi
> MAMA: Hadithi! Hadithi gani?
> KITARU: **Hadithi ya chewa**. Mbali sana, **ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa**. **Chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake. Anaweza kutoka huko aliko, kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa tu na mkondo wa maji, ikitaka isitake**. Na huyu chewa siyo chewa bali Shetani. *(Mashetani - uk 28*).

Kwa kumsimulia mama yake **hadithi ya chewa -** *(Mashetani - uk 28)*, Kitaru anaonyesha kwamba anaelewa kuwa kuna kasoro katika mfumo wa jamii yake inayosababishwa na kuweko kwa nguvu za nje zinazosababishia nchi za Afrika matatizo, "**ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa"**. Hizi ni nguvu za kikoloni zinazozidhibiti nchi za ulimwengu wa tatu zisiweze kujisimamia. Nguvu hizo ndizo huamua mkondo wa kisiasa na kiuchumi katika nchi za ulimwengu wa tatu ambazo ingawa zilijinyakulia uhuru, uhuru wao ulikuwa wa bendera tu na haziwezi kujiamlia zifanye nini zenyewe kwa ajili ya maendeleo yao ya ndani, "**Chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake. Anaweza kutoka huko aliko, kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa tu na mkondo wa maji, ikitaka isitake,"** *(Mashetani* - uk 28). Kitaru vilevile anaelewa kwamba nchi bepari za Magharibi huonea na kunyanyasa nchi changa za ulimwengu wa tatu kwa kuingilia njia zao za uzalishaji mali na ugavi wa mali ya nchi hizo. Mtunzi ametumia usimulizi wa hadithi ya chewa kwa njia ya kijazanda ili kuelezea kwa kumithilisha hali halisi ya ukoloni mamboleo unaozikumba nchi za ulimwengu wa tatu. Ugonjwa wa Kitaru vilevile ni jazanda ya matatizo yanayozikumba nchi changa za Kiafrika na ulimwengu wa tatu yanayosababishwa na kuweko kwa ukoloni mamboleo huo.

Baada ya kutambua kwamba nchi za ulimwengu wa tatu zimekumbwa na matatizo yanayosababishwa na ukoloni mamboleo, Kitaru anajifungia ndani kufikiria na kujisaka ili aweze kuelewa asili ya matatizo yao na uhusiano kati ya nchi yake na nchi wanazohusiana nazo za Kimagharibi; uhusiano kati ya matajiri na maskini ulivyokuja na kama wanaweza kuenda pamoja. Hali ya kujifungia chumbani kufikiria na kujisaka kunafanya wazazi kufikiria kwamba Kitaru amekuwa mgonjwa na kumwita daktari ili aweze kumtibu:

> KITARU: **… Nikawa najiuliza na kufikiri. Wazee wangu wakamwita daktari. Naye daktari ana manyoya kama sisi; tena mengi zaidi …** (*Mashetani - uk 49*)

Ebrahim Hussein anatumia taswira ya ugonjwa wa Kitaru na daktari wa kumtibu ugonjwa wa kufikiria sana kujenga taswira ya matatizo yanayoletwa na hali ya utabaka na ukoloni mamboleo. Matatizo ya nchi za Afrika kwa mujibu wa fikra mbaya zinazomsumbua Kitaru ni ya kiuchumi, kijamii na kisiasa yaliyosababishwa na nchi za kigeni. Wazazi wa Kitaru wanamletea daktari wa kumwondosha hizo "fikra mbaya" kwa maoni yao kama Kitaru anavyoeleza, "**… Nikawa najiuliza na kufikiri. Wazee wangu wakamwita daktari"**. Kitaru anataka kuwe na usawa wa kijamii na kuondoa ukandamizaji na utabaka uliodhihirika katika hadithi ya chewa. Daktari wake wa kigeni ameletwa kwake ili amfanye awache kufikiria kuhusu matatizo ya jamii yake na asili ya matatizo hayo. Huyu alikuwa daktari wa kigeni anayekomesha fikra razini zinazokomboa wanaokwamizwa na mifumo mibaya ya uzalishaji mali na kuukomesha mwamko wa kisiasa usiotangamana na mifumo ya kibepari ya utawala kama Kitaru anavyoeleza, "**Naye daktari ana manyoya kama sisi; tena mengi zaidi …"**. Wazazi wanamwita daktari ampime na kumtibu Kitaru lakini daktari haoni kitu. Kwa sababu hiyo, daktari anatoa kisababu ambacho hakifai kueleza hali ya mgonjwa Kitaru:

> Daktari: Ugonjwa huu, **ninavyofikiria mimi** … kwa kweli, **pengine nikuchoka kwa akili tu**. Watoto wa chuo kikuu bwana, wana mengi wanayoyasoma na kuyafikiri. Pengine amepata, labda *neurosis*. (*Mashetani – uk 33. Msisitizo ni wetu.*)

Daktari aliyeletwa kumtibu Kitaru hana maarifa ya kutosha ya kumtibu kwa jinsi anavyodhania na kusema, "ninavyofikiria … pengine ni kuchoka kwa akili tu." Ukweli ni kwamba ugonjwa wa Kitaru haupo katika mwili wake bali katika mawazo yake na daktari hana maarifa ya kuona ugonjwa wa mawazo. Daktari haelewi ugonjwa kama huo na hivyo hana tiba yake. Kama Shetani anayesimuliwa katika

tamthilia, daktari na wazazi wa Kitaru hawawezi kuuelewa ugonjwa wa Kitaru kwani wote wana tatizo linalofanana. Katika kueleza tatizo hilo lao, mtunzi anamfanya Kitaru kupitia kwa ndoto au kwa fikira tu kumwona daktari akiwa ameota manyoya mengi sawa na wazazi wake. Kitaru anamweleza rafiki Juma hivi kuhusu ndoto hiyo katika dondoo lifuatalo katika Onyesho la 1 Sehemu ya IV:

> KITARU: … Sasa sijui saa ngapi nimelala. Lakini mara ninaona nina manyoya. Mimi nimeota manyoya, mzee ameota manyoya, kila mtu na kila kitu kimeota manyoya. … **Mara manyoya yakageuka mbawa: tukawa tunarushwa angani. Kwanza ilikuwa raha. … Mbawa zinaturusha zinapotaka. Vitu vinaruka angani – majumba, magari** na sisi …, nikaanza kuwa na hofu. Nikaanza kujinyonyoa manyoya yangu. Lakini kila nikijinyonyoa, mengine yanaota. … Makubwa zaidi na yenye nguvu zaidi kuliko yale. Nikaanza kuingiwa na shaka … Mimi Binadamu au ndege. Nikawa najiuliza na kufikiri. Wazee wangu wakamwita daktari. Naye daktari ana manyoya kama sisi; ke mengi zaidi, Basi akaniambia ninadekeza akili yangu. Na nikiendelea kuwa na shaka kama hii nitakuwa na kiarusi. Basi lile neno kiarusi likanitengua nguvu. Nikajiona naanguka chini … Mara nikafanya azimio lazima nitoke katika shaka hii. … nikaazimia lazima nitoke katika ugonjwa huu. … imechukua muda mrefu kutambua kuwa niliyo nikiyaona siyo ndoto au fikira mbovu, bali ni ukweli wa kawaida. (*Mashetani – kr. 48 - 49. Msisitizo ni wetu*)

Baada ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru, viongozi walioingia mamlakani walinyakua mali ya nchi kwa njia ambazo si halali. Watu hao wakaanza kupaa angani kama ndege kwa kutajirika kimiujiza kwa kujilimbikizia mali ya umma na kuishi maisha ya ubadhirifu na anasa, mambo ambayo Kitaru aliyaona katika ndoto yake; "**Mara manyoya yakageuka mbawa: tukawa tunarushwa angani. Kwanza ilikuwa raha. … Mbawa zinaturusha zinapotaka. Vitu vinaruka angani – majumba, magari," -** *(Mashetani - uk 49***).** Ni mabadiliko haya ya ghafla ya kijamii kwa watu wachache ambayo Kitaru alikuwa akiyafikiria na kuyaona katika ndoto

yanayompatia wasiwasi. Kitaru anafikiria namna ya kuleta usawa wa kijamii na kuondoa utabaka katika nchi za Kiafrika. Hii ndiyo sababu daktari aliyeletwa na wazazi wake kuja kumtibu Kitaru alihitaji kumfanya Kitaru asiuonyeshe mwamko wa kisiasa usiotangamana na matakwa ya watawala. Daktari ni mtaalamu wa tabaka la watawala, wazazi wa Kitaru na Wazungu wanaozitawala nchi za ulimwengu wa tatu kwa njia ya ukoloni mamboleo (**wote wana manyoya**). Watu hao hawapendi kuona mabadiliko katika mfumo wa jamii yao. Wasiwasi wa Kitaru ndio ulioifanya nchi ya Tanzania kupitisha azimio la Arusha katika mwaka 1967, kwa sababu wataalamu kama daktari hawakuelewa suluhisho la matatizo ya nchi za Afrika.

### 6.1.5 Taswira ya Suluhisho la Matatizo ya Nchi za Afrika katika Motifu ya Safari

Taswira ya suluhisho la matatizo ya nchi za Afrika inajengwa kupitia kwa usimulizi nafsi wa mhusika Binadamu anayefafanua kwamba, nchi za Afrika zinahitaji kuisaka historia yao na kuelewa asili ya matatizo yao. Baada ya kujinyakulia uhuru, nchi za Afrika zilimlaani mkoloni kwa matatizo yaliyokuwa yanazikumba. Hata hivyo, baadaye nchi hizi zilitambua kuwa matatizo yao yalitokana na kukosa kupanga na kuweka sera kabambe za kuwawezesha kwenda mbele. Nchi ya Tanzania kwa mfano ilipitisha Azimio la Arusha mwaka wa 1967 ili kuanza kupiga sogi maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii (Njogu na Chimera 1999). Mhusika Binadamu anayewakilisha Waafrika baada ya uhuru anasema hivi:

> BINADAMU: Kosa limefanyika. **Sasa lililobaki ni azimio: kosa hili halifanyiki tena** … nina haja na vitu vitatu … **bidii, ari na ukweli**. … Kuna lile lipaswalo kufanywa, na yule apasaye kulifanya. Kuna kitendo na mtendaji … mtendaji ni nani. (*Mashetani - Kr 11 – 12*)

Baada ya kutambua kuwa kosa limefanyika, Watanzania waliazimia kuutafuta ukweli ili kosa lisifanyike tena. Azimio la Arusha linakuwa mwamko wa safari ndefu ya

kujitafuta na kujisaka ili mwafrika ajijue yeye mwenyewe na kuelewa historia yake ili aweze kulifanikisha azimio hilo (**Sasa lililobaki ni azimio: kosa hili halifanyiki tena)**. Ni lazima nchi za Afrika zianze kuelewa historia ya taifa lao na maana ya uhuru walioupata kutoka kwa wakoloni ambao kama asemavyo Binadamu; **unahitaji bidii, ari na ukweli** na Mwafrika anapaswa kutambua na kuelewa wajibu wake na analopaswa kulifanya ili kuendeleza uhuru wa nchi yake. Binadamu anaeleza hivi:

> BINADAMU: **Mimi ni nani? Mimi-mimi au yeye-mimi anayetaka kuitekeleza azimio hili**? (*Mashetani - uk 12*)

Waafrika wanafaa kujitofautisha kutoka kwa wakoloni waliowatawala wakati wa ukoloni na wanaodai kwamba wanasaidia nchi za Afrika kujitegemea. Wanafaa kujiuliza maswali ili kujisaka kama afanyavyo mhusika Binadamu; "**Mimi ni nani? Mimi-mimi au yeye-mimi anayetaka kuitekeleza azimio hili"**. Waafrika wanahitaji kujielewa wao ni nani na historia ya mataifa yao ili kuelewa maana ya uhuru na namna ya kuulinda uhuru wao. Kujielewa na kuelewa maana ya uhuru wa Mwafrika ni suala la kufanya safari ndefu kama asemavyo Binadamu:

> BINADAMU: **Lazima nisafiri, safari ndefu, nikajitafute, nikajisake ili nijijue mimi nani?** Ili nijue maana ya kitendo changu. (*Mashetani – uk 12*)

Binadamu anabadilika na kuwa mhusika Kitaru baada ya kujiuliza maswali katika dondoo la hapa juu, **"Lazima nisafiri, safari ndefu, nikajitafute, nikajisake ili nijijue mimi nani?"** Katika kujisaka, Kitaru anajifungia ndani ili kupekua historia ya jamii yake kwa kusoma vitabu vya historia ya jamii yake kama *Outline of African History*. Ni katika usomaji wake, ambapo Kitaru anatambua kwamba baada ya mapinduzi ya 1964 nchini Tanzania, mali ya mabwanyenye wakati wa ukoloni yalitaifishwa na kizazi kipya kinachowakilishwa na baba yake kikayanyakua mali hayo. Asili ya matatizo ya nchi za ulimwengu wa tatu na watu wake wa tabaka la chini, yanatokana na tamaa ya watu katika uongozi wa nchi kujilimbikizia mali ya

umma kwa kununua magari ya thamani kubwa, kunyakua pesa za umma, kuwaoa wanawake wengi na kufanya anasa nyingine afanyavyo Baba Kitaru. Safari ya kujisaka kwa wananchi wa kawaida wa Afrika inaonyesha kuwa hali yao mbaya ya umaskini imesababishwa na ukoloni mamboleo.

Mhusika Kitaru, vilevile, anabaini kwamba mataifa ya Kiafrika yamefungamanishwa kiuchumi, kisiasa na kijamii na mataifa ya wakoloni ambao wanaendeleza ukoloni mamboleo kupitia kwa mfumo wa utandawazi. Kwamba ingawa Waafrika wanaazimia kujisimamia na kujitegemea, jahazi lao haliwezi kuchukua mkondo wanaoutaka kama Waafrika kwani kuna nahodha mwingine mwenye nguvu (Shetani) anayeliongoza kwingine, ambaye ni mkoloni mamboleo (King'ei, 1987). Nguvu za ukoloni zinaendelea kuwatenganisha matajiri na maskini. Mhusika Mfaume anasisitiza ukweli huu katika mazungumzo yake na Kitaru:

> MFAUME: … **Juzi hapa, dereva mmoja bwana … Mara peke yake** bwana **kachepuka njia akenda kulilaza basi miguu juu chini**. Kaulizwa, **kwani kasema nini? Kasema, 'Shetani, kazi ya Shetani,' Kaona njia mbili … Mashetani wapo** … lakini tumezibwa macho tu, hatuwaoni *(Mashetani – uk 29)*

Matatizo ya nchi za Afrika yanasababishwa na nchi nyingine zenye uwezo mkubwa (uwezo wa **Mashetani**) unaobadilisha mkondo wanaoazimia kuuchukua. Kama asemavyo mhusika Mfaume katika tamthilia ya *Mashetani* na Mhusika Prof. katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, mkoloni mkongwe bado yuko, (**Mashetani wapo)** na anaendelea kuliendesha upogo jahazi la nchi za Afrika. Viongozi wa Afrika kama dereva wa basi aliyelilaza chini basi alilokuwa akiliendesha baada ya kukosa njia na kudai kuwa hiyo ilikuwa kazi ya Shetani katika dondoo la hapo juu, pia wameangusha, kukwamisha na kuuendesha upogo uchumi, siasa na utawala wa nchi za Afrika kwa sababu ya athari mbaya ya wakoloni wanaoziangusha nchi za Afrika. Mfaume anaeleza hivi katika dondoo; "**Juzi hapa, dereva mmoja bwana … Mara**

**peke yake** … **kachepuka njia akenda kulilaza basi miguu juu chini** …. **kwani kasema nini? Kasema, 'Shetani, kazi ya Shetani,' Kaona njia mbili … Mashetani wapo", -** (*Mashetani* - uk 29**).** Wakoloni kama Mashetani bado wako katika bara la Afrika na wanaendelea kukwamiza maendeleo ya nchi za Afrika na kujitegemea kwao.

## 6.2 Taswira ya Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Tamthilia ya *Pungwa* – Said A. Mohamed

Utafiti wetu katika sehemu hii ulichunguza matumizi ya tanzu za masimulizi ya kingano, ndoto, majigambo na Sauti ya Mzuka ambazo ni tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa mahoka na pungwa wa Kiafrika katika kuibua taswira zinazojenga dhamira katika tamthilia ya *Pungwa* kwa mujibu wa lengo letu la pili la utafiti huu. Katika usomaji wetu wa awali, ilikuwa imebainika kwamba matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika yametawala tangu mwanzo hadi mwisho wa tamthilia hiyo na kwamba tanzu hizo zimetumiwa kuibua taswira mbalimbali zinazojenga dhamira mbalimbali za mtunzi Said A. Mohamed katika tamthilia ya *Pungwa*.

### 6.2.1 Taswira ya Ukoloni Mamboleo katika Majigambo ya Sauti ya Mzuka

Tamthilia nzima ya *Pungwa* imewasilishwa kwa muhtasari kupitia kwa utanzu wa jigambo moja la mhusika Sauti ya Mzuka. Majigambo ni utanzu wa kishairi katika sanaa za maonyesho ambao hutumiwa na fanani ambaye aghalabu huwa mwanamume ambaye hujigamba na kujitapa kuhusu matukio ya kishujaa aliyofanikiwa kuyatenda. Mtunzi, kupitia kwa jigambo hili anadhamiria kusimulia historia ya utawala wa nchi za Afrika na ulimwengu wa tatu tangia ukoloni mkongwe hadi kipindi cha sasa cha kutawaliwa na nchi za Magharibi katika utawala wa ukoloni mamboleo ambao Said A. Mohamed katika tamthilia yake nyingine ya *Mashetani Wamerudi* anaurejelea kwa

jina utandawazi. Mtunzi anaanza kwa kushangaa ni kwa mara ngapi mataifa ya Afrika na nchi za ulimwengu wa tatu kwa jumla zitatawaliwa na nchi zilizoendelea za ulimwengu wa kwanza. Afrika ilitawaliwa kikoloni hapo awali na Wazungu kutoka nchi za Magharibi. Mara ya pili ambayo ni wakati wa sasa nchi za Afrika zimetawaliwa kiukoloni mamboleo na nchi kutoka Magharibi. Pia, mtunzi anahofia kwamba huenda Afrika na nchi nyingine za ulimwengu wa tatu zikatawaliwa tena kwa mara ya tatu kwa njia nyingine katika siku zijazo. Mtunzi Said A. Mohamed kupitia kwa sauti ya kuogofya ya Mzuka inaeleza hivi katika chanzio cha tamthilia yake:

> SAUTI YA MZUKA …
> … Mara ngapi shahada …
> Shahada mara ngapi?
> Moja?
> Mbili?
> Au tatu? (*Pungwa - uk 1)*

Wazungu walitoka kwao ng'ambo wakavuka bahari nyingi ili kufika katika bara la Afrika na kudai kuwa bara la Afrika lilihitaji kugawanya katika nchi ndogondogo ili liweze kutawaliwa na Wazungu kwa sababu kwa madai ya nchi hizo, nchi za Afrika zilikosa miundo misingi ya kiuchumi, kisiasa, kiutawala na uongozi. Mhusika Shetani katika tamthilia ya *Mashetani* anaeleza ya kwamba Wazungu walikuja Afrika ili kuzisaidia nchi za Afrika "**kuondoka kwenye tumbo la giza jeusi na kuingia katika ulimwengu wa nuru nyeupe,**" (*Mashetani* – uk 4). Akimtambua mtawala dhalimu huyo aliyejipa mamlaka ya kuwatawala na kuwahangaisha Waafrika, mtunzi anaonyesha jinsi Mzungu mkoloni anavyojitapa katika utanzu wa jadi wa sanaa za maonyesho wa jigambo hilo kwa njia ifuatayo:

> …
> **Mimi ndiye mimi**
> **Mpiga mbizi**
> Mpiga-mbizi pasi ukomo wa pima
> Huzamia kuliko mkizi
> Wa kufika kusikofikwa – vina vya ajabu

> Mimi mzuka wa bahari saba na mgaagaa fukwe saba
> Mhodhi wa miamba saba, mkwepa mawimbi saba … (*Mashetani – uk 1. Msisitizo ni wetu*)

Mtawala wa kikoloni mamboleo ni nchi za Kimagharibi ambazo zimeabiri meli kutoka ng'ambo na kuvuka bahari nyingi ili kufika Afrika jinsi Said A. Mohamed anavyosema katika dondoo la majigambo la hapa juu. Mkoloni mamboleo ni mgeni kwa nchi za Afrika na nchi za ulimwengu wa tatu ambaye alikuwepo wakati wa ukoloni mkongwe na ambaye ameselelea Afrika na hivyo bado yuko sasa katika mfumo mpya wa udhalimu na unyonyaji wa ukoloni mamboleo na utandawazi. Akijitambulisha katika dondoo, mkoloni anasisitiza kuwa ni yeye aliyepiga mbizi kutoka ng'ambo – **Mimi ndiye mimi, Mpiga mbizi** (*Mashetani* – uk 1)**.** Kimwingilianomatini, Ebrahim Hussein vilevile alikuwa ametumia utanzu wa majigambo katika kumfafanua mkoloni ni nani katika tamthilia yake ya *Mashetani*. Ebrahim Hussein anaeleza hivi kupitia kwa jigambo la mhusika Shetani:

> SHETANI: Unanijua mimi nani?
> Mimi Shetani.
> Siyo jini wala kuhani,
> Mimi Shetani.
> Uwezo wangu hauhifadhiki.
> Wema wangu hauhisabiki.
> Ubaya wangu hausemeki.
> Ninajenga.
> Ninabomoa.
> Ninatukuza.
> Ninadhalilisha nitakavyo.
> Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi.
> Mimi ni uwezo na uwezo ni mimi.
> (*Mashetani – kr 1 – 2*)

Mkoloni kama wasemavyo Ebrahim Hussein na Said A. Mohamed katika madondoo ya majigambo ya hapo juu ni Shetani mwenye uwezo mkubwa unaoangamiza na usiokuwa na kifani wa kuzidhulumu na kuziangamiza nchi maskini za Afrika. Neno "Shetani" limetumiwa na Said A. Mohamed kijazanda ili kurejelea Mzungu mkoloni aliyeligawa na kulitawala bara la Afrika kwa mabavu. Mkoloni alizinyemelea nchi za

Afrika na kuzinyakua kiujanja na kuzifanya tawala zake. Wakoloni hawa walikuwepo wakati wa ukoloni mkongwe na bado wako wakati wa sasa wa ukoloni mamboleo. Mkoloni mkongwe amerudi tena Afrika kuzitawala nchi za Afrika kupitia kwa kuwateka na kuwatawala viongozi wa nchi za Afrika kwa kuwafanya vikaragosi wake wa kutekeleza majukumu yake ya ukoloni mamboleo. Bwana anaeleza hivi:

> BWANA: Sina Shetani. Mimi mwenyewe Shetani. Mimi mwenyewe pepo. Mimi mzuka (*Pungwa - uk 13*).

Waandishi wote wamemrejelea mkoloni kwa majina "Shetani, pepo au jini" ila Said A. Mohamed amemwongeza jina "Jogoo." Utanzu wa shairi huru la Mhusika Sauti kali ya kuogofya na ya mhusika Mzuka vilevile unasisitiza kuwa mkoloni ni mzuka, jini na pepo aliye na nguvu za kiajabu kama inavyodhihirika katika dondoo lifuatalo:

> SAUTI YA MZUKA: Mimi **mzuka** wa wazuka,
> Mimi **pepo** wa pepo,
> Mimi **jini** wa majini,
> Mimi wa ardhini na wa baharini,
> Mimi niwezaye ruka angani,
> Mimi niwezaye tua ardhini,
> Mimi niwezaye kupasua ardhi na kuzama na kuibuka …
> (*Pungwa - uk - 4)*

Shairi huru la jigambo la mhusika Sauti ya Mzuka katika dondoo la hapa juu ni msisitizo na ufafanuzi wa Shetani ni nani. Mwandishi anatumia maneno tofautitofauti kama "**pepo, jini, Shetani** na **mzuka"** kusisitiza dhana ya Shetani. Neno "mimi" vilevile limerudiwarudiwa ili kutia mkazo kuhusu mhusika anayezungumziwa. Majina yote yaliyotumiwa kumweleza Shetani ni nani yana sifa za ubaya uliokithiri. Ni dhamira na msimamo wa mtunzi kumwonyesha mkoloni (Shetani) kuwa kiumbe mbaya ambaye ni hatari kwa Waafrika. Sifa zote alizolimbikiziwa mkoloni zinamdhihirisha kuwa kiumbe laghai kinachodhulumu na kuwanyonya wanyonge. Kama njia ya kutaka kuwahamasisha Waafrika wasiojua kuhusu mkoloni ni nani, mtunzi anaeleza kuwa Shetani mwenyewe ni yule Mzungu aliyehama kutoka kwao

katika nchi za Magharibi kuja kuwadhulumu Waafrika katika miliki yao. Wao ni wanyonyaji wanaowalaghai Waafrika na watu wa nchi za ulimwengu wa tatu.

Mtunzi anatueleza vilevile kuwa mkoloni alikuwepo wakati wa ukoloni, amejigeuza na sasa yuko katika umbo jipya la ukoloni mamboleo na atakuwepo siku zijazo labda katika mfumo tofauti. Ingawa haonekani, mkoloni yupo na yupo hata kama hatumhisi asemavyo katika jigambo kwamba, "**Na kwamba hamnioni, si kama sipo, Najigeuza nitakavyo … Pengine ni miongoni mwenu, ndani ya damu yenu**" (*Pungwa* - uk 2). Katika mbinu ya Kimwingilianomatini, Said A. Mohamed anazua taswira ambayo ilikuwa imezuliwa na Ebrahim Hussein ya mchezo wa Shetani na Binadamu ya Shetani kujigeuzageuza kama jini na kuwa vitu mbalimbali katika Sehemu ya Kwanza, Onyesho la Kwanza la tamthilia ya *Mashetani,* ambapo Hussein anaandika ifuatavyo:

> SHETANI: …
> Ninadhalilisha nitakavyo,
> Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi,
> Mimi ni uwezo na uwezo ni mimi,
> Tazama muujiza. (*anajibadilisha*) sasa mimi nani?
> BINADAMU: Kama ndege … vile … ndege.
> SHETANI: Sawa. Nimejigeuza ndege. Ninaweza kadhalika kuwa upepo, nikawa kila mahali. Naweza kuwa nafsi, nikaingia katika roho yako au ya wenzako. Sasa tazama. Unaona nini?
> BINADAMU: Unarukia tawi.
> SHETANI: Na sasa, unaona tawi?
> BINADAMU: Tawi limegeuka kiti!
> SHETANI: Umeshuhudia miujiza. Nimekuonesha miujiza ili uamini uwezo wangu. … *Mashetani - uk 2*).

Said A. Mohamed vilevile ametumia imani za kiuchawi za pungwa ili kuelezea kitaswira mbinu za mkoloni kujibadilisha anapokuja Afrika na athari yake kwa Mwafrika wakati wa mahusiano yao hasa wakati huu wa ukoloni mamboleo. Mahoka ambaye ni mganga anapojaribu kumwagua mhusika Bwana ili kufahamu ugonjwa wake katika sehemu ya pili ya tamthilia ya *Pungwa* anamwona kama aliyekumbwa

na pepo mkubwa zaidi aliyetoka ng'ambo ughaibuni. Pepo huyu mgeni aliyevuka bahari saba kama asemavyo mtunzi, ametumiwa kijazanda na mtunzi kurejelea Wazungu wakoloni waliokuja Afrika kuzitawala nchi za Afrika na nchi zingine za ulimwengu wa tatu. Baada ya kumtazama kwa kusoma katika kitabu chake kidogo katika tamaduni na mbinu za Kiafrika za pungwa za kumwagua mgonjwa, Mahoka anasema hivi kumhusu mhusika Bwana aliyekuwa amepandwa na pepo:

> MAHOKA: (*Anatoa kitabu kidogo mfukoni. Anasoma kidogokidogo kwa kumung'unya midomo*). Mumeo kwa n'navyomwona amekumbwa na pepo mkubwa. lililovuka bahari kuja kumdhili na kumnyanyasa yeye na watu wake. Pepo lililovuka bahari kuja huku kumdhili na kumnyanyasa yeye na watu wake.
> BIBIYE: Mbona pepo huyu hawapandi watu wengine?
> MAHOKA: **Yeye ndiye kiti chake ati. Ana kiaga kwake; ana deni kwake; ana makubaliano … na mumeo sasa anapata tabu, kwani ahadi hiyo inamsimanga katika hali ngumu iliyopo sasa. Isitoshe watu wake wanamsumbua mumeo awache kumridhi pepo huyo, lakini hawezi.** (*Pungwa* – kr 14 -15. *Msisitizo ni wetu*)

Kama asemavyo Abdallah Ali (k.h.j.) pepo husemwa kuwa wametokana na mababu waliokwisha kufa na hivyo hufufuka tena kuja kuwaadhibu wale walio hai wanapovunja miiko walioweka nao. Baada ya mababu kufa, wanafufuka tena na kuibuka wakiwa wamegeuka na kuwa na nafsi mbaya inayodhuru. Kuondoka kwa mkoloni mkongwe na nchi za Afrika kujinyakulia uhuru, kunamithilishwa na kifo cha mababu ambao wanazikwa na kuondoka baada ya kifo chao. Mkoloni kuondoka Afrika na kurudi kwao Ulaya kunachowakilishwa kitaswira na kifo cha mhusika Shetani ambapo nchi za Afrika zilijishindia uhuru wao. Wakoloni hao kama pepo katika tamaduni za Kiafrika "wanafufuka" tena wakiwa wamejibadilisha kimiujiza na kuwa pepo na kurudi Afrika wakiwa wabaya zaidi ambapo wanawapanda viongozi vichwa. Viongozi wa nchi za Afrika waliowakaribisha kwa njia ya biashara, mawasiliano, uhawilishaji wa pesa na njia zingine wameweka miadi nao ambayo

imewafunga kwao. Hii inafanya pepo kuwafanya viongozi kuwa watu wao wa kupanda vichwa na viti vyao vya kukalia wafanyavyo pepo. Mahoka katika dondoo hili anafafanua kwa kusema kwamba, **Yeye ndiye kiti chake ati. Ana kiaga kwake; ana deni kwake; ana makubaliano … na mumeo sasa anapata tabu, kwani ahadi hiyo inamsimanga katika hali ngumu iliyopo sasa. Isitoshe watu wake wanamsumbua mumeo awache kumridhi pepo huyo, lakini hawezi** uk 15). Pepo (wakoloni) hao wamewateua viongozi wa Afrika na watu wa nchi zao kuwa viti ambavyo wanavikalia. Baada ya kupanda vichwa vya Waafrika, wanawatesa na kuwaletea madhara kwa sababu ya miadi waliyoweka nao.

Mashetani waliomwingia mhusika Bwana kichwani katika tamthilia ya *Pungwa* na kumsababishia Bibiye dhiki kubwa ya kumshughulikia ni athari ya wasiwasi wa kunyang'anywa uongozi. Tamaa ya uongozi wa Kiafrika kushikilia mamlaka bila kung'atuka hata baada ya wakati wao kuisha au uongozi wao kukosa umaarufu na kukataliwa kidemokrasia, inawafanya viongozi wengi kuwaua kikatili wapinzani wao na kuwaangamiza au kuwaondosha kwa kuwafunga jela wale wote wanaoonyesha dalili ya kupinga sera za uongozi wao kama anavyodhihirisha mhusika Bibiye katika mazungumzo yake na Bwana.

> Bwana: Nambie basi, miaka kumi na nane nyuma, lilitokea tukio gani … ?
> Bibiye: **Ulimdidimiza hasimu yako, akadidimia dididi**!
> Bwana: Kweli, na baada ya miaka mitano?
> Bibiye: **Ulimsagasaga adui yako mkubwa, akasagika sagasaga kama unga**. (*Mashetani Wamerudi - uk 40. Msisitizo ni wetu*)

Watawala wa sasa wa nchi huru za Afrika wanawaua wapinzani wao na kujigamba kuwa wamewadidimiza kama inavyodhihirishwa katika dondoo la hapa juu, "**… ulimdidimiza hasimu ... ulimsagasaga adui**" (*Mashetani Wamerudi* - uk 40). Kwa maelezo ya mhusika Bibiye ambayo yanatoa taswira ya dhuluma na ukandamizaji

unaofanywa na viongozi, wadhalimu wanawanyanyasa na kuwakandamiza kwa kuwapiga na kuwaua watawaliwa wao wa tabaka la chini ili kuwanyamazisha wanapolalamikia unyanyasaji wao.

Ebrahim Hussein ambaye ni miongoni mwa watunzi wa kwanza kabisa wa Kiafrika kutunga tamthilia ya Kiswahili amewaathiri watunzi wa baadaye katika utunzi wao kimuundo, kimtindo na katika maudhui kama inavyodhihirika kwa Said A. Mohamed katika tamthilia zake za *Pungwa* na *Mashetani Wamerudi* na kwa Emmanuel Mbogo katika tamthilia yake ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Kuna ukuruba wa kimuundo na kimtindo katika tungo za watunzi Emmanuel Mbogo na Said A. Mohamed na mbinu za utunzi za mwandishi mkongwe wa tamthilia ya *Mashetani* zinazowafanya kuonekana kuwa wameathiriwa na Hussein. Tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilizochotwa na watunzi hawa na kutumiwa kama malighafi ya utunzi wa kazi zao na dhamira zilizojengwa na tanzu hizo zinadhihirisha mfanano mkubwa usiokuwa wa kiajali bali uliotokana na athari ya kusoma na kutazama sana kazi za Ebrahim Hussein kabla ya kuandika kazi zao. Mbinu za watunzi hao wote zinadhihirisha Mwingilianomatini kati ya kazi zao na ile ya Ebrahim Hussein ya *Mashetani*. Labda ni muhimu kusema kwamba kimwingilianomatini, watunzi Said A. Mohamed na Emmanuel Mbogo wa tamthilia za *Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* wameathiriwa na mbinu za utunzi za Ebrahim Hussein ambaye ni mtunzi wa tamthilia ya awali ya *Mashetani* katika utunzi wao.

### 6.2.2 Taswira ya Utabaka, Unafiki na Uongozi Mbaya katika Ndoto za Bwana

Watawala wa Kiafrika waliochukua hatamu za uongozi punde tu baada ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru walijaa tamaa ya uongozi kiasi kwamba mhusika Bwana katika tamthilia ya *Pungwa* ambaye ni kiwakilishi cha viongozi wa Afrika anaonekana kuwa mwenye wasiwasi anayehofia kupokonywa mamlaka kila mara

kupitia kwa ndoto za kila wakati. Mwandishi Said A. Mohamed anatumia utanzu wa ndoto kisanaa kuwasilisha dhamira ya unafiki na uongozi mbaya katika tamthilia yake. Bwana anaeleza hivi:

> Bwana: **Mimi kila siku naoteshwa ndoto mbaya**
> Sijui mara kuna dhoruba, mara kuna tetemeko
> la ardhi, mara tunagharikishwa, mara … (*Pungwa* – uk 8).

Mhusika Bwana ambaye ni mfano wa kiongozi wa nchi moja huru ya bara la Afrika anaota akinyang'anywa mamlaka ya uongozi kwa kueleza hivi; **Mimi kila siku naoteshwa ndoto mbaya** (*Pungwa* – uk 8). Wasiwasi wa viongozi wa nchi za Afrika kunyang'anywa mamlaka hata katika ndoto wakati wa kulala ni dhihirisho la unafiki unaowasumbua viongozi wa Afrika na nchi zingine za ulimwengu wa tatu kuliko matatizo ya uongozi wenyewe yanayofaa kuwashughulisha wao. Viongozi hao wana wasiwasi kwa sababu wanaelewa kuwa uongozi wao ni mbaya na wanaweza kuondolewa mamlakani na wananchi wanaowaelekeza vibaya.

Wasiwasi wa kuondolewa mamlakani huwasumbua viongozi wa nchi za Afrika kiasi kwamba wanapatwa na magonjwa ya akili. Baada ya kuugua ugonjwa wa wasiwasi wa kupokonywa uongozi, mhusika Bibiye anamtafutia kiongozi Bwana tiba kwa waganga wa kienyeji ambao licha ya kushindwa kumtibu Bwana kwa njia ya kumpunga pepo, wanadai malipo ya juu.

> **Mahoka**: Sisi hufanya wema mara nyingi bila kutarajia malipo,
> lakini kwa maskini wenzetu. Matajiri, ndio matajiri tena,
> lazima mtulipe**. Tena …**
> **Mahoka: Ikipasa mtulipe malipo halali (*Pungwa* – uk 13).**

Kwa mujibu wa Mahoka ambaye ni daktari wa kienyeji anayejaribu kumtibu Bwana katika dondoo la hapa juu, kuna tofauti kubwa kati ya matajiri na maskini. Waganga wa kienyeji huwafaa maskini wenzao kwa kuwatibu bila kutarajia malipo. Hata hivyo anavyoeleza Mahoka, wao hudai malipo kwa matajiri kama mhusika Bwana ambaye

ni kiongozi mtawala anayeugua ugonjwa wa wasiwasi wa kunyang'anywa mamlaka. Madai ya Mahoka yanadhihirisha utabaka kati ya watawala na watawaliwa, "**Sisi hufanya wema … bila kutarajia malipo, lakini kwa maskini wenzetu. Matajiri lazima mtulipe …**" (*Pungwa* – uk 13).

Utatuzi wa matatizo ya nchi za Afrika utakuwa wa gharama ndogo ikiwa Waafrika watatafuta suluhisho la matatizo yao papa hapa nyumbani na utakuwa ghali ikiwa Waafrika wataenda kuwatafuta wataalamu wa nje katika nchi za Magharibi kuja kuyasuluhisha matatizo ya nchi za Afrika. Madai ya Mahoka yanadhihirisha kuwa matatizo ya nchi maskini za Afrika yanafaa kutafutiwa suluhu nyumbani hapa Afrika kwa wataalamu wa kienyeji wanaoelewa matatizo yao wenyewe wala si ng'ambo kwa nchi tajiri za Wazungu ambao wanadai malipo ya juu na kufanya ukombozi wa nchi za Afrika kuwa ghali. Akiongezea dharau na kiburi cha viongozi na watawala wa Afrika kwa wataalamu wa nyumbani kwa kutoshirikiana nao, mhusika Bwana ambaye ni kiwakilishi cha viongozi wa Kiafrika anaeleza hivi kumhusu Mahoka na kundi lake maskini:

> Bwana: **Mahoka hajui hata umaskini wake. Na aende tu mimi mzima. Kwanza mimi na mahoka hatukai baraza** (*Pungwa* - uk 14).

Usemi wa mhusika Bwana katika dondoo la hapa juu unadhihirisha, dharau, kiburi na utabaka katika jamii ya wapungwa unaosababishwa na kiburi cha viongozi na ambao ni dalili ya uongozi wao mbaya. Kiburi cha uongozi wa Kiafrika hauziruhusu nchi hizi kutafuta suluhisho la matatizo yao kwa wataalamu wa nyumbani. Watawala ambao wameiba mali ya umma na kuwa matajiri hawawezi kukaa pamoja na wataalamu maskini katika baraza moja kwa sababu ya tofauti zao za utajiri au umaskini unaoleta tofauti za kimatabaka. Kiongozi huyo katika kiburi chake anajitapa kwa kusema hivi; **Mahoka hajui hata umaskini wake. Na aende tu mimi mzima.**

**Kwanza mimi na mahoka hatukai baraza** (*Pungwa* - uk 14). Mahoka anayerejelewa katika dondoo hili ni mtaalamu wa utamaduni wa Kiafrika wa kufanya pungwa. Mhusika Bwana katika tamthilia ya *Pungwa* ambaye amepandwa kichwa na pepo anahitaji kufanyiwa pungwa na mtaalamu kama Mahoka. Hata hivyo, katika kiburi chake, Bwana anamkataa Mahoka ambaye ni mtaalamu wa kienyeji wa kumtafutia suluhu la tatizo lake. Pamoja na kumkataa Mahoka, Bwana anajitapa kuwa yeye ni tajiri asiyehitaji usaidizi wa maskini kama Mahoka.

## 6.3 Taswira ya Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* – Emmanuel Mbogo

Uchanganuzi wetu katika sehemu hii ulitambua tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika za masimulizi ya kingano, ngoma mbalimbali, majigambo na kufafanua namna zilivyotumiwa kujenga taswira za ukandamizaji, ukoloni mamboleo, unyanyasaji, ukombozi na utabaka katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1999). Ilibainika kwamba, mtunzi Emmanuel Mbogo ametumia tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika katika kuibua taswira zinazojenga dhima mbalimbali katika tamthilia yake. Data tuliyoichunguza katika tamthilia yenyewe na uainishaji wake tulioufanya kwa mujibu wa lengo letu la pili imewasilishwa hapa chini.

### 6.3.1 Taswira ya Ukandamizaji na Ukoloni Mamboleo katika Masimulizi ya Kingano

Tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* inaanza kwa utanzu wa masimulizi ya kisa cha msichana mrembo kwa jina Nyamiti aliyekuwa akikamilisha mipango ya arusi yake na mchumba wake Chibupa kuuawa kwa uchawi wa misukule siku moja tu kabla ya arusi yenyewe. Nyamiti alikuwa peke yake chumbani ambako alikuwa amefungiwa kama ilivyokuwa kawaida ya tamaduni za Kiafrika kwa mwanamwali

anayetayarishwa kwa ajili ya arusi. Katika hali ya kujirembesha, Nyamiti anajipaka mafuta ambayo alikuwa ameuziwa kiulaghai kwa kukopeshwa kijanja dakika ya mwisho na Mahube, kijakazi wa mchawi hatari Chidama. Anapoisikia ngoma inavyopigwa kule nje katika uwanja ambapo arusi inatayarishwa baada ya kujipaka mafuta ya uchawi, Nyamiti anapandwa na jaziba na kuanza kuicheza ngoma hiyo ya sindimba kwani hangeicheza siku yenyewe ya arusi. Hata hivyo, ngoma ilivyopamba moto, ndivyo Nyamiti anapata kuchoka na kichwa chake kuwashwa kama aliyechomwa kichwa na moto. Nyamiti Analia hivi katika dondoo la hapa chini; "**Joto, moto! Sasa umefika kifuani. Mama wee!** (*Ngoma ya Ng'wanamalundi* - uk11):

> NYAMITI: **Joto, moto! Sasa umefika kifuani. Mama wee!**
> CHIBUPA: (*kwa hasira*) **Tazama Nyamiti, kesho tunafunga ndoa! Kesho! Unaelewa?! (*kimya*) Umekuwaje? (kimya) Kwa nini unaugua wakati mbaya kama huu?** *(hasira zaidi*) Yuko wapi naye huyu Seche! Mwanamke kakabidhiwa mwali halafu anamtelekeza, haonekani!

Mwishoni mwa usimulizi wa tukio katika dondoo la hapa juu kuhusu kujirembesha na kucheza ngoma kwa msichana mrembo, ni kifo cha Nyamiti ambaye alikuwa mzima dakika chache zilizopita. Baada ya kujipaka mafuta yaliyorashiwa uchawi, Nyamiti anaanza kusikia maumivu ya kichwa kinachowaka moto hadi anakufa. Mchumba wake Chibupa pia anajaribu kumrai kwa maneno matamu na kumkumbusha kuhusu arusi yao ambayo ingefanyika kesho yake lakini kifo hicho hakikuzuilika kamwe. Chibupa anamsemesha Nyamiti hivi; "**Tazama Nyamiti, kesho tunafunga ndoa! Kesho! Unaelewa?! (*kimya*) Umekuwaje? (kimya) Kwa nini unaugua wakati mbaya kama huu?" -** (*Ngoma ya Ng'wanamalundi* - uk 11). Kifo chake kama kile cha wenzake waliouawa mbeleni na mganga Chidama kinatokea ghafla bila kutarajiwa na kusababisha taharuki. Kifo cha Nyamiti hakikuonekana kama kitatokea kwa sababu hakuwa mgonjwa, hakuwa mzee wala hakuhusika katika ajali. Kifo chake

kimepangwa kutokea kisanaa kupitia kwa uwezo wa ajabu wa uchawi ili kujenga taswira ya ukandamizaji unaofanyiwa watu wanyonge na watu wenye uwezo wao wa juu kama Chidama.

Siku tatu baada ya matanga ya Nyamiti, mganga mashuhuri kijijini kwa jina Chidama analinyemelea kaburi lake tena kwa nguvu za kichawi na kumfufua na kumpeleka katika shamba lake kwenye vizuu wengine. Nyamiti tena anafanyiwa uchawi katika shamba la Chidama ili kumfanya zuzu aliyepumbaa akili, asiyelalamika bali anayekubali kufanya kila kitu anachoamriwa kufanya bila kuuliza swali kama vizuu wengine waliokuwa shambani kule. Vizuu ni aina ya watu waliopumbaa akili walio katika hali ya kukubali kuwa na bwana anayewamiliki, anayewafuga kama wanyama na anayewafanyisha kazi kwa lazima na katika hali mbaya isiyokuwa ya kibinadamu ya kufanya kazi bila chakula wala malipo yoyote. Unyakuzi wa watu kutoka kwa jamii kwa kuwaua kwa kutumia uchawi na kuwafufua baadaye ili kuwaweka katika utumwa wa kufanyishwa kazi ya lazima bila malipo, ni namna moja ya taswira ya kijazanda aliyoitumia mtunzi ili kudhihirisha ukoloni mamboleo katika jamii ya waafrika ulioletwa na mchawi mzungu. Emmanuel Mbogo anasimulia kisa cha udhalimu wa kichawi kwa msichana mrembo Nyamiti ambaye ndoto yake ya kufanya arusi na mpenzi wake Chibupa inakomeshwa kwa kifo cha ghafla ili kujenga taswira ya ukatili na unyanyasaji.

Kisa cha Nyamiti ni taswira ya kijazanda inayomithilisha unyakuzi wa nchi za Afrika na wakoloni bila hiari ya nchi zenyewe. Unyakuzi huu wa nchi za Kimagharibi, unazifisha nchi hizo kiuchumi, kitamaduni na kisiasa alivyofishwa Nyamiti na mchawi Chidama siku moja kabla ya arusi yake. Baada ya kujinyakulia uhuru, nchi za Afrika zilitarajia kujisimamia na kujifanyia mambo yao ya ndani zifanyavyo nchi huru jinsi mhusika Nyamiti alivyotarajia kuanzisha na kuendeleza familia yake

mwenyewe baada ya arusi. Mizungu ya wakoloni kama uchawi wa Chidama inahatarisha uhuru wa nchi hizo kwa kuzinyakua kikoloni na kuzifanya ziwe tegemezi katika kila wanachokihitaji na wanachokifanya. Baada ya kumfufua Nyamiti kutoka kaburini, Chidama anampeleka kwake mashambani ambapo anamnajisi, anamdhibiti, kummiliki kama mali yake binafsi na kumfanya kijakazi wake anayeishi maisha mabaya yasiyokuwa ya kibinadamu bali yanayofaa wanyama tu. Hali ni hivyo katika nyingi ya nchi za Kiafrika zilizojinyakulia uhuru lakini zikajipata katika mtego wa utegemezi katika misaada na madeni yenye masharti magumu baada ya kunaswa na nchi za Kimagharibi na kufanywa koloni upya katika mfumo wa ukoloni mamboleo. Nchi za Kimagharibi zinazidhibiti nchi za Afrika na kuzielekeza kufanya kila kitu wanachokihitaji kama watumwa wao. Hakuna usawa wa kibiashara kati ya nchi za Kiafrika na zile za Kimagharibi. Kila wakati nchi za Magharibi zinazifanyia nchi za ulimwengu wa tatu ulaghai wa kibiashara, kama ule uliofanywa na mhusika Mahube kwa mteja wake Nyamiti (*Ngoma ya Ng'wanamalundi – kr. 8 - 10* ). Katika uhusiano kama huo wa kibiashara, nchi za magharibi hupanga kujinufaisha zenyewe kwa kuzinyonya nchi za Afrika na za ulimwengu wa tatu kupitia kuziwekea masharti ya kilaghai yanayowanufaisha wenyewe.

### 6.3.2 Taswira ya Unyanyasaji katika Ngoma ya Chidama

Mtunzi Emmanuel Mbogo ametumia tanzu za ngoma na nyimbo za sanaa za maonyesho ya jadi kudhihirisha dhima ya ukandamizaji na unyanyasaji katika mfumo wa ukoloni mamboleo uliopo katika jamii. Ngoma na nyimbo ni tanzu za msingi za sanaa za maonyesho ya jadi. Katika tamaduni za Kiafrika, ngoma na nyimbo zilitumika kurembesha sherehe na miviga ya kijamii ambapo waliojumuika walitumbuizwa, waliendeleza na kudumisha utamaduni na historia ya jamii mbali na kukielimisha na kukielekeza kizazi kichanga cha jamii hiyo. Hata hivyo, watunzi wa

tamthilia ya Kiswahili wametohoa amali hizo za kijamii kiubunifu kuwawezesha kujenga na kuimarisha umbo na dhima katika tamthilia zao. Mtunzi ametumia ngoma na nyimbo mbalimbali kujenga dhima katika tamthilia yake kupitia matumizi ya tanzu hizo kitaswira.

Mojawapo ya ngoma alizozitumia mtunzi katika kujenga dhima ya ukoloni mamboleo ni ngoma ya Chidama. Ngoma ya Chidama ina wahusika wanne ambao ni Chidama mwenyewe, Mahube kijakazi wa Chidama, Melo mkewe Chidama na vizuu wa Chidama. Mwandishi ametumia ngoma ya Chidama kisitiari ili kuonyesha mbinu zinazotumiwa na viongozi kuwahadaa na kuwavyoga fikra vijana na umma kwa jumla kwa njia za kijanja na za kichawi ili kuweza kuwamiliki na kuifanya iwe rahisi kuwakandamiza na kuwanyanyasa kwa manufaa yao wenyewe katika mfumo wa sasa wa biashara huria na utandawazi unaoendeleza ukoloni mamboleo. Watu wa nchi za Afrika hawawezi kujiamulia wenyewe wanalolitaka katika maisha yao bali nchi zilizoendelea zimezitwaa nchi zinazoendelea kwa njia za kiujanja kama zilivyo njia za kichawi zilizotumiwa na mganga Chidama katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* bila Waafrika wenyewe kuelewa. Mhusika Chidama ambaye ni mganga anayetumia uchawi wa msukule kuwaroga watu, anaeleza hivi kuhusu ngoma ya Chidama:

> CHIDAMA: … siku zote nimekwambia lazima wacheze **dansi ya Chidama**. Ngoma ya kuwafanya wakakamavu wa mwili lakini mazimbwezimbwe wa roho na bongo. Dansi ya kutia mbolea nyongo ya unyonge wao. Dansi ya kurutubisha nidhamu katika kazi yao
> (*Ngoma ya Ng'wanamalundi -27 - Msisitizo ni wetu*).

Ngoma ya Chidama ni taswira ya kistiari inayowakilisha makundi hasimu yanayodhulumu maskini na watu wa tabaka la chini kwa kuwateka fikra ili kuwalazimisha na kuwakandamiza kufanya wanavyotaka wao bila wanaokandamizwa kutambua wenyewe. Vizuu wanacheza dansi ya Chidama bila kuielewa na bila

kuuliza maswali. Vizuu ni watu waliokuwa wakiishi maisha yao ya kawaida wakauawa na kufufuliwa kwa mbinu na uwezo wa kichawi wa mganga Chidama ambaye anawaroga tena ili wasiwe na ubongo razini bali ubongo taahira unaokubali kunyanyaswa na kudhulumiwa anapowalazimisha kumfanyia kazi kwa nguvu. Vizuu wanachapwa ili kuwalazimisha kucheza dansi na hawana furaha wala hawaelewi wanalolichezea. Wao ni kama vibonzo vinavyochezeshwa na mtu fulani. Mbinu za madhalimu hao ni kama uchawi wa Chidama unaovyoga na kuvuruga fikra razini za vizuu wasielewe dhuluma wanazofanyiwa. Ngoma ya Chidama ni ngoma ya kichawi inayoafiki dhima ya dhuluma na unyonyaji katika jamii ya kisasa. Ngoma yenyewe ina athari za kichawi kwa wachezaji kwani wanapoicheza hufanana vichaa au watu wanaovuta bangi au wanaotumia dawa za kulevya.

Baada ya vizuu kuicheza hiyo ngoma ambayo si ya asili ya Kiafrika kwani mtunzi anaiita "dansi ya Tilantiki", Chidama anayaonea fahari mafanikio yake katika kuwateka vizuu ambao sasa ni wafanyakazi wake. Katika kuonyesha furaha yake kwa vizuu kwa kazi wanayoifanya, kwa bezo na kiburi Chidama anawaahidi vizuu zawadi ambazo ataletewa na meli kutoka Tilantiki:

> CHIDAMA: (*Mwisho wa dansi anacheka karibu azimie!)*
> Lo! Safi! Safi! Kesho nawaletea zawadi! Lo! Safi sana. Kesho nawaletea chakula safi! **Meli toka Tilantiki** imetia nanga jana. Watu wa Tilantiki watu wazuri sana. Wema na wakarimu. Wametuletea meli imejaa mabenzi ya kupanda siye, lakini hawakusahau za unga wa njano na mweusi, kwa ajili yenu. Unga mzuri kwa nguruwe kule Tilantiki, lakini utawafaa nyinyi pia. Basi kesho nanunua gunia moja kwa ajili ya mafyondogoo yenu. (*Ngoma ya Ng'wanamalundi* – uk 27)

Mtunzi ametohoa jina "Atlantic' na kuliandika "Tilantiki" ili kuswahilisha matamshi ya neno hilo la Kiingereza. Muziki wanaoucheza vizuu ni wa Tilantiki na bidhaa zinaletwa na shehena ya meli kutoka Tilantiki. Tilantiki ni dhana aliyoitumia mtunzi

kurejelea utawala na bidhaa kutoka ughaibuni zinazoletwa na biashara huria ya utandawazi. Viongozi wa nchi za Kiafrika wanaingiwa na kiburi na kutumia vibaya mali ya nchi kwa kujiagizia bidhaa za anasa kama magari ya aina ya 'benz' ilhali wananchi wa tabaka la chini wanaofanya kazi kama vizuu wananyanyaswa na kupewa chakula kibaya cha unga mweusi na wa njano unaoliwa kule ng'ambo na nguruwe. Wafanyakazi wanadunishwa na kunyanyaswa na viongozi wao ambao wanafaa kujali maslahi yao na kuwatunza vizuri. Badala yake viongozi hao wanaendeleza unafiki na ubadhirifu kwa kuagiza bidhaa za anasa kutoka ng'ambo na kushirikiana na nchi za nje kuwanyanyasa wananchi maskini. Ngoma ya Chidama au ngoma ya Tilantiki kwa jina lingine ni ngoma ya kuendeleza unyanyasaji na dhuluma za tabaka tawala kwa watu wa tabaka la chini.

Mtunzi ametumia ngoma ya Chidama kiubunifu kuonyesha kwamba kuna taasisi, nchi na watu wenye nguvu wa tabaka la juu ambao hutumia mamlaka yao vibaya kwa namna ya kichawi ili kuzikandamiza nchi changa ambazo hazijaendelea pamoja na watu wake wanyonge wa tabaka la chini. Mfumo huu wa ukoloni mamboleo ambapo nchi zilizoendelea zinazinyakua nchi zinazoendelea na kuzinyanyasa kiuchumi, kiutawala na kijamii umeelezwa vizuri na kisa kielelezo alichokisikia mtunzi Emmanuel Mbogo nchini kwao akisafiri kwa garimoshi. Abiria aliosafiri nao mtunzi walikuwa wakipiga gumzo kumhusu mzee mchawi aliyewaroga na baadaye kuwatumikiza watu aliowaonea wivu katika kazi zake za kuzalisha mali. Baada ya kuwaua kichawi, mganga huyo angerudi kaburini baada ya mazishi yao ili kuwafufua kiuchawi. Mchawi huyo angewafanyia dawa ya kuwafanya mazuzu au vizuu wasiojielewa na wasioweza kulalamikia hali yoyote ya kuwanyanyasa. Chidama kama kielelezo cha viongozi fulani wa Kiafrika na nchi za Kimagharibi zilizoendelea, angewatumikiza vizuu hao katika mashamba yake kuzalisha mali bila hiari yao na bila

malipo yoyote. Masilahi ya vizuu katika shamba la Chidama hayashughulikiwi hata kidogo. Vizuu hao ambao ni watu waliorogwa na kuwafanya kuwa na bongo taahira zilizochanganyikiwa wanakula na kulala zizini kwa manyasi na wanyama kama nguruwe na ng'ombe. Aidha, vizuu wanafanyishwa kazi ngumu katika hali na mazingira mabaya ya kazi. Waafrika kama vizuu wamerogwa kwa njia ambayo hawaijui wasiweze kulalamikia hali yao mbaya ya kazi. Mtunzi anatumia utanzu wa hotuba kwa njia ya Kimwingilianomatini na kumfanya mhusika wake Chidama kueleza ifuatavyo kuwahusu wafanyakazi wake vizuu:

> CHIDAMA: (*peke yake*) Watoto wangu hawana gharama. Hawana gharama watoto wangu. Hawana makuu wala mahitaji. Watoto wangu watiifu. Hawana kelelekelele kama za wale wenzao mjini. Wale vijakazi na watwana wa viwandani hububujika maneno toka ndimi zao ndefu kama za kinyonga … Kila kiwanda ukiingia vurumai, ghasia. Ati wenyewe wameunda vikundi vyao vya ujambazi na madai chungu nzima. Madai ya kugoma kazi. Madai ya chakula. Si wazimu? Utagomaje kazi halafu udai chakula? (*anafikiri).* Mimi hapa kwangu nimeisha kata kilimilimi. Hakuna mdudu anayeweza kufurukuta. Nikimwona mmoja: namfua sawasawa kabla sijamwanika juani … (*Ngoma ya Ng'wanamalundi* - *uk 28*)

Akiwalinganisha wafanyakazi wake na wale wanaofanya kazi katika viwanda na mashamba mengine, mhusika Chidama anajitapa kuwa wafanyakazi wa huko kwingine wanagomea kazi na kusababisha ghasia zisizopendwa na waajiri. Katika mashirika na viwanda vingine, wafanya kazi walilalamikia unyanyasaji wa waajiri ambao pia walikosa kukidhi mahitaji yao muhimu katika viwanda vyao. Kinyume na hali ilivyo katika viwanda vingine, Chidama anajitapa kwamba kwake amewazima na kuwanyamazisha wafanyakazi wake wasiseme neno lolote hata kama wanadhulumiwa. Hali hii inashuhudiwa katika viwanda, mashirika na nchi ambapo wafanyakazi wamezimwa kwa kuwekewa masharti na sheria ngumu zisizowaruhusu wafanyakazi kutangamana na wafanyakazi wengine wa nje wala kujieleza kwa njia

yoyote ili ulimwengu wa nje usije ukajua yanayoendelea katika nchi au mashirika hayo. Mtunzi Emmanuel Mbogo amezifananishwa mbinu hizo za nchi katili zinazowanyamazisha na kuwanyanyasa wananchi wake na uchawi wa Chidama anaowafanya wafanyakazi wake vizuu ili kuwazima na kuwanyamazisha. Huu ni unyanyasaji na ukandamizaji wa wafanyakazi wa hali ya juu. Mchawi Chidama ni kiwakilishi cha waajiri, viongozi, matajiri, watawala dhalimu wa nchi za Kimagharibi ambazo huzihadaa nchi changa na watu maskini wa tabaka la chini na kuwapunja kwa manufaa yao wenyewe. Chidama anazalisha mali katika shamba lake kwa gharama ndogo mno bila kujali maslahi ya wafanyakazi wake. Huu ni mfano mzuri wa unyanyasaji na ukandamizaji wa wafanyakazi wa wenye nguvu katika nchi zinazoendelea.

Matumizi ya taswira hii vilevile ni ya kijazanda kwani yanawakilisha jinsi nchi za Kimagharibi zinavyoziteka nchi za Afrika na kuzifanya miliki yao kwa ajili ya uzalishaji mali wao. Nchi za Afrika zinanyakuliwa bila hiari yao na kufanywa koloni bila kupenda.

### 6.3.3 Taswira ya Ukombozi katika Ngoma ya Shujaa Ng'wanamalundi

Ngoma katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* imetumiwa na mtunzi wake Emmanuel Mbogo katika kujenga taswira ya ukombozi. Ngoma yenyewe inajumuisha wahusika Ng'wanamalundi, Dude, Sango, vizuu wa Ng'wanamalundi na baadaye Seche na Chibupa ambao wanahusishwa katika kuicheza. Ngoma hii ilifundishwa washiriki wake kuicheza kwa utaratibu na kwa malengo maalumu kama inavyodhihirishwa katika mazungumzo ya Ng'wanamalundi. Kama ngoma ya kivita na utamaduni wa Kiafrika, ngoma ya Ng'wanamalundi inachezwa kwa kutumia silaha za ujadi wa Kiafrika kama **mishale na mikuki** inavyodhihirishwa katika maelezo ya jukwaa katika dondoo la hapa chini ngoma inapoanza:

NG'WANAMALUNDI: Njooni tuanze kucheza (**vizuu wanaingia kila mmoja ana mkuki, hata Dude ana mkuki wake)**. Ng'wanamalundi.

NG'WANAMALUNDI: (*Anapaaza sauti*) SASA WAKATI UMEFIKA WA KUCHEZA NGOMA YA NG'WANAMALUNDI. (*Vizuu na wengine wanaitikia. Sasa ngoma inapamba moto.* ***Wanacheza hadi wanapagawa hasa wale vizuu …)*** **-** *(Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 61).*

Ngoma ya Ng'wanamalundi ambayo ni kinyume cha ngoma ya Chidama ambayo ni ngoma ya ukandamizaji katika tamthilia hii ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ni ngoma inayowahamasisha waliodhulumiwa kuhusu hali yao ili kupigania haki zao na kujiweka huru kutokana na mikatale ya unyanyasaji wa madhalimu. Ngoma hii inaendeleza ukombozi kutokana na udhalimu wa viongozi wanaodhulumu. Ng'wanamalundi anaeleza hivi kuhusu mapambano ya ukombozi:

NG'WANAMALUNDI: Nimewaonya tangu mwanzo kuwa **haya si mapambano ya binafsi dhidi ya udhalimu. Sio wewe peke yako unayetiririka machozi ya damu hapa kijijini. Watu wengi wamewapoteza ndugu zao kwa mavumba ya zongo. Jukumu la ngoma ya Ng'wanamalundi ni kuleta ukombozi kwa maskini wote.**
*(Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk. 59)*

Kama anavyoeleza mhusika Ng'wanamalundi katika dondoo la onyo kwa wanyonge la hapa juu katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, ukombozi ni mapambano ya watu wachache waliojitolea mhanga na wasiokuwa na ubinafsi kukabiliana na udhalimu unaoendelezwa na watu wachache dhidi ya watu wengi, "**haya si mapambano ya binafsi dhidi ya udhalimu" – (***Ngoma ya Ng'wanamalundi uk. 59).* Mtu binafsi hawezi kufanikiwa katika kuendeleza juhudi za ukombozi dhidi ya madhalimu ambao aghalabu huwa ndio wenye nguvu. Ngoma huwakusanya pamoja wengi waliodhulumiwa ili waweze kuwa na nguvu zinazoweza kumkabili dhalimu.

Ngoma hii imetumiwa kimakusudi na mtunzi kwa ajili ya kujenga taswira ya ukombozi dhidi ya ukandamizaji na unyonyaji kama asemavyo mtunzi kupitia

mhusika wake Ng'wanamalundi, "**Jukumu la ngoma ya Ng'wanamalundi ni kuleta ukombozi kwa maskini wote" –** (*Ngoma ya Ng'wanamalundi uk. 59*). Kinyume na ngoma ya Chidama ambayo ni kelele zisizokuwa na utaratibu, ngoma ya Ng'wanamalundi inaimbwa na kuchezwa kwa utaratibu na mpangilio mzuri. Ni ngoma inayowashirikisha wote waliodhulumiwa na kunyanyaswa wala sio ya kumtukuza mtu mmoja anayewanyanyasa wenzake. Ni ngoma inayohubiri umoja kati ya nchi zote zinazodhulumiwa kuja pamoja ili kupigana na adui anayewadhulumu ili kujirudishia hadhi na uhuru wao. Ngoma hii haichezwi kwa ajili ya kuburudisha bali kwa ajili ya kuwakomboa waliodhulumiwa na kunyanyaswa kama anavyodhihirisha mhusika Ng'wanamalundi katika dondoo lifuatalo:

> NG'WANAMALUNDI: Njooni tuanze kucheza (*vizuu wanaingia kila mmoja ana mkuki, hata Dude ana mkuki wake*). Ng'wanamalundi.
> NG'WANAMALUNDI: (*Anapaaza sauti*) SASA WAKATI UMEFIKA WA KUCHEZA NGOMA YA NG'WANAMALUNDI. (*Vizuu na wengine wanaitikia. Sasa ngoma inapamba moto. Wanacheza hadi wanapagawa hasa wale vizuu …)*
> NG'WANAMALUNDI: **Yuko wapi adui!**
> KIZUU 1: Yuko wapi adui!
> NG'WANAMALUNDI: **Ua Chidama! Ua!**
> KIZUU 1: **Ua Chidama! Ua!**
> NG'WANAMALUNDI: **Ua Chidama! Ua!**
> KIZUU 2: Ua Chidama! Ua!
> NG'WANAMALUNDI: Damu! Damu! Damu!
> KIZUU 3: Damu! Damu! Damu!
> *(Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk. 61)*

Dondoo la uhamasishaji wa vizuu la hapa juu, lina ujumbe kwa vizuu kumwondoa Chidama ambaye ni kiwakilishi cha udhalimu, unyanyasaji na viongozi laghai ambao ndio chanzo cha kuteseka kwao. Ng'wanamalundi ambaye ndiye kiongozi wa wimbo huu anaita wito kwa kuuliza, "**Yuko wapi adui!"** Kupitia kwa ngoma ya Ng'wanamalundi, vizuu wanapewa hamasisho la asili ya matatizo yao ili waweze kujitambua na kujikomboa kimawazo. Adui anayewatesa vizuu anatambuliwa kuwa

Chidama aliyewaua na kuwafufua vizuu ambao wamefugwa na kudhulumiwa kinyama na dhalimu huyo. Ng'wanamalundi anamtambua na kukata kauli ya kumuua kwa kusema, "**Ua Chidama! Ua!"**

Watu na nchi za ulimwengu wa tatu zilizonyanyaswa na nchi zilizoendelea wamelinganishwa na kuwakilishwa na vizuu wanaoelezwa katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Mtunzi ana ujumbe kwa mataifa na watu wa mataifa kwamba wanafaa kuja pamoja ili kuweza kupigana vita vya ukombozi dhidi ya unyanyasaji wala si nchi moja tu inayoweza kufanikiwa kujikomboa bila kushirikisha nchi zingine zinazonyanyaswa na nchi tajiri. Hili ndilo hamasisho linalofaa nchi za Afrika na nchi zingine za ulimwengu wa tatu ili ziweze kujikomboa. Pamoja nchi hizo zitaweza kushinda vita dhidi ya udhalimu na unyanyasaji wa nchi tajiri za Kimagharibi zinazoendeleza mfumo wa utandawazi unaozinyanyasa nchi maskini kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Katika dondoo hili, utanzu wa ngoma na wimbo wa Ng'wanamalundi umetumiwa kuwasilisha taswira na dhamira ya ukombozi inayoingiliana vizuri Kimwingilianomatini na ujumbe wa ukombozi katika tamthilia za *Mashetani*, *Pungwa* na *Mashetani Wamerudi*.

### 6.3.4 Taswira ya Utabaka katika Majigambo ya Ngoma ya Ng'wanamalundi

Mtunzi Emmanuel Mbogo vilevile ametumia utanzu wa majigambo wa sanaa za maonyesho ya jadi kujenga taswira ya utabaka. Katika majigambo ya Chidama anapoonyesha ubahili wake kwa mganga mwenzake Ng'wanamalundi kwa kumurushia **joka la vichwa saba – (***Ng'wanamalundi, - kr. 15 – 16)*, Chidama anadhihirisha kuwa yeye ni wa tabaka la juu la matajiri wenye nguvu za kiuchumi na kiutawala. Tabaka hili linatumia uwezo wao vibaya ili kudhulumu na kunyanyasa wengine ambao ni wanyonge. Chidama katika majigambo yake anajitapa hivi:

CHIDAMA: … **Joka la vichwa saba**

Lakini ni joka moja tu
Moja katika saba na saba katika moja,
Ewe mtambaa chini,
Mwenye meno ya sumu
Mwenye kinywa kilichojaa misumari na miiba ichomayo
**Na kurarua bila kuruma**, bila kusita …
Haya nawende, nakutuma.
Enda ukatumbukize ukucha wako
Wako wa chuma ubavuni mwake,
Ukamfutue na kumfumua matumbo yake
Ukamzingire na kumzingara figo zake
Umkamue anye na kujinyea
Umuminye akojoe na kujikojolea
Ajue kuwa Chidama ni Chidama kweli.
(*Anamtemea mate kichwani kisha anamrusha nje kupitia dirishani).*
*(Ngoma ya Ng'wanamalundi – kr. 15 – 16. Msisitizo ni wetu)*

Mhusika Chidama ametumiwa na mtunzi Emmanuel Mbogo kijazanda ili kuwakilisha tabaka tawala ambalo ni la juu. Chidama ni kiwakilishi cha viongozi katili wanaotumia uwezo wao kuwanyanyasa watu wa tabaka la chini. Chidama vilevile ni kiwakilishi cha mkoloni anayewakilishwa na **joka la vichwa saba** (k.h.j) ambalo linatambaa chini na kinywani lina meno inayofanana na misumari na miiba inayochoma. Mkoloni anapokuja Afrika, anasababisha madhara na uharibifu mkubwa kwa nchi za Afrika jinsi anavyofanya nyoka aina ya chatu "**anayerarua bila kuuma**" katika jigambo la Chidama. Baada ya kuzinyakua koloni katika bara la Afrika, wakoloni waliweka mikakati ya kulinda hiyo mali yao kwa hali na mali kama nyoka afanyavyo anaporarua windo lake. Suala la utawala na unyakuzi wa malighafi ya nchi ni suala muhimu linalohusisha mipango kabambe na uundaji wa sera ya kuendeleza mbele nchi lakini kila wakati Mwafrika hahusishwi na mkoloni katika uamuzi wa yale yanayofanyika katika nchi yake.

Matendo ya ukatili ya Chidama kwa Ng'wanamalundi, yanamfanya Ng'wanamalundi pia kujigamba na kutenda mambo fulani katika hali ya kujikinga na madhara ya

uchawi wa huyo hasimu yake. Katika malumbano yake ya majigambo kwa Chidama, Ng'wanamalundi anamrudishia kwa kujigamba kama katika jigambo lifuatalo:

NG'WANAMALUNDI: (…*anampiga yule nyoka kwa mgwishu wake. Nyoka anatulia. Sasa anamkamata na kuanza kunuiza na kusema naye*)
Najua aliyekutuma
Lakini huyo si mlume sawasawa
Wewe ni tonga, hujawa tui bado.
Hu'chochote bali garasa,
Shushu la nyoka mgonjwa,
(*anamtemea mate*)
Lakini nakutambua wewe nani.
Najua ndiye wewe ule unukae damu ya maskini.
Huwezi kunizuga na mavazi uliyovaa.
Kwani sabuni na manukato
Havitoshi kutoharisha nuksi
Iliyoko ndani ya kichwa,
Roho, na matendo yako.
Kwani nani hajui kuwa
Wewe ni mchawi wa *msukule*?
**Nani hajui kuwa wewe hupika**
**Vitumbua kwa maji ya**
**Kuoshea wafu ili vitoke?**
**Nani hajui kuwa wewe**
**Hutumia kiganja cha mtoto**
**Aliyekufa kuchotea na**
**Kuuzia vitumbua hivyo?**
**Nani hajui kuwa:**
**Wewe hutumia vipara**
**Vya Binadamu kuvulia**
**Matanga kwa matanga**
**Ya samaki …**
Ukanadi, ukachuma ndarahimu?
(*kimya*)
**Lakini saa wakati umefika wa kucheza Ngoma ya Ng'wanamalundi!**
*(Ngoma ya Ng'wanamalundi – kr. 48 – 49)*

Katika dondoo la Majigambo ya Ng'wanamalundi la hapa juu, kunadhihirishwa taswira ya ubaguzi wa kitabaka katika jamii ya Ng'wanamalundi, hasa kwa tabaka la chini la maskini ambalo ndilo Ng'wanamalundi analipigania na kutetea haki zao. Ng'wanamalundi anamtambua Chidama kama dhalimu anayewafanyisha kazi watoto, vijana na wazee kwa lazima kwa hila za kichawi, **Nani hajui kuwa wewe hupika,**

**Vitumbua kwa maji ya, Kuoshea wafu ili vitoke? Nani hajui kuwa wewe, Hutumia kiganja cha mtoto aliyekufa kuchotea na Kuuzia vitumbua hivyo? Nani hajui kuwa: Wewe hutumia vipara Vya Binadamu kuvulia, Matanga kwa matanga, Ya samaki …** Ng’wanamalundi anatoa azimio kuwa sasa ni wakati wa kukomesha unyanyasaji, dhuluma na uchawi wa dhalimu Chidama kupitia kucheza ngoma ya Ng’wanamalundi ambayo ni ngoma ya ukombozi **Lakini saa wakati umefika wa kucheza Ngoma ya Ng’wanamalundi!** Licha ya Ng’wanamalundi kuwa mganga, uganga wake si wa kufanyia wengine maovu kwa kuwanyanyasa na kuwadhulumu bali kwa kuwaleta pamoja na kuwahamasisha kuhusu haki zao na kuwashajiisha kupigania haki hizo. Ng’wanamalundi ni kinyume cha mganga Chidama anayeendeleza uovu katika jamii kwa kutumia wivu na ulaghai wake kwa wenzake.

### 6.4 Taswira ya Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* - Said A. Mohamed

Katika sehemu hii, tulichunguza taswira za tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika zilizotumika katika utunzi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kwa mujibu wa lengo letu la pili. Ilidhihirika kwamba taswira za ukoloni mamboleo, utandawazi ambapo dunia inaonekana kama kijiji kimoja na vizingiti vya ukombozi kupitia kwa tanzu mbalimbali za jadi zilizotumika kijazanda zilikuwa malighafi adimu ya kubuni tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Said A. Mohamed, mwandishi wa tamthilia hiyo, ametumia tanzu mbalimbali za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika ili kuibua taswira mbalimbali zilizowasilishwa katika maelezo ya hapa chini.

### 6.4.1 Taswira ya Ukoloni Mamboleo katika Jazanda Mbalimbali

Suala la ukoloni mamboleo limeshughulikiwa Kimwingilianomatini na watunzi wote wa tamthilia tulizoziteua kushiriki katika utafiti huu. Watunzi hao wametumia tamathali ya usemi ya jazanda ili kujenga dhamira ya ukoloni mamboleo katika tamthilia zao. Jazanda kwa mujibu wa Ruo (1989) ni mbinu ya matumizi ya lugha inayochora picha ya mahali au vitu kwa kutumia tamathali za usemi. Aidha, hali au vitu viwili hulinganishwa bila kutumia maneno ya kuleta hali ya mfananisho wa moja kwa moja. Said A. Mohamed vilevile amechota tamathali mbalimbali za usemi za jazanda kutoka kwa tanzu za jadi za sanaa za maonyesho kuzua na kujenga taswira ya ukoloni mamboleo.

Mwandishi Said A. Mohamed ametumia jazanda ya Mashetani kujenga taswira ya mkoloni na ukoloni katika tamthilia yake. Katika hali ya kurejelea tamthilia ya *Mashetani* Kimwingilianomatini, mtunzi Said A. Mohamed naye anafafanua kuwa Mashetani bado wapo Afrika pale anapotumia maneno “waltz” na “Mchezo” yaliyotumiwa na mwandishi Ebrahim Hussein. Said A. Mohamed anatumia dhana ya Mashetani kijazanda katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* kurejelea ukoloni mkongwe uliokita mizizi na kukataa kuondoka Afrika hata baada ya nchi za Afrika kupata uhuru wao. Mohamed ameandika hivi:

> Kijana: **Pana Mashetani hapa**.
> Prof.: **Walewale waliotuchezesha mchezo wa maneno na dansi ya *waltz* huku wakijidai kwamba wangeondoka kwenda kwao. Kumbe wangerudi na sisi tumewaita na kudhani ni wakweli.** *(Mashetani Wamerudi – uk. 7*)

Kijana anapoeleza kuwa, “**Pana Mashetani hapa” -** *(Mashetani Wamerudi – uk 7*), mhusika Prof. naye anasisitiza kuwa wakoloni walewale walioondolewa katika vita vya uhuru wamerudi tena. Katika mbinu ya Mwingilianomatini, Said A. Mohamed anatumia maneno “waliotuchezesha mchezo wa maneno” na “*Waltz”* yaliyotumiwa

na mwandishi Ebrahim Hussein katika tamthilia yake ya *Mashetani* kwa kusema hivi, "**Walewale waliotuchezesha mchezo wa maneno na dansi ya *waltz* huku wakijidai kwamba wangeondoka kwenda kwao. Kumbe wangerudi na sisi tumewaita na kudhani ni wakweli" –** (*Mashetani Wamerudi – uk. 7)***.** Wakoloni waliozikandamiza nchi za Afrika wakati wa ukoloni hawakutoka hata baada ya kudai kuwa walitoka na kuziacha nchi za Afrika kuwa huru. Wakoloni bado wapo na wanaendelea kuzitawala na kuziathiri nchi za Afrika.

Mashetani hutisha na kuwaogopesha umma. Katika tanzu mbalimbali za jadi za sanaa za maonyesho hasa katika masimulizi ya kingano, visakale na katika utamaduni wa Kiafrika, Mashetani huchorwa kuwa viumbe hatari wenye maumbo ya kiajabu wanaohusishwa na mambo mabaya ya kutisha ambayo huhatarisha amani na mfumo wa kijamii. Said A. Mohamed ametumia dhana hii kongwe kijazanda kurejelea Wazungu wakoloni waliozitawala nchi za Afrika wakati wa ukoloni na ambao wanazitawala nchi za Afrika kupitia utandawazi na ukoloni mamboleo.

Nchi za Kimagharibi zimezidhibiti nchi za Kiafrika kiuchumi, kisiasa na kitamaduni mithili ya viongozi wa nchi za "Afrika kupandwa vichwa" vyao na Mashetani. Kudhibitiwa kwa nchi za Afrika kunazifanya kukosa uhuru wa kujiamulia mkondo wa maendeleo wa nchi zao na kujitegemea kijamii, kisiasa na kiuchumi bila kuathiriwa kiutamaduni. Kijana 1 anapojaribu kumfukuza kutoka nyuma ya kibanda chao, Jogoo anamwathiri vibaya kwa mazushi anayatoa hivi kwamba Kijana 1 anaporudi kutoka nyuma ya kipanda anapepesuka kama mlevi, (***Halafu kimya. Kijana anajitokeza nyuma ya kibanda huku anapepesuka kama mtu aliyekunywa pombe. Anamwelekea Prof. - (Mashetani Wamerudi – uk 12*).** Haya ndiyo madhara yanayosababishwa na nchi za Kimagharibi zinazowakilishwa kijazanda na Shetani na

Jogoo katika tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* kwa nchi za Afrika na ulimwengu wa tatu ambazo pia zinawakilishwa na mhusika Binadamu.

Nchi za Afrika zinafaa kuogopa na kumwambaa Mzungu anayeendeleza ukoloni mamboleo kama wanavyoambaa majini katika utamaduni wa Kiafrika kwa sababu athari zake ni mbaya na hatari kwa uhuru wao kama inavyodhihirishwa kupitia kwa jinsi mhusika Kijana katika *Mashetani Wamerudi* anavyoathiriwa anapothubutu kumfukuza jogoo kutoka nyuma ya kibanda. Anapotaka kwenda kumfukuza jogoo kutoka nyuma ya kibanda, mhusika Prof. anamhatarisha Kijana 1 kuwa tendo hilo ni hatari kwake lakini Kijana 1 anakaidi. Anapoathiriwa na "masushi ya jogoo" ambayo yanamfanya kupepesuka kama mlevi, Prof. anatoa ushauri wa kumwonya Kijana (Waafrika) dhidi ya kutangamana na wakoloni (jogoo) kwa kusema hivi, "**(*Ana hasira kidogo. Anamkaripia kijana*). Nilikwambia usimfukuze wala usimkamate. Usiwe karibu naye. Ni hatari kuwa naye karibu" – (***Mashetani Wamerudi – uk. 12)***.** Kama Prof. anavyomwonya Kijana 1 kuwa Jogoo ni hatari na anafaa kukaa mbali naye, ndivyo Waafrika nao wanafaa kumwogopa na kumwambaa mkoloni kama wanavyomwambaa jini katika masimulizi ya kingano katika utamaduni wa Kiafrika na sanaa za maonyesho ya jadi. Mazungumzo kati ya wahusika Prof. na Kijana 1 yanaendelea kama ifuatavyo:

> Kijana 1: Ngoja nimfukuze. (*Nyuma ya kibanda. Kijana anamfukuza jogoo. Jogoo anapaparika. Kokoro kokoro, kokoro kokoro – jogoo anakokoreka.* ***Halafu kimya. Kijana anajitokeza nyuma ya kibanda huku anapepesuka kama mtu aliyekunywa pombe. Anamwelekea Prof.***)
> Prof.: **Mbona unapepesuka?**
> Kijana 1: **(*Anakamata kichwa chake huku akikaa pale kitini ambapo tayari Prof amekwisha kukaa pale kitini. Analalamika*). Kichwa kinaniuma!**
> Prof.: **(*Ana hasira kidogo. Anamkaripia kijana*). Nilikwambia usimfukuze wala usimkamate. Usiwe karibu naye. Ni hatari kuwa naye karibu.**
>
> (*Mashetani Wamerudi – uk 12*)

Matumizi ya Shetani katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni ya kimuktadha kuashiria viongozi dhalimu wanaowakandamiza wanyonge katika jamii yenye utabaka. Kama katika uhistoria mpya ambapo jamii ya kibepari inapendelea matajiri, Shetani anayewakilisha na kuashiria viongozi wa kikoloni vilevile aliwanyanyasa na kuwadhulumu Waafrika. Shetani kumtupia mhusika Kijana 1 mzinga na kumkojolea ni taswira ya dhuluma na unyanyasaji unaosababishwa na mkoloni kwa Mwafrika.

Mhusika Shetani katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* anamwambia Profesa kwamba Mashetani huwasababishia Waafrika (Binadamu) ugonjwa wa kizunguzungu. Mhusika Sheta anayemwakilisha mkoloni anaeleza hivi, "**Sisi unajua kwamba tuna mazingaombwe. Tena ni wepesi kwetu kuwapa watu ugonjwa wa kizunguzungu. Ndiyo maana mmetupa jina kizunguzungu?".** Mhusika Prof. ni msomi anayewakilisha watu wa tabaka la chini kwa jinsi anavyotoka katika kibanda ambacho ndio nyumba ya watu maskini. Kibanda vilevile ni kiwakilishi cha kijazanda cha nchi za wananchi maskini wa Afrika. Mashetani ambalo ni jina la kijazanda linalorejelea Wazungu kutoka nchi za Magharibi husababishia nchi za Afrika madhara mengi ambayo yanarejelewa kijazanda kwa jina 'ugonjwa" katika mfumo mpya wa utawala wa ukoloni mamboleo. Mhusika Sheta anaeleza hivi:

> Sheta**: Sisi unajua kwamba tuna mazingaombwe. Tena ni wepesi kwetu kuwapa watu ugonjwa wa kizunguzungu. Ndiyo maana mmetupa jina kizunguzungu?** (*Mashetani Wamerudi* – uk. 20)

Sheta mwenyewe, ambaye ni mhusika anayewakilisha mkoloni katika dondoo la uzungumzi nafsi la hapa juu, anakiri kwamba wao wanayo mazingaombwe yanayowaathiri wananchi wa nchi changa za ulimwengu wa tatu kwa kuwaambukiza ugonjwa ambao ni jazanda ya madhara ya ukoloni kwa nchi hizo za Afrika na zingine za ulimwengu wa tatu. Matatizo yanayowakumba Waafrika ni matokeo ya nchi za Kimagharibi kuziambukiza ugonjwa nchi za Afrika kupitia kwa utawala wa kikoloni

mamboleo unaoendelezwa na mfumo wa utandawazi unaotumika kusambaza madhara hayo.

Mtunzi vilevile ametumia mbweko wa mbwa kijazanda katika kujenga taswira ya ukoloni mamboleo katika tamthilia yake. Kundi la watu likiongozwa na mhusika Prof. walipokuwa wameketi wakijadiliana kuhusu kuandamwa na wakoloni, mustakabali wa demokrasia katika nchi yao na madukuduku ya jinsi nchi za Afrika zilivyofanywa kuwa vinyago na mabwege wasiokuwa na mtazamo wa uongozi kwa kutoa hoja zao kwa zamu, waligutushwa na sauti za mibweko ya mbwa.

> Kundi la Watu: (*mfumko wa sauti za pamoja zimejaa katika mazingira yaliyopo).* Hatukubali … Hatukubali kamwe … Utamaduni wetu una uzuri pia! *(Gafla, kundi la watu linasikia mibweko ya mbwa. Kundi la watu linaonekana kuwa na wasiwasi. Prof. anasimama imara bila ya hofu. Anawapa wenzake onyo).*
>
> Prof.: Tulieni jamani tulieni. Msiwe na wasiwasi. Msiogope. Hilo si kundi la mbwa. Ni sauti ya Shetani anayetaka kututisha ili tutawanyike. Hizo ni ishara za woga wao tu. Sisi tusiwe na woga hata kidogo, maana sisi tupo hapa. Tumesimama kwa miguu miwili miwili kuambizana na kuhamasishana kwenye ardhi yetu. Hatumtukani mtu. Hatumpigi mtu. Hatufanyi zogo. Sisi tuko nyumbani lakini Mashetani hapa si pao. *(Mashetani Wamerudi – uk. 60*)

Mbweko wa mbwa katika jamii za Kiafrika ni ishara ya hatari inayowakabili watu wanaokabiliana na mbwa anayebweka. Mbweko unaorejelewa katika dondoo la hapa juu ni wa kijazanda unaojenga taswira ya onyo la aina fulani ya hatari inayolikabili kundi la wanaharakati hao wa mapinduzi. Jazanda za "Shetani" au "jogoo" na mbweko wa mbwa alizozitumia mtunzi katika kubuni tamthilia yake ni tanzu za jadi ambazo zilikuwa zinatumiwa katika Fasihi Simulizi tu wala hazikuwa zimeandikwa kama asemavyo Matiang'i (2004). Matumizi ya utanzu wa jazanda katika utunzi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* umesimuliwa kwa mbinu tofauti na ile iliyotumiwa katika tanzu asili za sanaa za maonyesho na ile iliyotumiwa katika tamthilia nyingine.

Matumizi haya ya jazanda yana nyongeza ya mbinu za utunzi na maswali yaliyoibuka wakati wa utunzi wake.

### 6.4.2 Taswira ya Utandawazi katika Jazanda ya "Remote Control" katika *Mashetani Wamerudi*

Utandawazi ni hali ya dunia kuonekana kama kijiji kimoja ambapo kuna uhuru wa kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine mbali na uhuru wa kufanya biashara. Matumizi ya lugha katika kazi mahususi ya fasihi huathiriwa na kinachotokea katika jamii yenyewe ambamo msanii huchota fikra, maudhui, falsafa, itikadi, jazanda, mitindo, maumbo na miundo ya lugha hasa wakati jamii yenyewe imo katika mabadiliko makubwa ili kudhihirisha hali ya utandawazi. Kwa kawaida inachukuliwa kwamba, utandawazi una faida kwa nchi zinazoendelea kwani huziwezesha kufungua milango ya biashara, masoko huria ya bidhaa na kuufanya utamaduni wa taifa moja ukutane uso kwa uso na utamaduni wa mataifa mengine kwa mujibu wa Jauch, (2001). Mtunzi Said A. Mohamed akieleza kuhusu umuhimu wa utandawazi kupitia kwa mhusika Sheta anayathibitisha madai haya kwa kusema ifuatavyo:

> Sheta: … wewe peke yako ndiye unayekataa ukweli wa maisha mazuri yatakayotazamiwa karibuni. …lakini wewe hukubali ukweli wa mfumo huu wa utandawazi. Mfumo huria unaosukumwa na nguvu za teknolojia mpya ya mawasiliano na mfupisho wa wakati wa biashara huria. Na siasa ya 'liberalizimu' yaani *liberalism*, na vyama vingi vyenye chaguzi wazi zisizo na demokrasia, na mtawanyiko wa mabenki pande zote za dunia. *(Mashetani Waerudi – uk. 19*)

Hata hivyo utandawazi ni kisingizio cha nchi zilizoendelea kuzipunja nchi an ch kwa kutumia maendeleo yao makubwa ya kiteknolojia kuzinyonya nchi za ulimwengu wa tatu na kuziwacha kuwa maskini kwa kutumia mbinu zisizo wazi ambazo mwandishi anaziita "remote control." Mhusika Sheta anayewakilisha Wazungu wakoloni anaeleza ifuatavyo kuhusu udhibiti wa Wazungu wakoloni wa nchi za Afrika na nchi za ulimwengu wa tatu:

> Sheta: Hapana nguvu yoyote ya kutudhibiti, maana sisi tuko nchini mwetu tunabonyeza *remote control.* Kwani mmesahau kwamba **utandawazi ndio *remote control* zaidi kuliko ukoloni mamboleo**. *(Mashetani Wamerudi – uk. 61. Msisitizo ni wetu*)

Licha ya madai ya manufaa yanayoletwa na utandawazi kwa nchi za ulimwengu wa tatu, utandawazi kwa tamko la mhusika Sheta anayemwakilisha mkoloni unaelezwa hivi, "**utandawazi ndio *remote control* zaidi kuliko ukoloni mamboleo.**" Utandawazi ni mbinu isiyo wazi ya kuzidhibiti nchi changa ambazo hazina maarifa na teknolojia ya ulimwengu wa kwanza na kuzitumia katika kujipatia malighafi na soko la bidhaa zao. Manufaa ya utandawazi ni kwa nchi za ulimwengu wa kwanza unaozidhibiti nchi za ulimwengu wa tatu katika biashara, teknolojia, maendeleo ya viwanda na utamaduni.

Akielezea kuhusu lililowaleta tena katika bara la Afrika, Wazungu wakoloni waliofurushwa awali baada ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru na kurudi baadaye kiujanja kwa njia ya utandawazi, mtunzi wetu Said A. Mohamed kupitia kwa mhusika wake Prof. anaeleza hivi:

> Prof.: **Shina la mbuyu**, shina la mbuyu – **walilibadilisha jiti kubwa lenye virutubishi. Wakalifanya tanda la kulalia na kisha pahala pa kurukia katika maendeleo yao**.
> Kijana: Nani hao?
> Prof.: Mashetani.
> Kijana: Pana Mashetani hapa?
> Prof.: Ndiyo. Waliokuwepo. Wakajifanya hawapo kwa ujanja wao. Sasa wapo waziwazi. Wamesharudi … Wamesharudi … Wamesharudi. Nakwambia wamesharudi.
> Kijana: Mashetani? Mashetani gani hao?
> Prof.: Walewale waliotuchezesha mchezo wa maneno na dansi ya waltz huku wakijidai kwamba wangeondoka kwenda kwao. Kumbe wangerudi na sisi tumewaita na kudhani ni wakweli. (*Mashetani Wamerudi – uk. 7*)

Mbuyu (**Shina la mbuyu** - *Mashetani Wamerudi – uk 7*) ni dhana ya kijazanda aliyoitumia mtunzi Said A. Mohamed kurejelea nchi za Afrika na za ulimwengu wa tatu. Kwa madai yake, Mohamed anaeleza kuwa Wazungu wakoloni wamerudi tena

Afrika kwa njia ya ujanja baada ya nchi hizo kujinyakulia uhuru na kuzifanya nyenzo ya kujirutubisha na kujipatia maendeleo makubwa, “**walilibadilisha jiti kubwa lenye virutubishi. Wakalifanya tanda la kulalia na kisha pahala pa kurukia katika maendeleo yao.”** Utandawazi unaziwezesha nchi zilizoendela kurudi Afrika kiujanja kupitia kwa biashara na teknolojia ili kuzinyanyasa na kuzinyonya rasilimali katika biashara yenye masharti magumu na ambayo haina usawa. Kulingana na madai ya mhusika Sheta katika Onyesho la Kwanza la Sehemu ya Pili ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi,* wakoloni Wazungu wanarudi Afrika mmoja mmoja kila siku na watakuwa wengi siku zijazo kwa uwezo wa nguvu na akili zao kupitia utandawazi:

> Prof.: … Mambo yamebadilika tokea ulipopanda mbuyu huku ukicheza! Sasa huwezi kucheza juu ya mbuyu utakavyo, maana mbuyu umepogolewa na unatoa chipukizi mpya.
> Sheta: Hatuutegemei tena mbuyu. Uwe wa jana au wa leo. **Tunachokitegemea ni nguvu na akili zetu tu.** (*Mashetani Wamerudi* – uk. 24)

Kwa mujibu wa Jauch (2001) na Offiong (2001), utandawazi ni neno dhahania lenye maana zinazotatiza kutegemea msisitizo wa anayelitumia. Neno utandawazi hufumbata mfungamano na uhusiano uliojitokeza katika miaka ya 1980 sio tu katika biashara na uchumi bali pia katika utamaduni miongoni mwa jamii tofauti za dunia. Hivi sasa maana ya utandawazi husisitiza kuwekeza mtaji kwa ajili ya kupata faida ya kujijenga kisiasa, kiuchumi na kitamaduni ukisaidiwa na maendeleo makubwa ya kiteknolojia hasa ya vyombo vya mawasiliano ambavyo vimefupisha na kuondoa vikwazo vya masafa na wakati. Hata hivyo, nchi za Magharibi zimetumia mbinu hizi za utandawazi kwa njia ya kinafiki ili kujinufaisha wenyewe kwa kubuni sheria ambazo nchi za Afrika na za ulimwengu wa tatu lazima zizikubali ili kufanya biashara na nchi hizo (*Mashetani Wamerudi* - uk 25).

> Sheta: **Kwa sababu sheria zetu lazima mzikubali na mzifuate,** (*kwa nguvu*).

Sheria zinazorejelewa na mhusika Sheta katika dondoo la hapa juu zinapotumiwa na nchi za magharibi kuongoza nchi zinazohusiana katika biashara, uchumi, teknolojia, usambazaji wa habari na utamaduni katika utandawazi unaziwezesha nchi hizo kuziibia na kuzipora mali yao asili. Mhusika Sheta anathibitisha madai haya kwa kukubaliana na Prof kwamba mahusiano ya kiutandawazi yanazifuja nchi za Afrika kwa kusema kuwa:

Sheta: **Si m'mesema utandawazi ndio ufujaji wa mataifa yenu?**

Kiutamaduni, utandawazi unahusishwa na kuenea kwa tamaduni za Kimagharibi kwa njia ya biashara na uenezaji wa habari kwa njia ya teknohama. Mhusika Prof. katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* anamweleza Sheta kwamba, **"Usisahau kwamba sisi tumeelimika kwa namna mbalimbali. Si kwa utamaduni wa *Oksidanta* au *Occidental*, bali kuna *Oriental* pia. Sikwambii tamaduni zetu mnazozikanusha na kusema hazipo"** - (*Mashetani Wamerudi* – kr. 17 – 18). Tamaduni hizi hujumuisha utazamaji wa video na televisheni, mifumo mipya ya mavazi na uvaliaji, mitandao ya kompyuta na simu, mienendo mipya ya vyakula na vinywaji (ulevi na vyakula vya mafuta vinavyonenepesha na ambavyo havijulikani katika ulimwengu wa tatu). Utandawazi vilevile huwa na athari kwa jamii. Kwanza, utandawazi hufuta mipaka na kufanya tamaduni za nchi mbalimbali za dunia kuingiliana. Aidha, husababisha soko huria duniani ambapo uhuru wa kuuza na kununua bidhaa yoyote duniani huwa umeendelezwa. Kwa sababu hii, nchi zilizoendelea hupata nafasi ya kutupa (dump) bidhaa zao ghushi katika nchi changa ambazo hazijaendelea. Ingawa kuna malalamishi na madai ya nchi za ulimwengu wa tatu kunyanyaswa na nchi zilizoendelea katika biashara ambayo haina usawa, mhusika Prof. mwenye busara kubwa katika majibizano yake na mhusika Sheta anahamasisha wasomaji wa mchezo kuwa ni wajinga waliwao kwa kusema ifuatavyo:

> Prof.: Utandawazi ni *remotecontrol* yenu una ukweli, lakini pale tu watu wanapokuwa wajinga. Werevu una nguvu zaidi kuliko *remote control*.(*Mashetani Wamerudi – uk 61*)

Utandawazi ni dhana ya kimaendeleo ambayo imepata msukumo kupitia kwa matukio ya kisasa ulimwenguni kupitia kwa biashara huria, teknolojia, usambazaji habari na ubadilishanaji wa tamaduni. Utandawazi unaweza kuwa na manufaa kwa nchi zinazohusiana kwa njia hizo mbalimbali kukiwa na usawa na kuaminiana bila kuhusisha njia zisizo wazi za udhibiti za (remote control) za ukoloni mamboleo.

### 6.4.3 Taswira ya Vizingiti vya Ukombozi katika Mhusika "Prof." wa Kimajazi katika Mashetani *Wamerudi*

Watunzi wengi wa tamthilia za Kiswahili na fasihi kwa jumla wametumia kazi zao kudhihirisha kuwa njia za kujinyakulia ukombozi kutoka kwa mikono ya mdhalimu si wazi bali imejaa vizingiti na vikwamizo vingi. Kuna vizingiti vingi vya ukombozi vilivyojengwa na watunzi wa tamthilia ya Kiswahili kupitia kwa matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi. Vizingiti hivi ndivyo vilivyochangia katika kuzuia watu, vikundi na mataifa mbalimbali kufikia ukombozi wao kiuchumi, kitamaduni, kisiasa na kiutawala.

Mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* analalamika kwamba wasomi na viongozi wa nchi za Afrika wanaowakilishwa na wahusika kama mhusika Prof. katika tamthilia hiyo wametupilia mbali nafasi yao ya uongozi na ya kuelekeza nchi zao katika kujitawala na kujitegemea. Viongozi hawa wamekimya wakati mambo yanaharibika katika nchi zao. Kijana 1 katika tamthilia hiyo akimkabili Prof. katika mazungumzo yao anamuuliza ni kwa nini kwa miaka mingi Prof. alikuwa hasemi lolote – kwamba watu wengine wanasema na kutenda lakini yeye Profesa hubaki kimya.

> Kijana 1: *(Kijana1 anaelekea upande wa hadhira na kisa anamrudia Prof na kumwambia*) Mbona miaka yote hii hujasema Prof? Umebaki kimya. Wao wanasema. Wewe kimya.

Husemi. Kwa nini? Unamwogopa nani? Shetani? Unamwogopa Shetani? Unaogopa nini hasa? Hata Shetani anayepita tu? Tuseme umekwisha? Au sisi sote tumekwisha? Tuseme sisi ndio tuliokwisha? Tuseme tumo katika usingizi? Au umekufa? Au sisi tumekufa? …

Kijana 1: Labda miaka. Labda karne. Labda tulisema. Lakini sasa tunanyamaza. Hutuna midomo ya kusema.

(*Mashetani Wamerudi – uk. 3*)

Mhusika Prof katika dondoo si mtu wa kawaida kama walivyo watu wengine katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Mbali na kuwa msomi wa haiba ya juu, yeye ni mfanyakazi wa daraja la juu aliyepata mafundisho ya kitaalamu ya juu zaidi. Yeye ndiye mtaalamu wa juu zaidi katika ngazi ya viwango vya utaalamu. Prof. anasema hakuna anayeweza kumpinga kwani yeye huwa anaheshimiwa na jamii yote kama mjuzi wa kila kitu.

Prof., vilevile, ni kiwakilishi cha viongozi wa nchi za Afrika ambao hawaelewi nafasi yao katika kuelekeza nchi zao katika kujitawala na kujitegemea bila kuzikubalia nchi za Kimagharibi kuzitawala tena nchi za Afrika. Mara nyingi wanajamii walio na masomo ya juu na viongozi wenye busara yao huhudumu chini ya utawala mbaya wa kikatili na unaonyanyasa watu wake kwa madai kwamba kwa kufanya hivyo wataweza kuleta mabadiliko ya uongozi wakiwa ndani ya mfumo wa utawala huo ulioharibika. Wao hutumia uongo huu ili kujikinga kutokana na maswali ya wanajamii wanaotaka kuelewa nafasi yao. Wengine hukimya tu kwa kuogopa kunyamazishwa kwa njia hatari ya kuuliwa au kufungwa jela, Prof. anaeleza hivi:

Prof: Kusema ninasema. Lakini ninasema kichwani. Ukweli haupo. Uongo ndio usimamao kama kijiti kilichoota machoni. Uongo unacharaza ovyo pamoja na udanganyifu ili kuukandamiza ukweli (uk. 5).

Prof: Kusema ninasema, lakini ninasema kichwani. Hatusemi waziwazi kwa sababu **ukweli siku hizi ni mwiko**. Uongo ni msimamo mwepesi kama njakuti mara moja hukatika kwa mwenye kujua.

(*Mashetani Wamerudi – kr. 5 - 6*)

Viongozi na watu wengine katika jamii wanaona makosa katika jamii lakini wanaogopa kusema kwa kuchelea athari ya makabiliano na viongozi walio uongozini kwani asemavyo Mohamed katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi*, **ukweli siku hizi ni mwiko**. Wengine huamua kunyamaza tu kwani pia ukisema uongo msimamo wake mwepesi kama njakuti huenda ukakatika na kukubwaga matatani. Woga wa kusimama imara na kusema ukweli jinsi ulivyo na kunyamaza tu bila kuyasema matatizo yanayoikabili jamii ya Kiafrika ndicho kikwazo kikubwa kinachochangia na kuchelewesha nchi za Afrika kupata ukombozi kutoka kwa mwanaukoloni mamboleo.

### 6.5 Muhtasari wa Taswira katika Tamthilia Teule za Kiswahili

Lengo la pili lilituwezesha kuchanganua taswira zilizojengwa na kuibuliwa kupitia kwa tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika zilizopambanuliwa katika sura ya tano kuwa zilitumika katika utunzi wa tamthilia teule za Kiswahili za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi*. Uchunguzi wetu katika sura hii ulifafanua taswira zilizojengwa kwa mujibu wa tanzu za jadi za sanaa za maonyesho za masimulizi ya kingano, uigaji na utendaji wa michezo, majigambo, ngoma na nyimbo, ushairi simulizi, hotuba, malumbano ya utani, shoga, jazanda, stiari na tamaduni za Kiafrika na tanzu nyingine za jadi zilizotumiwa kujenga umbo na dhamira katika tamthilia ya Kiswahili.

Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) ina mfanano mkubwa na tamthilia ya *Mashetani* (1971) iliyotungwa na msanii mashuhuri Ebrahim Hussein ambao si wa kiajali sio tu katika matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho bali pia katika masuala muhimu yaliyoshughulikiwa na watunzi hawa wawili. Emmanuel Mbogo, Said A. Mohamed na Ebrahim Hussein wametumia tanzu mbalimbali za jadi za sanaa

za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika ili kuibua taswira mbalimbali zilizowasilishwa katika maelezo ya hapa chini.

Ebrahim Hussein na Said A. Mohamed walitunga tamthilia zao kwa utanzu wa mchezo wa kuigiza wa Shetani na Binadamu walioutumia kijazanda ili kuibua taswira ya unyanyasaji, kudhibitiwa na kutawaliwa kwa nchi za ulimwengu wa tatu na nchi za ulimwengu wa kwanza katika mfumo wa ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo kuwa asili ya matatizo ya nchi hizo. Said A. Mohamed kupitia kwa tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* anasisitiza kuwa ukoloni umerudi kwa kurejelea Kimwingilianomatini masuala yaleyale ya *waltz,* aliyoyataja Ebrahim Hussein. Kwa kulinganisha ukoloni mamboleo na Shetani, wote Ebrahim Hussein na Said A. Mohamed katika tamthilia zao za *Mashetani, Pungwa* na *Mashetani Wamerudi* wanakubaliana kuwa ukoloni mamboleo kama Shetani huwa na nafsi yenye ncha nyingi, humwingia Binadamu kwa namna nyingi na kumzuga akili.

Said A. Mohamed katika *Mashetani Wamerudi* kupitia kwa tanzu za masimulizi, mazungumzo na jazanda ya "remote control" alijenga taswira ya utandawazi ambapo nchi zilizoendelea huzipunja nchi changa kwa kutumia maendeleo yao makubwa ya kiteknolojia kuzinyonya nchi za ulimwengu wa tatu na kuziwacha zikiwa maskini. Ebrahim Hussein vilevile alitumia jazanda ya bahari na hadithi ya chewa kurejelea nchi zinazodhibitiwa na kudhulumiwa na nchi tajiri za ulimwengu wa kwanza kiutandawazi katika siasa, uchumi na katika masuala ya kijamii.

Ngoma na nyimbo ni tanzu zilizotumiwa katika tamthilia zote teule kuibua taswira ya unafiki, uongozi mbaya, ubadhirifu wa mali na unyanysaji. Baada ya Waafrika kujinyakulia uhuru wao kutoka kwa wakoloni katika tamthilia ya *Mashetani,* Waafrika waliingiwa na kiburi wakajitungia nyimbo na kusherehekea uhuru wao kwa

ngoma. Emmanuel Mbogo katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* alitumia ngoma ya Chidama kudhihirisha unafiki na unyanyasaji wa tabaka tajiri la juu. Ngoma ya Ng'wanamalundi hata hivyo inatumiwa na Mbogo kujenga taswira ya ushindi na ukombozi wa wanyonge kupitia kwa vita na mapambano ya kujinyakulia uhuru wao kutoka kwa udhalimu na uongozi mbaya. Wimbo wa "Papa black sheep" umetumiwa na Ebrahim Hussein katika tamthilia ya *Mashetani* kudhihirisha na kujenga taswira ya ubadhirifu wa mali ya umma. Kununua magari ya anasa kunakofanywa na viongozi na wafanyakazi wa nchi maskini za bara la Afrika wanaodhani kuwa kupata uhuru ni kupata nafasi ya kutowajibika na kutofanya kazi ni hali ya unafiki na ubadhirifu wa hali ya juu. Sura zote kumi na mbili za tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* zinatangulizwa na nyimbo zinazofafanua kwa muhtasari masuala muhimu yanayoshughulikiwa na mwandishi wake.

Tamthilia zote nne zinadhihirisha matumizi ya tanzu za jadi za majigambo na ushairi simulizi ili kumbainisha pepo au Shetani anayewakilisha mkoloni mkongwe na mkoloni mamboleo ni nani na hivyo kujenga na kuibua taswira ya dhalimu anayewanyanyasa Waafrika katika nchi zao maskini. Kiburi cha Shetani katika majigambo ya Shetani katika tamthilia za *Mashetani*, *Pungwa* na *Mashetani Wamerudi* kinadhihirisha ukatili na udhalimu wa mkoloni anayewakilishwa na kumithilishwa kisanaa na Shetani huyo anayejigamba. Malumbano baina Chidama na Ng'wanamalundi katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ni mfano wa malumbano ya utani aliyoyatumia mtunzi Emmanuel Mbogo kujenga taswira ya utabaka, udhalimu, unyanyasaji, ukatili na ukombozi kwa wakati mmoja. Watunzi wa tamthilia ya Kiswahili walidhihirisha upendeleo wa kutumia utanzu wa majigambo na ushairi simulizi katika kupitisha dhamira zao kwa hadhira yao kama mbinu ya utunzi.

Matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi kitaswira katika utunzi wa tamthilia zote za *Mashetani*, *Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* yametawala tangu mwanzo hadi mwishoni mwa tamthilia hizo. Walipokuwa wakibuni tamthilia zao, mfumo wa utawala uliokuwepo haukuwaruhusu raia wa kawaida kuwakosoa viongozi. Hivyo utunzi wa waandishi wetu na wengine wa wakati wao ulipelelezwa na kuwekewa vikwazo vilivyowaogopesha wengi kubuni kazi za sanaa zilizochukuliwa vibaya kuwa za uzushi na uchochezi. Uandishi wa kiubunifu ulihitaji kuwa na ustadi mkubwa ili kujikinga na athari za serikali yenye mkono mrefu wa kuwadhulumu raia, kufungwa jela au hata kuuawa kwa kuikosoa sera ya serikali ili kuonekana kudhibiti uongozi wa serikali zao. Ikumbukwe ya kwamba watunzi wengi wa wakati huo kama Ngugi wa Thiong'o na Alamin Mazrui miongoni mwa wengine walifungwa jela au walilazimishwa kuzikimbia nchi zao kama watoro ili kujisalimisha kwa sababu ya uandishi wao kukosoa viongozi na serikali. Ebrahim Hussein, Said A. Mohamed, Emmanuel Mbogo na watunzi wengine wa tamthilia wametunga tamthilia zao kwa kutumia tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi kiubunifu kwa njia ya kuibua taswira kijazanda kama mbinu ya kuendeleza dhamira katika tamthilia zao ili kuzuia kubashiriwa vibaya na mahasimu wao serikalini kwa urahisi wanapowakosoa.

### 6.6 Hitimisho

Katika sura hii, tumechunguza na kuchanganua taswira zilizojengwa kupitia kwa matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho za asili ya tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia teule za Ebrahim Hussein, Said A. Mohamed na Emmanuel Mbogo zilizotumiwa kujenga maana na hali za kweli katika kazi zao. Tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho zilizotumika katika tamthilia teule zilibainishwa na kuhakikiwa kwa mujibu wa lengo letu la pili la utafiti huu. Ilibainika kuwa watunzi teule wametumia tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho ya jadi

Kimwingilianomatini katika utunzi wa tamthilia zao na tanzu hizo ziliweza kujenga dhima mbalimbali kitaswira na kuchangia katika uimarishaji wa umbo, mtindo na maudhui katika tamthilia zao. Hivyo, aina mbalimbali za tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilizothibitishwa kuwa zilitumiwa katika utunzi wa tamthilia teule zimeainishwa ili kudhihirisha maana na dhamira zao. Nadharia zilizoongoza uchunguzi huu ni nadharia za Mwingilianomatini na Uhistoria Mpya.

Sura inayofuata imeangazia mabadiliko yaliyotokea kufikia sasa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na umuhimu wa matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika kama mbinu za utunzi ya kujenga na kuimarisha dhamira za watunzi katika mapito ya wakati katika kipindi cha karibu miaka hamsini.

# SURA YA SABA

# MABADILIKO NA UMUHIMU WA MATUMIZI YA SANAA ZA MAONYESHO YA JADI KATIKA UTUNZI WA TAMTHILIA

## 7.0 Utangulizi

Katika sura ya sita, tulibainisha na kufafanua taswira za ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo, utandawazi, unafiki, ubadhirifu, unyanyasaji na ugandamizaji wa wananchi wachochole na suluhisho la matatizo yanayozikumba nchi za Afrika zilizoibuliwa kupitia kwa tanzu za jadi za sanaa za maonyesho zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi.* Ilidhihirika ya kwamba tanzu za jadi zilizotumika katika kubuni tamthilia ya Kiswahili zimetumika kibunifu katika kuibua taswira mbalimbali zinazojenga dhamira ya watunzi teule.

Uchanganuzi wa data katika sura hii umeegemezwa katika matokeo ya utafiti katika sura za tano na sita. Sura hii imeshughulikia mabadiliko na maendeleo ya matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika kama mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika mapito ya wakati. Sura hii pia imeshughulikia umuhimu wa sanaa za maonyesho kama mbinu ya utunzi na uimarishaji wa umbo la tamthilia ya Kiswahili kwa mujibu wa lengo letu la tatu la utafiti huu.

## 7.1 Mabadiliko na Umuhimu wa Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Utunzi wa Tamthilia ya Kiswahili

Utunzi wa tamthilia andishi ya Kiswahili kwa kawaida hufuata muundo wa Kimagharibi kama ilivyopendekezwa na mwanafalsafa wa Kigiriki kwa jina Aristotle. Tamthilia za ki-Aristotle kwa mujibu wa Mulokozi (1996) huwa na muundo wa mazungumzo au dayalojia baina ya wahusika katika maigizo, huambatana na vitendo, huwa na maonyesho na huwa na migogoro inayosuluhishwa mwishoni mwa tamthilia.

Katika kazi yake ya *Poetics*, Aristotle anafafanua sanaa ya utunzi wa tamthilia ambayo inarejelewa hapa kama tamthilia ya ki-Aristotle ambamo alifafanua sheria za utunzi wa tamthilia. Sheria au kanuni hizi ndizo ambazo zimekuja kuwa na athari kubwa katika taaluma ya uigizaji na sanaa ya utunzi wa tamthilia katika bara la Ulaya na dunia nzima kwa jumla. Kwa karne nyingi, sheria hizi za Aristotle zilichukuliwa na wanasanaa wengi wa michezo ya kuigiza kuwa mwongozo wa kuandika tamthilia. Aidha, Aristotle alipendekeza vipengele muhimu ambavyo ndio msingi unaojenga tamthilia ya Kimagharibi:

i. Tamthilia iweze kuwa na sehemu ya nyimbo mwishoni mwa tamthilia.
ii. Matamshi ya kishairi yanayozingatia mpangilio na idadi maalumu ya mizani.
iii. Tamthilia iweze kuwa na mtiririko mzuri.
iv. Tamthilia iwe na mawazo mazito.
v. Uigizaji uweze kutumia jukwaa lote.
vi. Iwe na wahusika wanaoaminika.
vii. Mchezo wa kuigiza uwe wa kufurahisha na kuchekesha au uwe wa kuhuzunisha na kuleta majonzi.

Aristotle aliendelea kuigawanya tamthilia katika vijisehemu vidogo zaidi alipopendekeza sehemu tatu kuwa sehemu za mchezo wa kuigiza ambazo ni:

i. Tamthilia iweze kuwa na mwanzo au utangulizi.
ii. Tamthilia iwe na mwili wenye kitendo kinachoigizwa na ambacho kinapaswa kutia hofu au huruma moyoni.
iii. Iwe na kimalizio cha wimbo.

Licha ya mapendekezo haya, waandishi wa tamthilia teule za Kiswahili za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* na wengine kutoka bara la Afrika hawafuati mapendekezo ya muundo wa tamthilia wa Aristotle kipekee kwa muda mrefu sasa.  Waandishi wengi kama Ebrahim Hussein, Said A. Mohamed na Emmanuel Mbogo walioteuliwa katika utafiti huu wametumia vikale vya nyimbo na ngoma, majigambo, ushairi simulizi miongoni mwa mbinu zingine kutoka tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia zao tangu mwanzo hadi mwisho wa

tamthilia hizo. Mwandishi Saidi A. Mohamed ameanzia wimbo mwanzoni mwa kila onyesho katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* (tazama kiambatishi 4 *Mashetani Wamerudi; i) Wimbo wa Mchezo Mpya: "Roho haifi" ii) Jambo lile lile la ukoloni mamboleo iii) Mazingaombwe: Vuta nikavute - sauti ya kujenga ubwana iv) Ya jana si ya leo … Colonial discourse v) Wimbo na ngoma ya utetezi vi) Sheria walizoturithisha vii) wimbo wa kejeli – vijana wanachachamaa viii) Wimbo wa urazini – ushirika wa wanaokaa vitini ix) Wimbo wa umoja, x) Wimbo wa tamaa xi) Wimbo wa barabarani na xii) Safari tafika, Enyi dunia ya tatu*) kinyume na pendekezo la Aristotle lililosisitiza uwepo wa wimbo mwishoni mwa tamthilia.

Waandishi wengine wa tamthilia ya Kiswahili na tamthilia nyingine zisizo za Kiswahili hawatumii lugha ya kishairi wala utunzi wao hauzingatii sheria za kimapokeo za utunzi wa mashairi kama vina vya kati na mwisho, idadi ya mishororo katika kila ubeti, idadi ya mizani katika mishororo ya tungo zao miongoni mwa sheria zingine. Waandishi wa tamthilia zetu teule pamoja na watunzi wa mashairi ya kisasa wamepinga matumizi ya muundo wa kimapokeo wa shairi unaosisitiza vina na idadi ya mizani katika kila mshororo kinyume na alivyopendekeza Aristotle kwa madai kwamba kusisitiza kufuata matumizi ya sheria za utunzi wa mashairi ya kimapokeo kunaua ubunifu wao.

Waandishi wa tamthilia ya Kiswahili hata hivyo wanasisitiza na kuunga mkono utumiaji wa mazungumzo ya kitamthilia baina ya wahusika. Akipinga maoni ya Aristotle, Brecht (1999) alieleza kuwa mapendekezo ya Aristotle yalimpatia mtunzi wa tamthilia nafasi nyembamba na finyu mno isiyomwezesha kuwa mbunifu. Matumizi ya lugha na maigizo ya tamthilia katika tamaduni za nchi zingine kama Afrika, Japan, Hindi na kwingineko pia hazikubaliani na mapendekezo ya Aristotle.

Hali hii inaipa tamthilia ya Kiswahili nafasi kujitambulisha na kujinasibisha na muundo wake wa pekee. Tanzu za nyimbo na mashairi zilizotumiwa na watunzi wetu hazijazingatia matumizi ya sheria za utunzi wa mashairi ya kimapokeo licha ya sehemu nyingi ya kazi zao kuwa na mapigo na muwala wa mawazo wa kishairi. Mhusika Juma katika Sehemu ya III, Onyesho la I la tamthilia ya *Mashetani* anatongoa shairi huru ifuatavyo:

JUMA: Upweke
Upweke una mbawa.
Unarusha nyoyo za Binadamu juu kabisa.
Chini linabakia ganda
Macho yanaona, akili inafikiri …
Lakini .. kiwiliwili hakihisi
(*Anacheka polepole*)
Bibi anapuliza sumu.
Sumu au mapenzi?
Jaribu kupambanua:
Mapenzi hugeuka sumu.
Naam, mara nyingi
Mapenzi hugeuka sumu.
(*Mashetani – kr. 41 – 42*)

Shairi hili la Ebrahim Hussein katika tamthilia ya *Mashetani* linatiririka vizuri na lina muwala wa mawazo. Hata hivyo, mtunzi hajajifunga katika kuzingatia sheria za kimapokeo zinazoongoza utunzi wa mashairi. Kipande hiki cha shairi huru hakina vina vya kati wala vya mwisho, idadi ya mizani katika kila mshororo inabadilikabadilika na hakuna idadi mahususi ya mishororo katika ubeti wowote. Mtunzi amelitumia shairi la dondoo la hapa juu katika sehemu hiyo ya onyesho la tamthilia kama nyenzo ya kumwezesha kuhakiki na kuhukumu mawazo ya wahudumu Waafrika na wateja wao katika mkahawa kuhusu hadhi ya Mwafrika baada ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru. Waafrika hudharauliwa na Wazungu na hujidharau wenyewe hata wakiwa huru nyumbani kwao.

Majigambo mawili ya Chidama na Ng'wanamalundi katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (k.h.j.) vilevile yameandikwa kwa lugha ya kishairi ambayo hata hivyo haizingatii sheria za kimapokeo za utunzi wa ushairi wa kuzingatia urari wa vina na idadi ya mishororo. Chidama akijigamba kuhusu uwezo wake anaoufananisha na ule wa joka la vichwa saba ambalo lina sifa za uovu na ubabe unaozitendea nchi changa za ulimwengu wa tatu. Chidama anajitapa kwa kughani ifuatavyo:

Chidama: …
Joka la vichwa saba
Lakini ni joka moja tu
Moja katika saba na saba katika moja
Ewe mtambaa chini, mwenye meno ya sumu
Ngurumo lako kama radi ya kiangazi,
Wewe mbabe wababe
Haya na wende, nakutuma
Nenda ukatumbukize ukucha wako wa chuma ubavuni mwake
Ukamfutue na kumfumua matumbo yake …
(*Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk. 24*)

Shairi lingine alilolitumia Emmanuel Mbogo katika utunzi wa tamthilia yake ni lile la Ng'wanamalundi ambalo linaleta picha ya malumbano kwa jinsi linavyolijibu shairi huru na jigambo la mhusika Chidama la hapo juu. Ng'wanamalundi naye anajitapa ifuatavyo:

NG'WANAMALUNDI: (…*anampiga yule nyoka kwa mgwishu wake. Nyoka anatulia. Sasa anamkamata na kuanza kunuiza na kusema naye*)
Najua aliyekutuma
Lakini huyo si mlume sawasawa
Wewe ni tonga, hujawa tui bado.
Hu'chochote bali garasa,
Shushu la nyoka mgonjwa,
(*anamtemea mate*)
Lakini nakutambua wewe nani.
Najua ndiye wewe yule unukae damu ya maskini.
Huwezi kunizuga na mavazi uliyovaa.
Kwani sabuni na manukato
Havitoshi kutoharisha nuksi
Iliyoko ndani ya kichwa …
(*Ngoma ya ng'wanamalundi* - *kr 48 – 49* )

Emmanuel Mbogo kama Ebrahim Hussein, na Said A. Mohamed vilevile ametumia mbinu changamano kuwasilisha dhamira na maana kitaswira katika utunzi wa tamthilia yake kwa kuingiza vipengele vya mashairi huru ya aina ya mashairi simulizi ambavyo ni vya usanii wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi. Madondoo ya majigambo ya hapa juu ni mifano ya mashairi huru ambayo pia ni majigambo ambayo mtunzi ameyatumia kuumba tamthilia yake. Katika umbo zima la tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, hii ni mbinu mpya na ya kisasa anayoitumia mwandishi kuwasilisha hisia zake kwa kujenga taswira halisi inayomwezesha msomaji kuelewa dhamira za mtunzi na kuwa na maonjo kamili ya utamaduni wa Kiafrika. Matumizi ya mbinu hii mpya ya utunzi hasa ya sanaa za maonyesho ya jadi ya majigambo na ushairi huru unaotumia ishara za ndani kuwasilisha hisia na maono ya ndani yanampa msomaji na mtazamaji wa mchezo changamoto ya kujaribu kufasiri matumizi ya aina hiyo kiusomi na kitaaluma. Matumizi ya sanaa za maonyesho za jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili huzua athari fulani kwa msomaji, msikilizaji na mtazamaji wa mchezo wa kuigiza inayomwezesha mtunzi kuchanganua mawazo yake ya ndani pamoja na fikra za hadhira yake.

Holcombe (2007) anaeleza kuwa mitindo ya utunzi wa tamthilia na mashairi ya kisasa ni mwafaka katika kusawiri masuala ya kisasa. Watunzi wa sasa wa tamthilia wameasi urasimi wa tamthilia ya ki-Aristotle na ushairi wa kimapokeo na kujaribu miundo mipya ya tamthilia mpya ya Kiswahili. Utunzi wa tamthilia wa awali ulizingatia matumizi ya kanuni rasmi za ki-Aristotle. Waandishi hawa sasa ni waasi wa kanuni hizi kwani hawataki kufungwa na uhalisia na utamaduni wa uandishi. Kwa kuchanganya mbinu za ki-Aristotle na mbinu zilizohalisiwa katika sanaa za maonyesho ya asili ya Kiafrika, waandishi wa tamthilia wanadhihirisha kuwa wangependa kuwasilisha maoni yao wakiwa huru.

**7.2 Usimulizi Katika Tamthilia ya Kiswahili**

Licha ya uigizaji na utendaji wa sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika kupigwa marufuku na wakoloni kwa madai ya kupinga maendeleo na maenezi ya dini yao ya Kikristo na kuwa za kiuchawi, sanaa hizo zimetumiwa na watunzi wa tamthilia nyingi za kisasa kama malighafi na mbinu ya utunzi wa kazi zao. Watunzi wa tamthilia ya Kiswahili wametumia mbinu ya usimulizi na majibizano, katika kujenga fani na dhamira zao katika tamthilia ya Kiswahili kama ilivyopendekezwa na Aristotle. Masimulizi katika tamthilia teule za Kiswahili vilevile yanadhihirisha matumizi ya mbinu za usimulizi zinazopatikana tu katika sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika kama ilivyofanyika katika shughuli asili za Kiafrika za uzalishaji mali pamoja na shughuli zingine za kijamii na za maisha ya kawaida katika mazingira ya Kiafrika kama matambiko, pungwa, jando, unyago, arusi, matanga na sherehe zingine za kitamaduni za Kiafrika. Katika shughuli hizi za kitamaduni, watu wa jamii walipiga na kucheza ngoma, waliimba, walikariri mashairi na kughani majigambo. Nyumbani hasa wakati wa jioni, watoto na wakati mwingine watu wazima walimzunguka nyanya yao ili kumsikiliza akisimulia hadithi, visasili na matukio mbalimbali kuhusu historia ya kabila au jamii yao. Almuradi sanaa za maonyesho katika jamii za Kiafrika zilikuwa shughuli na sehemu ya maisha ya Mwafrika wa kawaida katika nyakati za jadi.

Katika tamthilia za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi*, watunzi wametumia mbinu ya kuwafanya wahusika wao kuongea moja kwa moja na hadhira wakiwa jukwaani. Uwasilishaji wa sanaa za maonyesho ya jadi na tanzu za Fasihi Simulizi katika jamii za Kiafrika ulifanywa kwa njia ya kutagusana kati ya fanani na hadhira yake. Tamthilia ya *Giza Limeingia* (1980) iliyotungwa na Emmanuel Mbogo vilevile inamfanya mhusika kuongea moja kwa moja na hadhira

yake kama mbinu ya mtunzi kuihusisha hadhira katika uwasilishaji wa kazi yake. Katika Sehemu ya I ya Onyesho la I la tamthilia ya *Mashetani*, mhusika Juma anawazungumzia moja kwa moja watazamaji wa mchezo wa **Mashetani** ili kuwaeleza lile linalofuata:

> JUMA: Wananchi**; kwa mara nyingine chini ya mbuyu huu mimi Juma, na rafiki yangu Kitaru, tutakuonyesheni mchezo wa Shetani na Binadamu. Mimi nitakuwa Shetani na Kitaru, atakuwa Binadamu** *(Mashetani – uk 1).*

Mtagusano kati ya wahusika na hadhira wa aina iliyoko katika dondoo la hapa juu unapatikana tu katika sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika. Ebrahim Hussein ameichota mbinu hiii ya kale na kuitumia katika utunzi wa tamthilia yake.

Katika utanzu wa ngano, utambaji hadithi na kama tulivyotangulia kutaja awali hapo juu, watoto na watu wazima wangemzunguka bibi fanani akisimulia ngano na visasili kuhusu jamii yao ambapo pia wangeshiriki katika usimulizi wenyewe huku wakiota moto na kungoja chakula cha jioni baada ya kazi ngumu na ada zingine za kutwa. Katika Sehemu II, Onyesho la III la tamthilia ya *Mashetani*, Ebrahim Hussein ameichota mbinu ya usimulizi wa kingano wa asili ya sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika pale anapomtumia mhusika wake Kitaru kumsimulia mamake hadithi aliyosimuliwa na bibi yake Juma. Kwa kuifanyia ufaraguzi wa kuwezesha utanzu wa hadithi kuchukuana na muundo wa utanzu huu wa tamthilia, mtunzi anamfanya Kitaru kuwa fanani msimulizi na mama yake kuwa hadhira yake wa pekee anayeisikiliza hadithi hiyo. Kwa kutaja kwamba Kitaru anamsimulia mamake hadithi ambayo yeye pia alikuwa amesimuliwa na bibi ya Juma, sifa ya masimulizi ya sanaa za maonyesho kuwa Fasihi Simulizi ni sanaa inayopokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine inadumishwa. Kitaru anamsimulia mama yake hadithi ya mnyama mkubwa hatari aitwaye chewa anayeishi katika bahari kubwa ya mbali inayofikiwa baada ya kuvuka

bahari saba. Mazingira na mbinu za usimulizi wa hadithi ya chewa katika tamthilia hiyo ya *Mashetani* zote ni za kimapokeo kama zilivyo katika usimulizi wa hadithi za kimapokeo za Kiafrika. Mtunzi anaitumia mbinu hiyo kama ifuatavyo:

> KITARU: Hadithi ya chewa. Mbali sana, ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa. Chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake, kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa tu na mkondo wa maji, ikitaka isitake. Na huyu chewa, siyo chewa bali Shetani *(Mashetani - kr 27 -28).*

Wakati wa ukoloni, drama ilikuwa kwa ajili ya kuwaburudisha Wazungu na kuwabagua Waafrika kwa kuwadhihaki na kuwacheka kwa hali yao ya umaskini wakilinganishwa na Wazungu. Tamthilia hiyo ya kichekesho ya kuwaburudisha wakoloni ilizingatia muundo wa ki-Aristotle. Watunzi wa Kiafrika vilevile walitumia muundo wa ki-Aristotle katika kubuni tamthilia zao. Tamthilia ya Kiswahili ya sasa imebadilika na inajumuisha mbinu mseto za ki-Aristotle na sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika.

### 7.3 Mitindo, Dhamira na Lugha ya Utunzi

Watunzi wa mwanzoni katika eneo la Afrika Mashariki walitumia Kiingereza na lugha nyingine za kizungu kutunga tamthilia zao. Hata hivyo, kufikia miaka ya 1970, watunzi wengi wa Kiafrika waliweza kutunga kazi zao kwa lugha zao za Kiafrika kama mbinu ya kuwawezesha kurudi katika mizizi ya utamaduni wao. Watunzi wa tamthilia katika nchi nyingine za Kiafrika kama Zaire (Democratic Republic of Congo ya sasa) hata hivyo waling'ang'ana kutunga tamthilia zao kwa lugha za watawala wao wa kikoloni kama Kifaransa na Kiingereza badala ya kutumia lugha zao za asili. Emmanuel Mbogo alitunga hadithi yake ya kwanza iliyochapishwa katika jarida la "Morani" la Chuo cha Ualimu wa Shule ya Msingi cha Morogoro alipokuwa anasomea taaluma ya ualimu katika mwaka wa 1967 kwa lugha ya Kiingereza. Huu

ulikuwa wakati wa nchi za Afrika kujinyakulia uhuru. Hadithi yake kwa jina, 'James I die for you" iliandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Katika miaka ya mwisho ya ukoloni, watunzi wengi wa nchi za Afrika Mashariki , walianza kutumia lugha ya Kiswahili katika kubuni tamthilia zao za Kiswahili. Katika mwaka wa 1967, Ebrahim Hussein alitunga tamthilia ya *Kinjeketile* na tamthilia za baadaye kama *Mashetani* 1971 kwa lugha ya Kiswahili.

Katika maudhui, tamthilia za Kiswahili za miaka ya themanini zilizungumzia masuala ya kijamii ya haki na usawa kama haki za wanawake na masuala ya kijinsia, haki za wafanyakazi na wanyonge kisiasa, kijamii na kiuchumi. Mifano ya tamthilia zilizoshughulikia usawa na masuala ya kijinsia ni pamoja na *Mke Mwenza (1982)* na *Wingu Jeusi* (1987) zilizoandikwa na Chacha, N. C., *Bibi Arusi* (1983) ya Kitsao, J., *Nguzo Mama* (1982) ya Mlama, *Lina Ubani* (1984) ya Muhando, P., *Ukame* (1984) na *Mkimbizi* (1988) za Mulwa na Yahya, A. S., *Maisha Subira* (1985) ya Omari, S. *Mama Ee* (1987) ya Mwachofi K. A.; miongoni mwa nyingine.

Miaka ya tisini na elfu mbili ilishuhudia tamthilia zenye dhima ya ukoloni mamboleo, mkengeuko na athari zake kwa maisha ya Mwafrika, ufisadi, ugaidi, magonjwa hatari kama UKIMWI na utandawazi miongoni mwa masuala mengine. Tamthilia hizo zinajumuisha *Kwenye Ukingo wa Thimu* (1988) ya Ebrahim Hussein, *Pungwa* (1988) ya Said A. Mohamed, *Wingu la kupita* (1999) na *Pango* (2003) zilizoandikwa na Wamitila K. W, *Kimya* (2011), *Janga la Werevu* (2011), *Mashetani Wamerudi* (2016) za Mohammed A. S., *Giza Limeingia* (1980) na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988); zote zilizoandikwa na Emmanuel Mbogo.

Mtindo wa uandishi pia ulibadilika kidogo na tukaanza kuona matumizi mengi ya sanaa za mashairi na nyimbo ambazo ni tanzu muhimu za sanaa za maonyesho ya jadi

katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Mbinu hii ilitumika kimakusudi jinsi ilivyo katika sanaa za maonyesho ya jadi na Fasihi Simulizi ya Kiafrika kwa lengo la kushirikisha watazamaji na hadhira nyingine na kuigiza utamaduni wa Mwafrika. Mbinu hii vilevile ilitumika kwa jinsi hii ili kuendeleza thamani za utamaduni wa Kiafrika. Tamthilia za *Pungwa* (1988) ya Said A. Mohamed, *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1999) ya Emmanuel Mbogo, *Kilio cha Haki* (1981) iliyotungwa na Mazrui, A., *Lina Ubani* (1984) yake Muhando, P. ni miongoni mwa tamthilia zingine ambazo zina matumizi mengi ya mashairi na nyimbo ambayo hayakuwepo katika tamthilia za hapo awali.

### 7.4 Matumizi ya Mwangaza Jukwaani na Mabadiliko ya Maonyesho

Katika miaka ya themanini na tisini, matumizi ya pazia na taa juu ya jukwaa au giza ni mbinu muhimu zilizotumika katika kugawa sehemu za tamthilia. Hata hivyo katika miaka ya baadaye ya elfu mbili mpaka sasa, kumekuwa na matumizi ya nyimbo zinazotumiwa katika utunzi wa tamthilia kwa ajili ya kugawa maonyesho ya tamthilia. Tamthilia ya *Pungwa* ya Said A. Mohammed na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ya Emmanuel Mbogo zilizoandikwa katika miaka ya themanini na tisini zinadhihirisha matumizi ya pazia, taa na giza jukwaani kwa ajili ya kugawa maonyesho ya tamthilia. Mbinu hii vilevile ilitumiwa jukwaani katika tamasha za muziki na maigizo ya shule za msingi na upili, vyuo anuwai na vyuo vikuu ili kugawa sehemu za maonyesho yanayoigizwa.

Mwangaza wa rangi mbalimbali vilevile hutumiwa katika kubadilisha mandhari ya maonyesho au hata katika kuleta athari fulani inayokusudiwa katika jukwaa kwa mfano ya hatari, huzuni au ya furaha. Mtunzi Emmanuel Mbogo katika maelezo yake ya jukwaa mwishoni mwa Onyesho la Pili la tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1999) kwa mfano, anadhihirisha hali ya huzuni ya matanga wakati wa kumzika

mhusika Nyamiti aliyekuwa amekufa baada ya kufanyiwa uchawi na mganga Chidama kama ifuatavyo;

> "*Sasa katika taa za rangi nyekundu tunaona maandamano ya watu wamebeba jeneza. Wanapita katikati ya hadhira wakielekea kwenye jukwaa dogoo. Mwisho wa msururu huu wa watu ni Chibupa kashikana na Seche – wanalia. Hali na mwendo huu wa tanzia unaenda sambamba na muziki wa taratibu kabisa, wa huzuni, wa ala. Wafikapo katika jukwaa hili dogo wanaweka – au tuseme wanazika, wanatoka ... Taa zinazima kwenye jukwaa dogo lakini muziki unaendelea sambamba na matayarisho ya Onyesho la Tatu*."
> (*Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 14)*

Taa za rangi nyekundu, muziki wa ala unaochezwa taratibu ukiandamana na watu wanaolia jukwaani wakibeba jeneza mwishoni mwa onyesho zimetumiwa vizuri na mtunzi ili kudhihirisha hali ya majonzi na simanzi iliyowagubika waombolezaji kwa ghafla kwa mtu aliyekuwa sawa dakika chache zilizopita. Matumizi ya taa hizo nyekundu pia yamefanyika vizuri katika kusababisha taswira ya matanga katika tamthilia bila kufanya matanga yenyewe na katika kuhitimisha na kufikisha kilele kisa cha msichana Nyamiti aliyekuwa ameuawa kwa uchawi wa misukule.

Mwangaza wa taa au taa iliyozimwa baada ya kila onyesho vilevile umetumiwa sambamba na matumizi ya nyimbo. Mwishoni mwa kila onyesho la tamthilia za *Mashetani*, *Pungwa*, *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na hata katika tamthilia ya baadaye kabisa ya *Mashetani Wamerudi*, watunzi wa kazi hizi wanahitimisha maonyesho yao kwa kuzima taa au kwa kuandika neno "giza" kama ishara ya kufikia kikomo cha onyesho hilo.

Said A. Mohamed vilevile ametumia mwangaza katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kudhihirisha mwanzo wa siku nyingine. Mwangaza unapotumiwa jukwaani wakati wa maigizo unaweza kuleta athari ya mabadiliko ya siku, majuma, mwezi au hata mwaka. Mwangaza unapotumiwa mwanzoni mwa onyesho katika jukwaa unaweza kuonyesha mapambazuko wakati wa asubuhi au machweo jua

linapotua wakati wa jioni. Rangi mbalimbali za mwangaza hutumiwa ili kuonyesha mabadiliko haya. Said A. Mohamed katika onyesho la kwanza la sehemu ya tatu ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, anatumia mwangaza wa kurunzi kuonyesha mapambazuko wakati jua halijatoka:

> (*Tochi inaonyesha kudamka kabla jua halijatoka. Prof. anaonekana akisimama katikati ya shina la mbuyu kuwakaribisha …*) (*Mashetani Wamerudi – uk 63*).

Katika Sehemu III, Onyesho II, tamthilia ya *Mashetani*, mtunzi Ebrahim Hussein ametumia mwangaza wa kurunzi ili kubadilisha maonyesho kutoka kundi moja la watu lililoketi katika meza kwenda kundi lingine katika jukwaa kwa kumulika na kubadilisha mwangaza kwa zamu ili kumwezesha kubadilisha maonyesho. Mtunzi vilevile alitumia mbinu hii ya kurunzi ili kugawa maonyesho na kuonyesha maigizo yaliyo kando ya igizo lenyewe. Katika onyesho hilo, kuna majibizano kati ya wahusika MTUMISHI I na MTU I kuhusu kiwango cha 'whisky, double or single' aliyokusudia kuiagiza. Kwa kutumia mwangaza wa kurunzi, mtunzi anawezeshwa kubadilisha onyesho moja kwenda lingine kwa kulenga mwangaza wa kurunzi na kumulika au kuangazia moja kwa moja katika meza au jukwaa ambalo mazungumzo yanaendelea kati ya wahusika na hivyo kuendeleza maonyesho mawili sambamba.

> MTU 1: Imekuwa taabu, taabu, taabu tu. Ukenda doshahi, unatukanwa, ukija uzunguni, unadharauliwa.
> MTU 2: Sivyo hivyo bwana. Sivyo hata kidogo.
> MTU 1: Alaa! Sivyo namna gani? Sivyo, na wewe mwenyewe unaona dhahiri hivi hivi bwana. (*Spotlaiti meza ya pili*).
> (*Spotlaiti meza ya pili* - ***KUBADILISHA MAONYESHO)***
> JUMA: Upweke.
> Upweke una mbawa.
> Unarusha nyoyo za Binadamu juu kabisa.
> Chini linabakia ganda.
> Macho yanaona, akili inafikiri …
> Lakini … kiwiliwili hakihisi.
> (*Anacheka pole pole*.)
> Bibi anapuliza sumu.
> Sumu au mapenzi?
> Jaribu kupambanua:

> Naam, mara nyingi
> Mapenzi hugeuka sumu.
> (*Spotlaiti meza ya kwanza*.)
> (*Mashetani – kr 40 – 44 - Msisitizo ni wetu*).

Mazungumzo katika Sehemu III, Onyesho II yanabishana baina ya meza mbili ambapo kuna mazungumzo baina ya meza mbili kati ya watumishi wa mkahawa (MTUMISHI I na II) na wateja wao (MTU I na II). Matumizi ya mwangaza wa kurunzi au spotilaiti kama mtunzi anavyoiita yanamwezesha kuendeleza maonyesho mawili sambamba katika jukwaa moja kwa wakati mmoja. Kwa kulenga mwangaza katika meza tofauti, mtunzi anaweza kubadilisha mazungumzo na kwa njia hiyo kubadilisha mada ya mazungumzo.

Maendeleo ya kiteknolojia yaliyokuwepo katika mwaka wa 1971 wa utunzi wa tamthilia ya *Mashetani* yaliwezesha watunzi wa wakati huo kutumia msamiati wa majina ya Kiingereza kama *whisky, double* or *single* au *spotlaiti* kama ilivyo katika dondoo lililopo hapo juu. Msamiati ni kiungo muhimu vilevile katika uwezo wa mtunzi kubuni tamthilia ya Kiswahili inayovutia. Watunzi wanaweza kuchanganya lugha au kutumia lugha moja tu katika utunzi wao. Said A. Mohamed katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* iliyoandikwa baadaye katika mwaka wa 2016 vilevile, anadhihirisha mbinu ya kuchanganya lugha kwa kuingiza majina ya Kiingereza kama, “abrogation, grand narratives, public narratives, occidental, oriental”, miongoni mwa mengine. Kupitia kwa matumizi ya mbinu ya kuchanganya lugha ambayo imekita mizizi kwa muda mrefu wa utunzi, mbinu hii inafanyika kuwa mbinu kongwe ya utunzi inayokubalika. Watunzi wengi hutumia mbinu ya kuchanganya lugha kwa ajili ya kusisitiza ujumbe unaowasilishwa, kutofautisha matumizi ya lugha ya makundi ya waliosoma na wale hawakusoma au kunukuu usemi jinsi ulivyo ili ujumbe usibadilike na wakati huohuo kusema maneno jinsi yalivyosemwa katika muktadha wake asili.

## 7.5 Ufaraguzi wa Tanzu za Sanaa za Maonyesho katika Utunzi wa Tamthilia ya Kiswahili

Watunzi wa tamthilia za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi na Mashetani Wamerudi* wametumia ufaraguzi ili kuingiza tanzu za jadi za sanaa za maonyesho katika utunzi wa tamthilia zao. Mbinu ya ufaraguzi inadhihirika katika ufunguzi wa kifomula unaotumiwa katika tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho hasa katika jinsi watunzi hawa wanavyoanza utunzi wa tamthilia zao. Mtindo wa fomula ya ufunguzi na fomula ya kufunga ni maarufu kama asemavyo Murimi (2016) katika kuanza na kumaliza usimuliaji wa kisa katika utanzu wa masimulizi au hadithi wa sanaa za maonyesho ya jadi.

Said A. Mohamed ametumia nyimbo mwanzoni mwa kila onyesho kama fomula ya ufunguzi katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Mbali na kuwa na vichwa kwa kila onyesho la tamthilia hiyo yake, mtunzi anatumia utanzu wa nyimbo unaopatikana katika sanaa za maonyesho ya jadi zilizoasisiwa katika tamaduni za Kiafrika na zilizotungwa kwa lugha ya kishairi ili kufungua maonyesho ya tamthilia yake na kutanguliza mada anayokusudia kuishughulikia katika kila onyesho. Said A. Mohamed ametumia jumla ya nyimbo kumi na mbili katika ufunguzi wa maonyesho yake kumi na mawili ya tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Mtunzi Said A. Mohamed ametumia nyimbo na ngoma au mashairi simulizi katika ufunguzi wa tamthilia yake kifomula kama ilivyo katika tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika kwa ajili ya kuvuta makini ya hadhira na kuwadokezea kwa muhtasari yale anayoyazungumzia katika tamthilia yake. Kila wakati mhusika Mwanambele akianza kuimba wimbo na kucheza ngoma, anadhihirisha utendaji unaopatikana tu katika sanaa za maonyesho ya Kiafrika kama inavyodhihirika hapa chini:

> Mwanambele: (*Anaimba. Anapiga ngoma. Anacheza karibu na hadhira. Anaimba!)* (*Mashetani Wamerudi – uk 1*)

Uimbaji wimbo na uchezaji wa ngoma wa mhusika Mwanambele katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ungebadilishwa na fanani kila ilipohitajika kwa minajili ya kuleta athari iliyokusudiwa na mtunzi kwa hadhira. Nyimbo na ngoma zilichezwa kwa ajili ya kuarifu na kuhamasisha hadhira kuhusu ujumbe fulani muhimu mbali na kuiburudisha hadhira kama inavyoonyeshwa katika onyesho la tatu la sehemu ya kwanza:

> (Mwanambele anajitokeza kutoa burudani kwa hadhira. Anabadilisha mahadhi, sauti, wimbo, ngoma na uchezaji) (*Mashetani Wamerudi – uk. 15*).

Mianzo ya maonyesho yote katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* inatumia mbinu inayofanana ya nyimbo na ngoma. Mtunzi anaitumia mbinu hii kiubunifu kwa kuibadilisha kila akihitaji kulingana na muktadha wa mahitaji yake. Uimbaji na uchezaji ngoma huo unaambatana na uigizaji na utendaji wa maonyesho ya mhusika Mwanambele ambayo yanafanana na yale ya fanani wa sanaa za maonyesho. Urudiaji wa matumizi ya nyimbo na ngoma katika mianzo ya maonyesho ya tamthilia hiyo ni wa namna ya kifomula kwa jinsi zilivyotumiwa. Nyimbo na ngoma zimetumiwa mara nyingi tu katika mianzo ya maonyesho ya tamthilia mbalimbali za Kiswahili.

Mtunzi Emmanuel Mbogo vilevile ameanza utunzi wa tamthilia yake ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* kwa utanzu wa ngoma ya arusi ya kiasili inayotawala katika utamaduni wa Mwafrika. Mbogo amechota malighafi hii adimu ya jadi na kuitumia sio tu katika kujenga na kuimarisha umbo na dhamira ya tamthilia yake bali pia katika ufunguzi wa onyesho la tamthilia hiyo. Mbogo anaanza hivi katika onyesho la pili la tamthilia yake:

> NYAMITI (*Baada ya kusikiliza milio ya ngoma huku akipanga vitu pale sebuleni) (Ngoma ya Ng'wanamalundi – Uk. 3)*

Mlio wa ngoma unaorejelewa katika dondoo hili ni wa wimbo wa arusi unaochezwa katika jamii za Kiafrika na ambazo huambatanishwa na mdundo wa ngoma wakati wa kufunga arusi. Ngoma hii ya arusi ni utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi unaotumiwa kama utanzu mwingine wa ngomezi ambao hutumiwa na jamii nyingi za Kiafrika kwa ajili ya kuarifu jamii kuhusu matukio maalumu na muhimu kwa jamii. Mdundo wa ngoma ya Sindimba iliyokuwa inasikika kwa mbali inatumiwa na mtunzi katika ufunguzi wa onyesho la pili la tamthilia yake kwa ajili ya kuivuta nadhari ya hadhira kuwaarifu wanajamii kuhusu arusi iliyokuwa inatarajiwa kufanywa karibuni na katika kumwezesha mtunzi kuendeleza dhamira zake:

> *… Mirindimo ya ngoma ya arusi inaongezeka; Sasa tunasikia wanabadili mapigo na kunasikika mirindimo ya Sindimba.* Nyamiti anaruka kwa furaha Ee! Sindimba – Unyago! Wote huko arusini wanachemka ila mie tu. (Mirindimo ya Sindimba inaongezeka). Iko wapi kanga (anachukua kanga). Heri nicheze leo, kesho chambilecho somo yangu, niweke soni usoni! *(kesha jifunga kanga mbili kiunoni sasa anaanza kucheza. Kwanza ni polepole huku akiimba pamoja na waimbaji wa nje. Sasa mirindimo ya Sindimba inapamba moto, nae Nyamiti anapamba moto. Vigelegele vinasikika; naye anachemka zaidi … anapepesuka – anachoka, anajibwaga chini kwa furaha).*
> *(Ngoma ya Ng'wanamalundi – Uk. 11)*

Kianzio cha ngoma hii ya arusi kinatumiwa sambamba na kianzio cha usimulizi wa kingano. Mtunzi ametumia ngoma ya Sindimba kumhusisha msichana Nyamiti anayefanya arusi katika kusimulia tukio la arusi. Kama katika utanzu wa ngomezi, mtunzi amefanyia ngoma ya Sindimba ufaraguzi ili kuifanya kulia kutoka mbali kama ngomezi ili mlio wake usikike kutoka mbali kuiarifu jamii yake kuhusu tukio la ndoa linalofanyika. Msomaji au mtazamaji wa mchezo mara hiyo anaarifiwa kuhusu ndoa ya Nyamiti iliyokuwa inatarajiwa kufanyika karibuni. Nyamiti anapousikia mdundo wa ngoma ya Sindimba kule kwake anakofungiwa unyagoni, naye anachemka na mara anainuka na kujifunga kanga mbili tayari kuanza kucheza. Kisha Nyamiti anasimulia, "--- Ee! Sindimba – Unyago! Wote huko arusini wanachemka ila mie tu."

Mirindimo na mapigo ya ngoma ya Sindimba huwapa waimbaji, wachezaji na hadhira mchemko ambao huwapa hamasa na ari ya kutaka kucheza ngoma. Athari hiyo hiyo huipata hadhira inayosoma au kuutazama mchezo wa kuigiza vilevile.

Katika hali ya kawaida ya utamaduni wa jadi wa Kiafrika, mchezo wa ngoma ya arusi ni mchezo unaohusisha wanajamii wote katika kuucheza. Mtunzi hapa ameleta mabadiliko ya kimakusudi ili matumizi ya ngoma katika kujenga na kuimarisha tamthilia yake yaweze kumfaa. Kwa kuifanya ngoma hiyo ya ndoa kusikika kutoka mbali na nje ya onyesho na kumfanya mhusika Nyamiti ambaye ndiye biarusi kuwa mchezaji wa pekee mbele ya hadhira, msimulizi na mhakiki wa ngoma hiyo katika jukwaa la tamthilia hii yenye misingi ya ki-Aristotle, mtunzi ameitenga hadhira ya mchezo na wachezaji wa ngoma ya arusi ya Sindimba. Hadhira ya ngoma ya Sindimba sasa haiwezi kutagusana na wachezaji wa ngoma hiyo kama ilivyo kawaida katika misingi ya uchezaji wa ngoma ya arusi katika tamaduni na mila za Kiafrika. Ngoma ya arusi ni ngoma ya furaha inayowahusisha wanajamii wote. Nyamiti anasema, "… *anaruka kwa furaha Ee! Sindimba – Unyago! Wote huko arusini wanachemka ila mie tu*" (k.h.j.). Katika ufaraguzi huu wa ngoma ya arusi unaofanywa na mtunzi, Nyamiti katika mabadiliko hayo anatumika kama msimulizi na mhakiki anayeifahamisha hadhira kuhusu yaliyokuwa yanafanyika arusini. Mtunzi amemtumia mhusika Nyamiti katika tamthilia yake mbali na maelezo ya jukwaa kama kiunzi kati ya waigizaji na watazamaji cha kufafanua matukio, hisia na mawazo mbalimbali yanayoigizwa, jambo ambalo si la kawaida kufanyika kwa jinsi hiyo.

### 7.6 Tamasha za Muziki na Drama katika Shule na Vyuo

Mabadiliko makubwa yameingizwa katika uwasilishaji na uhifadhi wa sanaa za maonyesho ya jadi katika miaka ya hivi karibuni. Kabla ya majilio ya ukoloni kama tulivyotangulia kutaja, watoto na watu wazima wangemzunguka fanani aghalabu bibi

wakati wa jioni wakiota moto na kumsikiliza akitamba ngano, kutega vitendawili, kuimba na kughani tendi na mashairi huku akiigiza kwa kukonyeza, kuming'inya na kunengua viungo huku wakiburudika na kumshangilia kwa njia mbalimbali kwa njia ya kushiriki katika uwasilishaji huo. Mabadiliko katika hali ya maisha na mbinu za uzalishaji mali umefanya watu wengi kuhamia mijini kwenda kufanya kazi viwandani na katika maofisi ambapo jamii nyingi zimetenganishwa. Kizazi kichanga hufanya kazi mijini ilhali kizazi kizee kinabaki vijijini, huku watoto wakienda shule za bweni. Ili kuwashirikisha vijana katika utamaduni wa Kiafrika, juhudi mbalimbali za muziki na maigizo zinaandaliwa katika jamii katika viwango mbalimbali. Hivi sasa sanaa za maonyesho ya jadi zinahuishwa katika Fasihi Andishi kupitia kwa utunzi wa tamthilia, riwaya, ushairi na hadithi fupi ambazo zinadhihirisha matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho. Mashindano ya tamasha za muziki na drama katika shule za msingi, upili na vyuo anuwai pamoja na vyuo vikuu yanayoandaliwa na Wizara ya Elimu nchini Kenya pia hudhihirisha matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi.

Kamau (2006) anaeleza kuwa hadi mwaka wa 2000 ambapo utambaji hadithi ulianzishwa upya kama kipengele kingine cha kuigizwa katika tamasha za kila mwaka za michezo ya kuigiza katika shule na vyuo nchini Kenya na maeneo mbalimbali ya Afrika Mashariki, hadithi na tanzu nyingine za sanaa za maonyesho ya jadi na Fasihi Simulizi kwa jumla zilikuwa zimefifia kwa kupuuzwa. Wamitila (2003) anashadidia maoni haya kwa kusema kuwa sanaa za maonyesho na Fasihi Simulizi kwa jumla ilipuuzwa kwa miaka mingi hasa katika uhifadhi wake kwa njia ya maandishi. Kuongezea, ukosefu wa utafiti wa sanaa za maonyesho ya jadi na taasisi za elimu kupuuza ufundishaji wa taaluma ya sanaa za maonyesho na Fasihi Simulizi kulichangia katika kusahaulika kwa sanaa hizi. Kupitia kwa mashindano ya tamasha za muziki na drama ya shule na vyuo, wanafunzi wanaoshiriki katika tamasha hizo

pamoja na watayarishaji wake wamechukua jukumu la kuendeleza na kudumisha sanaa za maonyesho.

Tanzu zinazowasilishwa katika mashindano ya tamasha za muziki na drama katika eneo la Afrika Mashariki hufanyiwa mabadiliko ili kuafiki na kusawiri hali ya sasa na masuala ibuka ya jamii. Hadithi, vitendawili, nyimbo, mashairi, ngoma na tanzu nyingine za sanaa za maonyesho ambazo ni za jadi hubuniwa na kuigizwa jukwaani upya kwa njia ambayo huzifanya zichukuane na wakati wa utunzi wa sasa. Tanzu hizo zinaweza kutokana na tanzu asili za jadi zilizokuwa zinatambwa na jamii mbalimbali ambazo zinasanifiwa upya kuzipa umbo na mvuto wa kisasa. Kwa njia hiyo hiyo ya ubunifu, tanzu mpya vilevile zimeweza kubuniwa kutokana na tanzu nyingine kwa njia ya Kimwingilianomatini. Hata hivyo, tanzu nyingine huwa ni mpya kabisa na ambazo hazijawahi kusikika au kutazamwa hapo awali. Uwasilishaji wa tanzu hizi hata hivyo huwa na mabadiliko mengi katika mbinu za uwasilishaji wake kwani kuna haja ya kuyajadili masuala ibuka katika jamii na kuyasawiri mazingira katika uhalisia wake.

### 7.7 Mwingilianomatini kati ya Tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*

Kama ilivyoelezwa na mtafiti katika sura ya pili, Mwingilianomatini ni nadharia ya utunzi na uhakiki wa kazi za fasihi iliyoasisiwa na mwananadharia wa Kifaransa kwa jina Julia Kristeva ambaye pia aliibua kutokana na nadharia ya Usemezano iliyoasisiwa na Mikhail Bakhitin. Mwingilianomatini ni mtazamo uliojengwa kwa misingi kuwa matini ya kisanaa si zao la mwandishi mmoja bali ni zao la jinsi matini hiyo huhusiana na matini nyingine pamoja na miundo ya lugha yenyewe. Mtazamo huu husisitiza kuwa matini zote za kisanaa zaweza kuchukuliwa kama matini moja kuu ambapo hujibizana – kila moja ikisemezana na nyingine kwenye usemezano uliotanuliwa (Plotell na Charney 1978). Matini zinazoingiliana huhusiana kwa njia

moja au nyingine na matini zenyewe hutegemeana ili kuzalisha maana. Hivyo kazi moja ya fasihi huwa na uhusiano na kazi nyingine au zingine zilizoandikwa kabla yake kwa namna moja au nyingine. Utafiti wetu katika sehemu hii ulikusudia kuchunguza jinsi tamthilia za *Mashetani* (1971), yake Ebrahim Hussein na *Mashetani Wamerudi* (2016), iliyobuniwa na Said A. Mohamed zinavyoathiriana kimwingiliano katika matini na katika tanzu za sanaa za maonyesho zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia hizo.

Kwanza, mtunzi Said A. Mohamed ameipatia tamthilia yake anwani *Mashetani Wamerudi* katika mwaka wa 2016, jina ambalo vilevile lilitumiwa na mtunzi Ebrahim Hussein katika tamthilia yake ya *Mashetani* katika mwaka wa 1971. Anwani hizi zinafanana ila ananwani ya Said A. Mohamed ina nyongeza ya neno Wamerudi ambalo linarejea mashetani waliotoka na ambao wanarudi tena. Matumizi ya jina “Mashetani” ni baada ya karibu miaka hamsini na bado yanaafiki matumizi ya kisanaa katika utunzi wa tamthilia mpya na ya kisasa. Matukio ya kishetani yaliyosawiriwa na Ebrahim Hussein katika tamthilia yake ya *Mashetani* katika mwaka wa 1971 bado yanadhihirika katika kazi za watunzi wa kazi za sasa kama Said A. Mohamed katika mwaka 2016, katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi*, karibu miaka hamsini baadaye.

Katika hali ya kurejelea sehemu za tamthilia ya *Mashetani*, mtunzi Said A. Mohamed anatunga tamthilia yake kwa kurejelea dhana ya Shetani ambayo pia ameitumia kijazanda kama alivyofanya mtunzi Ebrahim Hussein. Said A. Mohamed anaandika ifuatavyo:

> Kijana1: **Shetani gani**?
> Prof.: Aha, unakusudia wale waliofanya michezo ya ajabu hapo zamani, na sasa wanakuja na mazingaombwe mapya … (*Anatoka nyuma ya kibanda. Anakutana na Prof.*)
> Prof.: Ndio **wale walioruka mibuyu na kuning'inia**. **Wale walioomba wachomwe visu na kufa. Wale waliocheza na kufundisha wananchi dansi ya "waltz**" … Unamsikia huyo kijana anaporomosha mizinga sasa. Tahadhari – (*Mashetani Wamerudi* - uk 11)

Maelezo haya ya Said A. Mohamed katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* yanarejelea kwa uwazi maelezo ya Ebrahim Hussein katika tamthilia yake ya *Mashetani*. Hussein katika Sehemu ya Kwanza, Onyesho la Kwanza anaanza tamthilia yake kwa kututangulizia kazi yake kwa mchezo ndani ya mchezo wa **Mashetani** kwa wahusika wawili marafiki ambao ni Juma na Kitaru kutufahamisha ya kwamba wao wangeonyesha wananchi mchezo kati ya Shetani na Binadamu. Kwa namna ya ki-Mwingilianomatini, Said A. Mohamed naye anarejelea mchezo huohuo na matendo na maigizo yao katika mchezo mhusika Kijana anapouliza "**Shetani gani**?" na mhusika Prof. kumjibu "… **wale walioruka mibuyu na kuning'inia**. **Wale walioomba wachomwe visu na kufa. Wale waliocheza na kufundisha wananchi dansi ya "waltz**" – (*Mashetani Wamerudi uk 11)*. Hussein anaandika hivi katika tamthilia yake:

> JUMA: Wananchi: kwa mara nyingine chini ya mbuyu huu mimi Juma na rafiki yangu Kitaru, tutakuonesheni mchezo wa Shetani na Binadamu. Mimi nitakuwa Shetani, na Kitaru atakuwa Binadamu. (*Mbio, Juma anaingia katika pango la mbuyu. Anakaa muda mrefu*) - (*Mashetani* – uk. 1).

Urejeshi wa Said A. Mohammed kwa kazi ya Hussein ni wa kimakusudi kwani amelalamika katika dibaji ya tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* kwamba imekuwa muda mrefu bila ya Hussein mwenyewe kuirejelea kazi yake hiyo kwa kuandika kazi nyingine inayoirejelea. Said A. Mohamed anajikita katika kuzungumzia kuhusu ukoloni mkongwe uliojigeuza na kuwa ukoloni mamboleo kupitia kwa mfumo mpya wa utandawazi unaofanywa kupitia kwa biashara, uhawilishaji wa bidhaa,

uenezaji wa habari wa kasi, vita, ugaidi, mafarakano ya kidini, miongoni mwa mbinu zingine. Hussein alikuwa ameyagusia masuala haya katika kipindi cha mpito wa nchi za Afrika kutoka katika ukoloni mkongwe na kujipatia uhuru wa bendera. Zaidi ya miaka arobaini baadaye, wale wakoloni wanarudi kuzitawala nchi za Afrika na ulimwengu wa tatu kupitia kwa mbinu mpya ya biashara na utandawazi. Shetani na Binadamu ni majina yaliyotumiwa kijazanda kurejelea mkoloni (Shetani) na Mwafrika (Binadamu). Mwafrika alimshinda mkoloni kwa kumpiga kisu mabavuni na baada ya kifo chake, Binadamu akasherehekea kifo chake kupitia kwa dansi ya Kimagharibi ya *Waltz* aliyofundishwa na mkoloni huyo. Hussein anaandika hivi katika tamthilia yake:

> SHETANI: Aaa, umetoa ahadi kuwa hutaniua mpaka nimalize maombi yangu matatu …
> SHETANI: Ombi la kwanza, nipe ruhusa kukuuliza swali, lakini usinijibu sasa. Umepata kumsikia nani akajichinja mwenyewe? (*Kimya*)
> Ombi la pili, kabla hujaniua mimi na wewe tusherehekee kifo changu.
> Ombi la tatu, wewe uchague namna ya kusherehekea kifo changu.
> BINADAMU: Maombi yako yamekubaliwa. Sherehe itafanywa.
> SHETANI: Na vipi tutasherehekea?
> BINADAMU: Kwa *waltz*. (*Mashetani* - kr 7 - 8)

Baada ya Shetani kukubaliwa maombi yake na Binadamu, anacheka kwa furaha na baada ya muda wanaanza kucheza *waltz* kwa furaha kubwa na kwa ustadi. Kwa vicheko na hanjam wanakunywa mvinyo katika sherehe ambayo inaishia kwa Shetani kumtegea Binadamu ubavu wake vizuri na Binadamu anakitumbukiza kisu katika ubavu. Katika mchezo huu, mtunzi anatoa taswira ya mkoloni kukubali kung'atuka kutoka Afrika kupitia kwa taashira ya kukubali kudungwa kisu na Binadamu na hatimaye kufa. Afrika inapata uhuru wa bendera na nchi za Afrika zinasherehekea kupata uhuru wao kupitia kwa kujitungia nyimbo za ushindi na kucheza ngoma kusheherekea ushindi wao wa uwongo. Hata hivyo, wakoloni walikuwa

wamewafundisha Waafrika kuwa wategemezi wao kupitia kwa kufundishwa aina ya ngoma ya ughaibuni inayoitwa *waltz*. *Waltz* ni dansi ya Kimagharibi ambayo Wazungu waliwafundisha Waafrika kucheza baada ya kupata uhuru wao wa bendera. Waafrika kucheza *waltz* na Wazungu ni ishara ya wao kufundishwa kufanya mambo yao kwa kuwategemea Wazungu. Hivyo, kupitia kwa dansi hii, nchi za Afrika hazipati uhuru wao wa ndani, kwani Waafrika wamefundishwa kutegemea nchi za Kimagharibi.

Mbali na Said A. Mohamed kutumia jazanda ya "Mashetani" iliyotumiwa na Hussein, vilevile anaingiza jazanda nyingine ya 'jogoo asiyeonekana na anayetoa mashuzi' anapowika au kupaparika kama anavyopenda kusema mwenyewe. Hussein alikuwa akirejelea Mzungu wakati wa ukoloni na jinsi alivyowadhulumu Waafrika kwa kuzitumia mbinu za kumdhuru Mwafrika jinsi afanyavyo Shetani. Mohamed vilevile alitumia mbinu hiyo ya Shetani kurejelea mkoloni aliyerudi katika hali mpya ya ukoloni mamboleo. Mzungu anaporudi tena kwa njia zisizo wazi kuja kuzitawala tena nchi za Afrika, anaongezea mbinu mpya zinazomzuga mwenyeji (Mwafrika). Kwa kusema jogoo anapaparika na kutoa mashuzi, mtunzi anamaanisha kwamba mbinu alizozitumia Mzungu kurudi ni hatari hivi kwamba Mwafrika anapojaribu kumzuia kuingia barani Afrika na kujikinga kutokana na athari zake, nguvu za ukoloni mamboleo zinamdhuru na kusababisha hatari kwake. Ukaribiano wa kiukoloni mamboleo kati ya Mwafrika na Wazungu wakoloni unasababisha madhara yanayowakilishwa kijazanda na kuumwa kichwa kwa mhusika Kijana 1:

> (*Kijana anarudi nyuma ya kibanda. Jogoo analia mfululizo kwa sauti kali anafukuzana tena na kijana huku jogoo anatoa mashuzi …*)
>
> Prof.: Ha! Ha! Ha! (*Anacheka kicheko kirefu, halafu ananuna huku anahema*) mizinga ni nini na mashuzi ni nini? Si hayohayo maji ya futi na nyayo? Ukiuliza kuwa hiyo ni mizinga wao wanasema ni mashuzi. Wanakataa

Mashetani kuwa wanaangamiza watu, huku wanasema hakuna aliyeumia. Aaaa! Ni mashuzi tu hayo. Tokea lini mashuzi yana maangamizi ya watu na mali ya watu?

Kijana 1: Ngoja nimfukuze. (*Nyuma ya kibanda. Kijana anamfukuza jogoo. Jogoo anapaparika. Kokoro kokoro, kokoro kokoro – jogoo anakokoreka. Halafu kimya. Kijana anajitokeza nyuma ya kibanda huku anapepesuka kama mtu aliyekunywa pombe. Anamwelekea Prof.*)

Prof.: Mbona unapepesuka?

Kijana 1: *(Anakamata kichwa chake huku akikaa pale kitini ambapo tayari Prof. amekwisha kukaa. Analalamika*) **Kichwa kinaniuma.**

Prof.: (*ana hasira kidogo. Anamkaripia kijana*) Nilikwambia usimfukuze wala usimkamate. **Usiwe karibu naye. Ni hatari kuwa naye karibu.**

…

Prof.: … **ukiwa karibu naye na ushuzi wake, ukikuingia bongoni basi utaumwa na kichwa milele … kisha utaumwa ugonjwa wa upumbavu daima!**

Kijana 1: (*Anashtuka*) Milele! Daima?

Prof.: Milele ndiyo. Daima! Utaharibika akili.

Kijana 1: Akili … Akili … atawezaje kumbadilisha mtu … Hivi kweli anaweza kuiharibu akili yangu? *(Anacheka huku anasimama na kwenda huku na huku akitazama hadhira*) – (*Mashetani Wamerudi* - uk 12).

Masuala anayoyashughulikia Ebrahim Hussein katika tamthilia yake ya *Mashetani* ndiyo anayoyashughulikia Said A. Mohamed katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi,* lakini katika vipindi tofauti na kwa namna tofauti ya kisanaa. Jogoo katika dondoo hili ni Shetani anayerejelewa na Ebrahim Hussein katika tamthilia ya *Mashetani*. Jogoo na Mashetani wametumiwa kijazanda kurejelea Mzungu mkoloni aliyeitawala Afrika wakati wa ukoloni na ambaye amerudi wakati wa sasa katika mfumo wa ukoloni mamboleo na kuwaathiri Waafrika kiuchumi, kisiasa na kitamaduni.

### 7.8 Tanzu za Jadi za Sanaa za Maonyesho kuwa Mianzo ya Tamthilia

Watunzi wa tamthilia ya Kiswahili wametumia tanzu mbalimbali za jadi za sanaa za maonyesho kama kianzio cha tamthilia zao. Watunzi wa tamthilia teule wametumia mchezo ndani ya mchezo, ushairi simulizi, majigambo, nyimbo na ngoma kama

kianzio cha tamthilia zao. Matumizi ya tanzu hizi za jadi za sanaa za maonyesho ya Kiafrika yameandamana na ufaraguzi wa tanzu hizo ili kuzifanya zichukuane na muundo wa tamthilia ya kisasa. Aidha, tanzu hizi zimetumika kimwingiliano ili kujenga umbo la tamthilia zenyewe.

Ebrahim Hussein ameanza tamthilia yake kwa mchezo wa kuigiza ndani ya mchezo wa tamthilia (mchezo ndani ya mchezo). Tamthilia inapoanza mbele ya mbuyu, mhusika Juma anatangazia hadhira kuwa yeye na rafiki yake Kitaru wangewaonyesha mchezo wa Shetani na Binadamu. "**Wananchi; kwa mara nyingine chini ya mbuyu huu mimi Juma, na rafiki yangu Kitaru, tutakuonyesheni mchezo wa Shetani na Binadamu**" (*Mashetani* - uk 1). Tamthilia nzima imeegemezwa katika mchezo huu wa Shetani na Binadamu ambao umefumwa kijazanda ili kumithilisha uhusiano wa Mwafrika na mkoloni wakati na baada ya ukoloni.

Said A. Mohamed katika tamthilia ya *Pungwa* na Emmanuel Mbogo katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* nao wameanza tamthilia zao kwa utanzu wa ngoma. Ngoma hurejelea nyimbo na dansi zenye misakato ya kiasili inayochezwa kuambatana na midundo ya ala za muziki. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (k.h.j.) inaeleza ngoma kwanza, kama ala ya muziki iliyotengenezwa kwa kuwamba ngozi katika mzinga, pili, kama mchezo wa kufuatia unaoandamana na ala ya muziki. Ngoma za kiasili hutawala katika utamaduni wa Mwafrika. Watunzi Said A. Mohamed na Emmanuel Mbogo wamechota malighafi hii adimu ya jadi na kuitumia kujenga na kuimarisha tamthilia zao za *Pungwa*, *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi*.

Anwani za tamthilia *Pungwa* na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* zimechimbuliwa kutokana na tanzu za sanaa za maonyesho za ngoma na tamaduni za Kiafrika. Tanzu hizi vilevile zimetumiwa kujenga fani na maudhui katika tamthilia zenyewe. Anwani

*Pungwa* imetokana na tamaduni za Kiafrika za kuwatoa watu pepo waliowapanda vichwani mwao kama namna ya kuwaponya kutokana na madhara ya pepo hao. Matumizi ya tamaduni hizi katika utunzi wa tamthilia ni wa kijazanda na unakusudia kuonyesha namna ya kuwaondoa pepo wakoloni kutoka bara la Afrika. Tamaduni za pungwa huandamana na sherehe za sanaa za maonyesho ya jadi. Emmanuel Mbogo aliipatia tamthilia yake anwani "Ngoma ya Ng'wanamalundi" kutokana na wimbo na ngoma ya kienyeji ambayo katika tamthilia inachezwa kama mbinu ya kuwahamasisha, kuwashajiisha na kuwazindua watu waliodhulumiwa na kunyanyaswa waweze kuinuka na kupigania haki zao

Ngoma ya Nyamiti imetumiwa na mtunzi katika ufunguzi wa tamthilia yake ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* kama kivutio cha kunasa nadhari ya wasomaji. Kwa kupandisha ari ya wasomaji ya kutaka kujua ni lipi litakalotokea baada ya Nyamiti kujipaka mafuta ya uchawi kichwani, mtunzi anakuza mbinu ya taharuki. Kinyume na furaha inayoandamana na uchezaji wa ngoma na sherehe ya arusi, Nyamiti anapochemka na kuingia katika ngoma, joto kali linampanda mwilini kwa sababu ya mafuta ya uchawi aliyojipaka wakati wa kurembesha nywele yake. Ngoma ya Nyamiti inafikia upeo wake pale Nyamiti "anapokata roho" na taharuki kufikia upeo. Mbali na kuitumia ngoma katika ufunguzi wa tamthilia yake, Mtunzi Emmanuel Mbogo ametumia ngoma mbalimbali katika tamthilia yake ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* kimakusudi kwa ajili ya kujenga fani na kuimarisha umbo la tamthilia yake na katika kuzitoa vizuri dhamira zake. Mbogo anaitumia ngoma hii kutuonyesha ila za wenye wivu na mahasidi wa ndoa pamoja na mbinu za kisanaa na kitamaduni wanazozitumia Waafrika katika kukomesha maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Said A. Mohamed ameanza utunzi wa tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* kwa mhusika wake Mwanambele kucheza ngoma kwa jina *Mchezo Mpya: "Roho Haifi"*. Aidha, Said A. Mohamed ametumia ngoma mwanzoni mwa kila onyesho katika maonyesho yote kumi na mawili katika tamthilia yake. Kianzio cha nyimbo na ngoma katika kila onyesho la tamthilia ni kuafikiana na mapendekezo ya mwanafalsafa Aristotle mtaalamu wa Kigiriki, kwamba utunzi wa tamthilia unamhitaji mtunzi kuanza maonyesho ya tamthilia yake kwa wimbo katika misingi ya tamthilia ya ki-Aristotle.

## 7.9 Muhtasari wa Maendeleo na Manufaa ya Sanaa za Maonyesho ya Jadi na Utamaduni wa Kiafrika

Katika sura hii ya saba tuliweza kushughulikia lengo la tatu la utafiti huu lililotuwezesha kujadili maendeleo na mabadiliko yaliyofikiwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili kwa kutumia tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika kama mbinu ya utunzi na nyenzo ya kuendeleza dhamira ya watunzi katika miongo mitano ya utunzi tangu uhuru. Ilidhihirika kwamba pamoja na utunzi wa tamthilia ya Kiswahili kuzingatia muundo wa tamthilia ya ki-Aristotle, waandishi wa tamthilia ya Kiswahili wameingiza mbinu za utunzi wa Kiafrika kwa kuingiza tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika katika utunzi wao.

Uchunguzi ulionyesha na kuthibitisha kwamba tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi za asili ya tamaduni na mila za Kiafrika zimetumiwa kibunifu na watunzi wa tamthilia ya Kiswahili kwa namna inayojirudiarudia katika kujenga fani na maudhui katika tamthilia ya Kiswahili. Licha ya mbinu ya uigizaji na utendaji wa sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika kupigwa marufuku na wakoloni kwa madai ya kupinga juhudi zao

za kueneza dini ya Kikristo, sanaa hizo hivi sasa zimechotwa na kutumiwa kama mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

Tamthilia ya Kiswahili ya awali hasa ya wakati wa ukoloni ilibuniwa kwa ajili ya kuburudisha na kuchekesha kwa njia ya kukejeli umaskini na watu ambao walichukuliwa kuwa hawakustaarabika, kusoma na kuandika kama wazungu. Tamthilia za sasa zinashughulikia masuala yote ya kijamii na zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kiafrika. Tamthilia ya Kiswahili ya sasa inajumuisha majaribio ya matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika.

Ilidhihirika vilevile kuwa, watunzi wa tamthilia ya Kiswahili walitumia mbinu ya ufaraguzi ili kuwawezesha kutumia tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia zao. Matumizi ya tanzu hizo za sanaa za maonyesho ya jadi zilibadilishwa na kufaraguliwa ili ziweze kukidhi mahitaji ya mtunzi na muktadha wa matumizi yao.

Kwa jumla, ilidhihirika kwamba watunzi wa tamthilia ya Kiswahili wameasi kanuni za urasimi wa tamthilia ya ki-Aristotle na ushairi wa kimapokeo na kujaribu miundo mipya ya utunzi wa tamthilia kwa kuchanganya mbinu za ki-Aristotle na mbinu zilizohalisiwa katika sanaa za maonyesho ya asili ya tamaduni za Kiafrika. Kwa mujibu wa msimamo wao, ilidhihirika kwamba waandishi wa tamthilia ya Kiswahili wangependa kuwasilisha maoni yao katika fasihi andishi wakiwa katika mazingira huru.

### 7.10 Hitimisho

Katika sura hii ya saba, tumeshughulikia matokeo ya utafiti huu kwa mujibu wa lengo letu la tatu la utafiti. Tuliweza kufafanua umuhimu wa tanzu mbalimbali za

jadi za sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika katika uumbaji na uimarishaji wa umbo na dhamira za tamthilia ya Kiswahili. Tuliweza kudhihirisha kwamba tanzu za jadi za sanaa za maonyesho ni kiungo muhimu kilichotumiwa na watunzi wa tamthilia ya Kiswahili kama mbinu yao ya utunzi.

Vilevile, ilidhihirika kwamba pamoja na watunzi wa tamthilia ya Kiswahili kuzingatia mapendekezo ya mwanafalsafa Aristotle kuhusu umbo la tamthilia, waliweza kujumuisha tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wao wa tathilia ya Kiswahili.

Katika sura ya nane inayofuata na ambayo pia ndiyo ya mwisho katika tasnifu hii, tulishughulikia muhtasari wa matokeo ya utafiti, mahitimisho ya matokeo ya utafiti wote kwa jumla na mapendekezo ya utafiti mwingine wa baadaye.

# SURA YA NANE

# MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 8.0 Utangulizi

Sura hii ndiyo ya mwisho katika utafiti huu. Sura yenyewe imetoa muhtasari wa tasnifu nzima kwa kurejelea matokeo ya utafiti wetu katika kila sura. Sura hii vilevile inatoa mahitimisho ya matokeo ya utafiti wetu mzima pamoja na kutoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye kwa mujibu wa ufasiri wa matokeo ya utafiti wote. Muhtasari wa matokeo ya utafiti wetu katika tasnifu hii ni kama ifuatavyo:

## 8.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti wetu ulikusudia kuchunguza mbinu za matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na utamaduni wa Kiafrika na taswira zinazoibuliwa na ubunifu wa aina hiyo katika tamthilia teule za Kiswahili. Ukusanyaji na uchanganuzi wa data katika tasnifu hii umefanywa katika jumla ya sura saba. Sura zote tangu ya mwanzo hadi ya saba zinaingiliana, kutagusana na kuchangiana kimfumo katika kukamilisha na kuimarisha ukusanyaji wa tasnifu hii nzima kama inavyodhihirika katika muhtasari wa hapa chini.

Sura ya kwanza imeshughulikia kuhusu suala la utafiti na usuli wa mada ya utafiti. Suala la utafiti la tasnifu hii lilizingatia matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika kama mbinu ya utunzi wa tamthilia mpya ya Kiswahili. Tamthilia ambazo zilichunguzwa zilikuwa zimechota vipengele vya sanaa za maonyesho ya jadi hasa ya asili ya tamaduni na mila za Kiafrika na kuvitumia kiubunifu katika utunzi wa tamthilia andishi ya Kiswahili. Watafiti walikuwa na makisio kwamba watunzi wa tamthilia ya Kiswahili wamechota na kuzitumia kiubunifu tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika kama mbinu ya utunzi wa tamthilia zao. Utafiti huu ulikusudia kuchunguza mbinu na namna ya

matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia teule za Kiswahili na taswira zinazoibuliwa na tanzu hizo kwa ajili ya kufufua na kudumisha utamaduni asili wa Kiafrika na kuakisi maendeleo yaliyofikiwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika kipindi cha karibu miongo mitano. Aidha, sura hii ilishughulikia malengo ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti na upeo na mipaka ya utafiti huu.

Katika sababu za kufanya utafiti katika sura ya kwanza, ilielezwa bayana kwamba utafiti huu ulikusudia kupambanua mbinu wanazozitumia watunzi wa tamthilia ya Kiswahili kuchota maarifa kutoka kwa utamaduni wa Kiafrika uliohifadhiwa katika sanaa za maonyesho asili, nia ya watunzi hao kuamua kutumia sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wao, kueleza namna ukiukaji kutoka sanaa za maonyesho ya jadi kwenda kwa Fasihi Andishi ulivyofanywa, mchango wa watunzi wa tamthilia ya Kiswahili katika kufikia uhuru wa kitamaduni na kuchangia katika uelewaji wa utamaduni wa Mwafrika na kwa jumla kufafanua mchango wa sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Upeo wa utafiti huu ulijifunga katika uchunguzi na matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Tamthilia zilizoshirikishwa katika utafiti huu ni *Mashetani*, *Pungwa*, *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* zilizoteuliwa kimakusudi baada ya kuthibitisha kwamba zilidhihirisha matumizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika baada ya usomaji wa awali. Matokeo ya utafiti huu yameelezwa katika sura za tano, sita na saba. Ilibainishwa kuwa utafiti huu utachangia katika uelewaji, uendelezaji na udumishaji wa utamaduni wa Kiafrika mbali na kutoa mchango kwa usomaji na uhakiki katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili.

Sura ya pili ya tasnifu hii ilishughulikia yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti pamoja na misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti huu. Katika yaliyoandikwa kuhusu mada ya

utafiti huu, sura hii imetaja na kufafanua tafiti zilizofanywa kuhusiana na sanaa za maonyesho ya jadi, utunzi wa tamthilia, malengo, matokeo na mchango wa tafiti mbalimbali kwa uchunguzi wa mada hii na tofauti ya tafiti hizo na utafiti huu. Ilibainika ya kwamba tafiti mbalimbali zimefanywa kubainisha umuhimu na nafasi ya tanzu za sanaa za maonyesho katika kubuni tamthilia ya Kiswahili yenye mwonjo wa tamaduni za Kiafrika. Tulifafanua kuwa utafiti wetu ungechunguza mbinu za matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili, taswira inayoibushwa na tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilizotumiwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na maendeleo ya mbinu za utunzi wa tamthilia ya Kiswahili yanayodhihirika katika kipindi cha karibu miongo mitano ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Nadharia za Uhistoria Mpya na Mwingilianomatini zilizoongoza utafiti huu vilevile zilifafanuliwa katika sura hii ya pili.

Sura ya tatu imefafanua muundo na mbinu za utafiti, mahali pa kufanyia utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za utafiti na ukusanyaji data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data iliyokusanywa. Utafiti huu ulifanywa kwa njia ya ufasili na kimaelezo uliotuwezesha kuwasilisha maelezo mengi asilia na ya kina. Ukusanyaji data ulifanywa kwa njia ya usomaji wa ndani na nje ya maktaba. Kazi zilizohusiana na mada ya utafiti huu na nadharia zilizoongoza utafiti wenyewe zilisomwa na kuhakikiwa. Usomaji zaidi ulifanywa kwa njia ya wavuti na mtandao ili kuendeleza uelewa wa mada na nadharia ya utafiti.

Sampuli ya vitabu vya tamthilia vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili vilivyoteuliwa kushirikishwa katika utafiti huu ilikuwa ya kimakusudi. Baada ya usomaji wa awali wa tamthilia nyingi za Kiswahili, ilidhihirika kwamba tamthilia za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi*, zote

zimechota tanzu za jadi za sanaa za maonyesho ya Kiafrika na kuzitumia katika utunzi wao. Aidha, tamthilia hizi zilizochapishwa kati ya 1971 na 2016 ziliteuliwa kimakusudi ili kudhihihirisha maendeleo yaliyofikiwa katika matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi kama mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili pamoja na kuwakilisha miongo mitano ya utunzi wa tamthilia andishi ya Kiswahili.

Mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu zilihusisha usomaji wa ndani na nje ya maktaba na katika mtandao hasa kuhusiana na malengo yote matatu ya utafiti ili kuleta uhalisia na uhalali wa matokeo ya utafiti wote kwa jumla. Tamthilia ziilizoteuliwa, vitabu vingine vingi, makala na machapisho mengine yaliyohusiana na nadharia iliyoongoza uchunguzi pamoja na kazi nyingine zilizokuwa na umuhimu uliohusiana na mada ya utafiti zilisomwa na kuchanganuliwa. Data iliyokusanywa ilinukuliwa, kuhaririwa, kufasiliwa na changanuliwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu na mihimili ya nadharia za Uhistoria Mpya na Mwingilianomatini. Baada ya uchanganuzi wa data, matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya uchanganuzi elezi. Hivyo, ripoti ya utafiti iliwasilishwa kwa njia ya maelezo ya moja kwa moja kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu, yakiambatana na ufafanuzi wa maelezo hayo. Ufafanuzi wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na maelezo mengine muhimu kutoka kwa vitabu, majarida na machapisho mengine yaliweza kunukuliwa kila kulipohitajika.

Sura ya nne imeshughulikia ufafanuzi wa dhana za tamthilia ya Kiswahili, sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika. Katika ufafanuzi huu, tulifafanua kuhusu chimbuko la tamthilia, maendeleo na matumizi, ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi katika vipindi vya ukoloni na baada ya ukoloni, mbinu za matumizi ya sanaa za maonyesho katika utunzi wa tamthilia, uainishaji wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na namna mbalimbali za matumizi ya sanaa za maonyesho katika kazi za fasihi.

Ilibidi kushughulikia kwa undani ufafanuzi wa aina hii kwa nia ya kudhihirisha pengo lililofaa kuchunguzwa kuhusu nafasi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

## 8.2 Matokeo ya Utafiti

Tuliwasilisha matokeo ya uchunguzi wetu katika sura za tano, sita na saba katika tasnifu hii kwa misingi ya malengo matatu ya utafiti huu ambayo tumeyawasilisha kwa muhtasari hapa chini.

### 8.2.1 Tanzu za Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Tamthilia Teule

Lengo letu la kwanza lilikuwa kupambanua tanzu za jadi za Sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika zilizotumika katika utunzi wa tamthilia teule za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* zilizoteuliwa kimakusudi kushiriki katika utafiti huu na kufafanua mbinu ya matumizi yao katika utunzi wa tamthilia hizo. Uchunguzi wetu ulibaini kwamba tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi za ngoma, nyimbo, mashairi simulizi, usimulizi wa kingano, majigambo, mazungumzo ya hotuba, soga, malumbano na semi za jazanda na mafumbo pamoja na tamaduni za Kiafrika za miviga ya unyago na arusi, pungwa, mahoka, uchawi na miujiza zilichotwa na kutumiwa na watunzi wa tamthilia zetu teule za Kiswahili katika kuumba na kuimarisha fani na dhamira katika tamthilia hizo kwa njia ya kujirudiarudia na kwa njia ya mwingiliano wa tanzu. Tamthilia zote zilizoteuliwa zilidhihirisha kuwepo kwa tanzu za jadi za sanaa za maonyesho mbalimbali zilizochangia katika uumbaji wa tamthilia hizo.

Tamthilia ya *Mashetani* ilidhihirisha matumizi ya tanzu za majigambo ya mhusika Shetani aliyejigamba kuhusu uwezo wake mkubwa wa kumfanyia Mwafrika mazuri na mabaya. Lugha ya kishairi ilitumika katika kutunga tamthilia yenyewe ikiwa na

mishorororo mifupimifupi, lugha ya kishairi yenye mnato na maneno na sauti zinazorudiwarudiwa. Mtunzi alitumia mbinu ya mchezo ndani ya mchezo kupitia kwa mchezo wa Shetani na Binadamu ambao aliutumia kiubunifu kujenga na kuendeleza tamthilia yake. Utanzu wa masimulizi umetumiwa kwa upana na marefu na wahusika mbalimbali katika tamthilia ambao wanahutubu au wanajizungumzia katika uzungumzi nafsi. Baada ya nchi za Afrika kujinyakulia uhuru wao, zilisherehekea uhuru wao kwa kujigamba, kujitungia na kucheza nyimbo na ngoma. Mtunzi Ebrahim Hussein amechota na kuzitumia vizuri tanzu za majigambo, nyimbo na ngoma kupitia kwa wimbo wa mhusika Binadamu anayesherehekea chini ya mbuyu baada ya kumuua Shetani (mkoloni) na kujinyakulia uhuru katika kubuni tamthilia yake. Wahusika Juma na Kitaru mbele ya mama yao wanadhihirishwa wakichongoana na wakifanyiana utani katika utanzu wa malumbano. Watunzi wa tamthilia ya Kiswahili kuendeleza kazi zao kupitia kwa mbinu hii ya malumbano ya utani na mchongoano, kunachangia katika uimarishaji wa umbo na uendelezaji wa dhamira za mtunzi wa tamthilia ya *Mashetani*.

Mchezo wa Shetani na Binadamu katika *Mashetani* vilevile umetumiwa Kimwingilianomatini kama fumbo. Mtunzi amefumba uhusiano wa Mwafrika na mkoloni kupitia kwa fumbo la Shetani na Binadamu wanaocheza mchezo wa Shetani na Binadamu. Mchezo wenyewe unawakilishwa kupitia kwa utanzu wa masimulizi. Mbali na mbinu ya mazungumzo, wahusika Shetani na Binadamu wanasimulia matukio mengi katika mchezo huo kupitia kwa uzungumzi wa nafsi ya kwanza. Matendo ya mhusika Shetani katika mchezo wa Shetani na Binadamu ya kujigeuza vitu mbalimbali kama ndege, upepo, kiti, nafsi na vitu vingine yanasheheni matukio ya kimiujiza ambayo yana misingi yake katika utamaduni wa Kiafrika.

Said A. Mohamed katika tamthilia yake ya *Pungwa* ameanza utunzi wake kwa ufunguzi wa kingomezi. Ngomezi ni utanzu wa sanaa za maonyesho ya jadi unaotumia mapigo ya ngoma na wakati mwingine kuuandamanisha na kilio au kamsa ya aina fulani ili kupitisha ujumbe wa dharura kwa jamii. Mtunzi anaanza utunzi wake katika chanzio cha tamthilia yake kwa kupiga kamsa ya kingomezi inayodhihirisha kwamba ana jambo la dharura la kulipitisha kwa jamii. Ngomezi inafuatilizwa na usimulizi wa kingano katika nafsi ya kwanza kupitia kwa mhusika Mzuka. Nyimbo na ngoma zimetumiwa na mtunzi kupitisha ujumbe wake na vilevile kujenga umbo la tamthilia yake. Mtunzi Said A. Mohamedvilevile amebuni tamthilia yake kwa utanzu wa majigambo kupitia maghani ya mhusika Mzuka. Mhusika Mzuka anajigamba kwamba hakuna mtu anayefahamu uwezo na vipawa vyake vya kuabiri mabahari na kufika mbali katika mabara ya Afrika na kwingineko kuzikofikika na wengine. Jigambo hilo linafumba kijazanda uwezo wa mkoloni kusafiri kutoka kwao mbali Ulaya kwa meli wakati wa ukoloni ili kuja kuzitawala na kuzikandamiza nchi za Afrika na za ulimwengu wa tatu. Umbo la jigambo lenyewe na tamthilia nzima kwa jumla ni la kishairi kwani kuna matumizi ya mishororo mifupimifupi, mapigo ya sauti zinazoimbika na zinazoweza kukaririwa, kusemwa au kughaniwa na kuwa katika mpangilio wa kishairi ambao ni huru na usiozingatia sheria mahususi za utunzi.

Imani na itikadi za kitamaduni za pungwa zimetawala katika utunzi wa tamthilia ya *Pungwa*. Pungwa ilielezwa kuwa njia mojawapo asili ya utamaduni wa Kiafrika ambayo hutumiwa na wanajamii kuwatoa watu mashetani na pepo wabaya waliowakumba na ambao husemekana kukaa kichwani mwao ambamo wamejiwekea viti na vilinge vya kukalia. Tamthilia yote ya *Pungwa* imejengwa juu ya kisa cha mhusika Bwana ambaye amepandwa na pepo ambao wanamsababishia ugonjwa wa wasiwasi ambao unamfanya kukosa usingizi. Kisa cha pepo kuwapanda viongozi

ambacho kinatokana na sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika ni mbinu ya kisanii anayoitumia mtunzi kuakisi na kuweka wazi matatizo ya ukoloni mamboleo, uongozi mbaya, tamaa na ubadhirifu wa viongozi, yanayozikumba nchi za Afrika na zile za ulimwengu wa tatu. Bwana ambaye ni kiongozi katika nchi yake alihitaji kupungwa na wachawi, mahoka, buruhani na waganga mahiri katika majaribio ya kutoa pepo waliompanda ili kumrejesha katika hali yake ya awali ya afya nzuri. Matumizi ya mbinu ya tamaduni za pungwa kujenga tamthililia ya *Pungwa* ni ya kijazanda inayotumiwa na mtunzi kumithilisha jinsi nchi za Afrika zilivyonyakuliwa na wakoloni ambao wanahitaji kuondolewa. Matumizi haya ya kijazanda ya tamaduni za jadi za Kiafrika yaliyoandamana na sanaa za maonyesho katika utunzi wa tamthilia ya *Pungwa* yalihitaji kufafanuliwa ili kuelewa maana ya ndani inayojengwa na johari hiyo ya kitamaduni.

Uchunguzi wetu, vilevile, ulionyesha jinsi mtunzi Emmanuel Mbogo alivyodhihirisha ufundi wa kutumia tanzu za jadi za sanaa za maonyesho katika kujenga tamthilia yake ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* kwa njia ambayo inajirudiarudia na ya Mwingilianomatini na tamthilia nyingine zilizoteuliwa kushiriki katika uchunguzi huu. Tanzu za jadi za sanaa za maonyesho za asili ya tamaduni za Kiafrika zilizotumika kujenga tamthilia hiyo ni pamoja na ushairi simulizi, usimulizi wa kingano, ngomezi, soga, malumbano ya utani, ngoma na nyimbo. Mtunzi alitumia ngoma ya Nyamiti ambayo ni ngoma ya furaha inayochezwa wakati wa arusi au wakati wa kumtayarisha mwanamwali kwa ndoa wakati wa unyago. Mtunzi aliitumia ngoma hii katika utunzi wa tamthilia yake ili kuonyesha na kusaili utayarishaji wa vijana wa sasa kwa maisha ya baadaye ya ndoa. Ngoma hii inaonyesha jinsi Nyamiti alivyokuwa tayari kuolewa na mwanamume ampendaye kwa jina Chibupa badala ya

kuponzwa na utajiri wa mwanamume ambaye ni mganga laghai asiyekuwa na maadili mema kwa jina Chidama.

Chidama ni mfano wa wanaume walio na wivu ambao hawajali kuhusu furaha ya watu wengine na ambao huwatendea maovu ya aina mbalimbali. Chidama amechorwa kuwa mhusika dhalimu ambaye huwaua watu na baadaye kuwafufua ili aweze kuwafanya watumwa wake mazuzu (vizuu). Mhusika huyu aliwatumikiza kwa lazima wafanyakazi hao vizuu katika kazi zake bila kujali haki zao. Aidha, ngoma ya "sindimba" ambayo pia ni ngoma tupu ya arusi imetumiwa na mtunzi kama utanzu wa ngomezi ili kupitisha ujumbe wa arusi kwa jamii. Katika mabadiliko aliyoyaleta mtunzi katika ubunifu wake wa kuifanya ngoma ya arusi kusikika kutoka mbali badala ya kuionyesha yenyewe ikitekelezwa hadharani katika tamthilia na kumfanya mhusika Nyamiti kuwa mchezaji wa pekee mbele ya hadhira, anamfanya Nyamiti ambaye ndiye biarusi kuwa msimulizi na mhakiki anayeifahamisha hadhira kuhusu yaliyokuwa yakifanyika kule arusini. Kwa njia hii uwasilishaji wa ngoma ya sindimba unabadilika na kuwa utanzu wa ngomezi wa utamaduni wa Kiafrika ambao ni mbinu ya kupasha habari na kuiarifu jamii kuhusu yaliyotokea au yanayotarajiwa baadaye katika jamii hiyo.

Ngoma ya Chidama ilitumiwa kama ngoma ya unyanyasaji na ukandamizaji wa watu wa tabaka la juu kwa watu wa tabaka la chini, hasa wale wasiokuwa na mitazamo inayofanana na ile ya viongozi na watawala wengine. Ngoma ya Ng'wanamalundi kwa upande mwingine ilitumiwa na mtunzi Emmanuel Mbogo kama ngoma ya ukombozi ya kuwazindua walionyanyaswa katika jamii kwa kuwahamasisha kupigania haki zao ili kujenga usawa wa kijamii.

Pia ilibainika ya kwamba mtunzi Emmanuel Mbogo ametumia tanzu za mazungumzo za hotuba, malumbano ya utani na soga katika kujenga tamthilia yake na kuwasilisha ujumbe wake kwa njia mwanana. Utanzu wa mazungumzo ni mbinu kongwe ya uwasilishaji wa sanaa za maonyesho ya jadi kwani tanzu nyingi ziliwasilishwa kwa hadhira kiubunifu kupitia kwa njia ya mdomo. Mbinu ya mazungumzo iliandamanishwa na tamathali za usemi kama methali, semi, nahau, mafumbo, jazanda na stiari zilizotumiwa kuupatia ujumbe uzito. Mhusika Chidama katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* kwa njia ya uzungumzi nafsi, anahutubia hadhira kuhusu wafanyakazi wake vizuu ambao amewazuga kwa mbinu za uchawi na kuwafanya mazuzu ambao hawalalamikii hali yao mbaya ya kufanya kazi wala kudai haki na mahitaji yao ya kibinadamu. Chidama vilevile anafanya mazungumzo ya hotuba ya pekee pale anapojigamba hadharani kuhusu uwezo wake wa ajabu wa kuwageuza Binadamu wa kawaida na kuwafanya watumwa vizuu wasiojielewa na wanaotumikizwa katika kazi ngumu za ujima.

Ilidhihirika ya kwamba tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi za soga na malumbano ya utani ziliwasilishwa kupitia kwa uzungumzaji wa aina moja. Soga ya kupitisha wakati kati ya wahusika Seche na Nyamiti katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* vilevile ilihitimu kuwa malumbano ya utani kwani marafiki hao wawili wanajibizana papo hapo kwa kutaniana na kufanyiana dhihaka iliyozoeleka kati ya marafiki na ambayo haidhamirii kuudhi.

Tanzu za sanaa za maonyesho zilizotambuliwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* zilijumuisha jumla ya nyimbo saba ambazo mtunzi Said A. Mohamed alizitumia kama kitangulizi cha kila onyesho la tamthilia yake pamoja na kuwa muhtasari wa ujumbe alioukusudia kuuwasilisha katika onyesho husika. Tanzu nyingine za ngomezi, tamathali za usemi kama nahau, methali, mafumbo na jazanda

zilibainishwa na matumizi yao kufafanuliwa. Usanii wa fanani uliambatanishwa na uigizaji na sanaa za maonyesho pale fanani alicheza akiimba, alisimulia na kughani vilevile, kuchezesha mabega na viungo vingine vya mwili, kukonyeza macho, kufanya ishara za mwili na nyuso huku akicheza ala za muziki. Uwasilishaji wa maigizo kwa njia hii, kuimba na kucheza ngoma kulibainishwa kuwa sifa muhimu ya sanaa za maonyesho ya tamaduni za Kiafrika za jadi zilizotumiwa na mtunzi kama nyenzo ya utunzi wa tamthilia yake ya Kiswahili. Matumizi ya msamiati "pepo", "Mashetani" na "jogoo" ambao pia umetumiwa Kimwingilianomatini katika tamthilia nyingine za *Mashetani, Pungwa* na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* yalidhihirishwa kuwa ya kijazanda na yalifafanuliwa kuwa taswira kongwe inayojirudiarudia iliyotumiwa na mtunzi kuwakilisha ukoloni mamboleo na madhara yake kwa nchi changa za Afrika na ulimwengu wa tatu. Tlifanikiwa kupambanua kuwa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrka ulitumiwa kisanaa kama mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ya kisasa. Utafiti wetu ulifanikiwa kudhihirisha kwamba sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika zimetumika kama mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

### 8.2.2 Taswira ya Tanzu za Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Tamthilia Teule

Uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti katika sura ya sita ya tasnifu hii uliegemezwa katika lengo letu la pili la utafiti huu la kuchanganua taswira zilizojengwa na kuibuliwa kupitia kwa matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia teule za Kiswahili. Tamthilia zote nne za *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* zilizoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu zilidhihirisha matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia za Kiswahili katika mapito ya kipindi cha karibu miongo mitano ambayo pia yaliibua taswira mbalimbali

ambazo vilevile zilichangia katika ujenzi wa umbo mahususi na dhamira za watunzi katika tamthilia hizo teule.

Utafiti ulidhihirisha kwamba tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho ya jadi zilitumiwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na ziliibusha taswira mbalimbali za kimaana katika tamthilia zote zilizoteuliwa za *Mashetani*, *Pungwa*, *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi*. Tanzu hizi za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika zilitumiwa Kimwingilianomatini kwa njia ya mwondoano. Mashetani na pepo ambao ni taashira ya wakoloni na mchezo wa Shetani na Binadamu umetumiwa na mtunzi Ebrahim Hussein kutoa taswira ya unyanyasaji na ukandamizaji unaosababishwa na ukoloni na ukoloni mamboleo ulioletwa na nchi za Magharibi na za ulimwengu wa kwanza kwa nchi maskini za Afrika na zingine za ulimwengu wa tatu. Ukoloni mkongwe uliozaa ukoloni mamboleo unaendeleza hali za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutawala katika nchi za Afrika zinazozifaidi nchi za ulimwengu wa tatu kimaendeleo na kuzinyanyasa nchi za Afrika.

Ukoloni mamboleo unatamalaki na kushakini nchi za Afrika afanyavyo Shetani anapowapanda vichwa wahusika Bwana katika *Pungwa* na Binadamu katika *Mashetani* na Kijana 1 anayefukuzwa na Jogoo katika *Mashetani Wamerudi*. Watunzi wa tamthilia hizi wametumia stiari ya Mashetani, jogoo na pepo zinazopatikana katika sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika kujenga na kuendeleza dhima ya nchi za Magharibi kuzinyima nchi za Afrika na za ulimwengu wa tatu uhuru wa kujifanyia mambo yao ya ndani kama nchi huru na kujiendeleza kiuchumi, kijamii na kiutawala.

Watunzi wote wa tamthilia zetu teule wametumia tanzu za ngoma na nyimbo za sanaa za maonyesho ya jadi kuchora taswira ya unafiki, ubadhirifu na unyanyasaji. Ebrahim

Hussein anawaonyesha Waafrika wakisherehekea uhuru wao wa bendera kwa kiburi kwa nyimbo na ngoma. Punde tu baada ya kujinyakulia uhuru wao, Waafrika walisherehekea kwa ngoma na nyimbo kwa sherehe kubwa zenye ubadhirifu na Waafrika wengi kuingiwa na unafiki wa mabepari waliotoka na kuanza kujilimbikizia mali kwa njia ya wizi na kutumia mali ya umma kiubadhirifu kwa mawazo potovu kuwa huu ulikuwa wakati wa Mwafrika kula. Mhusika Baba Kitaru anaimba wimbo kwa lugha ya Kiingereza kwa jina "Papa black sheep I like some money" kusherehekea kwake kununua gari jipya la bei ghali ambalo ni wazi amelinunua kwa pesa za umma.

Said A. Mohamed katika *Pungwa* alitumia utanzu wa majigambo kupitia kwa mhusika Sauti ya Mzuka kujenga taswira ya ukoloni mamboleo na madhara yake kwa nchi za ulimwengu wa tatu. Sauti ya Mzuka inatongoa historia ya utawala wa nchi za Afrika kuanzia kipindi cha wakati wa ukoloni hadi kipindi cha sasa cha ukoloni mamboleo na utandawazi. Mtunzi anatumia utanzu wa majigambo kudhihirisha ya kwamba Afrika ilitawaliwa kimabavu na nchi za Magharibi na sasa vilevile zinatawaliwa na nchi hizo katika mfumo mpya wa ukoloni mamboleo na utandawazi. Kwa kuwateka viongozi wa nchi za Afrika katika stiari ya kupandwa vichwa na pepo, viongozi hao wanafanywa vikaragosi vya kutekeleza majukumu ya wakoloni. Said, vilevile, alitumia imani za kiuchawi za pungwa kuzua taswira ya mkoloni ni nani na athari yake kwa Mwafrika ni gani katika mahusiano yao ya kiukoloni mamboleo.

Emmanuel Mbogo ametumia utanzu wa masimulizi ya kingano wa sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika kusimulia kuhusu kisa cha msichana kwa jina Nyamiti aliyeuawa kikatili siku moja tu kabla ya arusi yake. Chidama mganga mwenye wivu alimuua mhusika Nyamiti kwa uchawi wa msukule na baadaye

kumfufua kiuganga na kumpeleka katika shamba lake ili kumtumikiza yeye na wengine aliowaua kwa njia hiyo kwa ajili ya uzalishaji mali. Kisa cha Nyamiti ni taswira ya kijazanda inayomithilisha unyakuzi wa nchi za Afrika unaofanywa na nchi za Magharibi katika mfumo wa kikoloni na ukoloni mamboleo na kuzilazimisha kuwa katika mfumo wa kiuchumi unaozikandamiza kiuchumi, kisiasa na kiutawala.

Mbogo vilevile ametumia tanzu za ngoma na nyimbo kujenga taswira ya ukandamizaji na unyanyasaji. Ngoma ya Chidama inatumiwa na mtunzi kistiari kuonyesha jinsi viongozi watawala wanavyowahadaa na kuwavuruga akili vijana na umma kwa jumla kwa kutumia ulaghai na uchawi kuwamiliki na kuwadhibiti ili waweze kuwatumikiza katika uzalishaji bila malipo. Katika mfumo wa biashara huru na utandawazi unaoendeleza ukoloni mamboleo, Waafrika kama vizuu wa Chidama katika tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* wanafundishwa kucheza ngoma na nyimbo ambazo zinawafanya kuwa wakakamavu wa mwili lakini mazuzu wasioweza kutumia akili zao vizuri kung'amua unyanyasaji na ukandamizaji wanaofanyiwa wao.

Ngoma pia imetumiwa na mtunzi Emmanuel Mbogo kujenga taswira ya ukombozi kupitia kwa ngoma ya Ng'wanamalundi. Ngoma hii ilifundishwa watu wanaorejelewa kwa jina vizuu ambao ni watumwa waliotekwa baada ya kuuawa na kufufuliwa kichawi na mganga Chidama kwa ajili ya ujima wa lazima katika shamba la Chidama. Wachezaji wake wanafundishwa kuicheza kwa utaratibu ili kuwaletea ukombozi. Ngoma ya Ng'wanamalundi ambayo ni kinyume na ngoma ya Chidama ni ngoma inayotumiwa na mtunzi kama mbinu ya kuendeleza dhamira ya uhamasishaji wa waliodhulumiwa kuzinduka na kuanza kupigania haki zao ili kujinasua kutokana na mikatale ya unyanyasaji wa wadhalimu.

Ebrahim Hussein na Said A. Mohamed katika tamthilia zao za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* wametumia tanzu za usimulizi wa kingano kuchora taswira ya utandawazi. Hussein anatumia masimulizi ya chewa mkubwa anayeishi baharini anayebadilisha mkondo wa maji anavyotaka kwa kuvuta na kumeza maji mengi pamoja na vilivyomo kama samaki, mawe na vingine. Masimulizi haya yanajenga taswira ya nchi za Magharibi kumiliki njia zote za kiuchumi, kijamii na kiutawala na kwamba huweza kuamua mkondo nchi changa za ulimwengu wa tatu zitauchukua. Viongozi wa nchi maskini kama nahodha kwenye bahari ya mawimbi makubwa hawana udhibiti wa nchi zao. Nchi hizo zinaelekezwa na nchi za Magharibi ziende wapi kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa lazima. Wasemavyo Said A. Mohamed na Ebrahim Hussein, viongozi wa nchi za Afrika wamepandwa na pepo au Mashetani (wakoloni) ambao wanawadhibiti na kuwaongoza wanakotaka kwa nia ya kujinufaisha wenyewe.

Akielezea zaidi kuhusu utandawazi katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi*, Said A. Mohamed anaeleza kuwa ni hali ya dunia kuonekana kama kijiji kimoja ambapo kuna uhuru wa kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine mbali na uhuru wa kufanya biashara. Ingawa utandawazi huchukuliwa kuwa unafaidi nchi zinazoendelea kufungua milango ya biashara, masoko huria na kuufanya utamaduni wa taifa moja kukutana na wa taifa lingine, ukweli ni kwamba nchi zilizoendelea hutumia utandawazi kama kisingizio cha kufanya biashara na nchi ambazo hazijaendelea kuzilaghai, kuzidhibiti, kuzitawala na kuzinyonya. Mohamed anatumia utandawazi kuelezea kistiari jinsi nchi za ulimwengu wa kwanza zilivyotoka Afrika baada ya ukoloni mkongwe na kurudi baadaye katika mfumo mpya wa ukoloni mamboleo, kuja kuzidhulumu nchi zinazoendelea. Hivyo, mtunzi anautumia

utandawazi kusisitiza kwamba wakoloni bado wapo Afrika (Mashetani Wamerudi Afrika).

Said A. Mohamed, mtunzi wa tamthilia ya *Pungwa* vilevile, ametumia ndoto kudhihirisha utabaka, unafiki na uongozi mbaya unaoendelezwa na viongozi wa nchi za Afrika. Mhusika Bwana, ambaye ni kiwakilishi cha viongozi wa nchi za Afrika anadhihirisha wasiwasi wa kupokonywa mamlaka kupitia kwa ndoto za kila wakati. Kwa sababu ya uongozi wao mbaya, viongozi wa Afrika wana wasiwasi wa kupokonywa mamlaka hata katika ndoto zao jambo ambalo linadhihirisha unafiki wa viongozi wa Kiafrika. Kwa jumla utafiti ulifanikiwa kuonyesha kwamba watunzu wa tamthilia teule, walifanikiwa kutumia kitaswira tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika ili kujenga na kuimarisha dhamira na thima za tamthilia zao za Kiswahili.

### 8.2.3 Maendeleo na Umuhimu wa Sanaa za Maonyesho ya Jadi katika Utunzi wa Tamthilia ya Kiswahili

Katika sura ya saba, tulilenga kudhihirisha mabadiliko na umuhimu wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia teule za Kiswahili. Maendeleo makubwa yalipambanuliwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili tangu utunzi wa tamthilia ya *Mashetani* katika mwaka wa 1971 hadi 2016 mwaka wa utunzi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Karibu miaka hamsini ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili imeshuhudia maendeleo makubwa ya matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi za nyimbo, ngoma za Kiafrika, majigambo, ushairi simulizi, masimulizi ya kingano, maghani, malumbano ya utani, tamathali za usemi mbalimbali, miongoni mwa tanzu nyingine. Watunzi wa tamthilia teule za Kiswahili walichanganya mbinu za utunzi zilizopendekezwa na msanii na mwanafalsafa mkongwe wa Kigiriki, Aristotle, na mbinu za utunzi za sanaa za

maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika. Mwanzo wa kila onyesho la tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kwa mfano, unadhihirisha matumizi ya utanzu wa wimbo ambao ni wa ushairi simulizi wa Kiafrika ambao ulitumiwa na mtunzi kutanguliza maonyesho katika tamthilia hiyo.

Tamthilia teule katika utafiti huu zimeandikwa kwa lugha ya kishairi kama alivyopendekeza Aristotle. Hata hivyo, watunzi wetu wameasi matumizi ya sheria za utunzi wa mashairi ya kimapokeo na kuunga mkono matumizi ya mazungumzo huru ya kitamthilia baina ya wahusika. Tanzu za nyimbo na mashairi zilizotumiwa na watunzi teule zina mseto wa sehemu ambazo zina mapigo na muwala wa mawazo ya kishairi pamoja na mazungumzo ya kawaida baina ya wahusika.

Watunzi Ebrahim Hussein, Emmanuel Mbogo na Said A. Mohamed wametumia mbinu mpya ya kisasa ya kuwasilisha hisia halisi kupitia kwa majigambo yenye ishara za ndani na lugha ya kishairi inayomwezesha msomaji na mtazamaji mchezo kuelewa na kufasiri kiusomi na kitaaluma dhamira za mtunzi na wakati huohuo kupata maonjo kamili ya utamaduni wa Kiafrika. Matumizi ya mbinu changamano katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ambapo sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika zinatumiwa sambamba na mbinu za kimapokeo za Aristotle zinazomwezesha msomaji, mtazamaji na msikilizaji wa mchezo wa kuigiza kuchanganua mawazo ya ndani ya mtunzi.

Tamthilia zetu teule pia zimetumia mbinu za usimulizi wa kingano unaopatikana tu katika masimulizi ya sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika kama ilivyofanyika katika shughuli asili za uzalishaji mali pamoja na shughuli zingine za kijamii katika mazingira ya Kiafrika. Shughuli hizi ni kama matambiko, pungwa, jando, unyago, arusi, matanga na sherehe zingine za kitamaduni za Kiafrika.

Wahusika katika tamthilia za *Mashetani*, *Pungwa* na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* wanaongea moja kwa moja na hadhira yao kama ilivyofanyika katika sanaa za maonyesho ya jadi ambapo fanani alitagusana na hadhira yake. Mhusika Juma, katika tamthilia ya *Mashetani,* anaihutubia hadhira na kuiambia kwamba yeye Juma na rafiki yake Kitaru watawaonyesha mchezo wa Shetani na Binadamu. Kitaru, vilevile, anamsimulia mamake ambaye ndiye hadhira yake ya pekee, hadithi kuhusu mnyama hatari anayeitwa chewa, anayeishi katika bahari kubwa ya mbali ambaye anavuta mashua na kubadilisha mikondo yao baharini kwa kuvuta maji kwa nguvu.

Kumekuwa na mabadiliko katika matumizi ya mwangaza na giza jukwaani wakati wa maonyesho. Kitambo, maonyesho yangefanywa wakati wa usiku au katika milango iliyofungwa ili kusababisha giza kwenye jukwaa ili kuwezesha mabadiliko ya maonyesho na ili giza kuwakilisha mwisho wa onyesho. Katika miaka ya themanini na tisini, kulishuhudiwa matumizi ya pazia, taa na giza vilevile katika kugawa maonyesho. Hata hivyo, katika miaka ya elfu mbili mpaka sasa, kumekuwa na matumizi ya nyimbo katika kugawa maonyesho. Taa za rangi mbalimbali wakati mwingine hutumiwa sambamba na giza na nyimbo ili kuleta athari fulani inayokusudiwa kama vile woga, furaha, hali ya hatari miongoni mwa hali nyingine. Mwangaza wa kurunzi katika jukwaa lenye giza huweza kutumiwa kufanya maonyesho mawili au zaidi katika jukwaa moja kwa zamu.

Tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho ya jadi pamoja na utamaduni wa Kiafrika zimefaraguliwa na watunzi wa tamthilia teule tulizozichunguza katika utafiti wetu ili kuweza kutumiwa kama mbinu ya ufunguzi wa tamthilia hizo. Nyimbo, ngoma, usimulizi wa kingano, malumbano, majigambo, ushairi huru simulizi, tamathali za usemi, mafumbo, stiari miongoni mwa tanzu nyingine, zimefanyiwa ufaraguzi na watunzi ili matumizi yao yaweze kuafiki matumizi ya watunzi wa tamthilia.

### 8.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umechangia katika uelewa wa matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya asili ya tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho ya jadi zilizobainishwa katika tamthilia za Kiswahili zilizoteuliwa zilitambuliwa, kuainishwa na kufafanuliwa jinsi zilivyotumiwa kama nyenzo murua ya kutoa umbo na kuendeleza dhima ya tamthilia ya Kiswahili kwa ajili ya uelewaji wa wasomaji na wahakiki wa kazi za fasihi.

Ubainishaji na ufafanuzi wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi ya Kiafrika zilizotumika katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili ulichangia katika uendelezaji na udumishaji wa utamaduni wa Mwafrika.

Matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika katika utunzi, umeiwezesha tamthilia ya Kiswahili kujikatia nafasi ya pekee ambayo inaiwezesha kujitambulisha na kujinasibisha na muundo wa pekee wa tamthilia mpya ya Kiswahili.

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia mbili mtawalia za Uhistoria Mpya na Mwingilianomatini. Kupitia kwa matokeo ya utafiti huu, tumefanikiwa kuwezesha uelewaji wa matumizi ya nadharia za Uhistoria Mpya na Mwingilianomatini katika kutekeleza uhakiki na uchunguzi wa tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi zilizochotwa na kutumiwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili.

### 8.4 Hitimisho

Tasnifu hii ilikuwa na malengo matatu. Kwanza, tulilenga kuthibitisha kwamba tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi za asili ya utamaduni wa Kiafrika zimetumiwa kiubunifu na watunzi wa tamthilia teule ya Kiswahili katika kujenga fani na kuimarisha dhamira katika tamthilia zao.

Tulifanikiwa kudhihirisha kwamba tamthilia za *Mashetani*, *Pungwa*, *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi* ni tamthilia mseto ambazo ni zao la mchanganyiko wa mbinu za utunzi za ki-Aristotle za Fasihi Andishi na za tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi za asili ya tamaduni za Kiafrika. Watunzi wa tamthilia hizi wamechanganya mbinu za utunzi za ki-Aristotle na miundo na mitindo asili ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na kuzibadilisha kiubunifu ili kubuni tamthilia andishi ya Kiswahili ya kisasa.

Tanzu za majigambo, ushairi simulizi, nyimbo, ngoma, usimulizi wa kingano na kisakale, hotuba, soga, malumbano ya utani, mafumbo, mchezo wa kuigiza, tamathali za usemi za stiari, jazanda, semi, nahau na methali na tamaduni asili za Kiafrika za miujiza, pungwa, uchawi na uganga zilipambanuliwa kuwa zimetumiwa na watunzi wa tamthilia teule ili kujenga na kuimarisha taswira na dhamira za tamthilia ya Kiswahili kwa mujibu wa lengo letu la pili.

Lengo letu la tatu lilituwezesha kubaini ujenzi wa fani na maudhui wa tamthilia ya Kiswahili katika miongo mitano ya uhuru wa nchi za Afrika na utunzi wa tamthilia ya Kiswahili umefaidi kutokana na tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na tamaduni za Kiafrika. Watunzi wa tamthilia ya Kiswahili walikuwa na uhuru wa kufanyia sanaa za maonyesho ya jadi mabadiliko machache ya kiubunifu ili kuwawezesha kuleta umbo la tamthilia walilolidhamiria na kuendeleza dhamira zao. Matumizi ya tanzu za jadi za sanaa za maonyesho na tamaduni za Kiafrika katika utunzi wa tamthilia mpya ya Kiswahili yamekuwepo katika kipindi chote cha miongo mitano ya utunzi na tanzu hizo zimefanyiwa ufaraguzi wa kiubunifu ili kuafiki matakwa ya utunzi ya waandishi.

Tofauti na jamii za Kimagharibi ambapo sanaa za maonyesho ya jadi na Fasihi Simulizi kwa jumla imekufa, sanaa hii ingali hai katika jamii za Kiafrika na

zinachotwa kiubunifu na watunzi wa tamthilia ambao wanazitumia kama malighafi yao ya kuwawezesha kutunga tamthilia zao hususan tamthilia ya Kiswahili.

## 8.5 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu unapendekeza kuwa utafiti mwingine unaweza kufanywa kuthibitisha matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi na utamaduni wa Kiafrika katika utunzi wa tanzu nyingine za Fasihi Andishi za riwaya, hadithi fupi na ushairi.

Utafiti zaidi waweza kufanywa kuthibitisha kuwepo na Mwingilianomatini wa sanaa za maonyesho ya jadi katika tanzu za miviga ya kijamii, matambiko na makafara ya Kiafrika, muziki wa aina mbalimbali na nyimbo za dini na za maudhui mapana ya kidunia.

Utafiti huu ulifanywa kwa njia ya usomaji wa ndani na nje ya maktaba. Utafiti zaidi wa nyanjani waweza kufanywa kuchunguza matumizi ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi katika utunzi wa miviga na sherehe mbalimbali za kitamaduni za Kiafrika katika jamii na maeneo mbalimbali ulimwenguni.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili sambamba za Uhistoria Mpya na Mwingilianomatini. Utafiti mwingine vilevile, waweza kufanywa katika mada hii ya utafiti kwa misingi ya nadharia zingine tofauti ili kuakisi jinsi matokeo yatakavyojidhihiri.

**MAREJELEO**

Abdullah, A. (1998b). *Tambiko*. Karatasi ambalo halijachapishwa. Zanzibar.

Alembi, E. (2002). “The Construction of the Abanyole Perceptions on Death through Oral Funeral Poetry.” Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa. Helsinki University.

Allen, G. (2000). *Intertextuality*. London: Routledge.

Allen, J. W. T., (1971). *Tendi*. London, Great Britain: Richard Clay. (The Chancer Press) Ltd.

Bakhtin, M. M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Austin: University of Texas Press.

Bakhtin, M. M. (1990). *Art and Answerability*. Austin: University of Texas Press.

Beckett, S. (1956). *Waiting for Godot*. London: Faber and FaberLtd.

Beckett, S. (1958). *Endgame.* London: Faber and Faber Ltd.

Bessie, H. (1977). *The collector of Treasures and other Botswana village tales*. London: Heinemann Publishers.

Bosire, T. B. (2016). “Mwingilianomatini kati ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mstahiki Meya”. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Botunde, C. (1994). *Studies in Comparative Literature: New Introduction to Literature*. Edited by Olu Obafemi, Mary Tunuoye and Charles Botunde pg 55 - 74

Bryman, A. (2001). *Social Research Methods.* New York: Oxford University Press.

Cantalupo, C. (1993). *The world of Ngugi wa Thiong’o*. Trenton: African World Press

Chesaina, C. (1997). *Oral Literature of The Embu and Mbeere*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Chesaina, C. (1991). *Oral Literature of the Kalenjin*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Cruickshank, J. (1958). *Albert Camus: the literature of Revolution*. London: Oxford University Press.

Durkheim, E. (1957). *Suicide: A Study in Sociology*. New York: Free Press.

Finnegan, R. (1990). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.

Finnegan, R. (1992). *Oral Traditions and The Verbal arts; A Guide To Research Practices*. London: Routledge.

Frye, N. (1957). *Anatomy of Criticism: Four essays*. Princeton, New Jersey: Princeton University Press.

Gibbs, J. (1968). *Suicide*. New York: Harper and Row Publishers.

Hughes, R. (2012). *Testing for Language Teachers*. Cambridge: Cambridge University Press.

Hussein, E. (1967). *Wakati Ukuta*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1971). *Mashetani*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1976). *Jogoo Kijijini*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1976). *Ngao ya Jadi*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1967). *Alikiona.* Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1969). *Kinjeketile*. Nairobi: Oxford University Press.

Hyslop, G. (1957). *Mgeni Karibu*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Hyslop, G. (1957). *Afadhali Mchawi*. Nairobi: Oxford University Press.

Indagasi, H. (1991). *Notes on William Shakespear's Romeo and Juliet*. Nairobi: East African Educational Publishera Ltd.

Ionesco, E. (1962). *Rhinocerous / The chairs / The Lesson.* Harmondsworth: Penguin Classics.

Kabira, M. W. (1983). *The Oral Artist*. Nairobi: Heinmann.

Kamau, N. S. "Fasihi Simulizi na Sanaa ya Maonyesho: Tathimini ya hadithi kama kipengele cha Tamasha za michezo ya kuigiza katika shule na vyuo nchini Kenya". Katika, Kimani Njogu (et al) (2006). *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi. Twaweza Communications.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi: East African Literature Bereau

Kezilahabi, E. (1974). *Kichwa Maji*. Dar es Salaam: East African Publishing House.

Kiai, A. na Munungi, M. (1998). *A guide to looking for a Rain God and other short stories from Africa*. Nairobi: Longhorn Publishers.

King'ei, G. K. (1987). *Mwongozo wa Mashetani*. Nairobi: East African Publishers.

King'ei, G. K. na Kisovi, C., (2005). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Kobia, J. M. (2008). "Utendaji katika nyiso za Waigembe". Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A semiotic Approach to Literature and Art*. New York: Columbia University Press.

Kristeva, J. (1984). *Revolution in Poetic Language.* New York: Colombia University Press.

Langham, A. R. (1991). *Revising prose: A handbook of rethorics terms*. Berkely: University of California press.

Leech, G. N. na Short, M. H. (1981). *Style in Fiction*. London: Longmann Group.

Lemaster, T. (2012). "What is intertextuality". Great World Text. A programme of the centre for Humanities. Wisconsin: University of Wisconsin- Madson.

Madiang', O. (2003). "A story of the Power of Narratives" Seminar paper presented at the primary schools Drama Teachers workshop at Nakuru. Unpublished paper.

Maitaria, J. N. (2012). "Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili. Dhima ya Methali" Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Marete, J. K. (1998). "Ujadi katika tamthilia mbili za Emmanuel Mbogo" Tasnifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Moi.

Matti, G. N. M., (1993). "Sanaa za maonyesho za Kiafrika za jadi: Mfano wa Tohara ya Watharaka" Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu Cha Moi.

Mbogo, E. (1999). *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mbogo, E. (2004). *Vipuli vya Figo*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Merriams, S. (1998). *Quantitative Research and Case study Application in Education*. San Francisco: Base Publishers.

Miruka, C. (1994). *Encounter with Oral Literature*. Nairobi: East Africa Educational Publishers Ltd.

Mlama, P. O. (1983). "Hali ya Sanaa za Maonyesho Tanzania" Katika, *Fasihi: Makala za Semina ya Kitaifa ya Waandishi wa Kiswahili III.*

Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S. A. (1988). *Pungwa.* Nairobi: Longhorn

Mohamed, S. A. (2000). *Review of Ebrahim Hussein*. Swahili Theatre and Individualism. By Alain Ricard. Nordic Journal of African Studies 143: 418

Mohamed, S. A. (2016). *Mashetani Wamerudi*. Nairobi, Kenya: Sportlight Publishers (EA) Ltd.

Moi, T. (ed), (1986). "The Kristeva Reader" Oxford: Basil Blackwell.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha.* Indiana University. Educational Publishers and Distributors Ltd.

Mugenda, O. M. na Mugenda, A. M. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approches.* Acts Press.

Muhando, P. na Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa ya Maonyesho*. Dar es Salaam. T.P.H.

Muindi, A. (1990). "Usawiri Wa wahusika makahaba katika riwaya ya Said A. Mohamed" Tasnifu ambayo haijachapishwa. Chuo kikuu cha Kenyatta.

Muingo, R. A. (2015). "Tathimini ya Mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthilia ya Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liyongo" Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Muiruri, P. K. (2006). *Maandalizi Mufti ya K.C.S.E. Fasihi Simulizi, Maswali na Majibu.* Nairobi. Palco Enterprises Ltd.

Mulokozi, M. M. (1989). "Tanzu za Fasihi Simulizi" Katika, *Mulika* (Juzuu Na. 21) Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI.

Murimi, J. N. (2016). "Mwingilianotanzu katika Muziki wa Modern Taarab-mipasho". Tasnifu ambayo haijachapishwa. Chuo kikuu cha Moi.

Musau, P. M. (1985). "Euphrase Kezilahabi mwandishi aliyekata tamaa" Tasnifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mwamzandi, I. (2002). "Majadiliano ya Tanzu katika Ushairi wa Kiswahili" Katika Simala, K. I. (Mh), (2002). Jarida la *CHAKITA*. R.k 34-47. Eldoret: Moi University Press.

Ndege, M. S. (2003). "The Kimeru Folk Narratives: An Anthropoetics Study" Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Gent.

Ndimofor, N. (2011). "Oral Literature of the Akum People: A study of the Folksongs and Cultural Elements" Tasnifu ya Stashahada ya Juu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Yaunde

Ndungo, C. (2006). "The Image of Women in African Oral Literature: A case study of Gikuyu Oral Literature" Katika, *Gender Issues Research Report seire.* (No. 23 kr. 88 -100). Ethiopia. OSSREA.

Ngesa, A. K. Matundura, E. na Kobia, J. (2015). "Mwingilianomatini katika Tamthilia za Kiswahili: Mashetani na Kijiba cha Moyo" Katika, *Swahili Forum*. 22(2015) S. 42 - 71

Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari.* Nairobi. Phoenix Publishers.

Njogu, K. na Chimera, R. (2011). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Noordin, M. (2006). "Simulizi maalumu ya Pepo kama ufasiri wa Fasihi Simulizi". Katika, Njogu, K. Momanyi, C. na Mathooko, M. (Wahariri), (2006). *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza communications.

Obiechina, E. (1992). "Narrative Proverbs in African Novel" Katika: *Oral Tradition Journal.* (Juz. 17 kr. 45 - 62). Chuo Kikuu cha Pittsburg-Bradford.

Offiong, D. A. (2001). *Globalization: Post-Neodependency and Poverty in Africa*. Enugu Nigeria: Fourth Dimention Publishing Co.

Okpewho, I. (1985). *The heritage of African poetry.* England: Longman Group.

Plaks, A. H. (1976). *Archetype and Allegory in The Dream of the Red Chamber.* Princeton and Guildford, Survey: Princeton University Press.

Plotell, J. P. na Cherney, N. K. (1978). *Introduction to intertextuality; New Perspective in Criticism.* New York. Literary Forum.

Ruo, K, R. (1989). *Nguzo za Ushairi wa Kiswahili.* Nairobi: Macmillan Publishers.

Seitei, P. C. (1980). *See So That We May See: Performance and interpretation of Traditional Tales from Tanzania*. Bloomington: Indiana University Press.

Senkoro, F. E. M. K. (2011a). *Fasihi.* Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.

Senkoro, F. E. M. K. (1996). "Understanding Gender through Genre: Oral Literature as a Vehicle for Gender studies in East Africa" A Paper presented at the annual African Literature Association. Howard University press. Washington DC.

Senkoro, F. E. M. K. (2011b). *Mikabala ya Kinadharia ya Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.

Simiyu, W. F. (2015). "Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika. Mfano wa Embalu na Mwaka Kogwa". Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Soyinka, W. (1973). *The Strong Breed.* Newyork: Oxford University Press.

Soyinka, W. (1975). *Death and the King's Horseman.* Newyork: Norton Press.

TUKI, (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford University Press.

Wa Thiong'o, N. (1972). *Homecoming.* Nairobi. Heinemann Kenya Ltd.

Wa Thiong'o, N. (1981a). *Decolonizing the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.

Wa Thiong'o, N. (1981b). *Writers in Politics: Essays.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Wafula, R. M. (1992). "Nadharia kama mwongozo wa utunzi na uhakiki katika fasihi". Staff seminar Paper. Chuo Kikuu cha Nairobi. Makala ambayo haijachapishwa.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi na Vipengele vyake*. Nairobi, Kenya: Phoenix publishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2008). *Kazi ya Fasihi. Misingi ya Uchunguzi wa fasihi*. Nairobi. Vide Muwa Publishers Ltd.

Wanjala, F. S. (2011). *Kitovu cha Fasihi kwa shule. vyuo na Ndaki*. Mwanza. Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Wellek, R. na Waren, A. (1949). *Theory of Literature*. USA, Great Britain. Penguin Books.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho 1: *Mashetani*

### 1. Usimulizi wa Shetani 1

Mbuyu wenye pango. Vijana wawili katika matembezi yao wanafika mbele ya mbuyu huo.

JUMA: Wananchi: kwa mara nyingine chini ya mbuyu huu mimi Juma, na rafiki yangu kitaru, tutakuonyesheni mchezo wa Shetani na Binadamu. Mimi nitakuwa Shetani, na kitaru, atakuwa Binadamu.

(*Mashetani* - uk 1).

### 2. Usimulizi wa Shetani 2

SHETANI: Umeshuhudia miujiza. Nimekuonesha miujiza ili uamini uwezo wangu. (*Anakaa juu ya kiti kwa upole na huruma.)* Usiogope, usiogope. Kwako wewe mimi rafiki. Wala hutapata rafiki kama mimi. (*Anabadilika kwa ukali*.) Unaniogopa?

(*Mashetani* - uk 2).

### 3. Usimulizi wa Shetani 3

SHETANI: Rafiki mpenzi, rafiki mwandani. Rafiki wa milele, rafiki wa daima. Ninakupokea. Ninaifurahikia leo, siku ya uzao wako. Kutoka katika tumbo la giza jeusi, kuingia katika ulimwengu wa nuru nyeupe. (*Binadamu anaamka.*) Tanabahi, fahamu. Wewe ni mtoto, na mama. Pole kwa uchungu wa uzazi. Jivunie. Furaha. Wewe – mtoto – ni mzuri zaidi kuliko wewe – mama. Ni kanuni ya maisha: kinachozaliwa ni kizuri zaidi kuliko kinachozaa. Simama! (*Binadamu anataka kusimama*, *hawezi*. *Anaanguka.*) Simama katika uzuri wako. (*Mashetani* - uk - 4).

### 4. Majigambo ya Shetani

SHETANI: 1. Unajua mimi nani?

2. Mimi Shetani.
3. Siyo jini wala kuhani.
4. Mimi Shetani.
5. Uwezo wangu hauhifadhiki,
6. Wema wangu hauhisabiki,
7. Ubaya wangu hausemeki,
8. Ninajenga.
9. Ninabomoa.
10. Ninatukuza.
11. Ninadhalilisha nitakavyo.
12. Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi.
13. Mimi ni uwezo na uwezo ni mimi.
14. Tazama muujiza. (Anajibadilisha.) Sasa mimi ni nani? –

(*Mashetani* - kr 1 - 2)

**5. Mazingaombwe/muujiza ya Shetani**

Binadamu; Kama ndege … vile … ndege.

SHETANI: Sawa. Nimejigeuza ndege. Ninaweza kadhalika kuwa upepo, nikawa kila mahali. Naweza kuwa nafsi, nikaingia katika roho yako au ya wenzako. Sasa tazama. Unaona nini?

BINADAMU: Unarukia tawi.

SHETANI: Na sasa, unaona tawi.

BINADAMU: Tawi limegeuka kiti –

(*Mashetani* - uk 2).

**6. Fumbo la Shetani na Binadamu**

(*Shetani anatokeza. Binadamu anataka kumvamia.*)

SHETANI: Aaa, umetoa ahadi kuwa hutaniua mpaka nimemaliza maombi yangu matatu.

BINADAMU: Haya, fanya upesi.

SHETANI: Ombi la kwanza, nipe ruhusa kukuuliza swali, lakini usinijibu sasa. Umepata kumsikia nani akajichinja mwenyewe? *(kimya)*.

Ombi la pili, kabla hujaniua mimi na wewe tusherehekee kifo changu.

Ombi la tatu, wewe uchague namna ya kusherehekea kifo changu.

NINADAMU: Maombi yako yamekubalika. Sherehe itafanywa.

SHETANI: Na vipi tutaisherehekea?

BINADAMU: Kwa *walt.*

*(Shetani anacheka kwa furaha. Baada ya muda wanaanza kucheza waltz kwa furaha kubwa na kwa ustadi. Kwa vicheko na hanjam wanakunywa mvinyo. Baada ya muda wote wananyamaza. Kimya)*

SHETANI: Wakati wangu wa kufa umefika.

*(Shetani na Binadamu wanatazamana. Wote wanatabasamu. Shetani anampa Binadamu kisu. Wanashikana ndugu wawili wapenzi. Shetani anamwekea Binadamu ubavu sawa. Binadamu anatumbukiza kisu katika mbavu. Shetani anacheka. Kila pigo la kisu linasababisha kicheko zaidi. Kicheko kinajaa nyumba nzima. Kila akisikiaye anashikwa na hofu. Shetani anaanguka lakini kicheko kinaendelea. Mara kinanyamaza ghafla. Kimya. Na kimya kinatisha kama kicheko au zaidi. Binadamu anangojea. Hakuna kitokeacho. Binadamu anapumua. Anautazama mzoga.*) (*Mashetani* - uk 7)

**7. Wimbo wa Binadamu**

1. wako wapi walio wakijitapa?
2. Sasa twawataka.
3. Wako wapi walio wakijitapa?
4. Sasa twawataka.
5. Tumekwisha (*anacheka*) wakamata
6. Wakamata.
7. Tumekisha wabwatabwata.
8. Wako wapi waliokuwa juu jana?
9. Sasa twawataka. Wako wapi waliokuwa juu jana?
10. Sasa twawataka.
11. Tumekwisha waangusha
12. Waangusha.
13. Tumekwisha wasagasaga.

14. Tumekwisha wakamata
15. Wakamata.
16. Tumekwisha wabwata.
17. Tumekwisha waangusha
18. Waangusha.
19. Tumekwisha wasagasaga.

(Mashetani - *kr 9 - 10*)

**Kiambatisho 2:** ***Pungwa***

**8. Wimbo wa Sauti ya mzuka**
1. Aaaaaaa, a-a a-a …
2. Aaaaaaa, a-a a-a …
3. Aaaaaaa, a-a a-a …
4. Shahada mara ngapi
5. Mara ngapi shahada?
6. … Shahada mara tatu …
7. Shahada mara ngapi?
8. Moja?
9. Mbili?
10. Au tatu?
11. Mara tatu labda …
12. Labda?
13. Ata!
14. Hii ni Hakika,
15. Hakika hasa! Yakini!
16. Nani ajuaye ayajuayo mzuka?
17. Vipawa vyangu vimewakalia juu wanadamu …
18. Macho yamepakwa ukungu,
19. Masikio vipande vya chuma,
20. Pua vitomeo vya vijiti,
21. Hisia imezimwa kwa ganzi,
22. Na bongo limetomewa tope … vyote,
23. Vyote maradufu!
24. Mimi ndiye mimi,
25. Mpiga-mbizi
26. Mpiga-mbizi pasi ukomo wa pima.
27. Huzamia kuliko mkizi
28. Na kufika kusiko fikwa --- vina vya ajabu!
29. Mimi mzuka wa bahari saba na mgaagaa fukwe saba,
30. Mhodhi wa miamba saba, mkwepa mawimbi saba
31. na mfika mafungu saba
32. Mimi mpiga- mbizi na mwibuka hima,
33. Kufumba na kufumbua,
34. Pasi na kusongwa na maji …
35. Mzuka wa pepo za tezi na omo,
36. Na matlai ivumapo na Mande ingurumapo,
37. Nipo hamnioni,
38. Naishi, siishi,
39. Machoni mwenu siishi,
40. Niko mbali kumbe niko karibu,
41. Niliondoka kumbe bado nipo,
42. Nimeselelea, nimelowea,
43. Na kwamba hamnioni, si kama sipo,
44. Najigeuza nitakavyo …
45. Pengine ni miongoni mwenu,
46. Ndani ya damu zenu,
47. Pengine nipo, pengine sipo, pengine nimejaa tele …

48. Hewa, alama, nukta, kidudu, kinyama, vidogo na vikubwa,
49. Vyote naweza kuwa.
50. Naishi kote, niko kote,
51. Sifi hata nikiuliwa,
52. Nyundo hainivunji, mkuki haunitoboi,
53. Mshale haunitumbui, bunduki hainirarui,
54. Mwili wa shaba, moyo wa dhahabu na mifupa chuma …
55. Mikonzo yangu mithili ya pweza na Mungu wa kibaniani,
56. Huikunjua bara na bahari,
57. Kufika hata kwenye tundu za sisimizi na mchwa,
58. Kusomba hata punje ya nafaka na sukari,
59. Ili kujijengea milima ya manufaa,
60. Milima isiyoporomoka, iliyokita imara daima,
61. Huijenga kwa n’navyovinyakua na kuvichukua.
62. Vyenu navifanya vyangu,
63. Vya kunufaisha watani wangu wa kiShetani.
64. Na nyinyi ole wenu!
65. Nawapulizia usingizi,
66. Mzito wa ajabu,
67. Mlale daima
68. Usingizi utakaokuchukueni karne kwa karne,
69. Pasi na kujitambua,
70. Kabla hamjaamka.
71. Sitochoka kuwaingia vichwani,
72. Ndimo mwenye mustakabali wangu,
73. Kukuingieni vichwani na kukumilikini,
74. Kuzimiliki fsi zenu,
75. Na kila kilicho chenu,
76. Hata kufyonza damu yenu,
77. Na kupanda juu ya mabega yenu,
78. Kuwatenda na kuwatendekeza,
79. Na kuwafanya duni milele …
80. Aaaaaa, a-a, a-a, a-a …
81. Aaaaaa, a-a, a-a, a-a …
82. Aaaaaa, a-a, a-a, a-a …
83. Kweli shahada mara tatu.
84. Moja alikuwa jana,
85. Moja iko leo,
86. Na nyingine kesho …
87. Hali ileile,
88. Ya kuvilewesha vichwa vya hata walio bora miongoni mwao.
89. Mimi mzuka wa wazuka,
90. Mimi pepo wa pepo,
91. Mimi jinni wa majini,
92. Mimi wa ardhini na wa baharini,
93. Mimi niwezaye ruka angani,
94. Mimi niwezaye tua ardhini,
95. Mimi niwezaye kupasua ardhi na kuzama na kuibuka,
96. Kufumba na kufumbua kama mchezo …
97. Aaaaaa, a-a, a-a a-a …

98. Aaaaaa, a-a, a-a a-a …
99. Aaaaaa, a-a, a-a a-a …
(*Pungwa* – kr 1 -4)

**9. Majigambo na Ushairi Simulizi wa Mhusika Bwana aliyepandwa na pepo.**

1. aaaaaa, a-a, a-a, (Anachagawa)
2. a-a, a-a, Aaaaaa (Anayongoya)
3. Mimi ni mimi
4. Mimi ni pepo,
5. Niliyesafiri ng'ambo saba
6. Kuja hapa kulowea
7. Nilikuja hapa jana
8. Ninakuja hapa leo
9. Na kesho, kesho kutwa, mtondo na mtondogoo …
10. Nitakuja … Nitakuja … Nitakuja kila siku …
11. Nimo ndani ya kichwa cha mwele huyu
12. Nakwenda mbago naye,
13. Ameshalainika huyu …
14. Si mgumu tena,
15. Si mzito tena … mwepesi kama buwa,
16. Hakabi tena huyu … hanyongi tena huyu …
17. Hanyongi wala haui
18. Na sasa kajitia mawazo
19. Anafikiri ya jana, leo na kesho
20. Anafikiri juu ya ndugu zake
21. Na wanawe au na wenzake akina nyiye
22. Lakini sivyo tulivyoahidiana,
23. Sivyo tulivyoahidiana
24. Sicho kiaga chetu
25. Ndivyo nilivyoona nirudi nimkalie juu ya kichwa.

…

26. Ata! Hayupo hapa mume wako
27. Unasema na kivuli chake tu
28. Siye huyu mume wako
29. Kivuli chake labda
30. Ametekwa mume wako
31. Amegwiwa
32. Kavunja mkataba huyu
33. Nitamtesa
34. Nitamwadhibu
35. Adabu, adhabu, mateso
36. Ah, hayupo mume wako hapa
37. Huyu siye

…

38. Hapana mimi hapa
39. Hapana mimi mumeo hapa
40. Pana mimi mimi
41. Mzuka aliyezuka
42. Mzuka bin Mzuka
43. Na pepo bin pepo

44. Pepo wa kaskazi
45. Niogeleaye na theluji
46. Nina majira manne
47. Mwenye uwezo wa ajabu
48. Ninovunja miamba na majabali
49. Ninofua vyuma na kuumba maumbo
50. Na kuyaimbisha na kuyafanya yasuguane,
51. Yazalishe, yatoe milioni kwa milioni
52. Mimi mhodhi wa wahodhi
53. Mwenye kuuza visivyouzwa
54. Mwenye faida isiyo mipaka
55. Mwenye kumwaisha jasho
56. Na kufyonza damu ya watendaji
57. Mhodhi ardhi na bahari
58. Na hata anga la hewa
59. Vilivyo juu ya ardhi na tumbo lake
60. Vyote mali yangu
61. Vya mbali na karibu

(*Pungwa* – kr 8 - 10)

**10. Mahoka Kumpunga Mhusika Bwana aliyepandwa na Shetani/pepo**

Mahoka *(Anatoa kitabu kidogo mfukoni. Anasoma kidogo kwa kumung'unya midomo)* Mumeo kwa n'navyomwona amekumbwa na pepo mkubwa. Pepo lililovuka bahari kuja huku kumdhili na kumnyanyasa yeye na watu wake.
Yeye ndiye kiti chake ati. Ana kiaga kwake; ana deni kwake; ana makubaliano … na mumeo sasa anapata tabu.
(*Pungwa* – uk 14)

**Kiambatisho 3:** ***Ngoma ya Ng'wanamalundi***

**11. Ngoma ya Seche**

Seche: 1. Leo mambo mtaona
2. Leo mambo mtaona
3. Tumembadili kijana!
4. Tumembadili kijana

(*Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 8)*

**12. Ngoma ya arusi**

(*… Mirindimo ya ngoma ya arusi inaongezeka; sasa tunasikia wanabadili mapigo na tunasikia mirindimo ya sindimba. Nyamiti anaruka kwa furaha) – Sindimba – Unyago! (Mirindimo ya sindimba inaongezeka). Iko wapi kanga, (anachukua kanga) Heri nicheze leo, kesho chambilecho somo yangu, niweke soni usoni! (kasha jifunga kanga mbili kiunoni sasa anaanza kucheza. Kwanza ni polepole huku akiimba pamoja na waimbaji wa nje. Sasa mirindimo sindimba inapamba moto, nae Nyamiti anapamba moto. Vigelegele vinasikika; naye anachemka zaidi ... anapepesuka – amechoka, anajibwaga chini kwa furaha*)

(*Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 11)*

**13. Malumbano/Majigambo ya Chidama**

Sasa wakati umefika wa kumtumia Ng'wanamalundi joka hili la vichwa saba; liende likamfundishe adabu na heshima. (*anaanza tena kunuiza kimyakimya. Baadaye anaingiza mkono ndani ya kibuyu au kapu na kumtoa nyoka wa vichwa saba. Anamlisha dawa mdomoni huku akiimba kisha anasema nuizo huku anghali amemsika*)

1. Ewe mtambaa chini
2. Ewe chatu wangu, mvunja mbavu
3. Ewe kiboko wangu, mkoboa watoto
4. Ewe songwe wangu, msokomeza wana
5. Ewe swila wangu, mvimbisha matumbo
6. Ewe kipiri wangu, wa mate ya pilipili
7. Ewe moma wangu, mmogoa miamba
8. Ewe ndumakuwili, mwanzilishi wa kondo
9. Joka la vichwa saba
10. Lakini ni joka moja tu
11. Moja katika saba na saba katika moja,
12. Ewe mtambaa chini, mwenye meno ya sumu
13. Ngurumo lako kama radi ya kiangazi,
14. Wewe mbabe wa wababe
15. Haya na wende, nakutuma
16. Nenda ukatumbukize ukucha wako wa chuma ubavuni mwake
17. Ukamfutue na kumfumua matumbo yake
18. Ukamzingire na kumzingira figo zake
19. Ajue kwamba mimi Chidama ni Chidama kweli

(*anamtemea mate kichwani kasha anamrusha nje kupitia dirishani*)

(*Ngoma ya Ng'wanamalundi – uk 24)*

**14. Ngoma ya Chidama ya kumkaribisha kizuu mpya**

MAHUBE: (*kama Disco Jokey*) Wandugu wapenzi! Vizuu na Vizukule! Madudu na Maduduvule! Kwa mara nyingine tena tunawaletea magoma ya kumkaribisha: MDUDU MWENZE TUU!

(*Vizuu wanapiga makofi, wanashangilia*) …

MAHUBE: Sasa unakuja muziki moto moto! Magomo ya Tilantiki. Katiki magoma ya Labama. O.K. One – Two – Three –Go!

(Mara muziki unaanza na vizuu wanacheza dansi ambayo haina mpangilio; ni fujo na kurukaruka ovyo.

(*Ngoma ya Ng'wanamalundi* - kr 19 – 20)

**15. Malumbano/Majigambo ya Ng'wanamalundi**

(*kutoka chumbani, anakuja pale ukumbini kwa fosi; anampiga Yule nyoka kwa mgwishu wake. Nyoka anatulia. Sasa anamkamata na kuanza kunuiza na kusema naye*)

1. Najua aliyekutuma
2. Lakini huyo si mulume sawasawa
3. Wewe ni tonga, hujawa tui bado.
4. Huchochote bali garasa,
4. Shushu la nyoka mgonjwa,

(*anamtemea mate*)

6. Lakini nakutambua wewe nani
7. Najua ndiye wewe Yule anukae damu ya maskini.
8. Huwezi kunizuga kwa mavazi uliyovaa,
9. Kwani sabuni na manukato
10. Havitoshi kutoharisha nuksi
11. Iliyoko ndani ya kichwa,
12. Roho, nafasi na matendo yako.
13. Kwani nani hajui kuwa
14. Wewe ni mchawi wa *Mzukule*?
15. Nani hajui kuwa wewe hupika
16. Vitumbua kwa maji ya
17. Kuoshea wavu ili vitoke
18. Nani hajui kuwa wewe
19. Hutumia kiganja cha motto
20. Aliyekufa kuchotea na
21. Kuuzia vitambaa hivyo?
22. Nani hajui kuwa:
23. Wewe hutumia vipara
24. Vya Binadamu kuvulia
25. Matenga kwa matenga
26. Ya samaki …
27. Ukanadi, ukachuma ndarahimu?

(*kimya*)

28. Lakini saa wakati umefika wa kuichwza ngoma ya Ng'wanamalundi

(*Ngoma ya Ng'wanamalundi* - kr 48 – 49)

**Kiambatisho 4:** ***Mashetani Wamerudi***

**16. Ngoma ya Mwanambele – Mchezo Mpya "Roho Haifi)**
1. Walitumia na wanatumia ndimi,
2. Ndimi za uwongo,
3. Ndimi zilizoshikamana na lugha yao,
4. Sisi tunatumia lugha zetu,
5. Na wengine wanatumia Krioli na Pijini,
6. Kuwa lugha zao – Sawa kabisa!
7. Lugha hizo huianisha simulizi za historia,
8. lugha kama Kiswahili,
9. na zile zinazoitwa Krioli u Pijini,
10. lugha hizo husimulia ukoloni,
11. na baada-ya-ukoloni,
12. yenye ladha ya mapigo ya vita,
13. Ukoloni na ukoloni-mamboleo!
14. Pigeni makofi. *(Anaiambia nhadhira. Makofi yanasikika kutoka kwa hadhira. Kasha polepole anatoweka Mwanambele. Halafu kimya. Kimya kirefu kidogo …)*
*(Mashetani Wamerudi* – uk 1)

**17. Wimbo wa ngoma wa Mwanambele**
1. Jambo lile la kihoro
2. Lile jambo la kihoro,
3. Jambo lile la kiwewe,
4. Tena jambo la kiwewe,
5. Jambo lile la kidonda,
6. Tena homa ya kidonda,
7. Aaaa, 'ukoloni' ni kihoro,
8. Ukoloni ni kiwewe na kihoro,
9. Ukoloni homa ya kidonda!
10. Homa ya kidonda ukoloni!
11. Hasa sasa ukoloni mamboleo,
12. Umepewa jina jipya,
13. Linaloitwa Utandawazi!
*(Mashetani Wamerudi* – uk 10)

**18. Wimbo wa burudani wa ngoma wa Mwanambele – Mazingaombwe: Vuta nikuvute…**
1. Sauti kubwa ya kujenga ubwana,
2. Wakati uliopita na uliopo,
3. Sauti ya u- masta, sauti ya ubwana,
4. Lakini sasa ubwa unapiwa teke,
5. Lazima tuupige teke la ubwana,
6. Teke la 'grand narratives'
7. Ikipingana na 'public narratives'
8. 'grand narratives',
9. Hai baba, hai mama, hai kijana,
10. Hai kibinti – songeni mbele wananchi!
11. Katika 'public narrative',
12. Ni msemo wa kila mtu,

13. Msemo wa kijamii,
14. Msemo wa kila mtu kusema – public
narrative!
15. Tumeweza kusema pamoja,
16. Katika upya unaofaa!
17. Kauli ya pamoja!
((*Mashetani Wamerudi* – uk 15)

**19. Wimbo wa ngoma wa mwanambele – Ya jana si ya Leo**
1. colonial discourse ipo hadi sasa,
2. sema utakalo,
3. andika utakacho,
4. tupinge ubwana wao, mradi kejeli tu kilichopo,
5. kwa upande wetu, na upande wao,
6. sisi tuna counter discourse,
7. kaunta diskozi,
8. ndio lipizo letu,
9. kamwe si mabwege sisi,
10. kinyume na walivyosemwa wao!
*(Mashetani Wamerudi* – uk 22)

**20. Wimbo wa utetezi wa ngoma wa mwanambele – Kipimo cha usawa: Wakubwa na wadogo…**
1. Decolonization …
2. Amkeni watetezi wa uhuru na haki
3. Amkeni Waafrika, Amkeni Waasia
4. Amkeni Karebian,
5. Tatizo letu moja,
6. Amkeni Amerika ya Kusini,
7. Wawapi vijana wa Mahatima Ghandhi,
8. Wawapi vijana wa Patrice Lumumba,
9. Wawapi vijana wa Amilear Cabral,
10. Amkeni kusimamia Nationhood,
11. Mwelekeo wa uhuru wa utaifa umefika,
12. Amkeni kusimamia mataifa kamili,
13. Upeo wa nationalism,
14. Uzalendo ni upeo wa mwanzo na mwisho,
15. Upeo huu ni muhimu!
(*Mashetani Wamerudi* – uk 28)

**21. Wimbo wa sheria wa Mwanambele – Mpandangazi na Mshukangazi**
1. Sheria zilizotumika zamani na jinsi
2. Tulivyoachiwa sasa,
3. Sheria walizoturithisha,
4. Sharia ya kuchukua mali zetu,
5. Sharia wanazotupunja katika kandarasi,
6. Kwa pesa ndogo na thamani kubwa.
(*Mashetani Wamerudi* – uk 39)

**22. Wimbo wa kejeli na ngoma ya Mwanambele - Vijana wanachachamaa**
1. Uko wapi wakati wa kukandamiza,
2. Mimi nawe tunaanza kuondoa giza,
3. Ingawa bado macho kengeza,
4. Hebu ona, iwapi karne ya 'grand narrative'
5. Wakati wa kutisha na kutetemeka,
6. Sasa wakati mbaya lakini hatutetemeki,
7. Kuna mengi mapya ya kuiona dunia mbaya.
(*Mashetani Wamerudi* – uk 46)

**23. Wimbo wa urazini na ngoma ya Mwanambele – Watu na hoja**
1. Nani asiyejua ushirika wa wawili,
2. Baina ya ndugu zetu wanaokaa vitini,
3. Nakukaribisha majini na Mashetani,
4. Marafiki zao wanaoruka hewani,
5. Wanaowapa kingi nasi twapewa kidogo,
6. Ili matumbo yao yafure ziwake moto changoni,
7. Na sisi tunakubali eti kuna amani!
*(Mashetani Wamerudi* – uk 54)

**24. Wimbo wa umoja wa Mwanambele – Umoja**
1. Kamateni mikono,
2. Shikamaneni pamoja,
3. Vishindo vitakuja,
4. Lakini vitadunda,
5. Vitadunda vitadunda,
6. Vitadunda siku ya kudunda!
7. Kwa sababu sisi tumekamatana,
8. Kama nguvu za minyororo!
(*Mashetani Wamerudi* – uk 63)

**25. Wimbo wa tamaa wa Mwanambele – Mchezo wa ukweli**
1. Umoja umeshafika,
2. Hakuna lisilo na mwisho,
3. Wakati umeshafika,
4. Wa matendo si maneno,
5. Tuwachie nong'onezo,
6. Wakati wa wa vurumizo,
7. Hakuna tena kilizo!
8. Ukoloni mamboleo,
9. Uwe kwetu mfukuzo!
*(Mashetani Wamerudi* – uk 69)

**26. Wimbo wa barabarani, mchezo wa usanii wa Mwanambele – Barabarani …**
1. Mko barabarani,
2. Mwende polepole,
3. Mwende kwa amani,
4. Lenu li moyoni,
5. Na vigelegele,
6. Mko mbelembele,
7. Mwende kote nchini,

8. Huku na kule,
9. Msiogope,
10. Wafanyeni wao waogope!
(*Mashetani Wamerudi* – uk 74)

**27. Wimbo wa mwisho na ngoma ya usanii ya mwanambele – Mtu hafi, huzaliwa tena**

1. Hasha! Hasha kum!
2. Siage kwahari, tuko pamoja,
3. Eneo la kusi lino'legalega,
4. Dunia ya tatu yagongagonga,
5. Tushikane dhati safari 'tafika,
6. Safari tafika, safari tafika!
7. Enyi Dunia ya Tatu!
8. Sikilizeni sisi twanza!

(*Mashetani Wamerudi* – uk 77)

**Kiambatisho 5: Matokeo ya 'Plagiarism'**

MOTIFU YA SANAA ZA MAONYESHO YA JADI KATIKA TAMTHILIA YA KISWAHILI: MFANO WA MASHETANI, PUNGWA, NGOMA YA NG'WANAMALUNDI NA MASHETANI WAMERUDI

ORIGINALITY REPORT

| 12% | 11% | 1% | 5% |
|---|---|---|---|
| SIMILARITY INDEX | INTERNET SOURCES | PUBLICATIONS | STUDENT PAPERS |

PRIMARY SOURCES

| | | |
|---|---|---|
| 1 | repository.out.ac.tz<br>Internet Source | 3% |
| 2 | sw.wikipedia.org<br>Internet Source | 2% |
| 3 | ul.qucosa.de<br>Internet Source | 1% |
| 4 | ir-library.ku.ac.ke<br>Internet Source | 1% |
| 5 | pseudepigraphas.blogspot.com<br>Internet Source | 1% |
| 6 | Submitted to Kisii University<br>Student Paper | <1% |
| 7 | kisiwachamaarifa.co.tz<br>Internet Source | <1% |
| 8 | Submitted to The University of Dodoma<br>Student Paper | <1% |